
# MSAFIRI WA AMANI






*Mimi ni Msafiri, Msungukaji, nitaendelea kuzunguka hadi Mwanadamu atakapojifunza njia ya Amani, nitatembea hadi nitakapopewa hifadhi, nitafunga kula hadi nitakapopewa chakula.*

# *Msafiri wa Amani*

**MAISHA NA KAZI YAKE**
**KWA MAELEZO YAKE MWENYEWE**

**Kama yalivyokusanywa na kuandikwa na rafiki zake.**

**AN OCEAN TREE BOOK**
**Santa Fe, New Mexico • 1994**

**Pia kando ya kitabu cha Msafiri wa Amani kuna kitabu kidogo kiitwacho:**
**HATUA ZA KUELEKEA AMANI YA NDANI.**

Waandalizi wa vitabu hivi:
**FRIENDS OF PEACE PILGRIM**
43480 Cedar Avenue
Hemet, California 92544
(909) 927 - 7678.

Copyright © 1982, 1988, 1991, 1994, 1996 Friends of Peace Pilgrim.

Printed in the United States of America,
First Edition: December 1982
First Compact Edition: August 1988
Fourth Compact Edition: January 1994
First Edition in Swahili: July 1996.

Designed by Richard Polese with Patricia Yohn.
Cover Photograph by Jim Burton Topeka Capital Journal.

International Standard Book number: 0-943734-15-0

Kimechapwa katika Kiswahili na:
Dal-Rich Printers,
St. Jude's Complex[Ground Floor]
P.O. Box 3056,
Tel: 30881, 21334. Fax 21368,
KISII - KENYA. EAST AFRICA.

# Msafiri wa Amani

## KUMTAMBULISHA MSAFIRI WA AMANI

Alionekana anatembea kwa miguu mjini ama barabarani. Ni mwanamke mwenye nywele zenye mng'ao wa weupe wa mvi. Anavaa vazi la bluu. Juu ya vazi hilo ana gwanda kama kisibau lenye mfuko sehemu ya chini utunzao vifaa vyake vya kawaida kwa matumizi yake. Kifuani mwa vazi lake kuna maandishi meupe makubwa ambayo husomeka; "MSAFIRI WA AMANI." Mgongoni mwake kuna maandishi mengine meupe yasomekayo, "MAILI 25,000 KWA MIGUU AKIENEZA AMANI." Huyu mama ametembea kwa miguu maili ishirini na tano elfu (25,000) ambazo ni sawasawa na kilometa arobaini elfu (40,000). Hata hivyo anaendelea kutembea kwa miguu na kauli yake ni; " Nitabakia hujaji mtembeaji mpaka mwanadamu ajifunze njia ya kuishi kwa amani, nitatembea kwa miguu mpaka hapo nitakapopewa hifadhi na pia nitafunga mkanda tumbo langu kwa njaa hadi hapo nitakapopewa chakula." Anatembea bila fedha yoyote mfukoni mwake na hausiani na Jumuiya yoyote ya Ki-taifa au Ki-Mataifa. Anatembea akiwa mwombezi na akiwa chachu ya kuwafanya wengine wasali na kumuomba Mungu awape Amani kote duniani. Anaongèa na yeyote akutanaye naye njiani, mikutanoni, kama vile kwenye mikusanyiko yá makanisa au mikusanyiko ya watu vyuoni na mashuleni.

Anaeneza Amani kwa njia ya magazeti, majalida, redio na televisheni akitoa mijadala mbalimbali jinsi ya kuleta ufanisi wake. Hisia zake zinamtuma kuelewa kwamba jamii inajaribu kuleta Amani duniani kwa njia ya vita. Kwamba, usalama hauwezi kudumu kwa kulindwa na mlundikano wa mabomu ya kivita. Anagusia kwamba hiki ni kipindi cha hatari sana katika historia ya maisha ya mwanadamu hivyo sisi tunaoishi, hatuna budi kuchagua kati ya kuendelea kutegemea vita vya nyuklia ili kuleta Amani ama kuegemea kwenye enzi mpya yenye nuru ya Amani. Ingawaje haonyeshi wazi kutaka kuyaona matokea ya kazi yake, barua nyingi ambazo zimeandikwa na watu mbali mbali zinaonyesha kwamba hakufanya kazi isiyo na mafanikio, kwani jibu kuu la waliokutana nae ni kwamba; "Tangu tulipoongea na wewe, nimeamua kwamba nitafanya kadri niwezavyo kuleta Amani."

(Ujumbe huu ulipigwa chapa kwenye kijalida kifupi ambacho nakala zake, hujaji wa Amani alizoea kutembea nazo ndani ya mifuko ya shati lake kwa kujitambulisha).

# YALIYOMO

Kumtambulisha Msafiri wa Amani ........................................

1. Kukua kwake .......................................................... 1
2. Kukua Kiroho .......................................................... 5
3. Hija .......................................................... 21
4. Yaliyojionyesha kwenye Hija .......................................................... 35
5. Kuishi maisha ya kawaida .......................................................... 43
6. Utatuzi wa maisha .......................................................... 51
7. Kuishi maisha ya Kiroho .......................................................... 65
8. Mawazo ya Kutafakari .......................................................... 77
9. Njia ya Amani .......................................................... 85
10. Uendelezaji wa upatanisho .......................................................... 99
11. Watoto na Njia ya Amani .......................................................... 103
12. Mageuzi ya Jamii yetu .......................................................... 105
13. Njia ya Msafiri .......................................................... 111

## NYONGEZA

(I) Muhtasari wa maisha ya Msafiri wa Amani .......................................................... 119

(II) Chati ya Msafiri wa Amani ionyeshayo kukua kwake kiroho .......................................................... 120

(III) Maswali na Majibu .......................................................... 122

(IV) Tenzi sala na Nyimbo .......................................................... 154

(V) Msafiri wa Amani kwenye vyombo vya habari .......................................................... 162

(VI) Barua kwa Msafiri wa Amani .......................................................... 190

(VII) Barua kuhusiana na Msafiri wa Amani .......................................................... 193

(VIII) Uzoefu kwa Msafiri wa Amani .......................................................... 202

## UTANGULIZI

Msafiri wa Amani alikuwa na mvuto wa pekee kwa watu alipokuwa akitembea kwa furaha kuzunguka nchi. Aliamsha na kuchochea ari za maelfu ya watu katika kipindi chote cha miaka ishirini na nane; alichotembea kwa miguu akieneza Amani. Wale waliguswa na matendo yake wamebakia na kumbukumbu mioyoni mwao kuhusiana na ongea yake, cheka yake, tembea yake, mjumuiko wake pamoja nao; walipokuwa wakisikiliza mazungumzo yake kuhusiana na maneno aliyokuwa akieneza Amani. Mengi waliyapata alipokaa nao kula chakula ama wakati walipokuwa garini wakielekea kwenye maeneo ya mikutano. Wengine hawasahau upungaji wake wa mkono wa buriani alipowaaga akitembea kuelekea kwenye vituo vingine mbele yake.

Tangu mwaka 1953 hadi 1981 huyu mwanamke mwenye nywele nyeupe akiwa na wito uliomjengea uso wenye furaha na adabu alikuwa mtumishi wa Ulimwengu. Mara alipokuwa akiingia katika kila mji; uwe mdogo ama jiji, alibeba na kuonyesha kila aliyekutana naye ujumbe uliosema; "Wengi wetu tutakapokuwa tumepata Amani ndani mwetu; taasisi zetu zitakuwa na Amani na kamwe hakutatokea vita miongoni mwetu."

Baada ya kifo chake mwaka 1981 idadi kubwa ya marafiki zake kutoka sehemu mbalimbali za nchi walikusanyika mjini Santa Fe, New Mexico ikiwa ishara ya kumkumbuka hujaji wa Amani pamoja na kufanya mijadala kuhusiana na matendo yake. Kikundi kidogo cha marafiki zake kiliendelea kukaa mjini hapo ili kuhariri utunzi wa kitabu kihusucho matendo ya kueneza Amani aliyoyafanya mwanamke huyo wakati wa uhai wake. Wazo la kukiandika kitabu lilikuwa vichwani mwa watu kipindi kirefu kabla. Tumejaribu ndani ya kitabu hiki kuwasilisha maisha yenye mvuto usio wa kawaida ya hujaji wa Amani pamoja na mafundisho yenye ukweli yaliyotoka kinywani mwake. Maneno yanayokiunda kitabu hiki yalikusanywa kutoka kwenye kijitabu kidogo kiitwacho; **hatua kuelekea kwenye Amani ya ndani.** Sehemu zingine zilizochangia kuundwa kwa kitabu hiki ni magazeti kumi na tisa yanayoeleza maendeleo ya hujaji wa Amani, majadiliano yake na watu mbali mbali aliokutana nao, makala mbalimbali alizoziandika pamoja na mazungumzo yake, na baadhi ya watu yaliyonakiriwa kwenye kanda kwa kipindi cha miaka mingi. Pia kuna mkusanyiko wa makala maalum zilizotolewa ndani ya magazeti elfu kadhaa kuhusiana na Hujaji wa Amani katika maktaba ya chuo cha Amani cha Swarthmore nchini Marekani.

Ingawa maneno yaliyomo ndani ni yake mwenyewe, hiki kitabu hakukiandika yeye mwenyewe kueleza kuhusu maisha yake. Maneno mengine yalikusanywa na waandishi kwa njia ya kanda zilizonasa sauti yake hapo zamani na hivyo kuonekana kama mtu ajielezaye badala ya mwandishi mwingine. Ni vema kama angeandika kitabu chake mwenyewe. Wakati wa uhai wake; watu walimuomba aandike kitabu kuhusiana na maisha yake ya kueneza Amani, na yeye alikuwa anajibu: "Nimekwishaaandika mengi ambayo yanaweza kutengeneza kitabu ila hayako

katika utaratibu wa kusomekā kama kitabu." Na sasa kuyapanga maandishi yake ili yasomeke kama kitabu limekuwa jukumu letu.

Ingawaje mfumo mzima wa ujumbe wake haujabadilika ila taarifa inavyosomeka kitabuni inapambwa na utaalam wa uandishi wa vitabu. Utaweza kukuta baadhi ya vifungu vifupi vya mafundisho ama misemo vimerudiwa lakini katika wazo jipya.

Ujumbe wa kawaida wa Msafiri wa Amani ambao ndilo chimbuko la kitabu hiki alioutoa katika maisha yake, unao umuhimu mkubwa sana kwa wanadamu katika kuitafuta Amani. Ametuachia tumaini jipya kwa maisha yajayo ya Ulimwengu wetu. Tumaini ambalo wengi laweza kuwapatia amani ndani mwao ili kuujenga uwezekano wa kuwapo kwa Amani ya Ulimwengu.

Ametupatia mfano wa mtu aliyeishi akiwa na amani ndani mwake akawa amejazwa nguvu nyingi zisizo na mpaka zikakuzwa kuliko umri wake.

Katika jarida la Kihindi lijulikanalo kwa jina la Gandhi Marg, Robert Steele aliandika; " Hujaji wa Amani daima huongea kwa madaraka ya ajabu na kwa kujiamini. Anatukumbusha mmoja wa watu wanaoelezwa ndani ya Biblia waliokuwa wasemaji wa Mungu. Hata hivyo matamshi yake hayaonyeshi kuwa ya vichekesho wala ubunifu, badala yake yanasikika kuwa yenye mchomo wa ndani unaotolewa na mtu aliyejazwa na upendo, aliye na busara na maono ya ajabu sana....." .

Akijulikana kwa jina la Msafiri wa Amani kutoka Pwani moja hadi Pwani nyingine ya nchi, alikuwa na tabia ya kuusisitiza ujumbe uliotolewa badala ya kuwa tarishi tu.

Hakuwahi kueleza jambo lolote la maisha yake ambalo halikuwa na umuhimu kwa watu, kama vile kulitaja jina lake la asili, umri wake na eneo alikozaliwa. Kwa vile hiki kitabu kinahusiana na kuhiji kwake akijieleza mwenyewe katika kuineza amani, tumeamua tusitoe maelezo zaidi ya yale aliyojieleza kwenye safari zake alikopita akieneza Amani.

"Sikutaka watu wanikumbuke kwa lingine zaidi ya yale yanayohusiana na Amani." Alizoea kusema. Baadhi yetu tuliomfahamu Hujaji wa Amani vema, na kumuona kwa miaka kadhaa, atabakia kwenye kumbukumbu zetu kama mwanamke mtulivu, mwenye moyo mkunjufu, aliyejawa na upendo, mkweli na mwenye furaha maishani mwake.

Alizaliwa katika shamba dogo mashariki mwa Marekani mnamo kipindi cha mwanzo cha karne hii, na alikulia katika nyumba yenye maisha ya kawaida na kama binadamu wengine alijikuta anahitaji fedha na mahitaji mengine ili aishi. Baadaye aligundua kwambc maisha ya kutegemea malipo tu ya duniani hayakuwa na maana na ulikuwa mzigo mzito kwa mtu yakilinganishwa na maisha yaliyotegemea baraka za Mungu.

Siku moja usiku alitembea kwenye maeneo ya bustani ya miti akitafakari kwa undani jambo hilo, na huko alipata utashi kamili usiorudi nyuma wa kujitolea maisha yake kwa Mungu na kuwa tayari kumtumikia. Na taratibu alianza kukifanya

kile kilichoitwa miaka kumi na mitano ya kujiandaa, pamoja na kwamba hakujua alikuwa anajiandaa kwa jambo gani. Alifanya kazi ya kujitolea kwa ajili ya vikundi

ix vya Amani na pia akafanya shughuli zake kuwasaidia watu wenye matatizo ya mwili, akili na waliochanganyikiwa kimaisha.

Ilikuwa wakati wa kipindi hiki cha maandalizi alipojihoji kiroho akivuka milima na mabonde; ndipo alipopata Amani ya dhati na akawa ameitwa kiroho kumtumikia Bwana.

Matembezi yake ya kwanza yalianza asubuhi ya Januari tarehe Mosi, 1953. Aliahidi kuwa ataendelea kuhangaika hadi hapo mwanadamu atakapojifunza namna ya kuishi kwa amani. Msafiri wa

Amani alitembea bila senti yoyote mfukoni mwake na bila msaada wa mfadhili yeyote wa Kitaifa au Kimataifa. Alitembea akiwa mwombezi na akiwa chachu ya kuwafanya wengine wasali sana wakimuomba Mungu alete amani duniani kote. Alivaa vazi la suruali na shati rangi ya bluu, juu ya shati alivaa gwanda lililokuwa na mifuko sehemu ya chini ambamo aliweka vifaa vya kawaida kwa matumizi yake kama vile chanuo, mswaki, kalamu, nakala za ujumbe wake pamoja na barua kwa watu aliowasiliana nao.

Baada ya kuwa ametembea kwa miguu maili 25,000 (ambazo ni sawa sawa na kilometa 40,000) wakati huo mwaka 1964, aliacha kuhesabu maili (umbali) alizokuwa akitembea; akajihusisha zaidi na mazungumzo kwa wale waliokuwa wakikutana naye, ingawaje aliendelea kutembea kila siku. Ratiba yake ya kutaka kuongea na watu ilipunguza kasi aliyokuwa nayo ya matembezi yake kwa miguu akakubali kutumia usafiri wa haraka kama vile gari na vyombo vingine ili afike mapema kwenye vituo alivyokuwa amepanga.

Msafiri wa Amani aliongea na maelfu ya watu katika kipindi chote cha McCarthy, vita ya Korea, vita ya Vietnam n.k. Alikutana na watu mitaani, barabarani, majumbani mwao, viungani, jangwani, na kwenye vituo vya magari. Alihojiwa na watangazaji kwenye vyombo vya habari Redio na Televisheni.

Waandishi wa habari kote nchini waliziandika habari zake.

Kabla watu hao hawajamfahamu ilimbidi awatafute ili waandike habari zake katika kueneza amani. Aliongea na wanafunzi wa vyuo vikuu nchini, mabaraza ya shule mbali mbali, vilabu vya mijadala ya kisiasa na kwenye mimbari ya baadhi ya makanisa.

Kadri miaka ilivyozidi kusonga mbele ndivyo alivyozidi kujijengea umaarufu na upendo mkubwa kwa watu kutokana na hekima ya hali ya juu aliyoionyesha. Aliwashangaza sana watu na wakajiuliza maswali mengi sana kuhusu hekima ya mama huyu.

Kwenye maeneo ambayo wengi wetu tulishindwa kuyatembelea tukiyaona ni ya hatari kwa maisha yetu hasa nyakati za usiku, Hujaji wa Amani alionekana akitembea mle bila woga wowote na nyakati zingine alilala usingizi kando mwa barabara, ufukoni mwa bahari na kwenye vituo vya basi.Kwa miaka mingi watu wasiomfahamu walionekana marafiki, walimkaribisha awatembelee nyumbani

kwao, walipanga taratibu za kuongea naye wakitoa ahadi za kukutana naye kwa kipindi cha mwaka mzima ama zaidi kabla.

Hujaji wa Amani aliamini kwamba tumeingia katika kipindi cha vita vya nyuklia na udhalimu katika historia ya maisha yetu; " Ni chaguo letu kupita kwenye ukingo wa kuangukia kwenye vita vya nyuklia ambavyo vitatuangamiza kabisa ama tuchague maisha ya nuru yenye amani." Alijihisi kuwa na wito wa kuwatahadharisha watu waondokane na mawazo ya kivita katika ufumbuzi wa matatizo yao na badala yake wafanye kazi ya kudumisha amani. Na mara kwa mara aliwapa watu moyo wa kutafuta chimbuko halisi la amani miongoni mwao na kutumia njia ya amani kujenga uhusiano mwema na wengine.

Katika kipindi cha kufa kwake Msafiri wa Amani alikuwa ametembea kuzunguka nchi ya Marekani mara saba. Alikuwa ametembea kwa miguu katika majimbo hamsini ya nchi ya Marekani, majimbo kumi nchini Kanada na baadhi ya maeneo ya Mexico. Mwaka 1976, Bwana mmoja alimsafirisha kwa ndege hadi nchi za Alaska na Hawaiiambako alikutana na watoto wa Bwana huyo pamoja na kutembea akiongea na watu makanisani na kuongea na vyombo vya habari mwaka 1979 na 1980 alirudi Marekani akiwa na kikundi kidogo cha watu kilichoamua kuandamana naye kila mahali alikokwenda ili kujifunza mwenendo wa maisha yake. Alikuwa na mpango wa kurudi mara kadhaa huko Hawaii na Alaska, mnamo 1984 alikuwa amedhamiria kuwaalika watu wengi zaidi kujiunga na kikundi chake ambacho kingeendelea kuhiji sehemu mbali mbali kikieneza amani.

Alitangaza kile ambacho yeye alipendelea kukiita " Maisha mazuri ya mpito kuelekea kwenye uhuru wa maisha yenye amani mnamo tarehe 7 Julai 1981 huko Knox, Indiana; alikufa ghafla kutokana na majeraha ya kichwa aliyoyapata kwenye ajali ya gari alilokuwa akilitumia kusafiri kwenda mkutanoni. Marafiki zake wengi waliosikia kifo chake walishangaa sana. Hawakutegemea kwamba Msafiri wa Amani angeweza kuuacha ulimwengu huu ghafla hivyo. Rafiki mmoja aliandika; " Ninaamini kwamba kuamua kwake kuanzisha kauli ya maisha mazuri ya mpito haraka iwezekanavyo ilikuwa ishara yake kulionyesha tukio hili."

Katika mahojiano yake ya mwisho na waandishi wa magazeti alisema kuwa yeye yumo kwenye hali njema kiafya. Alikuwa anapanga kutoa taarifa yake kamili kutokana na safari zake za kueneza amani na pia alikuwa na ahadi za kukutana na watu hadi 1984. Ted Hayes wa Redio ya WKVI huko Knox Indiana, kwenye mahojiano yake na Hujaji wa Amani aliyoyanasa kwenye kanda tarehe 6 Julai alitamka; " Unaonekana kuwa mwanamke mwenye furaha kupita kiasi." Na Hujaji wa Amani akamjibu, " Kusema kweli mimi ni mtu mwenye furaha, itakuwaje mtu amfahamu Mungu na asiwe na furaha?"

Salamu za rambirambi kutoka kwa marafiki waliosikia kifo chake ziliendelea kumiminika Mjini Cologne kupitia kwenye posta ya New Jersey ambako barua zake zilikuwa zinatumwa na kupokelewa. Barua hizo zinaleta majonzi mazito kwenye

mioyo ya watu zikisema; " ***Mpendwa Msafiri wa Amani, ndiyo kwanza nimesikia habari za kutatanisha kuwa umetutoka kwenye mwili huu wa udongo. —Kama taarifa hii si ya kweli, tafadhali niandikie mara moja.*** " Barua nyingine ilisema; " ***Ninajua wewe huko uliko uko pamoja na Mungu—ninakuona ukiwa mbinguni.*** "

Mhariri mmoja aliyewahi kumhoji mnamo 1960 na baadaye akawa rafiki yake mkubwa aliandika, " ***—mizunguko ya sala imo moyoni mwangu ikitambulisha kwake sifa nzuri nimpazo kutokana na mafunzo yake ya mvuto wa ajabu alioniachia maishani. Ninamuombea mema kwenye safari yake.*** "

Rafiki yake mmoja wa huko Massachussets aliandika; " **Yalikuwa majonzi na msiba mkubwa, kwa kuwa tumepata hasara isiyomothilika kwenye safari yetu hii ndogo! Kwa muda huu moyo wangu umejaa huzuni, kwani mimi kama ilivyo katika maelfu ya watu humu nchini tulimpenda Msafiri wa Amani kwa kiwango kikubwa mno! Lakini pamoja na hayo nahisi kuwa uwepo wake utaendelea kuwapo kati yetu kwa njia ya mafunzo yake mazuri aliyotupa pamoja na mfano wa maisha aliouonyesha kwetu.** "

Tunaamini kitabu hiki kitakuwa chimbuko muhimu kwa waandishi wa sasa na wajao ili kujenga changamoto na msukumo wa kuleta amani kwa wale ambao hawakuwahi kuwa na bahati ya kukutana na mwanamke huyo.

Mmoja wapo aliyeguswa na roho yake ya upendo aliandika; " **Mbegu za amani zimetawanywa ipasavyo. Ni jukumu la wotewaliOguswa na kazi yake kuanza uvunaji wa matunda yake.** "

Ni tumaini letu kwamba maneno yake na mwenendo wake vitaendelea kuweka changamoto la kujenga amani. Tunaungana na wewe katika mzunguko wa upendo tukiwa pamoja na wale wote wengine waliomfahamu wakawa wameguswa naye—.

Uhuru wa kujitenga na mambo ya dunia hii, ni sawa na kuwa huru kama hewa, sasa waweza kusafiri safiri kila mahali.

Watano kati ya marafiki wengi wa Msafiri wa Amani Santa Fe, New Mexico.

Marekani.

**Machi 31, 1982**

## SURA YA KWANZA

### KUKUA KWAKE

Nilianza na mwanzo mzuri wa kupendelewa ingawaje wengiwenu mtalipinga hilo. Nilizaliwa maskini katika shamba dogo lililokuwa kwenye viunga vya mji mdogo. Ninamshukuru Mungu kwa hilo.

Nilikuwa na furaha sana utotoni mwangu. Nilikuwa na maeneo ya mazuri ya kuchezea michezo mbalimbali kama vile bustanini mwa miti, eneo la kuogelea pamoja na eneo la kuchezea michezo mingine. Laiti kila mtoto angekuwa na eneo la kutosha la kukulia, kwani ninafikiri mtoto ni kama mmea mchanga ukuao. Watoto wakikulia katika mbanano, miili yao huwa miembamba nao huugua mara kwa mara. Hawapati afya nzuri. Tunahitaji maeneo mapana ya kuchezea michezo ili tukue ipasavyo.

Kwa kawaida utotoni mwetu huwa tunajiandaa kufanya kazi fulani uzimani ingawaje kiutamaduni huwezi kujua kazi utakayoifanya hapo baadaye. Kwa hiyo mimi kama mtoto sikujua ni kazi gani nitafanya hapo baadaye. Na bado kwa uhakika nilikuwa katika maarifa. Nilikuwa ninajiandaa kwenda safari ya hija nilipoichagua kanuni ya; " Liwalo la kwanza na ndilo liwe la kwanza na nikaanza kuifanyia kazi maishani mwangu." Hii kanuni iliniongoza katika mpangilio mzuri wa maisha ikawa imenifundisha ile nidhamu yenye nafsi ya kujituma; ilinipatia somo zuri ama vinginevyo nisingeweza kuyafanya matembezi ya hija katika maisha yangu. Kanuni hii niliitumia katika maisha yangu ya utu uzima.

Utotoni mwangu sikupata elimu yoyote ya msingi ihusuyo mambo ya kidini. Mara yangu ya kwanza kuchungulia kanisani ilikuwa wakati nikiwa na umri wa miaka kumi na mbili. Napo nilichungulia kupitia mlangoni mwa Kanisa Katoliki. Nikawaona wahudumu wakisafisha kanisa. Nilipokuwa na umri wa miaka kumi na sita niliingia kanisani kwa mara ya kwanza kuhudhuria ibada ya harusi.

Nilipokuwa katika kumalizia muda wangu wa mwisho wa elimu yangu ya Sekondari, nilianza kumtafuta Mungu. Juhudi yangu yote ya kumpata Mungu iliongozwa pasipo penyewe. Nilizunguka nikitafakari; " **Mungu ni nini?**" " **Mungu ni nini?**" Nilikuwa mchunguzi sana na niliwauliza maswali watu wengi bali sikuambulia jibu lolote la kuniridhisha. Hata hivyo sikuwa wa kukata tamaa. Baada ya kutafakari kwa makini niligundua kwamba Mungu hawezi kupatikana kwa njenje tu. Kwa hiyo nilijaribu mwelekeo mwingine. Nilitembea mwendo wa kasi na mbwa wangu pembeni, nikitafakari kwa undani swali la; wapi nitampata Mungu likiwa limeyateka mawazo yangu yote. Nilipofika nyumbani nilijitupa kitandani kulala. Asubuhi yake nilijikuta ninayo majibu mengi kutoka moyoni mwangu nayo yaliletwa na sauti nyembamba imara ambayo ilikuwa inajibiwa na moyo wangu.

Sasa jibu langu la shuleni lilikuwa rahisi kwa kila mtu nalo ni kwa wanadamu tuache kila kitu ambacho kiko nje ya uwezo wetu kwa uwezo wa mbingu na nchi. Na hivyo vitu vyote kwa pamoja baadhi yetu huvipa jina Mungu.

Vema, na hiyo ilinifanya nitafute zaidi. Jambo la kwanza nililolifanya ni kuuangalia mti na hapo nikasema;" **Yupo mmoja.**" Sisi wanadamu wote,

tungefanya kazi pamoja tusingeuumba mti huo. Kwa hiyo, tuamini kwamba ipo nguvu ya uumbaji ambayo iko juu ya uwezo wetu. Pia niliangalia nyota zivutiazo huko juu angani;nikasema; " **Yupo mwingine.** " Ipo nguvu ya kudumu inayoziweka sayari zote katika mihimili yake.

Niliangalia kwa makini yale mabadiliko yote yanayotokea kwenye mbingu na nchi. Wakati huo walikuwa wanajaribu kuuokoa mnara wa kutolea mwanga (uliokuwa ukitumiwa kuongoza meli, isizame baharini). Hatimaye waliuvuta wakaufikisha ufukoni wakasema wameuokoa. Na yote niliyashuhudia kwa macho yangu na hapo nikasema " **Yupo mwingine.**" Kuna nguvu fulani inayohamasisha mabadiliko fulani ya kudumu kwenye mbingu na nchi.

Nilipofika kwenye uthibitisho wa ndani ya moyo wangu nilielewa bila shaka yoyote kwamba nilikuwa nimeugusa mwanga wangu ulio juu.

Kimaarifa nilimgusa Mungu mara nyingi akiwa kama ukweli na hisia zangu zilimgusa Mungu kama upendo. Nilimgusa Mungu kama wema. Nilimgusa Mungu kama uzuri. Ilinijia akilini kwamba Mungu ni nguvu ya uumbaji ihamasishayo, mwenye uwezo wa juu kimaarifa kuliko viumbe vyote, aishiye daima, ni Roho ya kweli iliyoenea kote ambayo imevifungia vitu vyote kwenye mbingu na nchi na kuvipatia uhai. Yote yanamfanya Mungu awe karibu sana nasi. Nisingekuwa mahali ambapo Mungu hayupo. Wewe umo ndani ya Mungu naye Mungu yumo ndani mwako.

Nilikuwa ninafanya kazi kwenye bohari la shilingi tano na senti kumi.

Wakati huo nilikuwa bado mwanafunzi katika Elimu ya Juu ya Shule ya Sekondari (sawa na kidato cha tano na sita hapa kwetu). Hakika niliipenda kazi yangu. Siku moja sikuwa na hesabu tosha ya fedha za kuwarudishia wateja kwenye rejista yangu ya kwanza, hivyo nilikwenda kwenye rejista ya pili nikasimamisha mauzo kwa muda ili nichukue fedha humo za kuwarudishia wateja kwenye rejista ya kwanza. Kumbe nilifanya dhambi kubwa sana isiyoelezeka. Niliwasikia watu wakinong'onezana kwamba huyo binti amesimamisha mauzo. Mwanamume mmoja aliyekuwa akiwaongoza wateja mle dukani alinijia na kuniita nimfuate. Tulikwenda hadi kwenye kona ya kaunta moja iliyohitaji huduma akaniacha pale. Baadaye aliporudi aliniuliza; " **Kwa nini umefanya hivyo?**"

" Mpaka sasa hivi sijui nilichokifanya." Nilimjibu.

" Nilichukua fedha za kuwarudishia wateja kutoka kwenye rejista , hivyo sikuiba fedha yoyote." Niliendelea kumjibu.

" Ulielekezwa kutosimamisha mauzo kwenye rejista yoyote." Alisema. " Sikuwahi kuelekezwa juu ya jambo hilo." Nilimjibu.

Baadaye alikwenda kumuona mwanamke aliyekuwa akiwaongoza wateja mle dukani. Mwanamke huyo ndiye aliyestahili kunielekeza mimi kwenye mambo yote ya kazi. Baadaye nilirudishwa kwenye kazi yangu. Kutokana na tukio hilo, huyo mwanamke alinichukia sana. Moyoni mwangu nilielewa kwamba ilinibidi nifanye iwezekanavyo kuizuia hiyo chuki. Kipindi fulani nilipita mezani kwake nikakuta

ameweka mapambo ya maua fulani yaliyonyauka. Kesho yake nilimletea mganda wa maua mazuri niliyoyachukua kutoka bustanini mwangu. Nilipoyafikisha kwake nikasema, " Nilikuta maua yaliyonyauka mezani kwako, najua unapenda maua na haya ni baadhi kutoka bustanini kwangu. Hakuyakataa. Kufikia mwishoni mwa juma tuliweza kutembea tukiwa tumeshikana mikono, uhasama ukawaumekwisha.

Nina hakika nilikuwa ninajiandaa kwa safari ya kwenda kuhiji. Niliposoma katika historia kanuni yenye maandishi ya dhahabu isemayo; " Wafanyie wenzako yale ambayo unataka wenzako wakufanyie." Kanuni hii imeelezwa katika fafanuzi tofauti ikithibitishwa kwamba, kila utamaduni unayo kanuni hiyo. Inao uthibitisho kutoka ndani mwangu iliyoyaathiri maisha yangu. Kusema kweli kulikuwa na vichocheo ndani ya kanuni hiyo yenye uzuri wa dhahabu ambavyo viliniongoza kufikia kwenye safari zangu za kuhiji. Nilipokuwa kwenye masomo ya Elimu ya Juu ya Sekondari, nilikuwa na usemi mdogo usemao; ***" Ukitaka kuwa na marafiki ni vema uwe tayari kuwa rafiki wa kila mtu."*** Ukiuchambua usemi huo utaamini kwamba hicho ni kichocheo cha kanuni yenye uzuri wa dhahabu. Hii pia inajitambulisha kwamba watu huitikia jambo kutokana na namna jambo hilo linavyojitokeza kwao. Hiyo imo ndani ya maisha yangu sasa, pamoja na usemi wangu usemao; ***" Ukitaka kuleta amani, huna budi uwe mwenye amani katika mwenendo wa maisha yako."***

Hii kanuni yenye thamani nilianza kuifanyia kazi katika kipindi chote kilichofuatia cha maisha yangu ya uanafunzi. Nilipewa kazi ambayo ilitakiwa na mmojawapo wa rafiki zangu. Nilichaguliwa kufanya kwenye ofisi ya klabu ya jumuiya kama nilivyosema; kazi hii ilitakiwa na rafiki yangu mmoja. Alizungumza maneno mengi yenye ubaya kunihusu mimi. Nilijua kwamba hali haikuwa nzuri. Ilinilazimu niitumie ile kanuni. Nilifikiri sana nikaona ni vema nitumie maneno mazuri ya kumsifia kadri ilivyowezekana. Nilijaribu kumpa upendeleo wa kwanza. Ilinilazimu kufanya hivyo. Kufanya mambo yawe mafupi, siku aliyoolewa mwaka mmoja baadaye nilifanywa msaidizi wake wa heshima kwenye arusi yake. Umeona jinsi ambavyo roho ikiachiwa kufanya kazi iwezavyo kuleta matokeo ya kazi ya muda mrefu? Ninajua kuwa nilikuwa ninajiandaa kwenye safari yangu ya kwenda kuhiji nilipofanya uchaguzi wa mambo kadhaa. Kwa mfano, siku moja nilikuwa katika shule ya lugha wakati mtu mmoja aliponipatia sigara kutoka kwenye paketi ili nivute. Sikuwa mvutaji, ila rafiki zangu walikuwa wavutaji.

Shuleni nilikokuwa, nilizoea kukaribishwa vinywaji kama pombe ambayo sikuwahi kunywa ila rafiki zangu walikunywa. Tena baada ya siku zangu za masomo nilikabiliwa na jaribio kubwa kwa sababu rafiki zangu wote walikuwa wanywaji wa pombe na wavutaji sigara. Nilikuwa na mapambano makali ya kuimarisha moyo wangu nyakati hizo. Nilikuwa na pambano lenye nguvu ya msukumo mkali kushindana na matakwa ya wenzangu ambao daima waliniona siyafanyi yale waliyoyafanya wao. Siku moja tulipokutanika wote kwenye chumba cha mwenzetu mmoja, niliwaambia; " Tazameni, maisha ni msululu wa chaguzi mbali mbali na hakuna mtu awezaye kukuzuia usichague yale uyatakayo. Na mimi ninayo haki ya kuchagua yale niyatakayo. Na nimechagua kuwa huru."

Pia nilifanikiwa kugundua mambo mawili muhimu kadri muda ulivyozidi kusonga mbele. Kwanza niligundua jinsi utafutaji wa fedha ulivyo rahisi. Nilikuwa nimeongozwa kuamini kwamba, fedha na mali nyingine vingenifanya kuishi maisha ya raha na yenye utulivu wa mawazo. Hiyo ndiyo njia niliyoitumia katika nafasi ya pili nikagundua kwamba ukipata fedha ukazitumia ovyo ovyo unakuwa ukifanya kitu ambacho hakina maana kabisa. Nilijua kwamba, hiyosiyo iliyonifanya niwe hapa, lakini wakati huo sikujua kwa uhakika nilikuwa hapo kwa jambo lipi.

Katika uchambuzi wangu niliona baadaye kuwa visingenifanya kuwa na furaha maishani mwangu na hiyo ndiyo iliyoniongoza kuyaanza maandalizi ya safari yangu kwenda kuhiji. Utashangaa jinsi nilivyohusisha fedha na vitu vingine katika nafasi yangu ya kwanza kuhusiana na ulimwengu, lakini unaona; tunafundishwa mambo haya kinyume na ndiyo maana matokeo yake yanachanganya mno. Nilikuwa na bahati kwamba nilichanganywa na mojawapo na vinyume vya seti mbili ziliwafuata walio wengi huchanganywa na zote. Upande mmoja nilifundishwa kuamini kwamba inanilazimu kuwa mwema na mpenda watu na kamwe nisimdhuru mtu, ambayo ni nzuri. Upande mwingine nilifundishwa kuamini kwamba, kama umeamuriwa ni vema kwa heshima kuitikia kujeruhi na ukaua uwapo vitani. Mara nyingine wayatendayo haya hutuzwa medali waikamilishapo kazi! Sasa hiyo haikunichanganya. Sikuamini kama utatokea wakati kwa hali yoyote ambapo itakuwa vema kwangu kumdhuru mtu. Lakini seti nyingine ya vinyume hivyo ilinichanganya kwa muda. Nilifundishwa kuwa mwema na bila ubinafsi na wakati huo huo nilifundishwa kuwa mwema na bila ubinafsi; na wakati huo huo nilifundishwa kuamini kwamba kama ningetaka kuwa na mafanikio ningekwenda mahali ninyakue mali ya dunia iliyo zaidi ya mgao wangu nijilimbikizie. Hizi falsafa zenye uhasama nilizozikusanya tangu kwenye mazingira ya utoto wangu zilinichanganya kwa muda, lakini hatima yake niliachana na hayo mafundisho haramu.

## SURA YA PILI

*KUKUA KIROHO*

HATUA ZANGU KUELEKEA KWENYE AMANI YA ROHONI.

Nilipouangalia ulimwengu niliona sehemu yake kubwa inachakaa. Nilijisikia kuishi bila raha kwani kile nilichokuwa nacho wenzangu walikuwa hawana. Nilikuwa na chakula wakati wenzangu wana njaa. Hatimae ilibidi nitafute njia nyingine ya kufanya. Mabadiliko maishani mwangu yalitokea wakati nikiwa katika hali ya kukata tamaa na mawazo tele kichwani kuhusiana na nini maisha ya kweli nilipoamua kutoka usiku mmoja, nikatembea kuzunguka maeneo ya bustanini na wakati huo mbalamwezi ilikuwa inawaka sana ikanibidi nipige magoti nisali. Nilijisikia utashi kamili bila mafundo yoyote kutoa maisha yangu yote kumtumikia Mungu. "Tafadhali Mungu nitumie." Nilimuomba na Amani ya ajabu nilihisi ikiujaza moyo wangu! Nikawa tofauti kabisa na nilivyokuwa hapo mwanzo.

Ninakueleza kwamba nilikuwa nimefika kwenye ngazi ya kutorudi nyuma. Baada ya tukio hilo kamwe huwezi kurudi nyuma katika maisha ya kuzitegemea nguvu tu za nafsi ya mwili wako.

Sasa nilielekea katika maisha mapya. Nilianza kuishi kwa kutoa na kutumikia kadri uwezo wangu ulivyokuwa badala ya kutafuta na kukusanya kadri uwezo wangu ulivyokuwa. Hapa nilikuwa nimeyaanza maisha mapya ya ajabu kabisa! Maisha yangu yalianza kuwa ya maana. Nilipata baraka za kuishi maisha yenye afya bora. Tangu hapo sikuwa na maumivu yoyote mwilini mwangu, mafua na wala kuwangwa kichwa (magonjwa mengi kama unavyofahamu huambukizwa kwa watu kisaikolojia). Tangu hapo na kuendelea, nimejua kwamba shughuli yote ya maisha yangu itakuwa kwa ajili ya Amani. Na kwamba yatafunika ile picha nzima ya Amani, yaani Amani miongoni mwa mataifa, Amani miongoni mwa vikundi, Amani kati ya mtu na mtu na zaidi ya yote ni kule kuwapo kwa Amani ya ndani mwetu. Hata hivyo; kuna tofauti kubwa kati ya kuwa tayari kuyatoa maisha yako kikamilifu yaani uamuzi wa kutoka ndani mwako na kule kuyatoa maisha yako kwa lengo la kupata kitu fulani maishani. Kwangu mimi, miaka kumi na mitano ya maandalizi ilikuwa ni kuutafuta ule utashi wa ndani ya moyo ili niyatoe maisha yangu.

Nilikuwa sijawa mzoefu kamili wa mambo ya kiroho nilipojikuta ninaguswa na kitu kile wanasaikolojia wanachokiita kuyategemea mawazo ya mtu mwingine kutenda jambo. Kitu ambacho hukiita unafsi wa chini na ule unafsi wa juu, ama tuseme ile asili ya ubinafsi wa mtu na asili ya mtu kuwa na unafsi wa kiroho wenye Mungu ndani mwake. Sasa ni kama vile kusema tumegawanyika katika nafsi za aina mbili ama aina mbili za utashi zinazogongana kimawazo. Unafsi wako wa chini huyaangalia mambo yauhusuyo mwili wako tu, wakati unafsi wako wa juu

hukufanya ufikirie hali yako ya kisaikolojia ama mafanikio yako katika maisha ya kiroho. unafsi wako wachini hukufanya wewe kama kitovu cha mbingu na nchi wakati unafsi wako wa juu hukuona wewe kama chembe ndani ya mwiliwa utu. Unapotawaliwa na unafsi wa chini umekuwa na ubinafsi pamoja na kupenda vitu vya kumiliki. Lakini unapofuata unafsi wako wa juu utaona vitu kwa uhakika na utatafuta upatanisho ndani mwako na watu wengine.

Mwili, mawazo na hisia ni vyombo ambavyo vinaweza kutumiwa na ama asili ya unafsi wa chini ama ile asili ya unafsi wa juu ambao ni wa Mungu. Asili ya unafsi wa juu ambao ni wa Mungu. Asili ya unafsi wa chini hutumia vyombo hivyo na bado haiwezi kuvidhibiti kikamilifu kwa hiyo yapo mapambano kati yao yasiyobadilika. Ni asili ya unafsi wa juu tu iwezayo kuvidhibiti kikamilifu vyombo hivyo.

Wakati unafsi wa juu unapochukua nafasi ndani mwako, tayari umepata Amani ya rohoni. Mpaka hali hiyo iwadie sehemu ya maisha yako huongozwa na nidhamu ya kiroho. Nidhamu hii yaweza kuja hata bila kuyapata mafunzo ya awali ambayo yamekuwa kiasi cha upande wa asili ya ubinafsi. Inaweza kuwa nidhamu inayochukuliwa kwa hiari; yaani nidhamu ya nafsi. Sasa kama unafanya mambo ambayo unaelewa hukustahili kuyafanya, na hakika hutaki kuyafanya, ni wazi kwamba unapungukiwa nidhamu. Ninapendekeza ukuaji wa kiroho na baadaye nidhamu ya nafsi.

Mnamo muda wa kukua kiroho, uhasama wa ndani kati yako na watu taratibu huenda unapungua makali yake. Tabia ya ugomvi na chuki huisha taratibu. Tabia hii kwangu ilikuwa ya wastani. Tabia ya ubinafsi wa tamaa ya mambo ya dunia ni adui ambaye ana ushindani mugumu. Hupambana muda wote ili aendelee kuiteka mioyo ya watu. Tabia hii hujitetea kw. ujanja mkubwa mno ukiichukulia kirahisi katika kushindana nayo. Ni tabia inayoyaelewa mapungufu yako yote uliyonayo na huyatumia kukushambulia unapojaribu kuitafuta ile nafsi ya kiroho yenye Mungu ndani mwake.

Katika kipindi hiki cha mapambano, jiundie hali ya kuheshimiwa na watu na usijihusishe na yeyote bali fanya mawasiliano ya karibu sana na ule unafsi wa juu.

Unafsi wa juu umepewa majina mbali mbali ya ajabu na viongozi wa madhehebu ya kidini. Baadhi huuita Nguvu itawalayo iliyo juu, Mwanga ulio ndani mwetu, ama Kristu aishie ndani mwetu. Wakati Yesu kristo aliposema; "Ufalme wa Mungu umo ndani mwenu." Ni wazi kwamba alikuwa anamaanisha ule unafsi ulio juu. Katika sehemu nyingine, husemwa; Kristo ndani mwako, Tumaini lako la utukufu, Kristo aishie ndani mwako. Yesu aliitwa Kristo kwa sababu maisha yake yalitawaliwa na nguvu hii iliyo juu itawalayo.

Wakati nninapoongelea hatua za ngu kuelekea Amani ya ndani ninaziongea kinadharia, lakini hakuna kitu chochote kiwezacho kuweka kanuni ama utaratibu wa mpangilio wa namba ya hatua hizi. Zinaweza kupanuliwa ama kupanuliwa ama kupunguzwa. Hii ni kwa namna unavyokuwa unaongelea jambo, lakini la muhimu ni kwamba: Hatua za kuelekea kwenye Amani ya ndani hazichukuliwi kimpangilio

wa aina moja tu. Waweza kuanza na hatua yoyote. Hatua ya kwanza kwa leo yaweza kuwa ya mwisho kwa kesho. Hivyo anza na hatua yoyote uionayo ni rahisi kwako. Na mara uchukuapo hatua chache za mwanzo, itakuwa rahisi kwako kuongeza zingine. Kwa hali hii tunaweza kugawana. Hakuna mtu kati yenu angeweza kujisikia anaulinzi wakati atembeapo hija, na siyo kwamba ninakushawishi ufanye hivyo. Lakini katika mazingira ya kutafuta upatanisho katika maisha yetu wenyewe, tunaweza kugawana. Na nina shaka kwamba wakati unisikiapo ninaeleza baadhi ya hatua za kuelekea kwenye Amani ya ndani utatambua kwmaba ni hatua ambazo hata wewe umezipitia.

## MAANDALIZI

Nitapenda kuyataja baadhi ya maandalizi ambayo yalihitajika kwangu niyafanye. Andalizi la kwanza lilikuwa kuchukua mwelekeo wa haki katika maisha. Hii maana yake ni wewe kuepukana na maisha ya kubabaisha yasiyo na mwisho wenye mafanikio. Wapo watu wa aina hii ambao idadi yao ni mamilioni. Na hawajaambua lolote la maana katika maisha yao. Uwe tayari kupambana na maisha yatakiwayo yenye ukweli na haki; na hiyo ndiyo tuifanyayo sasa.

Kuna suala zima la kuwa na muelekeo wenye maana unapokabiliana na matatizo ambayo maisha yanweza kukuletea.

Kama ungeweza kuiona picha nzima, na kuielewa hadithi nzima, ungegundua kwamba, hakuna tatizo liwezalo kukuijia bila kuwa na kusudi maishani mwako. Ambayo hayatachangia katika ukuaji wako wa ndani. Ukipatwa na mambo kama haya utagundua kwamba matatizo ni njia ya kukuelekeza kwenye mkondo wa maisha mema. Mtu hujifunza njia nyoofu kutokana na matatizo. Usingekabiliwa na matatizo ungeishi kwa kuelea elea katika maisha bila kujua uanziapo wala wapi utaishia. Tutayatatua matatizo yetu tuliyo nayo kwa msaada wa mwanga ulio juu kupitia kwenye ukuzi wa kiroho uliomo ndani mwetu. Matatizo mkusanyiko ni lazima yatatuliwe kimkusanyiko, na ni wajibu wa kila mmoja wetu kuuchangia utatuzi wa matatizo yanayojitokeza miongoni mwetu. Matatizo mkusanyiko ni yale yanayoigusa jamii kwa ujumla kama vile upunguzaji wa silaha kali duniani na uenezaji wa Amani kote. Sasa ni wajibu wetu kuyafikiria matatizo haya kwa umoja wetu kuyazungumza kwa umoja wetu.Na kwa umoja huo tuutafute ufumbuzi wake.

Andalizi letu la pili ni kuyasogeza maisha yetu katika upatanishi kutegemeana na sheria zinazotawala mbingu na nchi. Viumbe siyo tu ulimwengu na vile vilivyomo bali na sheria zinazoutawala uwepo wake. Iwe katika hali ya ki-maumbile ama ki-saikolojia, sheria hizo ndizo zinazoutawala mfumo mzima wa maisha ya mwanadamu. Kwa kiwango hicho mara tutakapokuwa tumeelewa na kuyaleta maisha yetu ndani ya upatanisho na sheria hizi, maisha yetu yatakuwa ndani ya upatanisho. Kwa kiwango hicho mara tutakapokuwa tumekwenda kinyume na sheria hizi; tunajiundia matatizo sisi wenyewe kwa kutokuzitii. Sisi ndio maadui wakubwa wa nafsi zetu. Endapo tutajivunjia uhusiano mwema kutokana na ujinga

wetu tutakuwa tunajiumiza wenyewe. Kama tuko nje ya upatanisho kutokana na ujinga wetu wa mambo ya kiroho tutaumia kwa kiasi fulani. Na kama tunajua vya kutosha kuhusu mambo ya kiroho na bado tuko nje ya upatanisho hapo tutaumia kwa kiasi kiasi kikubwa sana. Vema tuelewe kuwa mateso humuongoza mtu kuwa mtiifu wa sheria baadaye.

Niligundua kwamba zipo sheria baadhi zijulikanazo sana nazingine zisizojulikana ambazo ni lazima tukiishi kwa kuzitegemea zaweza kutufikisha kwenye Amani ya ndani mwetu.Zimejumuishwa sheria kwamba uovu waweza kuondolewa na mema; na kwamba ni njia za mema tu ziwezazo kuleta mwisho mwema. Tuongeze ufuataji wa sheria za matendo mema ambayo tunaamini daima huweza kuushinda ubaya. Wale watendao yasiyotakiwa daima hujidhuru kiroho.

Sheria hizi zinakubalika kwa wanadamu wote na lazima zitiiwe kabla upatanisho haujadumu.

Hivyo nilijizamisha sana katika kuushughulikia mradi wa kupendeza. Na hii ilikuwa niweze kuishi katika kuyafuata mambo mema yatakiwayo. Sikutaka nijichanganye kwa kuyachukua yote mara moja. kama ingetokea nikawa ninafanya jambo na baadae nikagundua jambo hili nililolifanya ni kosa, ilinilazimu kuacha mara moja. Na hii ni njia rahisi. Mafanikio ya uamuzi huu yanachukua muda mrefu na ni magumu.Na kama ningekuwa sifanyi jambo ambalo nilijua ningelikuwa ninalifanya, mara moja nilianza kulishughulikia. Ilinichukua muda fulani katika kuishi ili niliamini jambo. Na nikiisha kuliamini jambo siliachi. Vinginevyo hautakuwepo umaana wowote. Nilivyoishi katika kuutegemea mwanga ulio juu niligundua kwamba Mwanga mwingine ulitolewa kwangu na hivyo niliuweka moyo wangu wazi zaidi kuzidi kuupokea mwanga zaidi.

Kuna andalizi la tatu ambalo linahusiana na jambo ambalo ni la pekee kwa kila maisha ya wanadamu, kwa sababu kila mmoja wetu ana nafasi yake katika mzunguko wa maisha. Hakuna watu wawili walio na nafasi moja katika mpango wa Mungu. Kuna mwongozo kwa wale wasikiao lile lisemwalo. Kupitia kwenye mwongozo huu kila mmoja atajikuta amefikishwa kwenye sehemu yenye mpangilio wa maisha yatakiwayo.

Sheria za Mungu zaweza kujulikana kutoka ndani mwetu. Lakini pia watu wanaweza kujifunza sheria hizi nje, kama ambavyo imekuwa ikinenwa na walimu wa madhehebu ya dini. Lazima tujiweke wazi kwa uongozi wa Mungu. Mungu hatuongozi kuivunja sheria yake. Kwa hiyo kadri tuishivyo katika hali ya ushirikiano na mapatano mema ndani ya sheria ya Mungu ndivyo tuyapatavyo yaliyo mema. Ni lazima tujiweke wazi kuupata mwongozo wa Mungu. Kamwe Mungu hatuongozi kuzivunja sheria takatifu. Na kama mwongozo ulio batili unatujia; lazima tuwe na uhakika kwamba hatutoki kwa Mungu. Ni juu yetu kuweka maisha yetu ndani ya upatanisho mtimilifu na sheria takatifu, ambayo ni

sawa kwa sisi wote. Ni kutokana na hayo tu mara tubakiapo ndani ya upatanisho na sheria takatifu mambo mema hutujia.

Ukishaingia ndani ya ulimwengu huu, shughuli zako huwa tayari zimewekwa katika mpangilio mzima wa kuongozwa na nguvu za Mungu. Ambalo huwa limebakia ni wewe kuudumisha utaratibu wa kuwasiliana na Mungu ili zibarikiwe zizae matunda. Kama wewe hujui Mungu kakupangia shughuli gani katika maisha yako ni vema umtafute katika maombi na utaonyeshwa. Nilizoea kutembea kwenye maeneo yenye maumbile mazuri ya asili nikiwa nawasiliana na Mungu kimya kimya na moyo wangu ukawa unaonyeshwa maono ya ajabu!

Unaanza kufanya yale yaliyo katika mzunguko wa maisha kwa kufanya vitu vyote vizuri ambavyo unahisi umehamasishwa kwavyo, ingawa mwanzoni vinaonekana kama vitu vizuri na vichache. Unavipakipaumbele katika maisha yako vitu vyote vilivyo juu ya uwezo wetu ambavyo kwa desturi huyachafua maisha ya mwanadamu.

Kila siku asubuhi nilimfikiria Mungu nikafikiri mambo ambayo ningeyafanya siku hiyo kuwatumikia wanae. Niliangalia kila hali niliyokutana nayo kuona kama kungekuwapo uwezekano wa mimi angalau kutoa huduma. Nilifanya mambo mengi kadri ilivyowezekana kwa kila siku bila kusahau matumizi ya kauli ipendezayo pamoja na tabasamu usoni mwangu. Nilimwomba Mungu anijalie uwezo wa kuyafanya mambo ambayo kwangu yalionekana kuwa makubwa na mazito kuyabeba. Sala sahihi huhamasisha matendo mema.

Nilijazwa na hisia yenye nguvu kutaka kuwasaidia wenzangu, na mmoja angeweza kusema kwamba ukijitoa kuwasaidia watu kwa kila kitu, utakuwa umewanyima uwezo wao wa kiroho katika kuutumia kuyatatua matatizo yanayowakabili. Baadae niling'amua kwamba inanibidi kuacha kazi zingine nzuri kwa wengine kuzifanya, ili nao wabarikiwe.

Mwanzoni niliwasaidia watu katika kuzifanya shughuli zao ndogo ndogo, miradi ya bustanini pamoja na usomaji wa vitabu. Nilitumia muda wangu katika nyumba za wazee mbali mbali, niliwatembelea wagonjwa nikiwasaidia katika shughuli zao za tiba. Nilifanya shughuli ya kuwasaidia vijana waliochanganyikiwa kimaisha na waliosumbuliwa kisaikolojia na waliokuwa taahira kimaumbile na kiakili. Dhamira yangu haikuwa na mawaa na nyingi za kazi zangu zilileta matunda mazuri. Nilitumia kile ninachokiita tiba ya kiroho. Nilipata mambo mazuri ambayo pia yaliwapendeza wale nilowasaidia. Ilinibidi nionyeshe mapenzi makubwa sana kwa wale nilokutana nao. Upendo ukiyajaza maisha yako unakuondolea mipaka kwa yale uyafanyayo, dawa ambayo dunia hii inayougua inaitaka ni; upendo miongoni mwa watu wake. Kutokuwa kwangu na mipaka katika huduma kulikuwa zaidi kuliko malipo yake kutokana na mapenzi makubwa niliyoyasambaza kwa wengine. Wakati mapenzi yanapojaza maisha yako mipaka yako yote ya maisha hutoweka. Dawa ambayo ulimwengu huu unaougua unaihitaji ni upendo.

Pia nilifanya kazi za kujitolea kwenye kamati ya huduma ya Marafiki wa Kimarekani, jumuiya ya Amani na Uhuru wa wanawake wa kimataifa na Jumuiya ya usuluhishi kwa kipindi kisichopungua miaka kumi.

Nilishughulika na taasisi hizi kwa muda wa zaidi ya miaka kumi.

**Kuna watu waelewao mambo haya lakini hawataki kuyafanya. Hii inahuzunisha. Katika umri huu wa kuthamini vitu badala ya utu, walio wengi hushindwa kupima mafanikio kwa kuvitumia vigezo visivyo sahihi. Wengine tunayapima kwa kuuangalia wingi wa fedha ama vitu. Lakini furaha na Amani ya ndani haviko katika muelekeo huo. Kama unaelewa lakini hufanyi wewe ni mtu asiyekuwa na furaha kabisa.**

Lipo andalizi la nne, hili linahusiana na kuishi maisha rahisi. Hii inakuwezesha uishi maisha ya kuridhika ndani mwako na nje na iweze kukujengea mapatano kati yako na wale unaoishi nao. Hii kwangu ilinirahisishia maisha. Mara baada ya kuyaelekeza maisha yangu katika utumishi, nilijihisi kwamba nisingeendelea kupokea zaidi ya kile ninachokihitaji wakati wenzangu wenginehapa duniani wanachopungufu kuliko mahitaji yao. Hii iliyafanya maisha yangu kuwa na kipimo cha mahitaji. Mwanzoni, nilifikiri kwamba ingeniwia vigumu kuishi. Kwamba ingenipa mzigo kwenye shughuli zangu. Kumbe mawazo hayo kwangu hayakuwa sahihi. Badala ya ugumu wa maisha nilijikuta ninaishi maisha yenye furaha na Amani. Kuvitunza vitu ambavyo si muhimu kwako ni kujiletea mizigo isiyo na umuhimu wowote maishani.

Katika kipindi hicho niliweza kuwa na matumizi ya dola kumi za Kimarekani (ambazo ni sawa na shilingi elfu tano za Tanzania) kwa juma. Hivyo niliweza kuyagawa matumizi yangu katika sehemu kuu mbili: **Dola sita na nusu nilizitumia kwa chakula na tatu na nusu zingine kwa malazi.**

Sasa sina maana kwamba mahitaji yote yanalingana pote. Mahitaji yanatofautiana- Mahitaji yako yanaweza kuwa makubwa kuliko yangu. Mathalani, kama unayo familia utahitaji matunzo ya familia yako. Nikisemacho ni kwamba uepuke ulimbikizaji wa ziada ilimbikizwayo kwa ajili ya mahitaji ya mwili. kitu ambacho baadae chaweza kuwa mzigo kwako. kama unayo ziada hiyo ni vema uiangalie sana.

Upo uhuru mkubwa sana kama maisha unayoishi ni rahisi. Tangu nilipogundua hilo yapo mapatano makubwa sana kati ya imani ya ndani mwangu na matendo yangu ya nje. Hii inaujenga upatanisho mkubwa, si kwa mtu pekee na matendo yake bali hata kwenye jamii nzima. Hii inashindikana kwa sababu dunia hii wamekifuta kitu mapatano. Tunajali zaidi vitu kiasi kwamba tunapozivumbua nguvu fulani za kinyuklia mawazo yetu yanatuelekeza kuzitumia katika kuunda mabomu ili tuuane. Yote haya yanatokea kwa vile imani ya ndani mwetu haina upatanisho na matendo yetu ya nje. Uchunguzi wa wazi kuhusiana na maisha yetu ya baadaye unalenga katika udumishaji wa imani ya ndani mwetu pamoja na nguvu za kiroho. Vitu hivyo vikiunganishwa vitatoa msukumo wa matendo yetu ya nje yaonekane mema.

UTAKASO

Baadaye niligundua kwamba nilihitaji utakaso. La kwanza ni jambo rahisi; nalo ni utakaso wa mwili. Huu ulihusiana na tabia na mwenendo wa mwili wangu katika maisha. Nilizoea kula aina zote za vyakula. Nikikumbuka ninaogopa jinsi hili hekalu la roho yangu; nilivyokuwa nimezoea kulitupia vyakula hivi aina zote. Sikujali kuliangalia hili hekalu langu la mwili nilipokuwa bado mdogo. Hii pekee ilitokea baadaye katika maisha ya utakaso. Ilipita miaka mitano baada ya kuwa nimetoa mwili wangu kwa utumishi wa Bwana nilipoanza kujali ni kitu gani nikiingizacho kwenye hekalu la roho yangu. Miaka mitano, sasa hivi mimi hula matunda, mboga, nafaka za aina zote na labda maziwa kiasi na siagi.Hivi ndivyo vinipavyo nguvu ya kuishi na kutembea.

Kuna kipindi nilichopenda sana unywaji wa kahawa. Nilipenda nipate kikombe cha kahawa mara tu baada ya kuamka asubuhi. Siku moja asubuhi nilipokuwa nimemaliza kunywa kikombe changu cha kahawa; kama ilivyokuwa kawaida yangu, nilikaa chini nikakiangalia hicho kikombe cha kahawa na hatimae nikajisemea; " Unategemea kinywaji hiki ili uendelee kuwa unahangaika kukitafuta kila asubuhi! **Sitakuwa mtumwa wa kahawa.**" Tangu leo tabia hii ikome." Na ilikoma!

Sikugusa tena kahawa maishani.

Niliikosa kahawa kwa siku chache na nikawa ninaifikiria lakini

tangu niliposahau, kwa sasa nina nguvu kuliko zile nilizokuwa nazo wakati nilipokuwa ninakipata kikombe cha kahawa.

Nilianza kutanabahi kwamba nilikuwa ninavunja sheria yangu ya maisha inayosema; sitamuomba mtu yeyote kunifanyia mambo ambayo sikubali kuyafanya mwenyewe. Sasa hivi siwezi kuua kiumbe chochote kiishicho. Nisingeweza kuua kuku wala samaki; hivyo niliacha mara moja kula nyama. Sijala nyama ya kiumbe chochote kwa miaka mingi, iwe nyama ya kawaida, samaki ama ndege. Nilijifunza tangu hapo kwamba inadhuru afya zetu. Na kwa wakati huo niliongeza upendo wangu si kwa binadamu wenzangu tu; bali hata kwa viumbe wengine pia. Hivyo niliacha kuwadhuru na nikaacha kuwala.

Sikujua wakati huo kwamba ulaji wa nyama ni mbaya kiroho. Nilichojua ni kwamba; nisingeendelea kuutafuta kwa sababu ulipingana na taratibu za maisha yangu. Baadae nilielezwa na daktari mmoja kwamba ulapo nyama mwili wako hubakiwa na viini fulani vyenye sumu ya nyama hiyo. Hiyo nayo ingenilazimisha kwa vyovyote vile kuishi nikila mboga. Ninaamini kwamba kutegemea kinga kwani mwili wangu ni hekalu la roho yangu.

Tena nilijifunza kutokana na kitabu cha Profesa mmoja kilichohusiana na mambo ya chakula anaposema kwamba ardhi hutumia muda mrefu kukuza viumbe wake tunaowala kuliko mboga na nafaka tupandazo kwa chakula. Tangu hapo ninahitaji idadi kubwa ya watoto wa Mungu kupata chakula na hiyo ndiyo inayonifanya niwe mla mboga.

Ugumu ni kwamba hatujajifunza kuacha tabia ya kuuana. Hili ndilo somo letu -" **tusiuane.**" Tujifunze somo la kugawana kile tukipatacho pamoja na somo la kutouana. Somo la kutoua viumbe viishivyo litakuwa dogo sana huko mbeleni ingawa baadhi yetu tunaojua sana, tunahitaji maisha ya kuutegemea mwanga ulio juu.

• •

Nilipofahamu kuwa unga mweupe na sukari nyeupe ni vyakula vibaya kwa afya zetu, niliacha mara moja kuvitumia. Na nilipofahamu kuwa vyakula vingi vitengenezwavyo viwandani vina hali mbaya ambayo nyakati zingine huidhuru miili yetu niliacha mara moja kuvitumia. Hata maji ya mabomba yanayo madawa ambayo yanaweza kutuletea madhara. Ninapendekeza tutumie maji ya kuchujwa ama yale ya chupa.

Ninayajua mengi kuhusiana na chakula kinachoweza kuuimarisha mwili wangu, na afya yangu ni njema kabisa. Ninakifurahia chakula nilacho lakini ninakula ili niishi. Siishi ili nile kama wengine wafanyavyo. Ninajua ni wakati gani nile na wakati gani nisile. Mimi siyo mtumwa wa chakula.

Watu wengine wanaweza kuhisi njaa baada ya kuwa wamekula vyakula vingi visivyofaa. Kwa hakika waweza kuugua magonjwa yasababishwayo na ukosefu wa chakula ingawaje wanakula vyakula vingi visivyofaa. Unaweza kuanza kula chakula kifaacho kwa afya, utakapokula kile kilichopo kula taratibu na ukitafune chakula chako vema kama nifanyavyo. Kione chakula ni jambo lisiloyatawala maisha yako, bali ukione ni hitaji tu la kulinda maisha ili uweze kufanya mambo ya maana yaliyo mbele yako.

Katika tabia zangu za kula na kulala usingizi ninayo mahusiano ya karibu na asili ambayo inawezekana kwangu. Kila siku lazima nihakikishe kuwa, ninaipata hewa safi na nuru ya jua pamoja na kuhusiana na mambo mengine ya asili kadri iwezekanavyo.Kupumzika na mazoezi ya viungo ni vitu muhimu kiafya. Mimi si mmojawao wa wale wasiolala usingizi, inapowezekana mimi huenda kitandani wakati wa machweo ya jua na nikalala usingizi kwa muda wa saa nane. Nyakati zingine huwa ninayafanya mazoezi kwa kutembea na kuitupa tupa mikono yangu huku na huko.

Ungefikiri utakaso wa mwili ungekuwa wa kwanza kwa shughuli zote za mwanadamu. Lakini kutokana na uzoefu wangu wa matendo nimegundua kwamba ni jambo linalofanywa la mwisho.

Hii ni kwa sababu utakaso wa mwili hauendani na tabia zetu mbovu tunazo ziendekeza.

Kuna andalizi la pili: Utakaso wa mawazo kama ungetanabahi ni vipi mawazo yako yalivyo na nguvu, usingekuwa na fikra ambazo ni kinyume. Mawazo mazuri yaweza kukuongoza kwenye njia nyoofu lakini yakiwa na ubaya ndani mwake yaweza kuuguza hata mwili wako. Mimi huwa sili vyakula visivyotakiwa na wala mawazo yangu hayako juu yake. Ngoja nikwambie; mawazo mabaya yaweza kukuharibu kabisa hata kuliko chakula kibaya. Mawazo mabaya ni kitu cha kukwepa.

Ebu nikueleze hadithi ya Bwana mmoja aliyeathiriwa na mawazo kinyume. Bwana huyo alikuwa na miaka sitini na mitano wakati nilipomfahamu kwa mara ya kwanza. Alikuwa anaonyesha dalili wazi mawazoni mwake akidai kuugua ugonjwa wa mwili usiopona. Nilipoongea naye niligundua kwamba aliishi maisha yenye uchungu mwingi sana. Hata hivyo sikuweza kujihusisha naye sana kwa sababu ni

bwana aliyeweza kuishi vizuri na mke wake, watoto wake pamoja na watu wote kwenye mazingira yake. Lakini uchungu wake ulikuwa pale pale. Niligundua kwamba alikuwa anapambana na uchungu wa chuki dhidi ya marehemu baba yake aliyechukua uamuzi wa kumpeleka shule mdogo wake akamuacha yeye. Ni mtu aliyekuwa na akili ya kutosha kuweza kusoma lakini alikwamishwa na umaskini wa baba yake kukosa fedha za kumlipia karo shuleni. Baba yake wakati huo alikuwa na familia na watoto wengine wakiwamo dada zake. Baadaye baba yao alipoupata uwezo kifedha aliendelea kumhudumia mdogo wa bwana huyo kielimu. Wakati huo Bwana huyo asingeweza kurudi shuleni kwa kuwa umri wake ulikuwa mkubwa. Baadae alipogundua kwamba baba yao alikuwa amefanya alichoweza katika kuwapatia elimu watoto wake aliyaondoa mara moja mawazo mabaya dhidi ya baba yake. kwa hiyo ugonjwa wake wa mawazo mabaya uliokuwa unamuuguza taratibu ulianza kupona na baadaye ukaisha kabisa. Hali yake ikarudi kuwa nzuri.

Kama umejenga mawazo mabaya ya chuki dhidi ya mtu fulani ni bora uyaondoe mara moja. Mawazo hayo hayamdhuru mtu yeyote ila wewe tu. Hiyo ya kufanya yaliyo mema na kuzungumza yaliyo mema haitoshi. Ni vema pia kufikiri mambo mema ili maisha yako yawe kwenye upatanisho.

Katika kipindi changu cha maandalizi, sikuweza kutambua nilivyokuwa, nilikuwa ninajifunza. Nilikuwa nikiwasamehe wenzangu. Hiyo haikuwa tatizo, lakini mimi sikuweza kuisamehe nafsi yangu. kama nilifanya jambo ambalo halikuwa jemanilijisemea, " Ni bora uelewe vema." Na siku moja nilipokuwa mbele ya kioo cha kujitazamia nikichana nywele, nilijitazama nikasema; " huna ulifanyalo! kwa nini unafikiri unajua sana unapomsamehe mwingine kwa kutokujua. Wewe si bora kuliko wao."

Lazima ujifunze kujisamehe kama unavyowasamehe wenzako. Chukua hatua zaidi pamoja na nguvu nyingi ulizotumia kujisahihisha katika kujiweka kwenye hali ifaayo. hiyo ilisaidia kunifikisha mahali. **Kwa sababu yupo mtu mmoja tu uwezaye kumbadilisha naye ni wewe mwenyewe tu!**

Ukishajibadilisha wewe mwenyewe itakuwa rahisi kuwabadilisha na wengine.

Ilinichukua muda mrefu wa maisha yangu kuamini, na hatimaye nilifanikiwa. Na nilipofanikiwa, maendeleo yalianza ambayo hayakuisha. Na nilivyoishi ndani ya maisha yaliyo juu niliyokuwa nayo, juu, juu zaidi mwanga mwema uliniangazia.

Utakaso wa tatu ni utakaso wa tamaa. Ni vitu vipi uvitamanivyo? Unatamani vitu kama raha, nguo, vyombo vya nyumbani na mapambo yake ama gari la kutembelea? Kwa vile upo hapa kujiweka katika muafaka na sheria zinazotawala tabia za mtu na ukiwa na sehemu ya taratibu za vitu, tamaa yako inapaswa iwekwe katika muelekeo huu. Ni muhimu sana tamaa yako kumkabidhi Mungu ili yale yote uyafanyayo yaendane na utashi wa Mungu. Unaweza kuja kwenye hatua ya tamaa

**ya upande mmoja ili uweze kuelewa na kushughulikia sehemu yako katika mpangilio wa maisha. Ukifikiria juu ya jambo hili ni kitu gani muhimu unachokitamani?**

Upo utakaso mmoja zaidi nao ni utakaso wa msukumo (motive). Ni nini msukumo wako kwa jambo lolote ulitendalo? Kama ni msukumo wa uchoyo au ubinafsi pengine nafsi ya kujitukuza; ningesema usifanye vitu hivyo. Usifanye jambo lolote kwa kutegemeana na msukumo wa aina hiyo. Lakini si rahisi kwa sababu tunategemeana kufanya mambo kwa misukumo mchanganyiko. Sijawahi kuona mtu yeyote ambaye amefanya jambo kwa msukumo mbovu tu wa aina moja. Inawezekana akawapo, lakini sijakutana naye. Nimekutana na watu ambao hufanya shughuli zao kwa misukumo mchanganyiko. Misukumo iliyo mizuri na mibaya yote imechanganyikana. Mathalani, nilikutana na bwana mmoja kwenye ulimwengu wa biashara akanikubalia kwamba misukumo aliyo nayo katika shughuli zake haikuwa ya kupendeza na bado alikuwa amechanganya misukumo mingine mizuri ambayo ni kama kutafuta apate ahudumie familia yake, afanye mema kwenyejamii yake. Hiyo ni misukumo mchanganyiko.

Ninaongea na vikundi vya watu wanaojifunza mambo ya kiroho. Na wakati mwingine watu hawa wanashangaa kwa nini hawapati yale wayatakayo maishani mwao. Msukumo wao ni kupata Amani ya ndani mwao wenyewe. Na huu ni msukumo wa kibinafsi. Msukumo wa aina hii haukupatii mafanikio. Msukumo wenye kukuletea mafanikio ni ule unaosukuma moyo wako kutoa kwa ajili ya wengine. Msukumo wa kutumikia. Kutoa na wala siyo kupata. Msukumo wako waweza kuwamzuri kama kazi yako italeta matunda mazuri. Siri ya maisha ni kuhudumia.

Nilimfahamu Bwana mmoja aliyekuwa fundi sanifu wa majengo. Kwa kweli ilikuwa ni kazi yake ya ujuzi, lakini alikuwa akiifanya kwa msukumo mbaya. Msukumo wake ulikuwa ni kujipatia fedha nyingi ambazo zingemletea madhara. Alifanya kazi ambayo ilimpatia maradhi na ilikuwa pindi baada ya muda huo wakati nilipokutana naye; nilimueleza kufanya jambo dogo la kuhudumia. Nilimzungumzia furaha aipatayo mtu katika kuhudumia na nilijua kwamba baada ya yeye kuwa amezizoea shughuli hizo, kamwe asingerudia hali yake ya kutaka kujinufaiisha nafsi yake tu. Tuliendelea kuwasiliana naye kwa barua baada ya hapo. Miaka kadhaa baadaye nilishindwa kumtambua wakati nilipomtembelea. Hakika alikuwa amebadilika. Lakini alikuwa anaendelea na kazi yake ya usanifu wa majengo. Wakati huo alikuwa anachora ramani ya ujenzi fulani ambao alinieleza. " Unaona," alisema, " Ninasanifu hivi ili ramani hii iingizwe katika makisio yao na baadaye nitaiweka kwenye ardhi yao ili ionekane ya kupendeza." Sasa msukumo wake ulikuwa ni wa kuwahudumia watu ambao alikuwa akiwachorea ramani za ujenzi. Alikuwa mwenye furaha na aliyeonekana kubadilika. Mke wake aliniambia kwamba

shughuli yake ilikuwa imepanuka kwa sababu watu wengi walikuwa wakimjia na wengine kutoka mbali wakimtaka awasanifie majengo yao.

Nimekutana na watu wachache ambao walizibadili kazi zao ili kubadilisha maisha. Lakini nimekutana na watu wengi sana mabao iliwabidi waibadili misukumo yao kuwa ya kuhudumia ili wayabadili maisha yao.

## KUJIONDOA

Sehemu ya mwisho inahusiana na kujiondoa.

Mara moja utakapokuwa umejiondoa kwenye sehemu ya kwanza utakuwa umepata amani ya ndani kwa sababu huko ni kujiondoa kwenye utashi wa ubinafsi. Unaweza kujiondoa taratibu katika kufanya yaliyo mabaya ambayo yanakupa msukumo. Nakushauri uyaache taratibu kwa kubadilisha yanayotokeza mabaya kwa mazuri kiasi kwamba utashtukia matendo mema ya kiroho yanatawala maisha yako kama unasukumwa kusema ama kutenda lililo jema. Tumia ile nguvu ya kujiondoa katika msukumo wa kutenda mabaya utaona majibu yake.

Kujiondoa kwa pili ni kule kujiondoa katika hali ya kujisikia umetengwa. Tunaanza kujisikia tumetengwa na kuhukumu kila jambo linalohusiana nasi kana kwamba sisi ndio kitovu cha mbingu na nchi na vyote vilivyomo. Hata baada ya kufahamu zaidi kutokana na utaalamu tulio nao, bado tunakuwa na uamuzi wa vitu kwa njia hii. Kusema kweli sisi ni chembe chembe kwenye mwili wa utu. Sisi hatutengani na wanadamu wenzetu. Yote haya yanajenga ujumla wetu. Nikutokana na mtu kuwa na Baraka za yule aliye juu ndipo awezapo kujua ni nini maana ya mtu kumpenda mwenzake kama yeye ajipendavyo. Kutokana na maoni yatokayo juu inakuja njia ya kweli ya kufanyia kazi na hii ni kwa mema yote. Kadri unavyofanya katika hali yakujipendelea unamaanisha'kuwa wewe ni chembe moja ndani ya mwili ifanyayo kazi kinyume na zingine. Na hapo tayari uko mbali na upatanisho. Lakini mara tu unapoanza kufanya mazuri kwa ajili ya ujumla, utajikuta mwenyewe uko kwenye upatanisho nawenzako wote. Unaona, ni njia rahisi iwezayo kukupatia upatanisho na maisha.

Kuna kujiondoa kwa tatu, na huku ni kujiondoa kwa uambatanisho wa aina zote. Hakuna mtu aliye huru ambaye bado anajiambatanisha na vitu vya kumiliki, maeneo ama watu. Vitu ulivyo navyo uviweke mahali patakiwapo uvitumie kama inavyotakiwa na kamwe visikutawale vikakusahaulisha utu wako. Kama unaona havipo kwa ajili ya kukusaidia ondokana navyo uwape wale wanaohitaji kuvitumia. Chochote ambacho unacho na hukitumii ukiondoe uwape wanaohitaji. Katika kipindi hiki cha umilikaji wa vitu kwenye mazingira yetu, wengi wetu tumetawaliwa na vitu tulivyo navyo. Hivyo hatuko huru.

Nilijifikiria mwenyewe kuwekwa huru mapema sana kabla ya kuuanza mtindo huu. Kwanza nilijitawala mwenyewe kwa kujiondoa kwenye tabia mbaya, na nikaendelea kujiweka huru dhidi ya mapambano ya aina yoyote pamoja na mawazo potofu. Pia nimejiondoa katika umilikaji wa vitu ambavyo havina umuhimu kwangu. Nikijihisi naona huu ndio uhuru wa kweli.

Kuna aina nyingine ya umilikaji vitu. Mtu huwa hamiliki mtu hata kama upo uhusiano wa aina gani kati yao. Hakuna mume amilikaye mke wala mke kumiliki mume. Hakuna wazazi wamilikao watoto wao. Tunapofikiri kuhusu mtu kumiliki mwingine ina maana upo utaratibu wa kumiliki maisha ya mtu. Ndani mwake tokeo ni kutokuwepo na kitu upatanisho kati yao. Na mara tunapogundua kwamba hatuna uwezo wa kumiliki mtu ni wazi kwamba kila mtu anaweza kuishi kwa kuongozwa na hamasa za yule aliye juu. Tuachapo kutawala maisha ya wenzetu na hapo tunagundua kwamba tutaweza kuishi katika upatanisho mwema pamoja nao. Chochote utakachopambanisha kukiteka angalia kisikuteke wewe. Na kama unatamani uhuru ni lazima utoe uhuru na kwa wenzako.

Mahusiano yaliyoanzishwa kwenye maisha ya watu Duniani si muhimu katika kipindi chetu chote cha maisha. Migawanyiko huweza kushindwa na uwepo wa upendo miongoni mwetu. Upendo huo ndio uongezao nguvu za maendeleo ya kiroho.

Ni lazima tukubali na kusifia na tufurahie maeneo tunayoyatembelea, tukakaa na tukaondoka bila mapambano yoyote pindi tuhitajikapo mahali pengine.Katika maendeleo yetu ya kiroho mara kwa mara tunahitajika kukaza roho zetu ili kujiondoa kwenye uambatanaji navitu vya kumiliki na kupendana na wenzetu wote bila kufungamana nao kwa kila kitu.

Sasa ya mwisho ni kujiondoa katika hisia potofu. Nataka kutaja moja wapo ya hisia potofu ambayo watu wazuri sana huwakumba, nayo ni wasiwasi. Wasiwasi si jambo ambalo lingeweza kukusukuma kufanya kila kitu kiwezekanacho kwenye mazingira.. Wasiwasi ni jambo litupalo mawazo ambayo yako nje ya uwezo wetu. Ushauri wa mwisho niutoao kuhusiana na hisia potofu za watu, ulionisaidia mimi wakati fulani na umewasaidia wengine, ni kwamba hakuna lolote lijalo kutoka nje, hakuna yeyote awezaye kunidhuru kisaikolojia. Nilitambua kwamba naweza kudhurika kisaikolojia kwamatendo yangu mabaya ambayo ninao uwezo wa kujizuia hasa ukizingatia hali ya sasa ya Dunia na jukumu lililoko mbele yangu. Nilipata uhuru usiomithilika baada ya kutambua yote haya. Kwa hiyo niliacha kuumiza nafsi yangu. Mtu yeyote aweza kunitendea tendo baya na bado nikaendelea kumsikitikia na kumhurumia. Sisumbui nafsi yangu kwa kuhisi uchungu moyoni wala kukasirika kwa lolote baya nitendewalo. Unao uwezo tosha wa kudhibiti hisia za kisaikolojia ziwezazo kuleta mateso mwilini mwako.

Hizi ndizo hatua kuelekea Amani ya ndani ambazo nilitaka kuchangia na wewe. Hakuna lililo geni hapa. Huu ndio ukweli wa kiulimwengu. Mambo haya niliyaongelea kila siku kutokana na mazoea niliyokuwa nimekwisha yaona. Sheria zinazotawala mbingu na nchi huleta mema maadamu uwe tayari kuzitii na chochote kiendacho kinyume na sheria hizi huwa na mwisho mfupi.

Kinazo mbegu za uharibifu ndani mwake. Yaliyo mema katika kila maisha ya mwanadamu huwa ni changamoto ya kutufanya tuzitii sheria hizi. Tunao uhuru wa utashi kuyafanya haya yote. Na kwa hiyo upatanisho wake hutujia mara tu baada ya kuwa tumeanza kuzitii, sisi pamoja na ulimwengu wetu; ni juu yetu kuamua.

Katika kipindi hiki cha kukua kiroho, nilitamani sana kujua na kuyafanya yale ambayo Mungu angetaka niyafanye. Ukuzi wa kiroho haupatikani kirahisi, ni jambo lihitajilo juhudi kubwa. Linachukua muda kama vile kukua kwa aina nyingine kulivyo.

Njia ya kujiondoa taratibu kwenye utamanifu wa vitu huyakwamisha maendeleo ya ukuzi wa kiroho. Mpaka hapo utakapokuwa umejiondoa kikamilifu ndipo matunda huanza kuonekana. Njia ya kujiondoa mara moja kwenye utamanifu wa vitu ndiyo nyepesi kwani huleta baraka za mara moja. Na mara tu Mungu akishaingia katika maisha yako zawadi zake humiminika kukibariki chochote ukigusacho.

Kwangu mimi niliyakimbia yale yasiyo na mwisho mrefu; nikaingia kwenye utajiri wa kweli. Kwenye ulimwengu huu yaonekana nimeyaacha mengi. Nimeachia mzigo mkubwa wa umilikaji vitu, matumizi ya muda kiholela; nikiyafanya yale ambayo nisingeyafanya na kuyaacha yale ambayo nilijua ningeyafanya. Kwangu mimi yaonyesha kuwa nimefaidi kiasi cha kutosha angalau hazina kubwa isiyo gharama ya afya njema pamoja na furaha tele.

## MAPOKEO YA AMANI YA NDANI

Nilikutana na milima na mabonde mengi katika kipindi changu cha kukua kiroho. Badaye katika harakati za kupambana na hali hii nilijiwa na hali nyingine ya ajabu ya kujikuta niko juu ya mlima mrefu. Kiroho nilijikuta nimeupanda mlima ule. Hili lilikuwa onyesho langu la kwanza la maisha halisi ya Amani ya ndani yalivyokuwa.

Hali hii ilinitokea siku moja asubuhi nilipokuwa matembezini; nilihisi ghafla ninanyanyuliwa juu, juu zaidi, hali ambayo ilikuwa haijawahi kunitokea. Tukio hilo lilinipatia raha sana kiasi kwamba; ninaukumbuka muda na nafasi ni vituvilivyonipungua na mwili wangu ulihisi wepesi. Nilihisi ninatembea hewani bila kukanyaga chini ardhini. Sikuwa na mtu yeyote karibu wala mnyama ila maua tu. Kila kichaka na kila mti uliokuwa karibu ulionekana kupambwa na mng'ao wa dhahabu. kulikuwepo na mwanga wa dhahabu kwa kila kitu kilichoonekana mbele

yangu na matone yenye rangi ya dhahabu yakawa yanadondoka kutoka juu angani. Hali hii huitwa kipindi cha nuru.

Jambo muhimu katika yote haya si kwamba ninadhihirisha ugeni wa mambo bali nilionyeshwa kuwa upo umoja wa nafsi katika uumbaji wa vitu vyote kwenye mbingu na nchi. Vitu vyote vionekanavyo na visivyoonekana viko chini ya nguvu moja inayoviunganisha ikivipa uhai. Nafsi hiyo moja ndiyo iitwayo uumbaji. Nayo wengi huiita Mungu.

Tangu hapo sijawahi kujisikia kuwa mbali na nafsi hiyo. Nimekuwa ninarudi kiroho mara kwa mara kwenye kilele cha mlima ule nilioufikia siku nilipompokea Bwana.

Mvuto wa hija ulinijia tangu muda huo. Nilikaa juu ya kilima nikiwa ninatazama maskani ya New England. Niliwaza kuhisi upatanisho wangu na watu. Nilihisi jambo moja kwamba endapo ningekuwa mbali na upatanisho wa watu, umuhimu wangu kwa watu usingekuwapo kwani kila wakati nilipokuwa nje ya upatanisho hali hiyo ilidhoofisha huduma yangu kwa watu.

Nilipoamka mapema asubuhi sana roho yangu ilikuwa bado inaelea kwenye hali ile ya kipindi cha upatanisho. Kipindi cha kujiona nimezungukwa na vitu vya kuufurahisha moyo wangu, kama vile; mapenzi, Amani, na furaha. Inaonyesha kuwa hao ndio walinzi wa mazingira niishiino. Sitikisiki kwa lolote lijalo mbele yangu maadam vitu hivyo niwe navyo moyoni.

Kwenye uso wa ulimwengu unaweza kuonekana mtu mwenye matatizo lakini kama unao ulinzi wa ndani ya roho yako matatizo haya yatatatuliwa kirahisi mno. Hakuna lililo gumu. Hilo ndilojambo muhimu nililojifunza.

Kama maisha yako yamepatanishwa na wale wote wakuzungukao na kama wewe ni mtiifu wa sheria zitawalazo mbingu na nchi, kamwe maisha yako hayawezi kuwa na mlundikano wa mambo mengi kichwani.

Mara ujikutapo unayo michanganyiko ya mambo mengi kichwani ujue kuwa yale uyatendayo hayana haki ndani yake.

Sasa kuna kuishi kwa kutoa badala ya kupokea. Na kama utaelemea upande wa kupokea badala ya kutoa utagundua kwamba kiasi utakavyoendelea kupokea bila kutoa kamwe hutatoa bila kupokea hata angalau basi, vitu vya ajabu kiroho kama afya njema, furaha na amani ya ndani. Kuna ile hisia ya nguvu mwilini zisizokwisha. Zenyewe zinaendelea kuwepo kama uionavyo hewa kwenye mazingira. Nguvu hizo daima unaongezewa tu na si rahisi kujisikia unapungukiwa.

Sasa maisha yako yanaongozwa na uwezo wa ajabu. Ile nguvu ya ajabu ambayo inaongozwa na Mungu huuongeza mwili wako mawazo na matendo ya kiroho.

Yale mawazo ya kujipenda na ubinafsi huongozwa na ule utashi wa raha na mahitaji mengine ya mwili, na pia kuutegemea utashi wa mawazo ya mtu.

Mimi ninaweza kuuambia mwili wangu; " lala pale kwenye sakafu bila chochote cha kutandika usinzie," mwili ukatii. Ninaweza kuyaambia mawazo yangu; " funga kila kitu sasa hivi, na mawazo yangu yakakifanya kile kilichoko mbele yangu." Nayo(mawazo) yakatii. Ninaweza kuiambia roho yangu, "tulia hata kama uko mbele ya jambo lolote la hatari kubwa na roho yangu ikatulia bila ya kutikisika." Nayo roho yangu ikatulia bila ya kutikisika.

Mwanafalsafa mmoja mashuhuri aliwahi kusema; "Yule ambaye haendi sawa na wengine katika mchezo wa ngoma anaweza kuwa anaicheza ngoma nyingine tofauti na ile waichezayo wenzake."

Ukishakua kiroho; unagundua kwamba kila mwanadamu ni sawa na mwingine. Anao wajibu muhimu hapa duniani na anayo haki ya kuheshimiwa kwa umuhimu wake sawa na wengine. Tunatofautiana katika hali ya kukua. Hii ni kweli kwa sababu tunao utashi huria. Ule utashi huria ndio uwezao kututofautisha katika mafanikio yetu ya kukua kiroho ama kukwama kwetu katika matendo yetu ya kiroho. Utashi huria ndio ulionifikisha kwenye hatua hii ya kuitafuta Amani ya ndani ambayo iliniandaa kufanya safari za kuhiji nizifanyazo sasa.

Ukiutazama uumbaji wa Kimungu utaona umuhimu uonekanao wazi. Utamuona Muumba ndani ya uumbaji na ni ajabu, ajabu ya ulimwengu.

Niligundua mwaka 1952 kwamba ilikuwa ni kipindi kizuri kuzianza shughuli za hija. Vita ya Korea na kipindi cha Mc Carthy vilikuwa vimepamba moto. Kilikuwa ni kipindi ambacho kamati za Congress ziliwatuhumu watu kwa makosa mbalimbali mpaka mtu ajitetee hadi ithibitike kwamba hana kosa lolote. Wakati huo ilikuwa salama kwa mtu kuamua kuwa baridi katika matendo. Hali hii ingewaondoa watu kutoka kwenye kukata tamaa na kuwafanya wafikiri na wajishauri ni nini wakifanye. Kwa kiasi kidogo cha fedha ambacho nilibaki nacho; nilinunua karatasi na kalamu kwa ajili ya kuueneza ujumbe pia na vifaa vingine kwa ajili ya ushonaji wa vazi langu la Amani. Mshonaji wa vazi hilo alikuwa mwanamke mmoja kutoka Calfornia. Maandishi ya Amani mgongoni na kifuani mwa vazi hilo yaliandikwa na bwana mmoja fundi wa maandishi. Mara nilipolivaa vazi langu hilo kwa mara ya kwanza; sikusita kulikubali kwani lilinifaa. Na huo ndio uliokuwa mwanzo wangu.

## SURA YA TATU

### *HIJA*

Hujaji ni mzungukaji mwenye lengo maalum. Hija yaweza kufanyika mahali; ina mahali maalum panapoeleweka. Lakini pia yaweza kufanyika kwa ajili ya kitu, hija yangu ni kwa ajili ya amani, na ndiyo maana mimi ninaitwa hujaji wa Amani.

Hija yangu inahusika na suala zima la Amani; Amani kati ya mataifa, Amani kati ya vikundi, Amani ya mazingira yetu, Amani kati ya mtu na mtu na la muhimu, muhimu zaidi- **AMANI YA ROHO-**ambayo ninaizungumzia sana mara kwa mara kwani hapo ndipo Amani inapoanzia.

Hali katika ulimwengu utuzungukao ni kielelezo cha hali ilivyo kwa ujumla. Hatimae jinsi tunavyo kuwa watu wa Amani tunajikuta tunaishi katika ulimwengu uliojaa Amani. Katika zama za kati, mahujaji walitembea kama mitume walivyotumwa kufanya kazi zao bila fedha, chakula, wala mavazi ya kutosha na ninaifahamu desturi hiyo. Sina fedha na sikubali fedha yoyote katika hija zangu. Sihusiani na taasisi yoyote. Hakuna taasisi inayo nidhamini. Ninachokimiliki ni kile nilichokivaa, na nilichokibeba.

Hakuna lolote la kunikwaza. Niko huru kama ndege arukae angani. Ninatembea hadi hapo nipewapo hifadhi. Ninafunga hadi hapo nipewapo chakula. Siombi. Ninapewa bila kuomba, Je, watu si wema! Cheche ya wema iko ndani ya kila mtu. Hata pasipo kujali kwamba, imefichika ndani yake kiasi gani, lakini ipo. Inasubiri kuyatawala maisha yako kwa utukufu. Naiita cheche yenye asili ya Umungu au Utakatifu. Yesu aliita **Utawala wa Mungu ndani ya mwanadamu.**

Sasa hujaji anatembea huku akisali, na anatembea ikiwa ni njia ya kukutana na watu wengi na pengine kuwashawishi wafanye lolote lile kwa namna yao kwa ajili ya Amani. Kwa sababu hiyo ninavaa joho langu lenye maandishi kifuani HUJAJI WA AMANI na mgongoni MAILI 25,000 KWA MGUU KWA AJILI YA AMANI.

Hii inafanya mawasiliano yangu yawe kwa njia ya upole..... na ninapenda kuwa mpole.

Unakuwa katika hali nzuri ya kuongea na watu, kama wao wanaanza kukutaka maongezi kuliko wewe kuanza kuwataka maongezi. Hao wanaovutiwa na mimi pengine wamefurahishwa na hatua fulani ya Amani au wanayo sababu nyingine nzuri ya udadisi. Watu hao ni watu wa manufaa. Hatua hiyo inaniongoza kupata muda wa kuchangia na watu ujumbe wangu wa amani unaosema katika sentensi moja: **HII NI NJIA YA AMANI-SHINDA UOVU KWA WEMA NA UONGO KWA UKWELI, NA CHUKI KWA UPENDO.**

Kanuni Takatifu nayo ingefanya vivyo hivyo. Hakuna lolote geni kuhusiana na hilo isipokuwa utekelezaji wake kwa vitendo. Lakini mimi nauchukulia kama funzo kwa leo, hivyo unakuwa ujumbe wa hija ya Amani. Tafadhali usiseme juu juu kuwa haya ni mawazo ya kidini na hayatekelezeki. Hizi ni kanuni zinazotawala tabia ya binadamu, ambazo hutumika pasipo kubadilika kama ilivyo kanuni ya nguvu za uvutano, tunapozipuuza kanuni hizi kwa namna yoyote ile katika maisha. Matokeo

yake ni vurugu. Kwa kuzitii kanuni hizi ulimwengu wetu huu utaingia katika kipindi cha Amani na utajiri wa maisha kuzidi hata ndoto zetu nzuri. Neno la maana kwa wakatihuu ni KUTEKELEZA. Tunao mwanga wote tunaouhitaji, tunachotakiwa kukifanya ni kuuweka katika utekelezaji.

Ninachotembelea siyo nguvu ya ujana ni nguvu bora, natembea kwa nguvu isiyo na mwisho ya Amani ya Ndani ambayo haiishi daima! Unapokuwa njia ambayo kwayo Mungu hufanyia kazi zake hakutakuwapo tena kikwazo, kwa sababuMungu hufanya kazi KUPITIA KWAKO! Wewe ni chombo tu - na anachofanya Mungu hakina ukomo Unapofanya kazi ya Mungu huwezi kujikuta unapata taabu na kuwa na mawazo. Utajikuta mtulivu mwenye Amani na usiye na papara.

Hija yangu siyo vita vya Msalaba ambavyo vinaleta dhana ya hali ya hatari. Hakuna jaribio lolote la kulazimisha kitu kwa watu. Hija ni safari tulivu ya maombi na ya mfano. Kwanza kabisa matembezi yangu ni ya sala ya Amani. Ukijitolea maisha yako kuwa kama sala unazidisha ubora wa sala pasipo mfano.

Katika kufanya hija hii sijafikiri kama mtu mmoja bali kama sehemu ya moyo wa Ulimwengu huu ulilia Amani. Jamii ya Binadamu, kwa hatua za woga na kutetemeka inatembea katika makali ya kisu kati ya machafuko mabaya ndani ya kipindi kipya cha Elimu na Maarifa, wakati nguvu kuu zinaelekea kwenye machafuko. Hata hivyo kuna matumaini. Naona matumaini katika juhudi za waumini wachache wanaofanya kazi pasipo kuchoka. Ninaona matumaini katika tamaa halisi ya Amani iliyoko kwenye mioyo ya Binadamu, hata hivyo jamii ya Binadamu inatafuta Amani kwa kupapasa pasipo kujua njia.

Hija yangu ni fursa ya kuongea na Binadamu wenzangu kuhusu njia ya Amani. Pia ni kitubio kwa lolote ambalo pengine nilitenda kwa kuchangia au kutochangia katika hali mbaya ya Ulimwengu waleo. Ni sala pekee itakayoufanya Ulimwengu wetu huu uliochoka na vita kufuata njia ya Amani kabla maafa hayajauangukia.

Ujumbe wangu ni kusaidia kuendeleza Amani kwa kuwasaidia kuendeleza wengine kupata Amani ya roho. Kama mimi naweza kuipata wewe pia waweza. Amani ni wazo ambalo wakati wake umefika.

Nilianza safari yangu siku ya kwanza ya Januari 1953. Ni siku yangu ya aina yake ya kuzaliwa kiroho katika mengi. Ni kipindi ambacho niliunganishwa na ukamilifu. Sikuwa tena mbegu iliyofukiwa katika mchanga bali nilijisikia kama ua linalojongea taratibu kuelekea kwenye jua. Kwa siku hiyo nilikuwa mzungukaji anayetegemea wema wa wengine, ilikuwa safari ya hija iliyofanyika katika hali ya Asili! Kwa miguu na kwa imani. Niliachana na madai yote kuhusiana na jina langu, mali yangu, na vingine vyote vilivyohusiana nami. Ilikuwa ni safari ya furaha. Sehemu ilipozaliwa hija ni katika shindano la Gwaride la Miradi huko Pasadena,

California. Nilitembea mbele katika msitari, nikaongea na watu nikawapa ujumbe wa Amani huku nikigundua kwamba moyo wa uvivu hakupunguza ari halisi katika Amani. Nilipokuwa nimetembea mwendo kiasi hivi, askari akaja akanishika begani na nilidhani anataka kunizuia matembezi. Badala yake alisema; "Tunachohitaji ni maelfu ya watu kama wewe".

Yaliyonitokea mwanzoni kwa eneo la Los Angeles yalikuwa ya kustajabisha. Njia zote za mawasiliano zilifunguliwa kwangupamoja na ujumbe wangu mdogo wa Amani. Nilitumia muda mwingi kwa kuhojiwa na waandishi wa habari na kuchukuliwa picha na wapiga picha wa magazeti. Habari za Hija yangu pamoja na picha yangu zilikuwa katika vyombo vya huduma za mawasiliano kwa redio. Mbali ya kufanya maonyesho mawili ya Televisheni, nilitumia muda huo kurekodi kwa ajili ya matangazo ya Redio na Televisheni.

Magazeti yote kuanzia Los Angeles hadi San- Diego yalitoa habari za kuvutia. Huko San -Diego nilifanya onyesho moja la Televisheni na maonyesho manne ya Redio. Kiongozi wa Baraza la Makanisa ya San Diego alikubali ujumbe wangu na maombi yangu matatu na yalisambazwa kwa wingi kwenye makanisa yote.

Wakati nilipokuwa siko Barabarani nilikuwa naongea na kukusanya sahihi za watu kwa ajili ya maombi yangu matatu.La kwanza lilikuwa ni ombi dogo la Amani ya mara moja huko Korea. Linalosomeka hivi: ***" Na yaishe mauaji ya huko korea. Kisha unashughulikia hali hii ya mgogoro kulingana na uongo kwa ukweli na chuki kwa upendo."***

Ombi la pili lilielekezwa kwa Rais na Baraza la Uongozi likataka ianzishwe Idara ya Amani. Linasomeka hivi: ' ***Hii ndiyo njia ya amani, shinda uovu kwa wema na uongo kwa ukweli na chuki kwa upendo. Tunaomba ianzishwe idara ya amani yenye katibu wa amani anayekubaliana na kanuni hizi -na migogoro yote ya ndani na nje ya nchi ipelekwe kwenye idara hii ya amani'.***

Ombi la tatu lilikuwa ni ombi kwa Umoja wa mataifa na viongozi wa dunia kwa ajili ya upunguzaji wa silaha Duniani kuijenga upya dunia: '***kama umeona njia ya amani sharti uushinde uovu kwa wema uongo kwa ukweli na chuki kwa upendo. Tunawaomba mtuache huru kutokana na maangamizi ya silaha kali duniani, mtuache huru kutokana na chuki na woga ili tuweze kuwalisha ndugu zetu wenye njaa, tuikarabati miji yetu iliyobomoka na tufurahie utajiri wa maisha ambao waweza kupatikana tu katika ulimwengu usio na silaha na ujitoshelezao kwa chakula'.***

Nilikusanya na kusaini maombi toka watu mbali mbali, vikundi vya Amani, makanisa na taasisi nikiwa njiani na kuyatunza ndani ya mkoba kwa shughuli hiyo. Niliwasilisha kwa Maafisa Jumba la Ikulu ya Marekani (White House) na kwenye Umoja wa Mataifa. Hii ilikuwa baada ya kukamilisha safari yangu ya kwanza kuzunguka nchi. Na ninashukuru kwamba ombi langu la kwanza ' ***mauaji ya Korea na yaishe—,'*** angalau ombi hilo lilikubalika kabla ya mwaka kuisha.

Huko Tijuana, Mexico baada tu ya kuvuka mpaka toka San Diego nilipokelewa na Mayor wa Tijuana ambaye alinipa ujumbe wa kumpelekea Mayor wa jiji la New York. Pia nilikuwa na ujumbe toka kwa Wahindi wa California kwenda kwa wenzao wa Arizona. Wakati nilipopita San Diego katika mwaka huo wa kwanza nilikaribishwa kuzungumza na hadhara. Mwalimu mmoja wa Shule ya Sekondari alinifuata mitaani na kutaka kujua kama nitapenda kuongea na wanafunzi wa darasa lake. Nilimwambia kwa uhakika nikiwa Hujaji wa Amani kuwa; sijawahi kuongea na kikundi. Alinihakikishia kuwa mambo yatakuwa mazuri na akaniomba kujibu tu maswali ya wanafunzi wake. Nilikubali. Kama unalo jambo la maana la kusema. Vinginevyo kuna maana gani ya kutaka kuzungumza katika Ulimwengu huu.

Sina tatizo lolote kuzungumza mbele ya kundi la watu. Ujitoapo nafsi kutenda mapenzi ya Mungu, njia inakuwa rahisi na ya furaha. Ni wakati tu hujajitoa nafsi yako ndio njia inakuwa ngumu. Ninapozungumza, nguvu inatembea ndani yangu kama vile umeme unavyosafiri kupitia kwenye waya.

Mwanzoni, taratibu za maongezi yangu mara kwa mara zilipangwa katika taratibu maalum. Nilipokuwa natembea kupitia kwenye shule, Mkuu wa Shule alitoka nje na kusema; " Wanafunzi wangu wanakuchungulia kupitia madirishani. Kama utapenda kuingia na kuongea nao tutawakusanya katika ukumbi wa michezo. Hivyo nikakubali. Kisha, wakati wa mchana, mtu mmoja kutoka kikundi cha haki za Raia, aliniijia na kusema; " Mzungumzaji wangu hakutufurahisha. Je, waweza kuja kuzungumza wakati wa chakula cha mchana?" Na kwa kweli nilikubali.

Na mchana huo huo Profesa wa Chuo kimoja akiwa njiani kuelekea kwenye darasa lake alinisimamisha na kusema; "Je naweza kukupeleka kwa wanafunzi wangu? "Hivyo nilikwenda kuongea na Darasa lake.

Wakati wa usiku mzee wa Kanisa akiwa na mkewe wakienda kula chakula cha jioni huko kanisani walinisimamisha na kusema; "Je, waweza kufikiria ombi la kuja kula pamoja nasi?" Na nilikubali. Pia walinipatia malazi kwa usiku huo. Na haya yote yalitokea siku moja wakati natembea bila ya kuwa na mipango yoyote.

Sasa hivi ninafanya bidii sana kuongea habari za amani katika vyuo, shule za Sekondari, makanisa na kadhalika. Lakini daima nina furaha. Msimamo wangu wa ***lile linalokuja kwanza litekelezwe kwanza*** umeniwezesha kuimudu mipango ya maongezi yangu kujibu barua zangu kwa wakati hata kufanya matembezi.

Siku moja huko Cincinnati nilifanya mahubiri saba katika maeneo saba mbalimbali ya kuabudia. Kwa siku hiyo ya Jumapili niliwapa wazee wa kanisa mapumziko.

Sadaka na michango mingine hairuhusiwi katika mikutano ifanywayo kwa ajili yangu. Sikubali pesa yoyote kwa kazi niifanyayo. Fedha yoyote ninayotumiwa kwa njia ya posta inatumika kwa uchapaji wa majarida ambayo yanatumwa kwa yeyote anayeyahitaji bila ya malipo yoyote.

Ukweli ni lulu pasipo malipo. Huwezi kuupata ukweli kwa kununua. Unachotakiwa kukifanya ni kuutafuta ukweli wa kiroho, na unapokuwa tayari kuupokea utaupata bure. Kamwe ukweli wa kiroho hautauzwa vinginevyo labda muuzaji awe ameumia kiroho. Unapoteza mawasiliano yote ya kiroho mara tu

unapoufanyia biashara. Wale walio na ukweli hawawezi kuuweka kwenye vifurushi na kuuza. Hivyo yeyote anayeuuza kwa kweli hanao.

Wakati nilipoanza nilidhani hija yangu yaweza kunipa taabu. Lakini nilikuwa nimedhamiria kuishi maisha ya uhitaji yaani sikutaka zaidi ya mahitaji yangu wakati wengi wanacho kidogo kuliko mahitaji yao. Kutubu ni kukubali kupata taabu kwa ajili ya kupata mema. Nilikubali lakini taabu ilipojitokeza nilijikuta nimenyanyuliwa juu yake. Badala ya taabu nilijikuta katika hali ya ajabu ya amani, furaha na kuamini kwamba ninayafuata mapenzi ya Mungu. Baraka badala ya shida zinamiminika juu yangu.

Ninalikumbuka fundisho la kwanza nililolipata wakati wa hija lilikuwa ni fundisho la kupokea. Nimekuwa mtoaji kwa miaka mingi na nilihitaji kujifunza kupokea kwa furaha kama nilivyoweza kutoaili kumpa mtoaji furaha na baraka ya kutoa. Ni vizuri sana kama unaishi kwa kutoa. Kwangu mimi ndiyo njia pekee ya kuishi, kwa sababu kwa jinsi utoavyo ndivyo uzipatavyo baraka za kiroho.

Nilijaribiwa sana katika mwanzo wa hija yangu. Maisha ni mfululizo wa majaribio, lakini kama unafaulu majaribio yako unayaangalia ya nyuma kama matukio mazuri. Nafurahi nilipatwa na matukio hayo.

Kama unao upendo na nia njema kwa binadamu wenzako hutawaogopa. " Upendo thabiti huufukuza woga."

Jaribio moja lilitokea usiku wa manane katikati ya jangwa la California. Magari yalikuwa yameacha kutembea na hapakuwa na makazi yoyote ya binadamu katika eneo la maili nyingi. Niliona gari limeegeshwa pembeni mwa barabara. Dereva aliniita akisema " Njoo hapa ingia ndani upate joto." Nikasema; " Sitembei kwa magari." Akasema; " Siendi popote nimeegesha tu gari langu hapa." Niliingia ndani. Nilimwangalia yule mtu alikuwa mkubwa, pandikizi la baba- Kitu ambacho wengi wangekiita binadamu mwenye sura ya kutisha. Baada ya kuzungumza kwa muda alisema;" Hutahitaji kulala kidogo?" Nilimjibu, " Ooh, kwa kweli ninahitaji". Na nilijikunja kwenye kiti nikalala usingizi. Nilipoamka nilimuona mtu yule ameshangazwa na kitu fulani na baada ya kuzungumza naye kwa muda fulani alikiri kwamba wakati aliponitaka niingie kwenye gari kwa hakika hakudhamiria kunitendea mema, akaongeza; " Uliponyanyuka kwa imani kubwa na kwenda kulala nilishindwa kukugusa!"

Nilimshukuru kwa kunipa hifadhi kisha nikaendelea na safari yangu. Nilipoangalia nyuma nilimuona ameinua macho yake juu anaangalia mbinguni. Na nilitumaini kuwa alimfahamu Mungu usiku ule.

Hakuna awezaye kutembea bila matatizo kama yule anayetembea kwa unyenyekevu na pasipo kumdhuru mtu, kwa mapenzi makubwa na imani kubwa. Hivyo mtu wa namna hiyo anapata mema toka kwa wengine (Na kuna wema kwa kila mtu) na hivyo hawezi kudhurika. Hili linafanyika kati ya watu, linafanyika kati ya mtu na mtu, kati ya vikundi na kati ya mataifa, kama yangelikuwa na ushujaa wa kulijaribu.

Safari moja nilipigwa na kijana aliyechanganyikiwa kiakili ambaye nilimchukua kwenye matembezi. Alipenda kufanya matembezi lakini aliogopa kuwa angevunjika miguu na kubaki amelala barabarani. Kila mmoja aliogopa kwenda naye. Alikuwa na umbile kubwa na alionekana kama mwanasoka, na alifahamika kwa kuwa mshari wakati mwingine. Safari moja aliwahi kumpiga mama yake vibaya kiasi cha kumfanya alazwe hospitalini kwa majuma kadhaa. Kila mmoja aliogopa kutembea naye, basi mimi nilikubali kutembea naye.

Hadi tulipofika kwenye kilele cha mlima wa kwanza mambo yalikuwa yanaendelea vizuri. Kisha ngurumo na upepo ulioambatana na radi ukaanza. Aliogopa sana kwa vile mvua iliyoambatana na ngurumo na radi ilikuwa karibu sana. Ghafla fahamu zilimpotea akanijia akaanza kunipiga. Sikukimbia ingawaje nadhani ningeweza kufanya hivyo. Alikuwa na mfuko mzito mgongoni. Lakini hata wakati alipokuwa akinipiga nilichoweza kuhisi ni huruma kubwa kwake. Vipi mtu augue ugonjwa wa akili hata aweze kumpiga mamamzee asiye na kinga yoyote! Niliisafisha chuki yake kwa amani, hata wakati alipokuwa akinipiga, matokeo yake kipigo kilikoma. Alisema; "Wewe hukunirudishia! Mama yangu daima alinirudishia."

Tendo la mimi kutomrudishia kutokana na vurugu zake lilifikisha hali ya wema ndani yake. Ooh; wema uko pale hata kama umefukiwa chini kiasi gani na alipatwa na hali ya majuto na kujilaumu sana.

Je, mikwaruzo michache katika mwili wangu ni kitu gani ikilinganishwa na kuyabadilisha maisha ya binadamu? Kwa kifupi kijana huyu hakuwahi tena kuwa mshari. Leo hii ni mtu wa manufaa sana katika ulimwengu huu.

Safari nyingine tena niliitwa kumtetea msichana dhaifu wa miaka minane dhidi ya mtu mkubwa mkaidi aliyetaka kumpiga. Msichana aliogopa sana. Hili lilikuwa jaribio langu gumu kupita yote. Nilikuwa nikiishi kwenye shamba la mifugo; na ndugu zake walikuwa wamekwenda mjini. Msichana mdogo hakutaka kwenda nao, na kwa vile nilikuwwa pale waliniomba kama ningeweza kumwangalia yule mtoto. Nilikuwa dirishani nikiandika barua wakati nilipoona gari linafika. Mtu alitoka ndani ya gari hilo. Msichana alimuona na kukimbia, naye alimfuata akimfukuzia ndani ya ghala la chakula. Nilienda mara moja ndani ya ghala. Msichana alijikunyata kwa hofu ndani kwenye kona, na yule mtu alikuwa akimsogelea taratibu na kwa kukusudia kumdhuru.

Waijua nguvu ya fikra. Unaipata kwa jinsi unavyofikiri mfululizo. Na huvuta kwako chochote ukiogopacho. Hivyo niliijua hatari iliyomkabili kutokana na woga wake. Siogopi (lolote na ninayategemea mema hivyo mema hunijia!)

Mara moja nilisimama katikati ya yule mtu na yule msichana. Nilisimama tu na kumuangalia huyu mtu maskini, mgonjwa wa akili kwa moyo wa upendo na huruma. Alisogea karibu. Alisimama akaniangalia kwa kitambo kidogo. Kisha aligeuka na kuondoka na msichana alikuwa amebaki salama. Hapakuwa na neno lililozungumzwa.

Sasa kulikuwa na njia gani nyingine? Je, kama ingelisahau sheria ya upendo kwa kulipiza kisasi na kuitumainia sheria ya kinyama ya jino kwa jino? Hapana shaka ningelikuwa nimepigwa-pengine hadi kufa na hata huyo msichana mdogo pia. Kamwe usidharau uwezo wa upendo wa Mwenyezi Mungu. Unabadili! Unaenda hadi kwenye cheche za wema na kumnyang'anya mwovu silaha za kutendea uovu wake.

Nilipoanza hija yangu nilikuwa ninatumia safari zangu kwa malengo mawili. La kwanza lilikuwa ni kuwasiliana na watu na hilo linafanyika hadi leo. Lakini la pili lilikuwa ni nidhamu ya sala. Kunifanya nizame kimawazo katika sala ya amani. Na baada ya miaka michache niligundua kitu. Niligundua kwamba sihitaji tena ile nidhamu ya sala. Sasa ninasali pasipo kukoma. Sala yangu binafsi ni: ***Nifanye niwe chombo cha kuzungumza ukweli mtupu.***

Wakati wa hija yangu kupitia Arizona nilikamatwa na askari kanzu nikiwa ninatuma barua zangu katika posta ya eneo hilo huko Benson. Baada ya kuzunguka kwa muda ndani ya gari la doria nilifunguliwa mashitaka ya uzururaji. Unapotembea kwa imanikiutaratibu wewe unaonekana na kosa la uzururaji. Ndiyo, nimefungwa mara nyingi kwa kutokuwa na fedha yoyote, lakini mara nyingi wananiachia huru mara tu wanapoelewa.

Kuna tofauti kubwa kati ya **Gereza** na **Jela**.Gereza ni chombo kikubwa ambacho kinafuata kanuni za aina fulani. Jela ni chombo kidogo ambacho hakifuati sana kanuni. Na hii ilikuwa jela!

Waliniweka kwenye chumba kikubwa cha ndani kilichokuwa kimezungukwa na vyumba vidogo vidogo (selo) walimokuwa wakifungwa wanawake, wanne wanne walilala kwenye selo moja!

Nilipokuwa ninaingia nilijisemea moyoni; " **Msafiri wa Amani umejitoa maisha yako kwa ajili ya kutumikia -Tazama eneo lako jipya la ajabu la kuifanyia kazi."**

Nilipoingia ndani msichana mmoja aliguna; "Eeh! Wewe ni mtu wa vituko. Ni wewe pekee uliyeingia humu kwa tabasamu. Wengi wao waliingia humu wakilia na kulaani."

Niliwaambia, " Kama mngepata siku moja ya mapumziko nyumbani hamngefanya lolote la manufaa siku hiyo? " Walisema; " Ndiyo, sasa tutafanya nini?" Hivyo nikawafanya waimbe nyimbo ambazo ziliihamasisha mioyo yao. Niliwapa mazoezi rahisi ya kumfanya mtu ajisikie mwenye furaha na kusisimka mwili mzima.

Kisha niliongea nao kuhusu hatua za kuielekea Amani ya ndani.

Niliwaambia kwamba waliishi katika jamii na lolote ambalo lingefanyika katika jamii ya nje lingeweza pia kufanyika katika jamii yao. Walifurahi sana na kuniuliza maswali mengi. Ooh! ilikuwa ni siku nzuri.

Siku ilipokwisha walinzi walezi walibadilishana zamu. Wasichana wale hawakumpenda mwanamke aliyeingia zamu. Walisema alikuwa mtu wa ovyo na

wakasema wasiongee naye. Lakini ninajua upo wema ndani ya kila mmoja na kusema kweli niliongea naye. Nilijifunza kwamba mwanamke huyu aliitegemea kazi hii kwa kuwatunza watoto wake. Alijisikia kwamba inamlazimu kufanya kazi na mara nyingi hakujisikia vizuri ndio maana alikuwa mkali mara kwa mara.

Nilimtaka mlezi (matron) aone mazuri tu ya wafungwa wake. Na niliwataka wasichana waone mazuri tu ya mlezi wao.

Baadae nilimwambia mlezi; " Ninaona unayo nafasi ya kutosha hapa kwenye nyumba yako, ninaweza kulala kwa kustarehe hapa kwenye benchi la mbao." Badala yake aliwataka wanileteе kitanda kidogo cha mtoto chenye shuka safi, na nilioga maji ya moto na kujikausha kwa taulo safi na kuzipata faraja zote za nyumbani.

Asubuhi yake niliwaaga rafiki zangu na kusindikizwa mahakamani, hatua chache kutoka jela. Aliyenisindikiza alikuwa naibu mkuu wa jela. Sikufungwa pingu wala hakunishika. Lakini alikuwa na bunduki kubwa begani. Nilimwangalia na kusema; " Hivi ningekimbia ungenipiga risasi?" Kwa kicheko alisema, "Ooh! hapana sipigi risasi kitu chochote ninachoweza kukikamata."

Asubuhi ile mahakamani nililikana shitaka na shauri langu lilifutwa mara moja. Ndani ya mizigo yangu iliyochukuliwa usiku ule ilikuwapo barua ambayo iliongeza uzito katika kuniachia huru. Inasomeka hivi; ***" Mwenye barua hii amejitambulisha kama hujaji wa amani akitembea pwani hadi pwani kuelekeza mawazo ya raia wetu kwenye tamaa yake ya amani katika ulimwengu hatukumfahamu kwa undani kwa vile yeye anapita tu katika jimbo letu, kwa vile hapana shaka kwamba safari yake itakuwa ndefu, na ngumu, tunamtakia safari ya amani."***

Iliandikwa kwenye karatasi rasmi ya kiofisi na kuwekewa sahihi na Gavana wa Jimbo Bwana Howard Pyle.

Wakati nilipokuwa ninaachiwa huru ofisa wa mahakama alisema; " Huelekei kuchukia kwa kukaa siku moja jela." Nikasema waweza kuufunga mwili wangu lakini siyo roho yangu." Ni mwili pekee ambao wanaweza kuufunga gerezani. Sikujihisi ufungwa- labda ujifunge mwenyewe. Walinichukua hadi sehemu ile ile waliyonikamatia siku moja kabla. Lilikuwa tukio la kufurahisha.

Kila tukio huwa kama unavyolifanya na linakamilisha lengo, linaweza kukushawishi, kukuelimisha na linaweza kukupa nafasi ya kuwa mtoa huduma kwa namna fulani.

Mengi ya mazungumzo yangu yanafanyiwa matayarisho kabla, lakini bado ninapewa nafasi ya kuzungumza katika hali nisiyotegemea. Huko Minneapolis nilikuwa nikihojiwa na mwandishi wa habari, katika kusanyiko la wanachama wa klabu ya haki za raia waliokuwa wakimsubiri Gavana wa Minnesota awahutubie. Hakuweza kuhutubia hivyo walinialika nichukue nafasi yake. Kwa kweli nilikubali.

Na nikiwaongelea Magavana, mara nilipoingia ndani ya mlango mkubwa wa mbele wa Ikulu siku moja, muungwana mmoja katika hali ya urafiki alinisalimu kwa kunishika mkono na kuuliza anisaidie nini. Nilimwambia ninatafuta ofisi ya

Gavana na alinipeleka haraka sana. " Lipo jambo lingine niwezalo kukusaidia?" Aliniuliza.

." Nilidhani ningeweza kupata heshima ya kushikana mkono na Gavana." Nilisema.

" Tayari umeshashikana mkono na Gavana." Alisema rafiki mzuri muungwana-Gavana mwenyewe!

Ulikuwa ni mwaka wa kwanza wa hija yangu na nilikuwa mahali fulani kwenye barabara kuu kati ya El Paso na Dallas wakati nilipokamatwa kwa uzururaji. Nilikuwa sijawahi kusikia kikosi cha upelelezi cha FBI (sawa na kikosi cha upelelezi wa makosa ya jinai huku), kikiwapeleleza watu kwa uzururaji,. lakini nilipelelezwa. Mtu aliyekuwa ndani ya gari jeusi alisimama akanionyesha beji yake ya utambulisho. Hakutaka hata kunilazimisha nifuatane naye alisema tu; " Je, unapenda kuongozana nami?" Nilijibu "Ooh ndiyo. Nitafurahi sana kuzungumza nawe." Niliingia ndani ya gari lake, lakini nilichora alama kubwa ya " X " barabarani. Sehemu aliyonichukulia. Kipindi hicho nilikuwa nahesabu umbali kama ningeacha njia ningeweka alama kubwa ya " X " kisha ningerudi kwenye eneo hilo na kuanza safari upya.

Alinileta kwenye jela hii na kusema; " muweke ndani kwa uzururaji."Na nilipitia taratibu zote. Kwanza wanakupeleka kuchukua alama za vidole. Nilishangaa sana kwa sababu sikuwahi kuchukuliwa alama za vidole kabla - ama niseme tangu kuzaliwa! Kisha alichukua Kemikali na kama vile mwanzo alisafisha wino huu, kumbe, ulikuwa umekwisha.

Niliongea naye kama ambavyo ningeongea na mtu mwingineyeyote ambaye ningekuwa naye, na jambo la kufurahisha lilitokea. Ni dhahiri kwamba alizoea hali ya watu kutoshirikiana naye. Nilipomjali kama binadamu mwenzangu, alinipa maelezo kuhusu uchukuaji wa alama za vidole, na alinionyesha mipango ya kazi yao. Ilikuwa inafuarahisha sana. Kwa kweli sikuwahi kujifunza mengi kuhusu alama za vidole kabla. Watu walikuwa wanasubiri mstarini lakini sikujua hilo mpaka nilipotoka ndani ya chumba na kuona mstari mrefu. Kisha nilipelekwa kupigwa picha na kunifungia namba shingoni kwa mnyororo. Walipokuwa wananipiga picha kwa mbele na kwa upande, nilikumbuka zile picha za watu wanaotafutwa na Polisi unazoziona kwenye Posta. Nilikumbuka jinsi wote walivyoonekana kama vichaa, na nikajisemea moyoni, " Ngoja mimi nionekane tofauti". Na nilitabasamu kwa furaha kama nilivyoweza. Kuna uso mmoja wa tabasamu sehemu fulani katika jengo la kumbukumbu za watu laghai.

Kisha walinipeleka kunihoji. Walinikalisha chini ya mwanga mkali unaotegemewa kuwa na madhara ya Kisaikolojia kwako. Lakini nilikwisha wahi kuingia kwenye Studio za Televisheni, na nilijisemea, " Hivi kweli unadhani huu ni mwanga mkali? Wangeona mwanga kwenye Studio za Televisheni!" Enzi hizo mwanga wa Televisheni haukuwa mkali tu bali wenye joto.

Kwanza waliniuliza kama ningejibu swali lolote, na nilisema; "Hakika nitajibu maswali yenu, si kwa sababu nyie ni maafisa wasimamizi wa sheria, bali kwa sababu nyie ni binadamu wenzangu, na huwa ninajibu maswali ya binadamu wenzangu wote. Vyovyote uwavyo katika wadhifa wako wa kazi, kwanza na awali ya yote wewe ni binadamu. Na kama tungeshirikiana pamoja kama binadamu kwa binadamu tungefanya mambo kwa haraka sana".

Na yaliisha kwa namna hiyo!

Walianza kwa mbinu ya kunichanganya. Mmoja alinitupia swali. Nililazimika kusema; "tafadhali ungenivumilia kidogo wakati najibu swali la muungwana wa kwanza ."

Baada ya hapo waliniuliza maswali ya maana kama yale niliyokuwa naulizwa na wanavyuo. Jinsi nilivyoshinda hilo somo!

Kisha walirejea kwenye matumizi ya nguvu yakiwa ni kwa lengo la kudhuru. Walisema; " Je, wewe katika hali yoyote ile waweza kutumia au kuidhinisha matumizi ya nguvu? " Nilisema; " La hasha, ni kinyume na amri za Mungu. Niko radhi kuwa na Mungu katika upande wangu kuliko mamlaka yoyote yale katika nchi". Niliwaeleza habari za yule kijana aliyechanganyikiwa ambaye alinipiga wakati tuko pamoja kwenye matembezi.

Kisha walisema; "Je, kama ilikuwa ni muhimu kwako kumtetea anayempenda?" Nilisema; "Ooh, siamini kama ningeweza kumtetea mpenzi wangu kwa kuvunja amri takatifu ". Niliwaeleza habari za msichana wa miaka minane aliyeachwa chini ya uangalizi wangu na mtihani tulioupata toka kwa mgonjwa wa akili aliyetaka kudhuru.

Kisha walichukua mambo kwa utulivu (kifalsafa) na kusema; "kama ungetakiwa kuchagua kati ya kuua na kuuawa ungechagua lipi?"

Nilijibu; " Sidhani kama ningehitaji kufanya uchaguzi wa aina hiyo -- si wakati ambapo maisha yangu yameunganishwa na mapenzi ya Mungu. Labda kama kweli ulikuwa mwito kwangu kuifia imani. Huo utakuwa ni wito mkuu, hutokea mara chache sana. Siamini kama ndio wito wangu -- lakini dunia inajifunza kukua kupitia mashahidi wake wa imani. Kama ingekuwa nifanye uchaguzi,ningechagua kuuawa kuliko kuua." Hapa nilikuwa najaribu kueleza hali ya asili ya utu na hali ya asili ya Umungu ili waweze kuielewa! Niliwaambia kwamba kama ninavyoelewa mimi sikuwa mwili. Bali nilikuwa nimevaa mwili. Mimi ni kile kiupacho mwili uhai.

Huo ndio ukweli. Kama ninauawa, kifo kinaliharibu tu vazi la udongo, yaani mwili. Lakini kama ninaua kifo kinadhuru ule uhaiisi yaani roho!

Na waliniachia kama mtu mwenye muelekeo wa kidini katika hija yangu. Lakini je, kama ningesema hivi; " Hata hivyo umewahi kusikia kuhusu kujihami- kwa nini hata sheria inatambua kujihami?"

Kisheria, hili laweza kukubalika lakini si la kidini.

Kulikuwa na kipindi fulani wakati nilipojisikia kuwa kwa hakika ninapambana na mambo ya asili. Yalikuwa mazoea yangu kutembea kwenye upepo mkali

unaoambatana na vumbi ambao wakati mwingine ulivuma kwa kishindo kikubwa kiasi cha kunifanya nishindwe kuvumilia. Wakati mwingine vumbi lilikuwa zito kiasi cha kushindwa kuona mbele yangu na nilijiongoza kwa pembeni mwa barabara. Askari polisi alisimama kando yangu na kuufungua mlango wa gari lake na kuita kwa sauti kali; " Ingia garini mwanamke kabla hujauawa. " Nilimwambia kuwa natembea hija na sikukubali kuendeshwa kwenye magari wakati wa matembezi yangu. Pia nilimwambia kuwa, Mungu ndiye ngome yangu na hapakuwa na lolote la kuhofia. Wakati huo huo upepo ulitulia, vumbi likaisha na jua likaonekana mawinguni. Niliendelea kusafiri lakini jambo la ajabu lilikuwa kwamba kiroho nilijisikia nimeinuliwa juu ya taabu.

Kilichojificha katika kila tukio jipya linalotupata ni funzo la kiroho kwetu sisi na baraka za kiroho kwa ajili yetu kama tutajifunza. Ni vizuri kujaribiwa. Tunakua na kujifunza kwa kufaulu mitihani. Ninaiona mitihani yangu yote kama majaribio mazuri yanijengayo kiroho. Kabla ya kujaribiwa, niliamini ningetenda kwa upendo ama kwa njia ya kutoogopa. **Baada ya kujaribiwa** nilijua! Kila jaribio liligeuka kuwa jaribio la kuniendeleza. Nasi lazima matokeo yake yawe kulingana na mapenzi yetu.

Ninalikumbuka tukio moja wakati ilipoandikwa kwenye gazeti moja hapa nchini(Marekani) kuwa nitahutubia kanisani. Liliionyesha picha yangu kifuani na mgongoni, nikiwa nimevaa joho langu lenye maandishi. Mtu mmoja muumini wa kanisa lile alihofia sana alipogundua kuwa kiumbe huyu aliyevaa joho lenye maandishi alikuwa karibu kuhutubia kwenye kanisa lake. Alimuita muhubiri wake kuhusiana na suala hili, aliwaita marafiki zake kuhusiana na suala hili. Mmoja alinifahamisha kuhusu mtu huyo kuwa ni nani. Nilisikitika sana kwa vile; kwa namna fulani nilikuwa nimemuudhi mtu ambaye sikumfahamu. Hivyo nilimuita!

" Huyu Hujaji wa Amani anaita." Nilisema, nikimsikia akihema. Baadaye alinieleza kuwa alidhani nimemuita ili nimtoe nje kwa kumfokea. Nilisema, " Nimekuita ili nikuombe msamaha kwa sababu kwa hakika nitakuwa nimetenda jambo la kukuudhi, kwani hata pasipo kunifahamu umehofia mazungumzo yangu kwenye kanisalako. Hivyo kwa namna fulani nilijihisi ninakuwia samahani na nimekuita ili nikuombe msamaha!"

Je, unafahamu ya kuwa mtu yule alibubujikwa na machozi hata kabla ya maongezi kuisha? Na sasa tu marafiki- aliniandikia baada ya hapo; naam, sheria ya upendo inafanya kazi.

Mtu mwingine siku moja aliniambia; " Ninashangaa sana u mtu wa namna gani. Baada ya kusoma ujumbe wako kuhusu njia ya Amani nilitegemea ungekuwa mtu wa heshima sana. Lakini badala yake nimekuona kuwa mtu wa kufurahi na kucheka na watu wote.

Nilimwambia; " Ni nani awezaye kumjua Mungu asiwe na furaha? " Kama una uso wa kutisha na hali ya hasira, kama uso wako haung'ai kwa furaha na urafiki, kama hujajazwa hadi ukafurika kwa upendo pamoja na huruma kwa watu wote na viumbe vyote, jambo moja ni la uhakika: **Humjui Mungu!**

Aidha, maisha ni kama kioo. Tabasamu kwenye kioo na chenyewe kitarudisha tabasamu.

Kama unawapenda watu vya kutosha, nao watakurudishia upendo. Kama nikiwaudhi watu, ninajilaumu nafsi yangu. Kwani ninajua kwamba mwenendo wangu ungekuwa mzuri wasingeudhika hata kama hawakukubaliana nami.

***Kabla ulimi haujaongea, lazima uwe umepoteza uwezo wa kujeruhi.***

Ngoja nikueleze kuhusu wakati ambapo ilibidi upendo wangu usiwe wa maneno. Nilikuwa najaribu kumsaidia mwanamke mmoja ambaye alikuwa mgonjwa sana kiasi cha kushindwa kuendesha gari. Alitaka kufika kwa dada yake mkubwa kwa mapumziko ya wiki chache kitandani, hivyo nilikubali kumuendesha hadi huko. Wakati huo bado nilikuwa na leseni yangu ya kuendesha gari. Wakati tukiwa njiani alisema; " Amani ningependa ukae nami kwa muda- dada yangu mkubwa anapenda kutukuzwa. Ninahofu sana kuishi naye nikiwa peke yangu." Nikasema; " Sawa ninazo siku chache za ziada; nitakaa nawe kwa kipindi kifupi."

Tulipokuwa tunaingia kwenye eneo la nyumba ya dada yake, alisema; " Amani sielewi ni mapokezi ya namna gani utakayoyapata kwa dada yangu." Alikuwa mkweli kuhusiana na dada yake mkubwa. Dada yake aliponiona tu na joho langu; lenye maandishi " **ya Msafiri wa Amani**; " aliniamuru nitoke kwenye nyumba yake. Lakini ilikuwa ni usiku sana na alikuwa anaogopa giza hata akasema; " Sio usiku huu, usiku wa leo utalala kwenye kochi, lakini jambo la kwanza asubuhi lazima uondoke."

Kisha alimharakisha mdogo wake kwenda kulala mahali fulani juu ghorofani. Vema; hili lilikuwa baya kuliko nilivyotegemea. Hakika sikupenda kumuacha rafiki yangu katika hali hii lakini ningefanyaje? Hivyo niliangaza macho kuona kama kuna kitu chochote kinachoweza kuniruhusu niwasiliane na huyu dada mkubwa. Niliangalia jikoni nikakuta rundo la vyombo vichafu na hakuwepo muoshaji wa vyombo. Niliosha vyombo vyote kisha nikalisafisha jiko na kulala kwa saa chache.

Asubuhi yake, yule dada mkubwa alitokwa na machozi na kuniomba nisiondoke. Alisema; " Kwa kweli unaelewa usiku wa jana nilikuwa nimechoka sana hata sikuwaza nilichokuwa nikikisema." Na tulikuwa na wakati mzuri pamoja kabla ya kuondoka na kuwaacha.

Unaona, hili lilinipa nafasi ya kuuweka ujumbe wangu katika vitendo. Vitendo ni vizuri. Vitendo hukamilisha, wanasema watu.

Wakati wa safari zangu mtu mmoja anayemiliki mgahawa unaouza chakula na vinywaji aliniita ili anipe chakula kwenye mgahawa wake. Wakati nilipokuwa ninakula aliniuliza;" Unajisikiaje unapokuwa kwenye eneo kama hili?"

" Ninafahamu, watu wote ni wana wa Mungu." Nilijibu. " Hata wakati ambapo hawatendi kama wana wa Mungu, nina imani kwamba wangeweza, na nawapenda kwa hivyo ambavyo wangeweza kuwa."

Nilipoamka ili niondoke, nilimuona mtu mmmoja akiwa na kinywaji chake mkononi naye anaamka. Aliponiona alijenga uso wa tabasamu na hapo hapo na mimi nikatabasamu. " Unanionyesha tabasamu?" Alisema kwa mshangao!

" Nilidhani hungeweza hata kuongea nami, lakini umenionyesha tabasamu."

Nilitabasamu tena, siko hapa kuwahukumu binadamu wenzangu nilimwambia.

" Niko hapa kupenda na kutoa huduma."

Ghafla alipiga magoti mbele yangu na kusema; " Kila mtu alinihukumu, hivyo nilijitetea. Wewe hukunihukumu kwa hiyo sasa najihukumu mwenyewe. Mie si mtu mwema, ni mkosaji nisiye na manufaa yoyote! Nimekuwa nikiharibu pesa zangu katika ulevi. Nimekuwa nikiipatisha taabu familia yangu. Nimekuwa nikielekea kwenye ubaya zaidi!"

Niliweka mkono wangu begani mwake.

" Wewe ni mwana wa Mungu." Nilisema, " Na ungetenda kama hivyo. " Alikiangalia kinywaji chake kwa kinyaa na kukitupa kwenye mbao na kuivunja bilauri. Macho yake yaligongana na yangu.

" Ninakuapia sitagusa tena kitu hicho." Alisisitiza. Na kulikuwa na nuru mpya kwenye macho yake wakati akitembea kuelekea mlangoni kwa hatua ya ukakamavu. Hata ninauelewa mwisho mzuri wa hadithi hii. Baada ya mwaka mmoja na nusu hivi nilipata habari kutoka kwa mwanamke mmoja wa mji ule. Alisema kuwa kwa kadri kila mtu anavyoelewa mtu yule, alitunza ahadi yake. Hakugusa pombe tena. Sasa hivi ana kazi nzuri. Anaelewana vizuri na familia yake na amejiunga na kanisa. Unapowakabili watu kwa namna ya kuwahukumu wanakuwa wapinzani. Uwezapo kuwakabili kwa upole wa namna ya upendo pasipo kuwahukumu wanakuwa na hali ya kujihukumu wenyewe na kubadilika.

Wakati wa hija yangu magari mengi yalisimama kutaka kunichukua. Baadhi walidhani kuwa kutembea maana yake ni kusafiri kwa kuutegemea msaada wa magari ya watu. Niliwaambia siwezi kumdanganya Mungu. Huwezi kudanganya kuhusu umbali unapokuwa kwenye hija.

Ninakumbuka siku moja nilipokuwa ninatembea kwenye barabara kuu gari moja nzuri ilisimama na mtu aliyekuwa ndani akaniambia; " Ni ajabu iliyoje kwa wewe kuitika wito wako?"

Nilimjibu-kwa hakika ninadhani kwamba kila mtu angekuwa anakifanya kile anachohisi kuwa ni kizuri kukifanya.

Alianza kunieleza jinsi alivyoshawishika kufanya jambo, na hakika lilikuwa zuri. Nilifurahi sana na kumchukulia kuwa anafanya jambo hilo. Nilisema; Hilo linanistajabisha. "Unaendeleaje kulifanya jambo hilo?" Na alinijibu; " Ooh silifanyi tena!" Kazi aina hiyo hailipi chochote. Sitasahau jinsi mtu huyo alivyokuwa hana furaha kwa kukata tamaa. Katika kipindi hiki cha maendeleo ya vitu, tunakuwa na kigezo potofu namna hiyo kwa ajili ya kuyapima mafanikio. Tunayapima kwa njia ya dola ( fedha), kwa njia ya kuwa na vitu. Lakini furaha na amani ya ndani havipo

**kwenye muelekeo huo. Kama unafahamu lakini hutendi, wewe ni mtu asiye na furaha kabisa.**

Nilipata tukio jingine kando ya barabara wakati gari liliposimama na watu wawili bibi na bwana waliovalia vizuri walipotelemka na kuanza kuzungumza nami. Nilianza kuwaelezea nilichokuwa nikikifanya. Ghafla mume alianza kububujikwa na machozi. Nilishangaa. Alisema; " Sijawahi kufanya lolote kwa ajili ya Amani na wewe umeyafanya mengi."

Pia kuna wakati ambapo mtu mwingine alisimamisha gari kuongea nami. Aliniangalia si kwa ujeuri bali kwa mshangao mkubwa na udadisi, kama vile amekutana na mzimu. " Kwa siku hii, na umri huu." Alishangaa; " Pamoja na maajabu yote yapatikanayo katika dunia hii, kitu gani hasa kimekufanya utembee hija ya Amani?"

" Kwa siku hii na karne hii, " nilimjibu; " wakati binadamu wana tetereka kwenye ncha ya vita vya nyuklia vya kuteketeza dunia, haishangazi kwa mtu mmoja kujitoa mhanga kwa ajili ya amani- badala yake inashangaza kwamba maisha ya wengi hayajatolewa mhanga kwa ajili hiyo."

Nilipomaliza matembezi yangu ya mzunguko wa kwanza nilishukuru sana kwa vile sikushindwa kuutekeleza wito. Nilijisemea au tuseme kuwaza; " Si itakuwa ni ajabu kwamba Mungu anaweza kufanya jambo kupitia kwangu!"

Baada ya hapo nililala kwenye stesheni kuu ya kati ya gari la moshi iitwayo Grand kwenye jiji la NewYork. Usingizi ulipoanza kuniishia nilipata hisia kwamba sauti nzuri isiyo na mfano ilikuwa inanisemesha maneno ya kunitia moyo, **" Wewe ni mwanangu mpendwa nipendezwaye nawe."**

Usingizi uliponiishia kabisa ulisikika mziki mwororo toka juu mbinguni ukawa ndio unamalizika kuimbwa pale Stesheni, huku mwangwi wake ukiwa bado unasikika hewani. Nilitembea katika ubaridi wa asubuhi lakini nilijisikia mwili kuwa wa joto. Nilitembea kwenye baraza lililosakafiwa lakini nikajisikia kama ninatembea mawinguni. Hisia za kuishi ndani ya upatanisho na kusudio takatifu kamwe hazijanitoka.

<u>Tanbihi:</u>

Neno inner peace: Limetafsiriwa kama Amani ya ndani au Amani ya Roho. Tafsiri zote mbili zimetumika kwa maana moja.

## SURA YA NNE

*YALIYOJIONYESHA KWENYE HIJA*

Wakati Nilipoianza safari yangu ya hija ya Amani; vazi langu liliandikwa **Msafiri wa Amani**. Kifuani mwangu na mgongoni liliandikwa ***" Kutembea pwani hadi pwani kwa ajili ya Amani."*** Kadri miaka ilivyopita maandishi mgongoni mwangu yalibadilika **kutoka matembezi ya maili 10,000** (sawa na kilometa 16,000) **kwa ajili ya upunguzaji wa silaha kali duniani hadi maili ishirini na tano elfu** (ambazo ni sawa na kilometa arobaini elfu), **kwa ajili ya Amani**, na kuishia kwa ujumbe wa sasa usemao; **" Maili 25,000 kwa miguu kwa ajili ya Amani."**

Matembezi haya yamenichukua mara kadhaa katika majimbo arobaini na manane ya Marekani na Meksiko pamoja na majimbo kumi ya Kanada.

Mwishoni mwa mwaka 1964, nilimaliza matembezi ya mguu Washington D.C. Nilijishauri mwenyewe kuwa maili ishirini na tano elfu ambazo ni sawa na kilometa arobaini elfu zilikuwa zikitosheleza kutembea. Hii ilinifanya nijihusishe zaidi kwenye barabara kubwa ambako niliweza kuujua urefu wa barabara kutokana na umbali ulioonyeshwa kwenye ramani. Sehemu hizi hazikuniwezesha kukutana na watu. Ni sehemu nzuri tu za kutembea kwa vile utakuwa unajua umekwishakutembea maili ngapi.

Sasa niko huru kutembea sehemu waliko watu ambako pia maili hazionyeshwi. Sehemu ninazopendelea zaidi ni kama vile ufukoni, kwenye njia za mguu za msituni na kwenye maporomoko ya maji na mitelemko ya milima.

Mambo mengine huwa ni rahisi kama vile kwenda bila ya kupata chakula. Mara chache nilikuwa ninaikosa milo mitatu hadi minne bila ya kukifikiria chakula hadi nilipopewa. Muda mrefu ambao nimewahi kukaa bila ya chakula ni siku tatu hadi nilipobahatika kuokota matunda ya tofaa yaliyokuwa yamedondoka toka mtini. Niliwahi kufunga kula; kama nidhamu ya sala kwa siku arobaini na tano, hivyo ninafahamu ni vipi mtu awezavyo kuishi bila kula kwa kipindi kirefu. Tatizo langu siyo jinsi ya kukipata chakula kingi ila ni vipi niwezavyo kuishi vizuri bila ya kula kupita kiasi. Kila mtu hupenda kunipa chakula hata cha ziada.

Nimekuwa nikikosa usingizi mara moja moja bila kujali japo kwa shida. Mara moja, mnamo kipindi fulani mimi hukosa usingizi wa usiku, lakini hivi sasa siyo mara kwa mara. Mara ya mwisho ilikuwa mwezi Septemba 1977 nilipokuwa kwenye sehemu ya kuegeshea malori. Nilikuwa nimeamua kulala kidogo lakini palikuwa na pilika pilika kiasi kwamba nilikesha nikiwa sehemu ambayo haikutulia. Nilikaa macho naongea na madereva wa malori. Jambo la kwanza baada ya kuingia mle kwenye kituo, dereva wa lori ambaye alikuwa ameniona kwenye Televisheni alitaka kuninunulia chakula. Nilikaa kwenye kiti cha mwisho pembeni. Madereva

wengine walianza kufika mmoja baada ya mwingine na malori yalikuwa yamepangana katika msululu. Madereva baadhi yao walikuwa wananiuliza maswali haya na yale. Sikuweza kulala kutokana na kuongea nao usiku kucha. Baada ya hapo asubuhi, mmoja wao, alinipatia kifungua kinywa ambachobaada ya kula niliondoka.

Wakati mmoja dereva wa lori aliamua kulisimamisha lori lake pembeni mwa barabara na akanieleza kuwa aliwahi kunisikia kwenye televisheni nikieleza juu ya nguvu isiyokwisha ambayo na yeye aliwahi kuwa nayo. " Kuna wakati mji ulijawa na mafuriko. Sikupendezwa na hali hii kiasi ambacho nilijitoa kuwasaidia watu. Nilifanya kazi bila ya kula wala kulala na bila ya kuchoka. Kwa sasa uchovu wangu umenirudia baada ya hiyo nguvu kuniishia."

" Hivi sasa ni kitu gani ufanyiacho kazi?" Nilimuuliza.

" Fedha." Alijibu.

" Hiyo iwe ni kwa bahati mbaya tu, " niliendelea, " Utakuwa na nguvu ya kudumu tu utakapokuwa unafanya kazi kwa manufaa ya wote . Ni sharti uache mwenendo wa kufanya kazi kwa faida yako mwenyewe. Katika dunia hii utapewa kadri utakavyotoa. Hiyo ndiyo siri ya maisha."

Nimekuwa nikitembea wastani wa maili ishirini na tano kwa siku kutegemeana na idadi ya watu watakaonisimamisha kuzungumza nao njiani. Nimewahi kutembea umbali wa maili hamsini kwa siku kuitikia wito ama kutokana na kutokuwa na mahali pa kujihifadhi.

Nyakati za baridi kali usiku huwa ninatembea usiku kupata joto. Na wakati panapokuwa joto sana mchana ninatembea usiku kupunguza joto la mchana. Nimewahi kutembea nyakati za usiku zenye giza nene lenye milio ya wadudu mbalimbali wa usiku wenye kutoa miale pamoja na sauti ya viumbe vingineo.

Kuna wakati niliwahi kutembea maili thelathini na tatu na mtu mmoja mwenye urefu wa futi sita ambaye alikuwa akiniacha nyuma wakati wa kutembea. Hatimae alipochoka miguu yake ilipata vidonda na kuumwa na misuli. Yeye alikuwa akitembea kwa nguvu zake mwenyewe tofauti na mimi ! Kwani nilikuwa ninatembea kwa nguvu isiyokwisha itokanayo na Amani ya dhati ndani mwangu.

Mwanamke mmoja aliwahi kuniuliza iwapo angeweza kujiunga nami katika matembezi ya Hija. Alinieleza kuwa alikuwa anataka kuachana na mume wake. Inawezekana alikuwa na wito ila ari yake haikutosheleza. Mwanamke mwingine aliyejitokeza kutembea na mimi alishindwa kuendelea nyakati za mchana. Ilinibidi nimpakie kwenye gari la abiria kumrudisha nyumbani.

Sikuwahi kupata janga lolote katika matembezi yangu. Wakati fulani, walevi wawili walinifuata wakiwa na gari, lakini nilipowapisha kando ya barabara waliondoka.

Ni wakati mmoja tu mtu aliwahi kunirushia fedha za ki-Marekani alizokuwa amezibana kwenye kiganja chake. Mtu huyo alikuwa kwenye gari lililokuwa likienda kasi. Nilichoweza kukifanya, nilizitoa kwenye kanisa jirani ambako nilipita kuzungumza na waumini.

Wakati fulani mwanachuo aliwahi kuniuliza iwapo nimewahi kutukanwa, nikamjibu kuwa angekuwa mwendawazimu kunitukana wakati sidaiwi kitu chochote! Kuna wakati nilikuwa ninatembea nje ya mji wakati wa jioni nikaitwa na watu wenye uwezo mzuri kimaisha waliokuwa katika nyumba kubwa. Waliona ni jukumu lao la Kikristo kunionya juu ya sehemu moja hatari iliyokuwa mbele yangu ikiitwa**Kusini mwa Mpaka**. Walinionya nisilikaribie eneo hilo. Hata hivyo watu hao wawili mke na mume hawakunipatia chakula ama mahali pa kupumzika, hivyo niliendelea kutembea kwa saa kadhaa.

Lilikuwa giza totoro lililofunikwa na mawingu na baada ya muda mfupi mvua ilinyesha. Mkononi nilikuwa nimechukua barua zilizohitaji kujibiwa. Mara moja niliziweka mfukoni mwa gwanda langu nikatafuta sehemu ya kujikinga mvua ambayo wakati huo ilikuwa inanyesha kwa wingi sana!

Mbele yangu nilikiona kituo cha mafuta na hoteli yenye malazi na chakula. Nilijikinga chini ya dari lililokuwa juu ya mabomba ya gesi. Mtu aliyekuwa kwenye kituo cha gesi alitoka nje akiwa ana sema ; " Usisimame huko kwenye mvua ingia ndani hotelini." Kisha akasema; " Loh, tulisoma habari zako, tungependa kukupa chakula cha jioni ama kile chochote ukipendacho." Hapo nilielewa nilikuwa wapi. Ile sehemu iliyosemwa ya hatari **Kusini mwa Mpaka.**

Nilipewa chumba cha kulala na mtu aliyekuwa kwenye hoteli hii ambaye alikuwa ameketi pembeni mwa meza kutoka kwangu. Walinipa pia kifungua kinywa asubuhi yake.

Palikuwepo na michezo kama kamari kwenye vyumba vya nyuma vya hoteli hiyo. Pia kulikuwapo na aina nyingine ya mchezo lakini walinilea kwenye mazingira ya kikristo kuliko wale waliokuwa wamenionya dhidi yao!

Hii inaudhihirisha usemi wangu kuwa kila mtu anao uzuri wake.

Nimekuwa nikikaribishwa vema katika maeneo ambayo si ya kawaida. hii ni pamoja na kwenye sehemu ya mikutano huko Florence, Arizona ukumbi wa Jiji na Tombstone Arizona kwenye injini za moto. Kuna wakati niliachwa kwa saa kumi na tatu kwenye chumba tulivu cha mapumziko cha stesheni ya mafuta. Malazi yangu yalikuwa ya kimya bila usumbufu ingawaje hali ilikuwa baridi kiasi hiki.

Huwa ninalala vizuri, pawe kwenye kitanda chenye godoro ama kwenye majani pembeni mwa barabara. Nikipewa chakula na mahali pa kupumzika ama nisipate bado huwa nina furaha ile ile.

Mara nyingi nimekuwa nikipewa mahali pa kupumzika na watu nisio wafahamu, wapita njia. Mara nyingine ninakuwa kwenye vituo vya magari, vituo vya magari ya moshi na maeneo mengine ya kuegeshea magari makubwa, iwapo sikupata mahali pa kukaribishwa ninalala sehemu kama hizo.

Ninakumbuka nilipowahi kupewa kitanda chenye hadhi ya malkia kwenye hoteli moja mashuhuri jioni moja; na kesho yake kupewa nafasi kwenye sakafu ya kituo cha mafuta kifanyacho kazi kwa saa ishirini na nne. Pale nililala bila matatizo. Mara nyingi nilifunguliwa mlango wa chumba cha gereza kilichokuwa hakina mfungwa na mhudumu mwenye fadhila.

Nikikosa pa kujisitiri huwa ninalala nje ama pembeni mwa barabara tegemeo langu akiwa ni Mungu kunilinda.

Madaraja mara kwa mara yalinikinga na maafa, halikadhalika; magofu ya maghala na nyumba. Mifereji ya kupitisha majibarabarani na mabomba makubwa vilitumika kama hifadhi za malazi yangu. Sehemu niliyoipendelea zaidi kulala wakati wa usiku ilikuwa sehemu ya wazi kwenye mkusanyiko wa majani ya chakula cha mifugo kwenye shamba la karibu. Blanketi langu lilikuwa nyota za angani.

Makaburini ni sehemu nzuri pia ya kulala nyakati za usiku. hakuna mtu ajishughulishaye na kuingia huko. Huwa ni kimya na majani yamepunguzwa kwa kufyekwa. Hakuna maingiliano ya usumbufu miongoni mwa roho zilizokwisha hama. Inaelewa ninaitakia Amani.

Lakini meza ya chakula shambani kando ya barabara ama mkusanyiko wa majaniya miti ya misonobari ama kwenye matakia ya majani kwenye mashamba yavutiayo ya ngano husaidia kwa kupumzikia. Siku moja nilipokuwa nimelala huko Kansas, kwenye shamba la ngano niliamshwa toka usingizini na sauti kubwa. Niliamka ghafla nikaona mashine kubwa ya kuvunia ngano ikielekea nilikokuwa. Nilijiviringisha mara moja kuukwepa uelekeo wa mapanga yake yaliyokuwa yakizunguka katika uvunaji.

Ninajisikia kuwa na ulinzi kamili katika safari zangu za Hija. Mungu ndiye ngao yangu. Hakuna ajali katika mipango iliyo mitakatifu na wala Mungu hatuachi wenyewe. Hakuna awezaye kutembea kwa Amani kama atembeaye kwa upole na bila ugomvi akiwa na upendo pamoja na Imani kubwa.

Ninakumbuka wakati fulani usiku katika mwaka fulani, palikuwa na baridi sana. Ilikaribia theluji lakini mchana hali ilikuwa ya joto kidogo hivyo pakawa nafuu. Ilipofika jioni palikuwa na majani makavu yaliyokuwa yamedondoka chini. Nilikuwa katikati ya miti na palikuwa hakuna mji wowote karibu. Ilikuwa ni siku ya Jumapili yalikuwa machweo ya jua. Kulikuwako na gazeti moja la Jumapili ambalo lilikuwa limetupwa pembeni mwa barabara baada ya kusomwa kama vile halikutakiwa. Nililiokota nikatoka nalo nje ya barabara hadi kwenye kivuli cha mti mmoja mkubwa. Chini ya mti huo kulikuwako na shimo dogo lililokuwa limefunikwa na majani. Nilisukuma majani mengi ndani ya hilo shimo. Nilichokifanya ilikuwa kuweka makaratasi kiasi juu ya shimo hilo na karatasi zingine nikazitumia kujifunika. Nilipoamka asubuhi kulikuwapo na theluji nene iliyokuwa imesambaa sehemu mbalimbali chini lakini mimi nikawa nimekingwa na mti niliojihifadhi chini yake. Nilikuwa na furaha na mwenye joto kiotani mwangu

palipojengeka kwa majani ya karatasi. Hilo ndilo dokezo tu endapo utakwama usiku mmoja.

Watu wengi wapendao kwenda likizo ni wale wafanyao shughuli ambazo hawana wito nazo, ambazo hutaka kuziacha kwa muda. Sikudhania kuwapo umuhimu wa kuchukua likizo kutokana na ziara yangu ya Hija. Ni uzuri ulioje inapokaribia mwishoni mwa mwaka kusafiri maeneo ya kusini! kuona mazingira shwari wakati wa mavuno, ukiacha theluji. Kuona majani ya mimea mbali mbali yanavyopendeza nyakati za masika. Ni uzuri ulioje kusafiri kaskazini katika majira ya vuli na kufurahia maua ya vuli kwa miezi kadhaa badala ya majuma kadhaa. Yote haya yamenipa uzoefu eneo la katikakati la nchi hii.

Nilipokuwa New England wakati wa matembezi yangu ya maili 1,000 (Ambayo yalianzia Greenwich, Connecticut na kuishiaBurlington, Vermont) nilipita pita kwenye miji mikubwa na midogo niliyokuwa nimealikwa. Nilianza safari wakati matunda yalipokuwa yamekomaa yanakaribia kuiva. Niliyala nikichanganya na matunda damu na ya zambarau ya msituni yote yakawa yamenipatia ladha nzuri.

Katika nchi niliweza kuona majengo makubwa yakijengwa na niligundua kwamba barabara nzuri na reli zingine zilijengwa kupita chini ya ardhi milimani na kuvuka maporomoko ya maji ya mito.

Ilikuwa ni mandhari ya kupendeza sana. Kwenye ziara yangu ya Hija ninafurahi kuwa nilifuata barabara za zamani zilizoelekea milimani. Waliozawadiwa katika mazingira haya ni wale walioweza kufika kileleni na kuweza kuona hali ya nchi ilivyo kote. Ninajua huu ni ulimwengu wa kuwa na vyombo madhubuti ikiwa ni pamoja na barabara za kudumu ambazo zinategemewa zaidi lakini ninatumaini bado barabara za miguu zitakuwapo tu. Barabara zipitazo milimani.

Mara nyingine watu huniuliza jinsi ninavyotumia likizo yangu hasa Krismasi. Sikukuu kama hizo nimekuwa nikizitumia katika matembezi yangu. Wengine wengi huenda safari za magari kuonana na watu. Ninakumbuka Krismasi moja nilivyolala nje nikimulikwa na nyota. Nyota moja ilikuwa inang'aa sana kiasi kwamba ilikuwa kama nyota ya Bethlehemu. Kesho yake kukiwa na nyuzi joto 80 Faranheiti; nilitembea hadi New Orleans nikakuta maua mengi ya Krismasi yanachanua pamoja na kukutana na watu na marafiki wapya. Krismasi moja nilikuwa katika ngome ya Worth, Texas ambapo minara na majumba marefu yalikuwa yamepangwa yakiwa na machanganyiko wa rangi mbali mbali jambo lililonipa kumbukumbu isiyosahaulika kadri nilivyokuwa ninatembea katika jiji. Siku hiyo nilikaribishwa na nikawa na muda mzuri wa kuendelea kupata mawasiliano yangu kwa njia ya barua.

Wengine huniuliza iwapo sijisikii upweke wakati wa likizo. Nitajisikiaje upweke wakati muda wote najua ninaishi nikiwa na MUngu? Huwa ninapenda na ninafurahia kuwa na Mungu.

Mara nyingi kwenye miaka ya mwanzo nilikaribishwa na kupewa chakula na watu ambao sikuwafahamu. Ninakubali kila ninachopewa kama msaada kutoka kwa Mungu. Ninashukuru kwa mkate mkavu niliopewa kwenye nyumba ya wafanyakazi wahamiaji rafiki, halikadhalika na chakula cha gharama nilichopewa na mwanamke mmoja kwenye chumba cha maakuli cha hoteli ya Waldorf Astoria.

Ukishajitoa maisha yako kwa Mungu na kuwa unatembea kwa imani utagundua kwamba chakula unachohitaji na malazi vinapatikana bila shida. Kila kitu, hata vifaa vya kazi ninapewa. Vingine vya kustaajabisha ninapewa, ambavyo hata bado vinanishangaza.

Nilipata makaribisho ya kwenda Hawaii kutoka kwa rafiki ambayo yalikuwa kama zawadi. Baadhi ya rafiki waliniomba niongoze ziara hiyo ambayo moja ya kwenda Alaska ilikuwa wakati wa kiangazi mnamo mwaka 1979 na nyingine ya Hawaii mwaka 1980. Nilipanga ziara hizo ziwe za mafunzo na za kushawishi kwa wotewale waliohudhuria. Tuliishi na kusafiri bila gharama kubwa.

Sikukaa bila kazi katika majimbo mawili hayo yaliyokuwa mapya kwangu. Licha ya kuwatembeza rafiki nilizungumza na vikundi mbalimbali na pia katika Radio. Wengine waliopenda kujua jinsi maisha yangu ya hija yalivyo waliweza kuuliza. Na ninafikiri walifanya hivyo. Ilikuwa furaha kuwa nao katika sehemu hizi za kuvutia.

Kuna jambo lingine nilipokuwa ninapanga safari kuelekea kaskazini na kusini mwa Dakota, nilijua kwamba ningekatiza mipango yangu kuongoza msafara hadi Hawaii. Nilifahamu kwamba ingelinichukua juma moja kutoka Bismarck na kurudi tena Los Angeles ikiwa na maana kwamba safari ya majuma mawili kurudi kutoka Dakota ya Kaskazini na Kusini. Nilipokuwa ninawaza kuhusu safari hii; nilipata barua kutoka kwa mtu mmoja aliyenijulisha kuwa, amejitolea kunipa tiketi ya ndege kwenda na kurudi Bismarck. Hii ilikuwa kama muujiza kwangu japo ndicho nilikuwa nahitaji na huwa sikipokei nisichokihitaji.

Nilihitaji kuwahi kutokana na muda niliohitajika Dakota ya KAskazini na KUsini. Hili lilikuwa tuzo nisiloweza kamwe kulisahau moyoni.

Huwa ninapewa vitu halisi kama hivyo. Kuna wakati nilikuwa ninazungumza na mwandishi mmoja wa habari ambaye baada ya kumueleza kuwa mimi huwa ninazungumza na watu na wao huniuliza niwaaambie kama ninataka kula. Yeye alinijibu kuwa hajawahi kupewa chochote hata kipande cha mkate japokuwa amekuwa akizungumza na watu kwa miezi na hata miaka kadhaa. Nilimjibu kuwa yeye huwa si mtembezi kwa ajili ya Amani.

Kuna wakati nilikuwa ninapita kwenye nyumba moja ambako kulikuwa na mvulana mmoja Mmeksiko; wa miaka kumi na sita aliyekuwa amenisikia kwenye redio, alitoka nje kwa shauku akanikaribisha nyumbani kwao jioni hiyo. Familia yake iliishi katika banda la kimasikinilakini ninakumbuka nilivyohudumiwa kama mgeni rasmi. Baada ya chakula cha jioni, ambacho kilikuwa kande; familia hiyo ilitandika zuria lililotumika kama blanketi kwenye kitanda chao kimoja na tukalala.

Asubuhi yake kabla ya mimi kuondoka walinipa tena chakula kile kile walichonipa jioni yake kilichokuwa na mchanganyiko wa maharagwe.

Nilipokuwa ninapita Memphisi nilibana haraka kwenye chumba kimoja cha mbao kukwepa radi kali. Jioni hiyo nilikaribishwa kwenye nyumba ya familia moja ya kiafrika. Nyumbani mwao walitumia jiko la kuni. Kwa pamoja tulikula chakula chao kidogo ambacho kilikuwa ni ugali wa mahindi na maji. Chakula hicho pia kililiwa asubuhi kama kifungua kinywa. Wote tulilala chini palipofagiliwa. Sitayasahau makaribisho yao ya dhati.

Siku moja pale Oklahoma ilikuwa ni asubuhi ya baridi sana wakati mwanachuo mmoja aliponivulia glovu zake kutoka mikononi mwake pamoja na skafu yake kutoka shingoni mwake akaifunga shingoni mwangu. Usiku huo wakati hali ya hewa ilikuwa ya baridi zaidi wahindi mtu na mkewe; walinipa hifadhi nyumbani mwao.

Niliwahi kuonywa nisiende Georgia hasa hasa huko Albany ambako watu kumi na wanne watembea kwa mguu kwa ajili ya Amani walikuwa wametupwa jela. Lakini siwezi kusema kuwa baada ya kufika huko nilikutana na mtu ambaye hakuonyesha urafiki kwangu. Kusema kweli ukarimu walionionyesha ulizidi kiasi.

Vikundi vya watu wachache vilianza kuwa na mashaka na mimikwamba nisingebagua. Hadi hapo waliposoma maandishi kwenye vazi langu yahusuyo Hujaji wa Amani ndipo walipoanza kuniamini. Hawakusita kusimama na kuongea na mimi. Niliongea na watu ndani ya makanisa kadhaa pamoja na baadhi ya wazee wa kanisa ambao pia waliusoma ujumbe wangu kwa waumini kanisani.

Hakika, ninampenda yeyote ninayekutana naye. Kwa nini nishindwe? Ndani ya kila mmoja wetu ni cheche ya Mungu. Sihusiki na utaifa wa mtu, wala kabila wala rangi ya ngozi yake. Watu wote kwangu wanaonekana mwanga ung'aao. Ndani ya viumbe wote naona sura ya Mungu. Watu wote ni ndugu zangu. Watu kwangu ni wazuri.

Sisi watu wa ulimwengu twahitaji kupata njia ya kufahamiana kwa hiyo tutatambua kwamba kurandana kwetu ni kukubwa zaidi kuliko tofauti zetu. Hata kama kutakuwepo na tofauti kwetu kiasi gani kila chembe chembe hai ya kila mwanadamu ina umuhimu wa pekee hapa duniani.

## SURA YA TANO

***KUISHI MAISHA YA KAWAIDA***

Kuishi maisha ya kawaida ni mojawapo ya hatua kuelekea kwenye Amani ya ndani. Mtu akidumu katika maisha ya aina hii, hujijengea ubora wa maisha ndani na nje hali ambayo humuweka upatanisho na maisha yake. Kwangu mimi, hii ilinifanya nigundue kutokuwepo na maana ya kumiliki vitu ambavyo viko nje ya mahitaji yangu. Baada ya kujiweka katika maisha ya kawaida nilianza kupata faraja ndani na nje ya maisha yangu kiroho na kimwili.

Watu wengine hufikiri kwamba maisha yangu ya kujirahisisha ni ya shida na taabu lakini hawaujui uhuru uliopo kwa kujirahisisha. Kila wakati ninamshukuru Mungu kwa hali nzuri ambayo nimekuwa nikiipata. Maisha yangu yamejitosheleza na sina makuu. Kama maisha yako ni makuu, ni kwamba unafanya zaidi kuliko unavyotakiwa kufanya. Maisha yangu yalikuwa yametopea, nilijihisi uchoyo wakati kabla sijachukua kauli ya urahisi wa maisha; isemayo: **" Sitapokea zaidi ya hitaji langu wakati wengine duniani wanacho kidogo kuliko mahitaji yao."**

Inawezekana pia katika maisha kuwa uliwahi kuwa na vitu mbali mbali. Unaweza ukawa huru kama mimi ukiyarahisisha maisha yako. Utapewa kila unachokihitaji iwapo utakuwa na moyo wa kutoa.

Ambacho ningependelea na ambacho ninahitaji katika maisha yangu vyote ni sawa. Chochote cha ziada ya mahitaji yangu ni usumbufu kwangu. Usingeweza kunipa chochote ambacho sihitaji. Kutokuwa na fedha ni tatizo lakini mimi nimekuwa nikiishi hivyo. rafiki zangu wakubwa na wenye uzito wamekuwa wakinipa fedha nyingi ambazo mimi ninazikataa.

Nilizungumza na mtu mmoja ambaye alifikiri kuwa huwa nimenyimwa baadhi ya raha za dunia hii. Lakini hakuna chochote nisichotumia ama nisichoweza kufanya nilichopunjwa. Kujumuisha vitu vya kumiliki nilipochagua maisha ya upatanisho na Amani. Sikupenda maisha mengine.

Mimi siyo mfungwa wa starehe ama aliyeko hapa kupewa misaada. Vinginevyo nisingelikuwa mtu wa kuhiji. Tunaweza kuruhusu mawazo potofu kuyatawala maisha yetu na kuwa wafungwa kwayo.

Watu wengi hawapendi kuwa huru. Watapendelea kuomboleza na kulalamika isivyowezekana kuachana na utumwa wa vitu vya kumiliki, vyakula, vinywaji, uvutaji sigara na vinginevyo ambavyo vimekuwa ni vitu wasivyoweza kuishi bila kuwa navyo. Siyo kwamba hawawezi kuachana navyo; bali hakika hawajaamua kuviacha.

Mahitaji yetu ya kimwili hutegemeana na mahali tuishipo, hali za afya zetu na kadhalika. Kwa Ujumla tunahitaji nyenzo za kupikia, nguo za kuvaa na za kujifunika kusetiri joto, kupata hewa safi na maji pamoja na chakula. Vyote hivi tukiwa navyo twaweza kuishi. Yapo mahitaji mengine zaidi ambayo ambayo

yanatakiwa na miili yetu. Haya mara kwa mara huitaji fedha kidogo ama kutohitaji kabisa. Lakini hayo yasiyo muhimu sivyo yalivyo. Mathalani, wapo watu wengine ambao maisha yao hayajakamilika mpaka wasikilize muziki mzuri au wapige vyombo vya muziki. Hayahuwa ni maamuzi ya mtu kujirahisisha. Aina ya maisha ni chaguo la kila mtu.

Miaka arobaini iliyopita nilijifunza kuwa fedha na vitu haviwezi kumfanya mtu awe na furaha. Hii imekwishadhihirishwa mara nyingi kutokana na matajiri wengi wakubwa-mamilionea niliokwisha kukutana nao. Wote walikuwa na sifa moja. Hakuna hata mmoja wao aliyekuwa na furaha. Mfano ni tajiri aliyeitwa Howard Hughes aliyekuwa na dola za Kimarekani bilioni mbili na nusu. Wanasema alikuwa ni mtu aliyeonekana kuhuzunika sana na mwenye wasi wasi asiyewahi kutokea.

Pia kuna mwanamke mmoja aliyekuwa amerithi dola milioni nne na nusu. Hizi zilimharibu maisha yake. Kutokana na alivyozichukulia alipenda kuzitumia kwa uangalifu hatimae alijikuta amebeba mzigo mkubwa. Nafuu kama asingalikuwa nazo.

Inanidhihirishia kwamba kama mtu hana mali nyingi huwa hana furaha na akiwa nayo nyingi sana pia hana furaha. Walio na furaha zaidi ni wale wenye mali kiasi na wala siyo kupita kiasi.

Kuna mama mmoja wa umri wa kati ambaye alikuwa akilalamika kutokana na kazi nyingi alizokuwa akizifanya. Kisha nikamuuliza kwa nini anapenda kufanya kazi sana wakati hana mtu wa kumtegemea.

Jibu alilolitoa ni kwamba anatafuta fedha za kulipia kodi ya vyumba vitano anavyopanga.

Nilishangazwa na vyumba vitano. Nilimwuliza mbona yuko mwenyewe hawezi kuridhika kuishi kwenye chumba kimoja? Kwa masikitiko alijibu kuwa anazo samani za kutosheleza nyumba ya vyumba vitano. Alikuwa akifanya kila jitihada kuweza kuwa na nyumba ya kuvitosheleza vitu vyake vya nyumbani. Hii hutokea mara nyingi. Ninachoweza kukisema ni kuwa usiiruhusu hali hii itokee kwako.

Kutokana na mazingira yetu ya kupenda kuwa na vitu vya kumiliki tunapungukiwa na mengi ya msingi katika maisha yetu ambayo yanapatikana bure.

Kujilimbikizia vingi mno ni kujiongezea, mizigo isiyo muhimu. Ukiwa navyo sharti uende navyo kwa tahadhari.

Nitakueleza kuhusu mwanamke mwingine mmoja zaidi. Yeye alikuwa amekombolewa japo si katika njia iliyo nzuri. Nilimuona mara kwa mara. Lakini niliwahi kumuona wakati wa mwezi mmoja baada ya jumba lake ambamo yeye na mumewe walikuwa wanaishi peke yao baada ya watoto wao kukua na wakawa wametengena nao, kuungua moto wakati watu hao walipokuwa matembezini. Kila kitu kiliungua isipokuwa nguo walizokuwa wamevaa tu! Nikikumbuka namna alivyoumia kuipoteza nyumba yao pamoja na kwamba alikuwa na mzigo mkubwa wa kuitunza. Nilianza kumzungumzia maneno machache ya kumuliwaza Lakini

alisema; " Usinipe pole ya kuniliwaza! Huo ulikuwa ni wakati mwingine na siyo sasa tena, ulishapita muda wa kuniliwaza.

Fikiria ilivyokuwa kufanya usafi jumba lote hilo, kufua, kusafisha stoo, sijawahi kupata uhuru kiasi hiki nilicho nacho sasa. Ninajisikia kama ndiyo kwanza ninayaanza maisha upya.

Mama huyu na Bwana wake walikuwa wakijisetiri kwenye vyumba vya kawaida, na ninafikiri waliweza kuona tofauti kubwa ya mzigo waliokuwa nao. Lakini isingelikuwa bora kama wangelikuwawamejizoeza kutoa ziada ya walichonacho kusaidia wale wasio kuwa nacho? Wangebarikiwa kwa kuwa na moyo wa kutoa na wengine wangefarijika kwa kupokea. Kwa vyovyote vile hii ilikuwa ni nafasi iliyowafanya kuwa huru.

Kama uko huru fanya safari ya miguu maporini. Ni safari ya kushawishika kiasi gani kutembea mchana kutwa kwenye jua na usiku kulala nje chini ya nyota. Ni hali iliyoje kuishi maisha ya kawaida, ukiwa umebeba mambo muhimu tu unayoyahitaji, ikiwa ni chakula, malazi mepesi mgongoni utagundua kuwa; kuwa na vitu vya ziada ni sawa na kuwa na mzigo wa ziada. Hapa utaelewa ni nini muhimu kinachohitajika katika maisha, kinga nyakati za jua, baridi ama mvua, riziki wakati wa njaa, maji wakati wa kiu. Kila kitu kinatakiwa kiwepo kwa nafasi yake-wakati kihitajikapo na kisipohitajika huachwa. Hapa ndipo unaweza kuelewa na kufurahia uhuru wa kutokupenda makuu.

Tangu mwezi Mei hadi Oktoba 1952, kabla ya kuianza safari ya Hija yangu, nilitembea maili 2,000 kwenye miteremko wa milima ya Appalachian kutoka Georgia hadi Maine huko Marekani, nikaongeza ziada ya maili 500 kuyatembelea maeneo maalum yenye mandhari ya asili.

Niliishi maisha nje ya nyumba kwa muda mrefu nikiwa na suruali moja tu nyepesi pamoja na kaputula moja, blauzi na, sweta, blanketi nyepesi na shuka mbili. Aina ya mfuko wa nailoni ambao wakati mwingine nilishindilia majani. Mara kwa mara sikuwa mkavu na mwenye joto. Lakini niliifurahia hali hiyo kikamilifu. Chakula changu asubuhi na jioni kilikuwa mlo wa unga wa nafaka kama shayiri uliokorogwa kwenye maji na kuchanganywa na sukari. Niliweza kunywa kiasi cha vikombe viwili kwa kila mlo. Mchana nilipata vikombe viwili vya maziwa ya unga pamoja na matunda, karanga ama matunda jamii ya maembe yaliyopatikana msituni.

Kwa hali hii ya maandalizi magumu nilijiweka tayari kwa Hija. Kutembea katika njia za barabara kulionekana kama ni jambo jepesi. Ukilinganisha na maandalizi ambayo nilikuwa nimeyafanya.

Ni uzuri ulioje kula matunda yaliyoiva yenye ladha mbali mbali kutoka kwenye miti na mboga za majani kutoka msituni! Na tungelipata faida kiasi gani kwenye kilimo huko tuendako kama tungesisitiza matumizi ya vyakula ambavyo havitupatii sumu itokanayo na viwanda. Kwa hiyo chakula kingeweza kupatikana kutoka mashambani kutokana na mimea.

Siku moja asubuhi nilipata kifungua kinywa cha matunda yaliyokuwa na umande ambayo niliyachuma toka vichakani wakati nilipokuwa ninapita kwenye milima ya " New England."

Nilijilinganisha na watu wengine ambao huwa wanakula vyakula vilivyoandaliwa vyenye ladha mbalimbali na niliweza kufahamu kuwa ningelifanya uchaguzi wa mlo wangu wa asubuhi katika vyakula vilivyoko duniani, nisingeliweza kuchagua kingine isipokuwamatunda pori yaliyozungukwa na umande.

Nyakati za vuli na masika wakati mchana huwa mrefu, ni furaha ilioje, kuamka jua likiwa linawaka na kwenda kulala likiwa bado linawaka. Wakati wa baridi mchana unapokuwa mfupi unaweza kuufurahia usiku. Naelekea kukubali kuwa kuna chembe chembe fulani katika hewa, zilizoachwa huko kutokana na jua. Na pasipo jua haziwezi kuwapo na zinaweza kuingia mwilini iwapo utakuwa umelala. Kulala saa tatu na kuamka saa kumi na moja ni muda mzuri kwangu mimi.

Ni uzuri ulioje kufanya kazi katika hewa iliyo safi chini ya jua litoalo uhai ndani ya mazingira mazuri ya asili. Wako wengi wanaofahamu hili mfano kijana mmoja mdogo niliyekutana naye ambaye maisha yake yalikuwa yamekatizwa na mipango ya Hija. Alipokuwa hayupo nyumbani baba yake aliyekuwa hana uwezo alishindwa kulitunza shamba na ikabidi liuzwe. Kijana huyu sasa ilimbidi kufanya kazi kwa chuki ya kulipoteza shamba akiwa na lengo la kununua shamba lingine. Ni uzuri ulioje kufanya kazi kuiwezesha mimea ikue ili watu wapate chakula. Kwa maneno mengine ni uzuri ulioje kufanya kazi kikamilifu katika mazingira unamoishi! Ni wajibu wa kila mmoja hali kadhalika kwa jamii yoyote yenye afya.

Nguo zangu ni kamilifu kwa kazi yoyote. Ninavaa nguo nyepesi, shati ya mikono mirefu na suruali pamoja na suti yangu ya kisibau yenye maandishi. Pembeni mwa vazi langu hili upande wa mbele na nyuma kuna sehemu zinazoshirikiana zinazotumika kama mifuko. Mifuko hii hushika vitu vyangu vidogo vidogo vikiwemo, chanuo, mswaki wa kukunja na kalamu, ramani na kumbukumbu zangu pamoja na barua.

Unaweza ukaona jinsi niwezavyo kujibu taarifa zangu haraka kuepukana na mifuko yangu kutuna. Kauli yangu ni; " Kila wakia ina hesabu yake." Ndani ya nguo zangu za nje ninavaa nguo za riadha na shati la mikono mifupi. Kwa hiyo

wakati wote nimejiandaa kukabiliana na matatizo yasiyotegemewa mfano kuogelea nikikuta ziwa ama mto uliofurika.

Baada ya kuvaa nguo zangu nyepesi nilipokuwa nimekwisha kuogelea kwenye ziwa lililokuwa kwenye milima kimoja niliwaza jinsi watu wengine walio na nguo nyingi wanavyozitunza na wanavyoweza kusafiri nazo.

Nilishangaa jinsi watu wawezavyo kujipa mzigo kiasi hicho wakati mimi nilijisikia huru. Angalia nilivyo huru! Huyu ni mimi pamoja na mali yangu yote. Fikiria nilivyo huru. Kama nikitaka kusafiri, ninainuka na kuondoka. Sina jambo la kunizukawiza.

Nguo moja ya nje inanitosha.

Nimekuwa nayo moja tangu nianze safari ya Hija mwaka 1953. Ninatunza vitu vyangu vizuri. Huwa ninapata mahali pa kufulia kwenye chumba cha mapumziko katika nyumba ya wageni ama kwenye eneo lolote lililo na maji. Kuzikausha pia huwa ni rahisi. Ninazivaa na kuacha joto la jua kuzikausha zikiwa mwilini.

Ninaoga kwa kutumia maji tu. Sabuni huondoa hali ya mafutaya asili kwenye mwili, vile vile manukato na mafuta ya kujipaka ambayo wanawake wengi hutumia.

Viatu ninavyopendelea ni viatu vya bei rahisi vya raba za bluu. Ni laini kwa juu na kwenye kisigino chake. Huwa ninachukua vikubwa zaidi ili kuweza kuchezesha vidole vyangu ndani yake wakati ninapovivaa. Ninajisikia niko huru kama vile sikuvaa viatu! Ninaweza kutembea maili elfu moja na mia tano ambazo ni sawa na kilometa elfu mbili na mia nne kwa jozi moja. Ninavaa soksi za bluu. Sababu inayonifanya napendelea rangi hiyo ni kwa jinsi inavyohimili mazingira tofauti na haionyeshi uchafu na pia ni ishara ya Amani ya kiroho.

Huwa situpi vazi lolote hadi lifikie kiwango cha kutoweza kutumika tena. Kuna wakati nilikuwa ninaondoka mjini, mhudumu mmoja akaniita na kuniambia " Mpenda Amani, viatu vyako vinahitaji ukarabati," na ningeweza kujitolea gharama wakati nilifahamu sana juu ya ukarabati wa viatu kiasi kwamba viatu vyangu visingeliwezekana tena kukarabatiwa. Nilimjibu kuwa hilo ni jambo zuri. Ninajua kidogo kuhusu ushonaji kiasi kwamba sikujua kuwa viatu vyangu visingekarabatiwa. Hivyo nimemaliza ukarabati hivi sasa.

Kwenye miaka michache ya mwanzoni nilivaa kitambaa cha bluu cha shingoni pamoja na sweta ya bluu wakati wa baridi lakini baadae niliviacha, nikaona siyo muhimu. Kwa sasa ninakwenda na mazingira ninavaa nguo zile zile, iwe joto, baridi, ndani ya nyumba au nje.

Kama ndege wakati wa masika ninahamia ukanda wa kaskazini na wakati wa kipupwe ninahamia kusini. Ukitaka kuzungumza na watu wa nje ni lazima uwe nao pale ambapo hali ya hewa inawavutia vinginevyo watu hawatatoka nje ya nyumba zao.

Wakati kuna jua kali na joto linakuwa limepanda hakuna kitu kizuri kama kivuli. Kuna ubaridi mzuri chini ya kivuli cha mti. Lakini kama si mti mkubwa itakubidi kuhama kusogea na kivuli. Mawingu hutoa kivuli kadri yanavyosogea angani.

Jabari la jiwe hutoa nikiitacho kivuli kizito vile vile wakati wa asubuhi, kwenye mawio ya jua na jioni wakati wa machweo ya jua. Wakati mwingine hata kivuli cha kichaka kinafaa pia. Vitu vilivyotengenezwa na binadamu vinatoa kivuli pia.

Majengo na alama zilizowekwa kuonyesha hali ya ardhi. Madaraja husaidia kujikinga na mvua. Inawezekana mtu akavaa kofia ama akachukua mwavuli. Mimi sifanyi hivyo. Siku moja mwandishi wa habari aliniuliza iwapo nilikuwa na mwavuli wa kukunja katika mfuko wangu nilimjibu kuwa; " Siwezi kuyeyuka ngozi yangu inahimili maji." Sijali kuhusu mapungufu madogo madogo." Lakini wakati mwingine nimekuwa nikitumia kipande chepesi cha ubao kujikinga baridi.

Maji ni kitu cha kukumbuka wakati wa joto kali, lakini nimegundua kwamba nisipokula chochote isipokuwa tunda siwezi kuhisi kitu hadi niyamalizapo matembezi yangu kutwa hiyo.

Mahitaji yetu kimwili ni rahisi mno.

Baada ya matembezi yangu mbali na maeneo yenye watu, ninakumbuka nilipokuwa ninatembea kwenye barabara moja mashuhuri ambayo niliizoea kama nyumbani kwangu kwa kipindi fulani ndani yajiji moja maarufu.

Ilikuwa majira ya saa 7.00 mchana, watu wengi waliovalia vizuri wenye nyuso mbali mbali zilizopauka na zingine zilizoonekana kurembwa walikuwa wakifuatana haraka haraka wengine wakienda na wengine wakirudi makazini kwao. Nilipita kati yao nikiwa na nguo zangu zilizochoka. Viatu vyangu vya raba vyenye soli laini vilitembea pasipo kutoa sauti katika kelele mbali mbali zilizotolewa na miondoko mbali mbali ya viatu vyenye soli ngumu na visigino virefu.

Kwa namna nilivyoonekana, kwenye kundi la watu maskini nilivumiliwa. Na kwenye kundi la matajiri, mbele yao nilionekana kitu cha kushangaza na kwa wengine nilidharauliwa.

Kadri tulivyopita mbele yetu kulipangwa vitu mbali mbali kwa yeyote aliyetaka kununua. Vitu hivyo viliuzwa kwa kwenda na wakati. Kila siku na kila mwaka kulikuwa na mitindo mipya ya vitu. Vingine ukiangalia havina umuhimu wowote. Vingine ni vya ziada tu. Vingine ni kwa ajili ya urembo na vingine havivutii kabisa. Vitu aina mbali mbali viko kwenye maonyesho lakini rafiki zangu kitu muhimu sana kimekosekana. **Uhuru, Afya, Furaha wala Amani ya akili bado kabisa havijaenezwa.**

Rafiki zangu, kuvipata vitu hivi utaweza kukwepa hali hii ya mashindano lakini ukubali kudharauliwa.

Katika ulimwengu ningeweza kuonekana masikini sana, nikitembea bila fedha mfukoni mwangu nikiwa nimebeba vitu muhimu tu lakini ni tajiri wa baraka ambazo haziwezi kununuliwa kwa kiasi chochote kile cha fedha yaani afya, furaha na Amani ya milele.

Maisha yasiyo na makuu
Ni maisha matakatifu,
Uzidivyo kuwa mtulivu,

ndivyo upunguzavyo ugomvi,
Oh, maajabu yaliyoje,
Ukweli kuufichua,
Miradi iliyoshindikana kabla,
Sasa inafanikiwa,
Oh, maisha mazuri yaliyoje
yale yasiyo na makuu.

## SURA YA SITA

### *UTATUZI WA MATATIZO YA MAISHA*

Dhumuni la matatizo ni njia ya kumuongoza mtu kuwa mtiifu wa sheria za Mungu ambazo ni halisi na hazibadiliki milele. Tunao uhuru wa utashi, kuzitii au kutozitii.

Na kuzitii daima hutufikisha kwenye upatanisho na maisha matakatifu. Na kutozitii hutuingiza kwenye matatizo zaidi ya maisha.

Watu binafsi wanaweza kugundua kwamba, hawawezi tu kukua kiroho na kujifunza kutokana na matatizo yawapatayo katika ubinafsi wao, bali wanaweza kujifunza na kukua kiroho kutokana na utatuzi wa matatizo kwa ujumla yanayoikabili jamii. Vilevile wakati jamii huwa nje ya upatanisho matatizo hukua ndani ya jamii hiyo. Mkusanyiko wa matatizo ni njia ya kuweka msukumo kwenye jamii kuelekea kwenye upatanisho. Mtu binafsi atagundua kwamba hawezi kujifunza kuyatatua matatizo yampatayo mpaka asongwe na mkusanyiko wa matatizo. Mara nyingi mimi husema kuwa nimeondokana na matatizo yangu binafsi. Mara kwa mara mimi husema nimeondokana na matatizo yangu binafsi, hapo mara moja katika kipindi fulani tatizo moja dogo laweza kujitokeza mahali. Lakini mimi silitambui kuwa ni tatizo kwa sababu kwangu si muhimu. Hasa nataka kufanya mafunzd yangu yote na ukuzi wangu kiroho kwa kusaidia utatuzi wa mkusanyiko wa matatizo katika jamii.

Kuna muda ambapo nilifikiri kuwa ni jambo la upuuzi kupambana na utatuzi wa tatizo nilijaribu kuliondoa tatizo hilo. Nilijaribu kutafuta mtu wa kunitatulia matatizo hayo. Kipindi hicho ilikuwa zamani sana. Ilitokea siku ya maana sana katika maisha yangu nilipoligundua dhumuni la ajabu ni kwa nini watu wanapatwa na matatizo. Kweli, wanalo dhumuni la ajabu. Baadhi ya watu hutamani maisha yasiyo na matatizo. Lakini kamwe sikuombei uwe na hali isiyo na matatizo maishani mwako. Nikitamanicho wewe uwe nacho ni ile nguvu ya kiroho ndani mwako iwezayo kukutatulia matatizo endapo yatakutokea. Kupatwa matatizo ni kujenga uzoefu wa kupambana na maisha na pia ni fundisho la maisha kwako. Maisha bila matatizo yamefungwa hivyo hayana njia ya kumkuza mtu kiroho.

Niliwahi kukutana na mwanamke mmoja ambaye aliishi bila ya kukutwa na tatizo lolote. Nilikuwa katika kituo cha magari ya abiria nikisikiliza kipindi cha mwisho cha usiku kwenye redio jijini New York. Nilitegemea kulala pale kituoni. Mwanamke huyo alipiga simu pale kituoni, akiwa ananitaka niende kwake kulala. Nilimkubalia. Baadae alimtuma dereva wake akaja na gari kunichukua. Nilipofika kwake nilijikuta ndani ya jumba moja la kifahari, la watu wenye mamilioni ya fedha. Mle ndani nilikutana na mwanamke mwenye umri wa kati aliyeonekana kama mtoto mdogo kwa hali aliyokuwa nayo.

Alionekana mchanga kimawazo, nikawa ninajiuliza kwa nini yuko vile. Baada ya kuwa nimekaa naye kwa muda fulani niligundua kwamba alikuwa amekingwa na ngao ya kutokukutwa na matatizo.

Alizungukwa na kundi la watumishi aina aina pamoja na wanasheria. Alikuwa hajawahi kukutwa na mafundo ya matatizo ya maisha, hakuwa na matatizo ya kumkuza kiroho. Hivyo alikuwa bado hajakomaa. Matatizo hukugeuzia baraka!

Kama ningejitolea kutatua matatizo ya watu badala yao wangedumaa, wasingekua kiroho asilani! Mwelekeo wangu ni kutatua chanzo cha matatizo yao badala ya matokeo. Ninaposaidia wengine huwa ninaweka chachu miongoni mwao iwasukume kutatua matatizo yao binafsi. Ukimpa mtu mwenye njaa chakula, utamlisha kwa 'siku moja lakini umfundishapo kulima utakuwa umemlisha kwa kipindi chote cha maisha yake.

Ni katika kuyatatua matatizo kwa usahihi tukuapo kiroho. Kamwe mtu habebeshwi mzigo ambao hana uwezo wa kuutua. Kama kuna tatizo kubwa linalokupata lazima unazo nguvu za ndani za kupamabana nalo. Hakuna jambo liwezalo kukukatisha tamaa, kwa sababu matatizo ni njia ya ukuzi wa kiroho na kadri matatizo yawavyo makubwa ndivyo na kukomaa kwako zaidi kiroho.

Ugumu tuupatao kutokana na kuwa na vitu vya kumiliki, mara nyingi hutukumbusha kujitakasa kiroho badala ya kufikiria vitu vya duniani tu. Wakati mwingine matatizo yatupatayo kutokana na mwili hututambulisha kuwa mwili ni kama vazi tu, linalosetiri nguvu fulani iendeshayo vazi hilo. Lakini itokeapo tukasema; " Ahsante Mungu kwa matatizo yetu yatuwezeshayo kukomaa kiroho, huwa kwetu siyo matatizo tena, humalizika hapo hapo."

Hebu nikwambie hadithi ya mwanamke aliyekuwa na tatizo binafsi. Daima aliishi na maumivu moyoni mwake. Alikuwa na maumivu ya mgongo. Ninaweza kukumbuka nilivyomuona akikusanya mito mbali mbali ili auegemeze mgongo wake kupunguza maumivu. Kwa kweli alikuwa na maumivu makali. Nilimueleza maisha kuhusiana na matatizo yawapatayo wanadamu kuwa ni njia ya kuwaongoza kumfikiria Mungu badala ya kuyafikiri matatizo yake. Kwa kiasi kikubwa nilifanikiwa, kwani usiku mmoja badae alipokwenda kulala, mawazo yake yote yalikuwa kwa Mungu.

" Mungu yu karibu nami, mtu kama mimi ambaye ni chembe ndogo ya vumbi ananipa matatizo ya kuniokoa nikue kiroho, " alianza kufikiri. Alimgeukia Mungu akasema; " Ooh, mpendwa Mungu, ahsante kwa haya maumivu ambayo yataniwezesha kukua ili niwe karibu nawe." Hapo hapo maumivu yake yalitoweka mara moja na hakuweza kuyasikia tena. Labda hii ndiyo maana yake tusemapo; " **Shukuru kwa lolote likutokealo.**"

Ni vema mara kwa mara tusali sala ya kumshukuru Mungu kutokana na yale yatupatayo yaliyo mabaya. Sala ni shinikizo la mawazo mema.

Matatizo mengi yaliyo ya kawaida husababishwa na matendo mabovu. Watu hujiona wenyewe kama kitovu cha mbingu na nchi na hujichukulia uamuzi kwa lolote linalohusiana nao. Kwa asili huwezi kuwa na furaha.

Daima utakuwa na furaha ukishaona mambo yanakwenda kwa utulivu. Binadamu wote ni sawa mbele ya Mungu na wanayo majukumu katika mpango wa kiroho.

Nitakupa mfano wa mwanamke mmoja ambaye alipata ugumu katika kutambua wajibu wake kwenye mpango wa kiroho.

Alikuwa na umri wa miaka arobaini, hana mume na bado alihitaji matumizi katika maisha yake. Aliichukia sana kazi aliyokuwa akiifanya kiasi kwamba, aliweza hata kuugua. Ilimbidi kumuona mtaalam wa magonjwa ya akili ambaye alimwambia kwamba angemsaidia katika matatizo yake ya kikazi. Ingawaje aliendelea na kazi yake bado hakuipenda. Baadae alilazimika kuniona. Nilimwuliza ni nini ulikuwa wito wake wa kazi. Alinijibu kuwa hakujisikia kuwa na wito wowote.

Hiyo haikuwa kweli. Kile ambacho hakukielewa ni kwamba hakujua ni wito gani.

Nilimwuliza aniambie kile ambacho alihitaji kukifanya kwa moyo mweupe wenye furaha kama vile mimi nilivyofanya shughuli za hija. Niligundua alihitaji kufanya mambo matatu. Alihitaji kupiga kinanda- aina ya piano, ingawa hakuwa na utaalam kamili, alipendelea uogeleaji ingawa hakuwa na utaalam wa kazi hiyo, na la mwisho alipenda kushughulikia maua.

Nilimtafutia kazi kwenye duka la maua ili aweze kujipatia kipato kwa kufanya kazi ya maua. Aliipenda kazi yake vilivyo. Alisema angeweza kuifanya hata bila kuhitaji malipo. Lakini tulitumia vitu vingine pia. Kumbuka kuwa alihitaji kupata liziki.

Aliendelea kuhitaji mambo mengine kama kufanya mazoezi ya uogeleaji pamoja na upigaji kinanda. Alianza kupiga na kucheza nyimbo mbalimbali akiwa na watu wanamsikiliza, pia wakawa wanashirikiana naye kuimba na mwishowe akawa anafanya vizuri. Mambo yote matatu aliyoyahitaji yalimfanya akarudia afya yake, akapendeza. Mwaka mmoja baadae aliolewa akaishi maisha ya starehe.

Ninamkumbuka mwanamke mwingine aliyekuwa amezoea kujifungia chumbani mwake kwa kipindi fulani. Niliingia chumbani mwake na ninaweza kusema kwamba hali aliyokuwa nayo kiafya haikuonyesha uzima hata kidogo.

Sikumbuki kama niliongea naye kwa muda wa dakika tano kabla hajanieleza yote kuhusiana na matendo mabaya aliyokuwa anatendewa na dada yake. Maelezo yake yalionyesha uchungu mkubwa dhidi ya dada yake ambaye aliishi naye. Nilijikuta ninamueleza kwamba kama angesamehe yote aliyokuwa ametendewa, na yeye pia amuombe msamaha na afanye suluhu ya amani na dada yake angejikuta anaridhisha nafsi yake na kujenga upya afya ya mwili wake.

**" Eh!" Alistuka**

" Afadhali nife kuliko kuyafanya hayo." Alisema.

" Hujui huyo dada yangu alivyokuwa " aliongeza. Hali yake iiendelea hivyo mbaya mbaya.

Lakini siku moja asubuhi kwenye majira ya mapambazuko ya jua, mama mteswaji aliandika barua nzuri kwa dada yake ambayo alinionyesha. Niliichukua ile barua mara moja nikaipeleka posta ili itumwe kabla ya mwandishi hajabadili mawazo yake. Niliporudi kutoka posta nilikuta amebadili mawazo hivyo nilikuwa nimefanya vizuri kuipeleka mapema. Alionyesha kuwa na wasi wasi kidogo. Majibu yaliporudi kutoka kwa dada yake yalikuwa mazuri yenye kuleta suluhu kwa dada mtu. Siku hiyo hiyo barua ilipowasili, mama huyo akawa amepata nguvu za kunyanyuka kitandani akatembea tembea nje ya nyumba. Mara yangu ya mwisho nilipomuona alikuwamwenye furaha na afya njema. Kuna msemo usemao kuwa *" chuki humuumiza mchukiaji na wala siyo mchukiwa."*

Baadhi ya watu hutumia muda mchache kuwatafuta wenzi wao wa maisha kuliko wanavyotumia muda kuyatafuta magari. Wengi wanaangukia katika mahusiano kama haya.

Hakuna mtu awezaye kuingia kwenye taratibu za maisha ya familia labda awe na wito kama ule nilioupata wa shughuli za hija. Vinginevyo matokeo yake yatakuwa ya masikitiko. Ninaweza kumkumbuka mwanamke mmoja ambaye hakuelewana vema na mumewe; niliona hawakuwa na lolote. Hatimae nilimuuliza; " Kwa nini uliamua kuolewa na huyu bwana?"

Alinijibu kuwa shoga zake walikuwa wamewapata wanaume wa kuwaoa wakati huo akawa ameona huyo ndiye aliyekuwa karibu naye akamuoa. Haya hutokea mara kwa mara. Je, unajiuliza kwa nini kuna uvunjwaji wa ndoa nyingi? Watu huingia katika taratibu za familia kabla ya kufikia wito wake.

Hisia wakati mwingine huweza kuwa hatari kwa mwanadamu. Nilipokuwa nikishughulika na watu wenye matatizo mara kwa mara niligundua kwamba wengi wao walikuwa na matatizo yatokanayo na hisia ambazo zilihitaji kuondolewa kwao. Mmojawapo wa watu hao alikuwa msichana wa umri wa miaka kumi na sita. Kwa sasa hivi anaweza kuwa mwanamke mwenye furaha kwenye ndoa yake. Nilizoea kusema kuwa muda hutibu madonda yote. Lakini msichana huyo alifikiria kwamba moyo wake ulivunjika wakati alipoachwa na mchumba wake, ambaye aliamua kuoa mwanamke mwingine.

Ingawaje ilimchukua muda mrefu kupambana na machungu hayo baadae aliyaona kuwa ni matatizo ya kifalsafa amabyao humalizwa na umri wa muda kuwa mrefu. Mara nyingine watu huwa rahisi kusahau wanapofiwa na wale waliowapenda kuliko wanapoachwa na wale waliowapenda.

**KUWA KWENYE TABIA YA MASHAKA:**

Ishi siku ya leo! Jana ni ndoto; na kesho ni ono, lakini waishio vema leo kila jana yake itakuwa ndoto ya furaha kwao na kila keshoye ono lililo na tumaini. Kamwe usiishi kwa machungu ya yale yaliyopita na wala kuwa na mashaka na wasiwasi kwa yale yajayo. Ishi leo na ishi vema.

Mashaka ni tabia. Ni kitu ambacho waweza kukifanyia kazi. Ninaiita uondoaji wa tabia ya mashaka. Kuna njia zinazosaidia kuondoa tabia ya aina hiyo. Ninaongea na watu wa makanisa na ninagundua kwamba bado wanayo mashaka kwenye maisha yao. Hakika ni upotezaji wa muda na nguvu zao. Kama wewe ni muombaji ambaye anasali kwa imani, mara moja ungechukua yale yote yakupayo mawazo na mashaka umkabidhi Mungu kwa njia ya sala na uyaache mikononi mwake; mikono ambayo inawezekana. Huu ndio ufundi bora uwezao kuutumia. Mwanzoni utafanya maombi hayo kwa kurudia katika tatizo moja kabla hujaikuza ile tabia (ambayo kwangu imekua).

Mara ngapi unawaza mambo ya sasa? Ya sasa kwa kawaida ni safi. Kama unawaza waweza kuwa unaumizwa na yaliyopita ambayo ungekuwa umesahau muda mrefu uliopita ama unasumbuliwa na yajayo ambayo hata hayajafika. Tuyazingatie ya sasa ambayo muda huu Munguametukabidhi tushughulike nayo. Kama hushughuliki na sasa hivi tutaweza kuyazoea maisha uishiyo. Na kama unashughulika na ya sasa hivi tu, maisha yako hayawezi kuwa na wasi wasi na mashaka. Kwangu mimi kila wasaa ni muda mpya wenye msisimko mpya wa furaha kwa shughuli zangu.

## KUWA NA TABIA YA HASIRA:

Hapa nitataja tabia zingine mbili. Mojawapo ni tabia ya hasira. Nguvu za ajabu huja na hasira. Mara nyingine huitwa nguvu za hasira. Usiifiche moyoni nguvu hii ya hasira, ili kwamba; isije ikakudhuru kwa ndani, yaani ikaudhuru moyo wako. Usiionyeshe kwa watu isije zaidi ya kukudhuru pia ikakutangazia jina baya kwenye jamii inayokuzunguka. Uwezacho kukifanya ni wewe kuibadilisha ile nguvu ikusaidie kufanya shughuli ziwezazo kukuletea maendeleo.

Njia nzuri ni kukueleza mambo ambayo watu wenye nguvu hii waliyafanya. Mfano, mwanamke mmoja, yeye aliosha madirisha yote ya nyumba, mwingine alisafisha vumbi kwenye nyumba hata kama ilikuwa safi kabla ya hapo, mwingine alioka mikate, mwingine alipiga kinanda na kadhalika. Yote hayo yalifanyika wakati wakiwa na hasira.

Kuna mwanamume mmoja aliyetumia chombo cha kufyekea nyasi ambacho hakikutumia injini, hivyo alitumia nguvu zake kuifanya kazi hiyo. Niliishi jirani naye. Nilipomuuliza jinsi alivyokitumia, alinijibu; " Oh, bila kuwa na nguvu ya hasira nisingeweza kukisukuma chombo hiki. Unaona? Ni nguvu za ajabu!"

Pia alikuwepo bwana mwingine aliyeiokoa ndoa yake. Alikuwa na hasira kiasi kwamba alipokuwa anakasirika anatumia nguvu zake kusambaza vyombo ndani hata mke wake alikuwa tayari kumkimbia pamoja na watoto wake. Mara alipoligundua tatizo hilo aliamua kuwa anaimaliza hasira yake, kwa kuruka ruka, kugonga ukuta na mengine mengi ambayo yalipunguza nguvu zake wakati huo. Nilipokutana naye

baada ya miaka; nilimuuliza kama bado alikuwa anaendelea na tabia yake ile ya kurukaruka na kugonga vitu ili kuipunguza hasira. Alijibu kuwa alikuwa anaendelea kidogo kidogo kama njia ya kufanya mazoezi kwa ajili ya ujenzi viungo. Alisema kuwa hasira yake ilikuwa imeisha miaka mingi. Kadri unavyotumia hasira kwa mabo ya kujenga ndivyo kadri uimalizavyo.

Ufundi huu unatumika hata kwa watoto. Ninamkumbuka mtoto mmoja wa kiume aliyekuwa na umri wa miaka kumi. Nilikuwa ninajaribu kumsaidia mama yake kwa sababu alikuwa na wakati mugumu kumdhibiti. Alikuwa na tabia ya kupandwa na ahsira hadi anapagawa. Na siku moja alipokuwa katika hali yake ya kawaida isiyo na hasira, nilimwuuliza; " Katika mambo yote uyafanyayo ni lipi likuchukulialo nguvu nyingi zaidi?" Alijibu; " Ninadhani kukimbia hadi juu ya mlima ulioko nyuma ya nyumba." Na hapo tulipata ufumbuzi wa ajabu. Kila wakati mama yake alipokuwa akiona dalili ya hasira usoni mwa mtoto huyo, alimtoa nje ya nyumba na kumuamuru akimbie hadi juu ya mlima. Mafanikio yalipatikana kiasi kwamba, wakati fulani mwalimu mmoja wa shule aliniambia kwamba alikuwa na tatizo kama hilo kwa mtoto mwenye umri kama wa yule wa kwanza, nilimshauri awe anamuamuru mtoto huyo akimbie kulizunguka eneo la shule mara amuonapo kuwa na hasira. Mpango huo pia ulifanikiwa.

Sasa nitakueleza kuhusu watu wengine wawili bwana na bibi. Waliweza kukasirika kwa wakati mmoja, hivyo wakaazimia kutembea kulizunguka jengo. Kila mmoja alichukua njia yake na wakati walipokutana kwa amani walitembea kurudi nyumbani wakijadiliana kuhusu jambo lililosababisha hasira zao na ni hatua zipi wangezichukua kutibu tatizo hilo baadaye. Hili lilikuwa jambo la busara kwao. Usingeweza kuongea na mtu aliyekasirika, kwa sababu mtu huyo kwa wakati huo huwa hana busara.

Nitakueleza habari nyingine moja kuhusu amam mmoja aliyekuwa na watoto watatu ambao walikuwa bado kuanza shule. Alisema; " Ninapokasirika hujisikia kutaka kukimbia, lakini ninashindwa. Siwezi kukimbia na kuwaacha watoto wangu wadogo. Na kwa kawaida huwa ninaimaliza hasira hiyo kwa kuiondoa kwa ajili yao."

Nilimwabia; " Ulishajaribu kukimbia kimbia uwapo na hasira? " Na baadaye niliweza kumuona akikimbiakimbia.

Aliniandikia akisema; " Amani, nimefanikiwa kiajabu. Shughuli hiyo si kwamba tu inaondoa nguvu ya hasira bali inawafurahisha pia na watoto wangu."

## KUWA NA TABIA YA UOGA:

Woga nao ni tabia. Woga waweza kufundishwa kwa mtu. Tabia hii huendelezwa daima. Mimi siyo muoga. Mungu daima yuko pamoja nami. Nilikuwa na rafiki yangu ambaye alikuwa na tabia ya kuogopa aina fulani ya watu. Mumewe alikuwa mfanyakazi alihamishiwa sehemu nyingine ambako mwanamke huyo alijikuta anaishi na wale ambao alikuwa akiwaogopa. Nilifanya naye kazi na baadae akawa amezoea muziki uliokuwa ukipigwa na wenyeji wa pale kwani alikuwa mwanamuziki mzuri. Pia nilikutana na mwanamke mwingine aliyekuwa na watoto

wawili wenye umri sawa na watoto wa rafiki yangu wa kwanza. Hivyo tulikwenda kumuona. Wale watoto wawili wavulana na wale watoto wawili wasichana walianza kucheza pamoja na sisi tukawa tumeendelea kuzoeana. Kusema kweli baadae walikuwa marafiki wakubwa. Ninaikumbuka siku waliyoamua kwenda kusali kwenye kanisa ambalo alikuwa akisali mmoja wao. Walijenga urafiki kiasi kwamba ilibidi Jumapili moja waende kusali kwenye kanisa la mmoja wao na vivyo hivyo Jumapili nyingine kwa mwingine. Baadae waligundua kuwa walikuwa wakipendelea mambo yaliyofanana. Lilikuwa jambo la kupendeza kwamba walipokuja kufahamiana waligundua kwamba mambo waliyokuwa wakiyapendelea yalikuwa makubwa sana kuliko tofauti zao. Ilitokea wakapendana mara baada ya jambo hilo kugundulika.

Ninamfahamu msichana mmoja aliyekuwa profesa wa Kiingereza kwenye chuo fulani. Wakati wowote ilipotokea ngurumo ya radi toka mbali alipagawa kwa woga. Wakati alipokuwa msichana mdogo mama yake alizoea kukimbia pamoja na watoto wake hadi uvunguni mwa kitanda mara aliposikia ngurumo. Huu ni mfano mzuri ulioonyeshwa jinsi watoto wafundishwavyo uoga.

Ilivyo ni kwamba kila woga huwa ni woga kwa yale yasiyojulikana. Nini liwe suluhisho? Jibu, ni wewe kuyajenga mazoea na kitu kile ukiogopacho. Ilibidi tujifunze kanuni za usalama kabla hatujayajenga mazoea na mwanga wa radi, na hii inafanikiwa.

Nitakueleza habari nyingine ihusuyo uoga. Nimesikia kuwa wapo wanawake waogopao panya. Na mimi binafsi nimewaona wanawakena wanaume waogopao mbwa. Lakini mwanamke ninayekuambia habari zake ni muoga wa paka. Sisemei paka mwitu, la hasha. Ni wale wa kawaida tuwafugao nyumbani. Sasa kulikuwapo na paka jirani na eneo alikoishi huyo mwanamke. Rafiki zake wote walifuga paka. Wakati wowote alipomuona paka akimsogelea alipiga yowe, akakimbia hadi kupagawa kwa woga. Alinieleza kuwa yeye alifikiri kwamba kila paka aliyemsogelea alikuwa tayari kumrukia kooni. Sasa, mwanasaikolojia, anasema kwamba wakati mwanamke huyo alipokuwa mtoto mdogo alitishwa na paka hivyo woga huo haukufutika mawazoni mwake. Yaweza kuwa kweli. Nilimshauri kwamba, kama angependa kuondokana na woga wa paka ilikuwa vema azoeane nao. Hilo wazo langu alilikataa kata kata! Niliendelea kumuuliza kama alikuwa anamuogopa mtoto wa paka na akajibu kwamba kama bado ni wadogo hawaogopi. Ilinibidi nitafute kitoto kichanga cha paka nimletee. Nilimuomba akitunze, acheze nacho akizoee. Matokeo yake, kitoto hicho kilikua akawa paka mkubwa. Akaishi naye nyumbani, akawa ameuacha uoga wa paka.

Woga mwingine humpata mtu kutokana na matukio yaliyopita. Kwa hakika tatizo la mwisho nililolizungumzia chanzo chake kinaweza kuwa hicho. Na woga huo unashughulikiwa kwa njia hiyo hiyo. Ni kiasi cha kujenga mazoea na yale uyaogopayo.

Yapo maeneo machache ambayo unaweza kutumia chache za kuukabili uoga. Nitakueleza shauri moja la uoga ambalo tulilimaliza kwa njia za taratibu. Mwanamke mmoja alikuwa muoga wa kulala ndani ya chumba kidogo, aliweza kuingia ndani ya chumba chochote kidogo, lakini; alishindwa kulala mle mwenyewe! Woga wake huo ulitokana na matukio yaliyopita. Alikuja sehemu nilikokuwa nikifanya kazi ili kuniomba msaada. Tulimtengea kitanda cha kulala kwenye maktaba ili alale. Bado akawa anaogopa. Niliamua kulala kitanda jirani naye na bado akawa muoga. Baada ya kuwa amezoea kulala mwenyewe mle mwenye maktaba, tulitenga kitanda kidogo kwenye ukumbi wa chakula ili alale. Na mimi nililala jirani naye kwenye kitanda jirani. Taratibu aliendelea kuzoea na mwishowe akawa ameweza kulala mwenyewe kwenye chumba kidogo pasipo woga.

Si muhimu kutumia njia hizi za taratibu. Tulifanya hivyo kwa sababu zipo aina chache za uoga ambazo ni rahisi kuzishughulikia kwa kutumia mbinu za taratibu.

Upo woga mwingine wa kuogopa urefu wa kimo, na hii pia hutokana na matukio yaliyopita. Ebu, nikueleze kuwa vijana wadogo wenye juhudi huogopa urefu wa kimo. wadogo. Njia niliyoitumia kuwasidia watu wenye tatizo hili ilikuwa kuwapandisha taratibu hadi eneo ambalo waliona wao linafaa kufikia. Siku nyingine tunapanda ngazi kuelelkea eneo la juu kidogo zaidi. Tunaendelea kila siku na mwishowe kujikuta wamezoea kukwea maeneo ambayo hapo awali waliyaogopa.

Nimekuwa nikiulizwa kama aina fulani ya woga unatokana na ulinzi wa afya ya mtu. Sikubaliani Sifikiri kuwa kuna aina yoyote ya uoga utokanao na ulinzi wa afya ya mtu. Labda kama unaongeaukweli kwamba kama unaihofu barabara ya mtaa fulani, itakulazimu utazame mbele chini kabla hujavuka barabara hiyo. Lakini unaona, mimi ninaamini kwamba tunatakiwa kufanya lolote liwezekanalo kuhusiana na maisha yetu, kwa hiyo ninapotoka nyumbani kuingia barabarani daima lazima nitazame juu na chini. Lakini hiyo siifikirii kuwa ni uoga. Hilo ni jambo la busara. Kwa namna yoyote ile siliunganishi na uoga. Mathalani, ninajua kwamba kama ninapita juu ya mwamba mwororo ambao juu yake kuna changarawe kidogo sana zilizosambazwa ninaweza kuteleza nikaanguka endapo nitazikanyaga changarawe zile. Hivyo, lazima niwe muangalifu wakati nikanyagapo. Huo siyo uoga. Hilo ni tendo lifanywalo kwa busara. Huo nao siyo uoga bali ni tahadhari.

<u>ULINZI WA MUNGU:</u>

Majuzi nilipokuwa ninaongoza kikundi cha watu kwenye mafunzo ya wokovu wa kiroho kwenye kimojawapo cha visiwa vinne vya Hawaii askari polisi mmoja alituonya tusilale kwenye ufuko wa bahari.

Ilionyesha kulikuwa kumetokea mauaji eneo lile. Nilijisikia kuguswa na hali ya woga ambayo watu walikuwa wameipata kuhusiana na mauaji yaliyokuwa yametokea eneo hilo. Mimi binafsi sikuwa na woga. Mmojawapo wa wale

nilioongozana nao alijaribu kunieleza hatari iliyokuwa mbele yetu. Nilimwambia kwamba sisi sote tuko chini ya ulinzi wa malaika anilindae. Tulilala pale na hatukutokewa na lolote.

Usiku mmoja tulikuwa pale ufukoni na tulionekana ni sisi tu tuliokuwa wageni. Watu kadhaa walinijia na mmoja wao akanisemesha; " Miaka michache iliyopita nilikuona kwenye televisheni."

Ninafikiri ilikuwa miaka mitano kabla sijaanza kutembelea visiwa vya Hawaii. Hivyo ninafikiri tusiwe waoga. Sifikiri kwamba uoga unaweza kufanya lolote isipokuwa huleta mvuto. " Lile nililoliogopa lilinijia." Nilijisikia salama kabisa pale ufukoni na nilihisi watu wangu wote nilioandamana nao wakilindwa na ndivyo ilivyokuwa.

Nimekuwa nikihisi ulinzi timilifu kwangu. Mara mbili nimejaribu kutaka kutoka ndani ya gari lililokuwa nimelipanda na niliona sababu mara moja. Sasa, sikuweza kutoka ndani ya gari wakati nilipokuwa ninakuja kuelekea kwenye shamba la mizabibu huko Los Angeles nikiwa na wanafunzi wawili wa Shule ya Sekondari. Walikuwa wanaangalia ni kasi gani gari aina ya Chevy ingeweza kuchukua katika kutelemka kile kilima. Mimi nilikuwa kwenye kiti cha nyuma na nilijisikia salama salimini; ingawa gari hilo lilikuwa likienda kwa mwendo mkali sana.

Siku moja nilikuwa na Bwana mmoja aliyekuwa anakunywa pombe. Kutokana na hali aliyokuwa nayo nilimuomba niliendeshe gari badala yake. Nilimuonyesha leseni yangu ya udereva lakini hakuniruhusu niliendeshe gari. Hivyo nilimuomba aniteremshe endapo tungefika kwenye njia panda ya barabara. Kutoka pale nilipanda lori dogo ambalo baada ya kunifikisha mbele kama mwendowa maili tano (sawa na kilometa nane) tulikutana na gari jingine dogo. Gari hilo ni lile nililokuwa nimepanda kwa mara ya kwanza. Lilikuwa limeserereka kwa kasi hadi likaugonga mti. Upande nilokuwa nimekaa hapo awali ulikuwa umevunjika kioo cha dirisha na paa ya gari kubonyea. Mara moja nikaona kwa nini nilihisi kutoka nje ya gari hilo. Dereva hakuumia sana japokuwa alikuwa na majeraha kiasi.

Siku nyingine nikiwa garini sikuona tukio lolote lakini nilijisikia kutaka kutelemka. Dereva mwenyewe aliendesha gari kwa fujo. Aliweza kupita kwenye mistari ya magari yaliyosimama kwa kupangana njia panda na kupishana na magari bila uangalifu. Mwishowe nilitelemka. Nilipanda gari jingine hivyo siyajui yaliyolipata hilo gari baadae.

Kwa hiyo ni vema kuchukua tahadhari uonapo dalili ya hatari lakini siyo ile ya woga wa kijinga ambayo watu wengine wanao. Angalia suala la woga kama vile vitisho vya kulala ufukoni. Waweza kutishwa hata ukashindwa kulala nyumbani kwako. Tazama ni wangapi wameuawa wakiwa ndani ya nyumba zao. Ama ukiona vema kulala kwenye nyumba za wageni, hivi ni wangapi hata wameuawa wakiwa kwenye nyumba za wageni. Hii yaweza kukufanya uwe na tabia ya kuchekesha yaani woga usio na maana.

Mimi ninajisikia kuwa na ulinzi kamili. Kama ningekuwa na mawazo ya mambo niliyoyaona kwenye yale magari nisingekubali kukilaza kikundi changu ufukoni. Hata hivyo nilijiona ninalindwa. Sikuwa na woga wowote. Nilijua sote tuko salama pale ufukoni.

Yapo mambo mengi ambayo hatuyaelewi kwa ukamilifu. Tunachokijua ni kwamba yanatokea. Mathalani, nimekuwa nikilindwa dhidi ya mambo ambayo yangenidhuru. Nilikuwa ninatembea kwenye njia nyembamba ambayo niliielewa kuwa ni nyembamba. Mbele yake miti ilikutana. Sikuweza kuona ni wapi nilikokuwa nikienda. Lakini, niliijua njia hiyo kutokana na kuifahamu siku nyingi. Na ningeliweza kuona mwisho wake. Sasa nilikuwa ninatembea kasi wakati kitu tuwezacho kukiita kama nguvu fulani kiliponisimamisha ghafula. Nina maana kuwa, nguvu hiyo ilikuwa kubwa kiasi cha kunisimamisha. Kisha nilianza kuondoka kwa mwendo wa taratibu kuona ni nini kilichokuwa mbele yangu. Na tazama, kulikuwepo na seng'enge imefungwa kuikinga njia hiyo. Kule mbele mwishoni mwa njia walikuwa wanakarabati uzio wa ng'ombe,jambo ambalo nilikuwa silijui. Na walikuwa wamekinga seng'enge ili kuwazuia ng'ombe wasisambae. Ningejigonga na kuumizwa na seng'enge kama nguvu hiyo isingenisimamisha. Tunao ulinzi mkubwa sana kuliko tunavyodhania.

Kitu muhimu zaidi kingine kilinitokea wakati nilipokuwa ninaendesha gari. Hivi sasa nimeacha kuitumia leseni yangu ya udereva. Lakini katika kipindi changu chote cha udereva, nilikuwa dereva mzuri na imara. Na gari mara kwa mara nililimudu vema. Kipindi hiki nilikuwa ninaendesha gari la mtu mwingine kwenye barabara ambalo lilikuwa bado halijakamilika kutengenezwa. Kwenye mwinuko mbele yangu nilikabiliana na mwanga wa taa za usalama barabani ambao ulikuwa kwenye mwisho wa barabara ambapo ilibidi magari yatokee pande mbili kushoto na kulia kuelekea kule nilikokuwa. magari yalikuwa yanapinda kutokea njia zote mbili na kuja kupishana na mimi. Nilikanyaga breki mara nilipoona taa nyekundu zimewaka. Lakini kwa bahati mbaya breki hazikufanya kazi! Niligusa breki za tahadhari, nazo hazikufanya kazi! Nilifikiri kurudi kinyume nyume na hatimaye gari lingesimamaingawa hatua hii huenda ingeliweza kulisababisha kugongana na jingine kwa nyuma. Nilipojaribu kulirudisha kinyume nyume napo likagoma! Mbele yangu niliona gari moja; ndani yake wakiwemo watoto wawili wanachungulia nyuma dirishani. Sasa ilibidi nilisimamishe gari. Nisingeweza kulielekeza kushoto kwangu kwani ulikuwepo ukuta wa mwamba upande huo. na sasa magari yalikuwa yanakuja kwa wingi na kasi. Kulikuwepo na ukuta wa mwamba upande wa kulia kwangu pamoja na shimo, na mawazo yangu mafupi yalinielekeza kwamba nielekeze gari kwenye shimo ili lisisererekee kwenye ukuta wa mwamba na litasimama. Gari litaharibiwa lakini litasimama. Sikuwa na uwezo wa kufanya hivyo. huo ulikuwa ni muda wa pekee katika maisha yangu kushindwa kulimudu gari. Gari lilielekea kushoto likapenya katikati ya magari mawili likaenda kuelekea kwenye barabara chafu hadi kwenye mwinuko ambao ulilizuia gari kuendelea, likasimama. Sikujua kwamba kulikuwapo na barabara chafu. Nisingeiona.

Hivyo unaona, nimekutana na mambo ya kushangaza yakinitokea. Unaweza kuelewa kwa nini mimi ninajiona kuwa mtu mwenye ulinzi kamili. Ulinzi huo unasambaa ndani ya kikundi chochote cha watu ninachokuwa nacho.

MAWAZO YA KUSAIDIA:

Ninapenda kuchangia kwako mawazo haya machache ya kusaidia. Kwanza tulikubaliana kwamba ulinzi wa Mungu umetuzunguka?

Elewa kwamba wewe ni mtoto mzuri wa Mungu.

Kwamba muda wote wewe uko mikononi mwa Mungu? Mkubali Mungu----------. Ukubali ulinzi wake--------. Hakuna lolote litakalo kutisha. Elewa kwamba wewe siyo vazi la udongo. Elewa kwamba wewe siyo kitovu cha asili ya unnafsi ambacho hutawala maisha yako bila kuhitaji. Elewa kwamba wewe ni kitovu cha asili ya Mungu. Ufalme wa Mungu ndani mwako, Kristo aishiye. Wa milele na asiyeharibiwa. Ndio wewe.

Amani---dumu---jua---kwamba mimi ni Mungu.

Amani---dumu---jua---kwamba mimi---.

Amani---dumu

Amani-----.

Amani-----.

Amani----.

Amani.

Na sasa kwa kujua kwamba sisi ni watoto wa Mungu wasioharibika na wadumuo

daima, yatupasa tutawanyike kwa upendo lakini daima tubaki pamoja kiroho. Mungu awabariki na Amani idumu kwenu daima.

## SURA YA SABA

### KUISHI MAISHA YA KIROHO:

Mwanzoni niliyachukua matembezi yangu, si kwa ajili ya kuwasiliana na watu tu bali kama njia yangu ya nidhamu ya maombi kwa ajili ya amani. Bado nilikuwa sijajifunza kusali bila kuacha. Pia nilichukua kipindi cha siku arobaini na tano kwa ajili ya sala na kufunga kula ikiwa ni nidhamu ya sala.

Baada ya miaka michache ya mwanzo, nidhamu yangu ya sala ilikuwa haina umuhimu kabisa. Hii ni kwa sababu nilikuwa nimejifunza kusali bila kukoma. Nilifanya mawasiliano yangu na Mungu kwa sala nikiwa nimemuelekezea mawazo yangu yote wakati huo niliweza kuwasilisha hali yoyote ya kijamii ama mtu yeyote aliyehitaji msaada na yote yaliyosalia yalijipa yenyewe. Niliwachukua watu kimaombi nikawanyanyua juu hadi nikawakabidhi mikononi mwa Bwana Mungu. Hivyo maombi yangu huwashushia mwanga wa Mungu na hatimaye mimi huweza kuwaona wamesimama wakiwa wamenyoosha mikono yao juu wakiogelea kwenye mwanga mtukufu wa dhahabu. Baada ya hapo, mimi huwaaacha mikononi mwa Mungu.

Watu wote ninaokutana nao, ingawaje bado wengine wanayo hali ya mambo ya kidunia, mimi huona ndani mwao ule utukufu wa kimungu na hayo ndiyo ninayoyashughulikia. Watu wote kwangu ni wazuri na huonekana kama mwanga ung'aao. Daima nimekuwa na hisia za shukrani kubwa kwa Mungu kujikuta ninao watu wazuri ambao ninaishi nao kwenye dunia hii.

Sehemu ya maombi yangu ni kumshukuru Mungu kwa hayo pamoja na kujihisi ninao upendo mkubwa moyoni kwa watoto wote wa Mungu pamoja na viumbe vingine vilivyo duniani. Maombi ya sala ni shinikizo la mawazo mema. Hicho ni kiasi kidogo kuhusu sala.

### NJIA ZA MAOMBI:

Unaweza kuona mawazoni mwako mwanga wa Mungu kila siku na ukautuma kwa mwenzako aliye na shida na anahitaji msaada. Asili ya utakatifu ndani mwako inaweza kutoka ikagusa asili ya utakatifu iliyo kwa mwingine. Ndani mwako kuna mwanga wa ulimwengu ambao unaweza kusambazwa ulimwenguni. Kwanza uutawanye kwa wale walio karibu na wewe yaani ndugu zako, jamaa na marafiki na baadaye taratibu uueneze kote duniani. Miongoni mwenu upo mwanga wa ulimwengu ni lazima utumike ulimwenguni.

Na kama unayo matatizo yapeleke kwa Mungu kwa njia ya maombi na umuachie halafu uendelee na mambo mengine ukijua kwamba tatizo lako liko mikononi mwa mwenye nguvu.

***Piga picha mawazoni mwako ya mwanga wa dhahabu ndani mwako na uutoe ili uusambaze. Kwanza kwa wale walio jirani nawe yaani mzunguko wa marafiki na ndugu pamoja na jamaa na baadaye taratibu uueneze ulimwenguni. Endelea kuiona picha mawazoni mwako ya mwanga wa dhahabu utokao kwa Mungu ukiwa umesambaa dunia nzima.***

***Na kama unalo tatizo, peleka suala hilo kwa Mungu kwa njia ya salana uone picha ya tatizo hilo likiwa mikononi mwa Mungu. Sasa liache ukijua liko ndani ya mikono isiyoshindwa kitu, baadaya hapo elekeza mawazo yako katika mambo mengine. Hiyo siyo sala pekee uwezayo kusali, pia nimegundua kwamba; wale waliokuwa katika matatizo makubwa sala hii ya kuona picha mawazoni iliwasaidia sana. Nimesikia matokeo yake baadaye.***

Pia yapo maombi mengine yasiyohitaji kutafuta mwanga wa Mungu kwanza, ingawaje aina hii ya maombi iliwasaidia watu wengi waliokuwa na matatizo.

Yapo maombi mengine yadumuyo ya kutoa shukrani kwa Mungu. Mimi hudumu katika kushukuru. Dunia ni nzuri sana, ninamshukuru Mungu. Mimi ninazo nguvu zisizoisha, ninamshukuru Mungu. Nimewekwa karibu na chanzo cha mgao wa vitu vyote duniani, ninashukuru. Nimewekwa karibu na chanzo cha ukweli uishiyo, ninashukuru. Ninayo hali hii idumuyo ya shukrani kwa Mungu ambayo ni kwa njia ya sala.

Unapokuwa unajifunza, ni kweli lingekuwa jambo la thamani kutumia muda maalum hata kutumia taratibu maalum, ninaweza kuyaona haya.

Mara kadhaa watu wameniandikia na kusema; " Amani, utasali na mimi saa kumi alasiri au saa tatu usiku ama muda wowote mchana? " Na mimi huwaandikia nikawajibu; " Huna haja ya kuhitaji kuniona bali jiweke sawa kwenye maombi saa yoyote na utakuwa unasali na mimi. Na mimi huku nitakuwa ninasali na wewe kwani mimi husali bila kukoma."

Sala bila ukomo siyo tambiko na wala si shughuli ya kusema sema tu. Ni ile hali ya kujiona u-karibu na Mungu muda wote. Kitafutwacho hapo ni yale mema na mkazanio wa yale ya utukufu kwa njia ya imani. Sala zote zilizo za kweli zinayo matokeo mazuri na ukiyatoa maisha yako yote kwa ajili ya sala utazidisha nguvu yake----. Hakuna ajuaye nguvu kamili ya sala. Hakika kuna uhusiano kati ya sala na matendo. Sala ipokewayo huleta mapokeo ya kiroho ndani mwetu ambayo humotisha matendo mema.

Sikiliza nikuambie habari ihusuyo majibu kwa sala. Usiku mmoja nilikamatwa na kijana mmoja askari polisi wakati nilipokuwa ninatembea kwenye barabara moja ambayo haikuwa na watu. Ninaamini aliona kunisaidia mnamo majira yale ya usiku ilibidi aniweke mahabusi nilale ili nisidhurike. Aliniuliza ni kwa nini niliweza kuonekana sehemu ambayo hakuna mtu aliyediriki kutembea mnamo majira yale.

Nilimjibu kuwa mimi ninatembea bila wega. Nisingeweza kuvutia kitu chochote chenye mawazo mabaya dhidi yangu. Upo usemi usemao kwamba; " lile mtu aliogopalo ndilo limjialo."

Lakini mimi siogopi lolote bali nitegemealo ni lile jema tu.

Alinichukua kwa namna yoyote aliyoiona kwake ni sahihi hadi mahabusu. Nilipoingizwa kwenye chumba cha mahabusu nilikuta sakafu imejaa magazeti makuu kuu na vichungi vya sigara pamoja na takataka zingine. Vifaa vya kutumia vilikuwa godoro moja likiwa sakafuni na mablanketi manne yaliyochakaa. Walikuwamo wanawake wawili waliokuwa wanalilalia godoro hilo. Waliniambia kwamba usiku wa jana yake walilala humo wanawake wanane na walitumiavifaa hivyo hivyo. Kulikuwapo na hisia bora miongoni mwa wafungwa kwa ujumla. Waliniambia nitumie blanketi mbili nitandike chini sakafuni nilale. Hivyo nilichukua magazeti, nikatandika sakafuni kwanza, juu yake nikatandika blanketi moja na lingine nikajifunika nikalala usingizi mzuri.

Haikuwa mara yangu ya kwanza na wala ya mwisho kulala sakafuni. Kama moyo wako umeridhika unaweza kulala popote. Nilipoamka asubuhi nilimuona mwanaume anachungulia dirishani. Nilimuuliza muda ambao mahakama inaanza kazi. Alisema yeye hajui bali alikuwa amekuja pale kuona wasichana. Nilimuuliza kama alikuwa askari, akakataa kuwa hakuwa askari. Ilikuwa mojawapo ya mchezo wa mjini. yeyote angeweza kutoka popote mitaani kuja kuona ni nini walikuwa nacho pale jela siku hiyo; " Twende kuwatazama wasichana." Hiyo ndiyo iliyokuwa kauli ya mitaani. Mmojawapo wa wale wanawake alikuwa na umri wa makamo aliyekamatwa kwa kulewa na kufanya fujo na hilo lilikuwa shitaka lake la saba. Kwake alisema hiyo ni kawaida. Mwingine alikuwa msichana wa umri wa miaka kumi na minane ambaye alijiona kuharibikiwa na maisha. Niliwaambia kwamba kwangu mimi hiyo ilikuwa mara yangu ya pili na hakika sifikirii kwamba maisha yangu yalikuwa yameharibiwa! Niliwapa mazungumzo ya kuwachangamsha sana tukaongea mengi. Yule binti ilikuwa atoke siku hiyo ama kesho yake.

Baadaye waliwabadili walinzi. Nilikuwa sijawahi kumuona mlinzi mlezi wa wafungwa wanawake. Mlezi huyo mlinzi aliniona akasema; " Wewe unafanya nini? Niliiona picha yako gazetini. Pia, nilikusikia redioni." Baadaye waliniachia nikaondoka.

Kabla sijatoka pale, nilichukua ufagio kutoka kwa mtu mmoja mfagiaji wa mazingira, nikafagia sehemu yangu nilikolala nikawapa wale wasichana wafagie sehemu zao, nikawaachia na chanuo wazichane nywele zao kwani zilikuwa katika hali mbaya kwa muda wa wiki moja waliyokuwa mle ndani.

Kitu nilichotaka kukueleza ni kwamba yule msichana wa miaka kumi na minane alikuwa mtu wa dini ipasavyo. ALikuwa anasali kuutafuta msaada. Ninaamini kwamba kukamatwa kwangu na kupelekwa alikokuwa usiku huo ni ishara ya majibu ya sala zake.

Kitu muhimu sana katika sala ni zile hisia zetu na wala si maneno yatamkwayo mdomoni. Tunatumia muda mwingi kumueleza Mungu ni nini tunafikiria kifanyike na wala siyo muda wa kutosha kusubiri kimya majibu ya Mungu kuhusiana na nini tufanye.

Sasa zaidi ya sheria za Mungu ambazo ni zile zile zitutawalazo sisi wote, pia upo mwongozo wa Mungu ambao umeelekezwa kwa kila roho ya mwanadamu. Kama huujui mwongozo jinsi ulivyo, jaribu kutafuta kupitia mapokeo ya kimya. Mimi nilizoea kutembea kwenye maeneo yenye mandhari safi ya asili na wakati huo kimya, napata mapokeo kutoka kwa Mungu. Maajabu ya ndani mwangu yalinijia na nikayaweka kwenye matendo ya maisha yangu.

Waweza kupendelea vitu vizuri vizuri, muziki, usomaji wa vitabu n.k. Kwangu mimi uzuri wa maumbile ya asili ulikuwakichocheo cha kunifanya nijione mwenyewe karibu na Mungu. Isingenichukua zaidi ya muda wa saa moja kabla sijauona uwepo wa Mungu karibu na mimi.

Hivi sasa vijana wanaongea na mimi leo kuhusu mambo kama vile mazoezi ya viungo, mbinu za kutafakari ambazo kwenye hali ya utamaduni wetu ni matendo yanayokubalika kidini. Lakini tazama mimi kuwa karibu na Mungu nikijiona nimezungukwa na mandhari nzuri ya asili, uchocheo wangu kutokana na mapokeo ya kimya ndani mwangu, mawazo yangu pamoja na kutembea kwangu sehemu kadhaa yote kwa pamoja yananijengea afya njema na matumizi bora ya muda wangu. Na huwezi kujisikia kulazimishwa unapokuwa unayafanya mambo hayo kwa mara moja.

Watu walio wapumbavu wanatumia mazoezi yao kufanya mambo yawezayo kuyaharibu maisha yao na kuwapeleka kwenye hali isiyotakiwa badala ya kuwapeleka kwenye maisha mema ya kiroho.

Jambo hili ninalifananisha na tumba la ua. Tumba litunzwapo na kuangaliwa vizuri huchanua katika ua zuri. Lakini usipovumilia ukaanza kulichana wakati bado limefunga utalidhuru ua lililomo ndani mwake. Hivyo ua tunalifananisha na maisha ya mwanadamu. Maisha hayo yape ukuzi wa kiroho na yatachanua katika sura yenye uzuri wa ajabu.

Unapohisi haja ya kuinuliwa kiroho, jaribu kulala, mapema ili uamke mapema wakati wa mapambazuko uwe na muda mzuri wa ukimya na hapo umwimbie Mungu nyimbo tulivu ukiwa na hisia za mambo uyategemeayo yafanyike kwa siku hiyo.

Kwenu ninyi mtafutao maisha ya kiroho, ninapendekeza kila siku mfanye manne yafuatayo:

Tumia muda fulani ukikaa mwenyewe ukimtafuta Mungu kimya.

Kama umekasirika ama kuna jambo lililokukwaza chukua muda uwe peke yako na Mungu.(Usiongee na mtu yeyote aliye na hasira, mtu wa aina hiyo hana mawazo ya kufikiria alisemalo, hivyo muache umuombe Mungu). Utafute mwanga wa Mungu mawazoni mwako kila siku na uutume kwa yule aliyehitaji msaada wa kiroho. Mwili wako uufanyie mazoezi ya viungo kwani ni hekalu la roho yako.

KATIKA KUFUNGA KULA

Nimekuwa nikiulizwa kuhusu siku zangu arobaini na tano za kufunga kula na kuomba. Tabia hii niliichukua kama nidhamu ya sala ambayo ilinifanya nielemee zaidi maombi ya kuleta Amani. Ilikuwa katika mwaka wangu wa pili wa hija wakati nilipokuwa ninarudi taratibu kutoka safari yangu ya kwanza na sikuwa nimetembea eneo kubwa.

Kufunga kwaweza kuleta matunda yaliyo bora ya kiroho. Ingawaje nilikuwa nimekwisha ipata amani ya dhati ndani mwangu, kufunga na kuomba kulinijengea tabia ya kuomba bila kukoma.

Wakati nilipofunga nilikuwa nyumbani kwa mganga mmojaaliyekuwa na mazoea ya kufunga kula ili awatibu wagonjwa wake. Alitaka kujua jinsi mtu ambaye si mgonjwa angekuwa kutokana na kufunga kwake. Baada ya kuwa nimeongea naye kirafiki, alinichunguza tu, hakunipima. (Wapo waganga wengi wa kila aina ambao ni rafiki zangu lakini hakuna hata mmoja wao ambaye amewahi kunifanyia uchunguzi au kunitibu). Ingawaje nimewahi kutibiwa jino kutokana na uharibifu uliosababishwa na mlo mbaya utotoni mwangu. Mlo wangu wa mwisho kabla ya kufunga ulikuwa ni matunda ya zabibu na machungwa mawili hivyo sikuweza kupata kiu. Siku tatu za kwanza nilifunga bila kula chakula cha aina yoyote chepesi wala maji ya kunywa. Baada ya hapo nikawa ninakunywa maji ya mvuke. Nilipoacha kufunga ilikuwa pia kawaida. Kwangu ilikuwa ni njia ya kawaida kuacha kufunga. Nilianza kunywa maji ya chungwa lililokamuliwa kila saa kwa siku ya kwanza.

Siku ya pili nilikunywa maji ya machungwa mawili yaliyokamuliwa pamoja na maji ya zabibu kwa kila saa mbili. Maji ya zabibu na maji ya machungwa mawili mara tatu katika siku ya tatu. Niliendelea kuongeza kidogo kidogo mpaka baada ya juma zima nikawa ninaweza kula mlo kamili.

Haikuwa tofauti na utaratibu wa kawaida wa kufunga kula. Nilitii sheria za kufunga, kama vile kutokufanya kazi ngumu. Sikuweza kutembea mwendo mrefu ingawa nilitembea baadhi. Nilipunguza kutembea muda mrefu ingawaje niliendelea na matembezi. Nilikuwa ninachapa maandishi ya yule mganga hadi hapo baadaye alipoamua kuichukua mashine yake mnamo mwezi wa kufunga kwangu. Hakufikiria kwamba ningeweza kuwa na nguvu za kuitumia. Niliandika maandishi yangu kwa

mkono kazi iliyokuwa ngumu kuliko uchapaji. Lakini mimi ninaweza kufanya lolote niwezalo na mambo hayo.

Sikuweza kuonana na wagonjwa wake kama nilivyotaka kwa sababu hakutaka mimi nizoeane nao kwa kiasi kikubwa. Niliweza kwenda kuonana nao mara moja moja ili kuwaamsha kiroho.

Siku moja wakati nimefunga, ninakumbuka, na tazama; niliona maono nikiwa katika hali ya usingizi wa mang'amung'amu, nikaona msalaba ukiwa juu yangu unaning'inia, nilijua mtu lazima aubebe mzigo. Niliamka kuupokea na hapo hapo nikanyanyuliwa juu ya msalaba ambapo nilikuta mwanga na uzuri wa ajabu. Yote yaliyokuwa yanatakiwa ni ule utashi wa kukubali kuupokea mzigo na hapo nilinyanyuliwa juu yake. Badala ya kazi ngumu nilipata hali ya ajabu ya amani na furaha.

## KATIKA TIBA

Mtu lazima awe mwangalifu anapowaombea wengine ili kuondoa vyanzo vya matatizo waliyo nayo na siyo kuondoa dalili za matatizo.

Sala ya tiba ya aina hiyo ni hii; ***" Leta maisha ya upatanisho kwa makusudio ya Ki-Mungu— maisha haya yaje katika upatanisho kwa utashi wa Mungu. Uishi ili wote wanaokutana na wewe wanyanyuliwe juu. Wote wanaokubariki watabarikiwa na wote wanaokutumikia wataridhishwa. Kama atatokea yeyote wa kukudhuru, Mungu akuponyeshe."***

Waganga waitwao Eager Beaver Psychic ni wale wanaotibu kwa kuondoa dalili za maradhi na wala siyo kuondoa vyanzo vya maradhi hayo. Ukitamani jambo unapata jambo; humpati Mungu. Tuseme kwambamimi ni mganga wa aina hiyo, ninaishi jirani na wewe na wewe umechagua kuingia katika maisha haya kupambana na dalili za matatizo ya kimwili hadi hapo utakapoondoa chanzo chake. Sasa dalili zinapojitokeza dhahiri, mimi kama mganga ninaziondoa. Na baada ya muda fulani dalili hizo hujitokeza tena na hapo tena ninaziondoa. Hivyo hivyo ninaendelea kuwa ninaziondoa dalili hizo. Kama vile maradhi badala ya kuviondoa vyanzo hawamtegemei Mungu katika kuifanya kazi yake. Tiba ya dalili za tatizo haiishi kwani kila ukiiondoa dalili hii nyingine hujitokeza hivyo tatizo haliishi. Waganga wengi huyaangalia matatizo yanayojitokeza kwa kuonekana juu ya miili ya wagonjwa wao bila kuchunguza chanzo cha yote hayo.

Unapoingia kwenye maisha ambayo si ya kimwili, kwa sababu nyingine halikadhalika badala ya kubariki kwa kukuondolea hizo dalili utasema; " Huyo fedhuli! nilikuja kutatua tatizo hili lakini alikazania kuniondolea dalili kwa hiyo kamwe sikuweza kulitatua! "

Hii ndiyo maana yangu ninapoongea kuhusu baadhi ambao wameridhika katika kushughulikia uondoaji wa dalili. Wakati mtu anapokuwa fedhuli katika maisha ya mwingine si kwamba tu itasababisha dalili kujitokeza upya kwenye mwili bali pia zitaendelea kuwapo kwa kipindi kingine cha maisha. Waponyaji wengi hawalijui hili na huendelea kwa furaha kuziondoa dalili hizo.

Ninakubali kwamba muda mrefu uliopita kabla sijajua ni nini nilikuwa nikifanya, niliposhughulika na watu waliokuwa na matatizo niliwagusa shingoni na usoni nikiwaliwaza. Sikujua kwamba sikuwa nikifanya jingine zaidi ya kuwaliwaza. Tatizo lao lilikuwa pale pale. Sasa ninaweka kila tatizo katika sala itokayo moyoni kwenye mikono halisi ambayo ni ya Mungu na baada ya hapo ninaelekeza moyo wangu kwenye mambo mengine.

## NGUVU YA FIKRA

Je, wewe u mtumwa katika maisha yako ya kidunia au nguvu ya Mungu inakuongoza?

Je, wajua kwamba kila muda wa maisha yako, lolote lile ulifanyalo linatokana na kufikiri? Unajiundia hali ya ndani mwako ambayo inategemea unafsi wa maisha yako ya duniani tu. Unasaidia kunda hali zinazokuzunguka. Mafundisho ya kikristo yanatuambia kwamba " Lile alifikirialo mtu moyoni mwake ndilo yeye."

Usemi huu unatuambia wazi kwamba; tunajiundia hali ituzungukayo. Kama tungeweza kutazama kwa undani zaidi katika maisha tungeweza kuona kwamba, matatizo ya kimwili ni taswira halisi ya matatizo ya kiroho na hizo fikra na hisia potofu vinadhuru zaidi kuliko viini vya maradhi.

Kama ungegundua ni namna gani mawazo yako yalivyo na nguvu, kamwe usingefikiria kushindwa kwa yale uyapangayo. Kwa vile tunaunda mambo kutokana na fikra zetu zinavyotutuma tunahitaji kujihusisha kikamilifu katika fikra sahihi ili tufanye yale yaliyo sahihi. Fikra zako zikikuashiria kuwa huwezi kulifanya jambo fulani, jua hutaweza.

Na kama ukifikiria na kuamini kwamba utaweza, utashangaa kuona umeweza! Ni muhimu kwamba fikra zetu ziwe katika msimamo kwa faida ya yale yatakayojitokeza ndani ya mazingira yaani kwa ajiliya mambo mazuri ambayo tungependa kuona yanatokea.

Nimekutana na watu wa siku hizi ambao walikuwa wamesikia utabiri wa matukio mabaya duniani, na mawazo yao yote yalikuwa yametopea katika jambo hilo la hatari! Kwa nini kila muda wa maisha yetu tunautumia kujiundia fikra? Na hii inasaidia kuunda hali ituzungukayo kuwa mbaya.

Mathalani, wakati ulipotokea utabiri mara kadhaa kwamba nusu ya California huko Marekani ingedidimia ndani ya bahari kutokana na tetemeko la ardhi ambalo lingeikumba sehemu hiyo kwa makusudi nilipanga kwenda katika sehemu hiyo ya California. Hakukuwepo na tetemeko. Lakini niliwakosa baadhi ya rafiki zangu ambao walikuwa sehemu za pwani ya mashariki wakitafuta usalama.

Kumbuka mahali inaposemwa kuwa, kutatabiriwa jambo lakini halitakuwa? Sababu yake ni nini? Kwa sababu yale yote yatabiriwayo huwa yako kwenye mstari wa matukio. Kamwe huwezi kusema matokeo ya matukio hayo kwa sababu tunao

uwezo usiobadilika kulibadili kwa nguvu za Mungu lililotabiriwa kuelekea upande mwingine, yaani upande usio na uharibifu endapo tutashirikiana kwa maombi.

Lolote zuri ulifanyalo, lolote zuri ulisemalo, wazo zuri ulifikirialo, huendelea muda wote na matokeo yake hayaishi. Shetani hubakia na mapambano yake hadi hapo ashindwapo na mema. Lakini mema hubakia milele.

Egemea kwenye maisha ya fikra njema, maisha mema ndani ya upatanisho na sheria za Mungu na uwachochee wengine kufanya hivyo.

Kila wakati ukutanapo na mtu, fikiria kuzungumuza naye mambo yawezayo kumtia moyo kama vile kuongea naye maneno ya wema, ushauri wa kumsaidia, maelezo ya kustaajabisha kamwe usifikiri juhudi zilizo sahihi kutozaa matunda.

Uwe mwimbaji mzuri kwenye kikundi cha waimbaji badala ya kuwa na sauti ichukizayo. Dawa itakiwayo kwa ulimwengu huu unaougua ni upendo. Upendo lazima uwe badala ya chuki na imani iwe badala ya uoga hivyo upendo utadumu.

Wimbo unayo yafuatayo: ***" Upendo unatiririka kama mto. Unatoka kwangu na kwako. Unasambaa na kuelekea jangwani ukiwaweka huru mateka wote."*** Mateka ni wale ambao hawajifahamu wao ni nani.

Wasiojua kwamba wao ni watoto wa Mungu.

Yakumbuke haya: *Tulia na ujue kwamba mimi ni Mungu. Usisahau kwamba wewe u nani. Huwezi kuwa mahali ambapo Mungu hayupo.*

<u>MABADILIKO YAITWAYO KIFO:</u>

Maisha ni mpangilio wa majaribio ambayo unapoyashinda utajiona umepitia kwenye uzoefu wa kujivunia. Ninatazama nyuma katika majaribio yote ambayo nimewahi kuyapitia kama mafunzo mema ikiwa ni pamoja na usiku mmoja nilipokabiliana na tufani ya barafu. Ulikuwa mwaka wangu wa kwanza wa matembezi ya Hija na lilikuwa tukio moja zuri sana katika yote yaliyokuwa yamenitokea.

Nilikuwa nikitembea kwenye eneo pweke, kwenye milima ya Arizona ambako hakukuwa na masikani ya watu kwa maili kadhaa mbele yangu. Mnamo majira ya alasiri kulitokea tufani la barafu ambalo lilikuwa kubwa aina yake tena la kustaajabisha! Lilitokea katika kipindi ambacho hakikuwa cha majira yake.Nilikuwa sijawahi kuona tufani kubwa kiasi hicho! Kama barafu ingekuwa mvua, tungesema mawingu yalikuwa yamelipuka siku hiyo. Nilikuwa sijawahi kuuona mlundikano wa barafu ardhini kama ilivyokuwa siku hiyo! Mara ghafula nilijikuta ninatembea kwa kukanyaga ndani ya barafu na nilishindwa kukiona kile kilichokuwa kikianguka. Nilitanabahi kuona kwamba; magari yote yalikuwa yamesimama kutembea. Ninadhani yalikuwa yamekwama ndani ya barafu kiasi cha kushindwa kwenda. Baadaye hali ikawa ya giza. Lazima mawingu mazito yalilifunika jua. Nilishindwa hata kuviona viganja vya mikono yangu mbele ya uso na barafu ilikuwa inanipiga usoni na kusababisha niyafumbe macho yangu. Hali hii ilikuwa ya baridi. Tena ni ile baridi ipenyayo ndani ya mifupa.

Kama ningeipoteza imani yangu, niogope huo ungekuwa ndio mwisho wangu!

Badala ya kuyaogopa yote yale yaliyokuwa yananitokea muda huo niliyaona ya kawaida. Mungu tu ndiye si wa kawaida. Niliamini kwamba vazi langu la udongo ambalo huaribika laweza kuharibika lakini si roho yangu ambayo niliamini hali ile isingeliharibu.

Nilijisikia huru na nikaamini kuwa kila kitu kilikuwa salama. Nilijisikia huru na nikaamini kwamba kila kitu kilikuwa salama, ama kama ningeendelea kuishi maisha ya duniani ama ningekwenda kutumikia katika maisha mengine huru zaidi nje ya dunia yote kwangu niliona ni sawa kabisa. Nilihisi kuongozwa katika kuendelea na matembezi yangu, na kwa imani nilifanya, ingawa sikuweza kueleza kama nilitembea nikiwa barabarani ama nje ya barabara. Nisingeweza kuona chochote.

Miguu yangu ilikuwa kama mabonge ya barafu ikawa mizito kunyanyua. Mwili nao ulianza taratibu kuganda.

Baada ya kuwa nimehisi mgando mwili mzima zaidi ya maumivu, ghafla niliona maajabu!

Niliona maono. Ilikuwa kama vile nimepata fahamu upya, na fahamu hizo siyo tu zilitokana na upande wa maisha ya mwili wangu huu, ambayo wakati huo kwake kila kitu kilikuwa giza totoro, baridi kali, mzunguko wa barafu. Lakini pia karibu sana inaonyesha niliweza kuingia katika upande wa maisha yasiyo ya mwili ambapo wakati huo kila kitu kilikuwa joto zuri na mwanga mzuri. Ulikuwapo uzuri wa ajabu. Uzuri huo ulianza kwa rangi niliyoizoea lakini iliyo nzuri kuliko kifani. Pia na uzuri huoulianza na muziki niliouzoea lakini ukawa mzuri zaidi.

Aidha nikawaona watu walikuwa mbali na mahali pale nilipokuwa. Mmoja wao alinijia haraka. Aliponikaribia nilimtambua. Alikuwa mwanamke. Alionekana na umri mdogo kuliko alivyokuwa kabla hajafa.

Ninaamini nilikuwa kwenye mwanzo wa bediliko liitwalo kifo. Wale wapendwa na walio karibu nasi tupatapo badiliko la aina hii huja kutupokea. Nimewaona rafiki zangu wengi wakati wanakufa wanavyoongea na wale wawapendao kutoka pande

mbili tofauti yaani upande wa duniani atokako na upande wa mbinguni aendako kana kwamba wote anao pale chumbani.

Nilifikiri muda wangu wa kuiacha dunia umetimia, mara moja nilimsalimu. Yawezekana niliongea ama nilikuwa nikiwaza; " Umenifuata?"

Alitikisa kichwa kwa kukataa.

Aliniashiria nirudi nitokako.

Na mnamo muda huo huo nilikimbia kuingia kwenye jengo la daraja. Na papo hapo ono langu likatoweka.

Kwa vile nilikuwa ninalindwa muda wote huo nilipokutana na maono hayo, nilikuwa ninaendelea na safari yangu hadi nilipofika eneo hilo la daraja. Mle darajani nilikuta kasha kubwa na makaratasi mengine yamo ndani yake. Taratibu kwa kuvitumia vidole vyangu vilivyokuwa vimekufa ganzi niliyachukua makaratasi yale kuufunika mwili wangu baada ya kuwa nimeupenyeza ndani ya lile kasha. Mle darajani wakati dhoruba inaendelea nililala usingizi mzito. Hata pale darajani hifadhi yangu ilikuwa imeandaliwa na huyo mlinzi wangu.

Kama ungeniona wakati ninanyeshewa na hiyo dhoruba ya barafu ungejiuliza; " Ni mateso gani haya ambayo mwanamke huyu maskini anayapata?"

Na mimi kwa kujibu ninaweza tu kusema; " Ni ajabu iliyoje kukutana na hali iliyonionyesha kifo kilivyo bila ya kuwa na woga nikiwa na uwepo wa Mungu karibu nami."

Ninaamini nilipata upendeleo wa kushuhudia mwanzo wa badiliko liitwalo kifo. Hivyo sasa ninaweza kufurahi na wapendwa wangu wanapokuwa wanatekeleza kipindi kitakatifu cha mpito kuelekea maisha yale huru.

Ninatazamia mabadiliko hayo yaitwayo kifo kama mwisho wa visa vikubwa vya maisha ya duniani.

Nimeulizwa nina maana gani niliposema nimeanza hatua za kuelekea kwenye kifo. Hakika, badiliko liitwalo kifo ni hatua.

Kwanza unaanza kukabili siyo tu maisha ya upande huu tulio nao wa mwili bali upande wa maisha yasiyo ya mwili. Yaani peponi. Baabaye unaanza kuwatambua wale wapendwa wako waishio katika hali isiyokuwa ya mwili mara wakujiapo na hapo unapata kwamba unaweza kuwasiliana na pande zote mbili. Hiyo ndiyo hatua niliyoifikia. Tena unaanza kuwatambua wenzako ambao wako mbinguni wakija na kuwasiliana nawe. Na wakati huo huo unawasiliana na wale ulionao duniani. Hiyo ndiyo hatua niliyofikia. Sasa inakuja hatua ambayo inavunja lile fundo inayokupeleka kujiunga na wale walioko peponi inakufungia kuwasiliana na wale wa duniani ingawa unaweza kuwasikia na pia kuwaona. Unajikuta uko kwenye sehemu maalum naya ajabu ukiwa na wale wapendwa na baadaye unaifikia hatua ya kujifunza na kutumikia.

Upande wa watu wa peponi uko hapa ila sisi hatuna uwezo wa kuuona. Ni dunia mbili zilizoingiliana. Sisi tulio humu duniani tunayaelewa yale ya dunia yetu,

lakini wale wa peponi wanayaelewa ya dunia zote. Mawasiliano ni rahisi, kwa mfano tunaweza kuwaombea na wao pia wanaweza kutuombea.

Kifo ni uhuru wa maisha ya kupendeza, ambapo mwili ule wa udongo huwekwa kando. Ile hali ya unafsi wa mwili huenda na wewe huko ili ijifunze na kukua na baadaye kurudi hapa katika umbile zuri la mwili wa udongo kujifunza yale tutakayo kujifunza. Kama tungeweza kuona kwa undani maisha yetu, tungejiandalia mema tangu kuzaliwa na kufurahia wakati wa kufa. Kama tungejua jinsi maisha ya dunia yalivyo mafupi kulinganisha na kifo tusingesumbuka sana na ugumu wa maisha ya dunia, kama tusumbuliwavyo na ugumu wa maisha ya nyakati zetu hizi.

Ibada za ukumbusho zingekuwa za kusherehekea furaha ya kwa heri kwa kuyazingatia mazuri ambayo mtu aliyatenda kabla ya kufa kwake. Kusoma tenzi na kuimba nyimbo za kupendeza. Kama tungefanya haya wale walio huru wangefurahia pamoja nasi.

Nilivyoyakubali mabadiliko ya nywele zangu za rangi ya dhahabu za utotoni kuwa rangi yenye mchanganyiko wa wekundu na kahawia wakati wa ujana wangu, halikadhalika nikakubali mabadiliko ya nywele zangu na mwili wangu wa udongo kurudi kwenye vumbi vilikotoka. Wakati huo roho yangu itapepea kwenda kwenye uhuru uishio daima.

Ni musimu wa nywele zangu kuwa na mvi, na kila musimu wewe unalo somo lifundishwalo. Kila musimu wa maisha unayo maajabu yake kama utakuwa umejifunza somo la musimu huo kabla ya kuanza. Na kama utajikuta umeingia kwenye musimu bila kuuandalia hakika utatamani urudi nyuma.

## KWENYE DINI

Dini ama dhehebu haina mwisho.

Mtu aliye ndani mwake anapojihusisha na Mungu hilo ndilo lengo. Yapo madhehebu mengi ya kidini kwa sababu watu wasiokuwa na wokovu wakiroho huzingatia tofauti zisizokuwa na maana badala ya kuyaangalia mambo muhimu ya kiroho yawezayo kuwaweka pamoja. Tofauti zilizopo kati ya imani mbili za madhehebu zinaegemea kwenye kanuni na mitambiko badala ya taratibu za kiroho.

Vipi kuwapo kwa mgawanyiko wa njia katika wakati fulani, lakini siyo kwamba zote hufikia mahali zikakutanika juu ya mlima mmoja ambao ndio lengo la njia hizo? je, siyo kwamba zote zinaelekea kwenye utafutaji wa kitu kile kile?

Kama unaongozwa kuifuata imani ya dhehebu fulani ni vemasana kuitumia kama ngazi ya kumuona Mungu. Na wala isiwe kizuizi kati yako na watoto wa Mungu walio kwenye madhehebu mengine. Kama wewe hujaongozwa kuelekea kwenye imani ya dhehebu lolote (na hata kama unaongozwa) mtafute Mungu kwanza kwenye ukimya mahali ulipo.

Tunapojaribu kuwatenga wenzetu tujue kwamba tunajitenga wenyewe. Sisi sote ni watoto wa Mungu na wala hakuna anayependelewa zaidi ya mwingine. Mungu hujionyesha kwa yeyote amtafutaye. Mungu huongea na wote wamsikilizao. Tulia umfahamu Mungu.

Mimi ni muumini mashuhuri wa dini, lakini siko upande wowote. Ninachokifuata ni roho anayetii sheria za Mungu. Na wala siyo maandishi yenye sheria. Mtu anaweza kufungiwa kwenye alama na taratibu za dhehebu kiasi kwamba anasahau kiini hasa cha kuwepo kwa dhehebu hilo ambacho ni kumleta mtu karibu zaidi na Mungu. Tutaupata ufalme wa Mungu kwa kuamini jinsi ulivyo ndani mwetu wote. Tuelewe kwamba sisi sote ni chembe nyingi sana ndani ya bahari na kila moja ikitoa mchango wake kwa ajili ya nyingine.

Nilisoma katika kitabu cha Yakobo kwenye Agano jipya la Biblia pia nikasoma na vipengele kadhaa vya vitabu kutoka Agano la Kale. Hii ilikuwa baada ya kuwa nimeanza shughuli yangu ya hija. Ni vitabu muhimu kwa watu wengi, na nilihisi haja ya kuyachunguza yaliyomo ili kwamba ujumbe wangu kwa wengine uweze kuwafikia kikamilifu. Biblia imejaa ukweli mtupu. Lakini kwa kawaida ukweli huo haueleweki kwa walio wengi. Watu hubadilisha roho kwa sheria, kwa maneno ya sheria, hivyo ukweli hugeuzwa uongo. Kama unataka uthibitisho wa ukweli ni vema uutafute kutoka ndani ya roho yako na siyo kwenye kurasa za vitabu.

Utagundua kwamba Yesu husema, " **Kwa nini unaniita Bwana, Bwana na huyafanyi yale nikuagizayo?"**

Ameyaeleza haya zaidi ya mara moja. Kwa hiyo ni vema uamini kwamba, kwangu mimi, mkristo halisi ni yule anayeishi kwenye sheria za Mungu ambazo Yesu alitufundisha.

Yesu pia husema, " Usiseme, tazama yuko pale ama yuko kule kwani ufalme wa Mungu umo ndani mwenu."

Kwa ufafanuzi ulio mwingi, anawaambia watu yale yanayowastahili. Wakristo halisi waruhusu maisha yao kutawaliwa na ufalme wa Mungu ulio ndani mwao ambao wakati mwingine unaitwa " Kristo aishiye ndani mwetu."

Watu wengi wanautangaza ukristo. Ni wachache sana wanaoyafuata matendo halisi ya ukristo huo. Na unapoufuata ukristo huo kikamilifu watu wanakuona kama kichaa. Imekuwa ikisemwa kiukweli kwamba ulimwengu unastushwa na mtu anayeukana ukristo na mwingine anayeufuata.

Mimi ninaamini Yesu atanipokea kwa sababu yale yote nitendayo ni yale aliyowaagiza watu kufanya. " Hii haina maanakwamba wale wote wajiitao Wakristo watanikubali, " anasema. Hakika ninampenda na kumhimidi Yesu na laiti wakristo wote wangezitii amri zake, dunia hii tuishimo ingekuwa ya ajabu sana.

## NJIA YA UPENDO:

Ubaya haumalizwi kwa kutenda ubaya zaidi. Ubaya hushindwa na matendo mema. Hilo ndilo fundisho la njia ya upendo. Shindano lililopo ndani ya ulimwengu hivi sasa ni kati ya njia ya zamani ya ubaya kuushinda ubaya, yani kwa kutumia silaha za kisasa jambo ambalo litatufikisha kwenye machafuko makubwa, na njia ya kuushinda ubaya kwa kuyatenda yaliyo mema ambayo ingetufikisha kwenye maisha ya utukufu yaliyokomaa.

Hatuhitaji kujitokeza kuuangamiza ubaya kwa silaha za moto ama za aina nyingine yoyote ile kwani hakuna chochote kiwezacho kuishinda ile sheria ya Mungu inayoishi. Vitu vyote visivyokuwa vyema hapa ulimwenguni havidumu, kwani ndani mwavyo zimo mbegu kujiangamiza. Tunaweza kuwasaidia watu wenye mbegu za aina hiyo, kuondokana na mbegu hizo kwa kubaki ndani ya utiifu wa sheria za Mungu, kwamba ubaya lazima umalizwe na matendo mema. Wale wautumiao uovu kuyatatua matatizo yao ya kiovu watakuwa wanazidisha uovu mara mbili ndani mwao.

Sheria za Mungu zipo muda wote na kila kilichoko nje ya upatanisho na sheria hizo tayari kimefutika.

Kwa vipi mtu awe na mashaka kuhusiana na uwepo wa Mungu hapo? Ni kwa vile, itategemea ni muda upi utatuchukua kumkubali, yote yako ndnai ya uwezo wetu. Na ni kiasi gani cha mapambano ya kutumia silaha watakipitia hadi kufikia kumkubali Mungu nayo pia nndani ya uwezo wetu. Kama tutakuwa tayari kujenga dunia mpya yenye misingi ya kiroho kwenye msingi ule wa ile ya zamani, mapambano hayo ya uovu hayatakuwepo. Hivyo tuanze kazi. Ebu tumuamshe yule ndege wa hadithini ambaye kila baada ya miaka mia tano ama mia sita alijichoma moto na kufufuka pale pale katika majivu, ili aweze kupaa, ebu tusaidie kuongeza nguvu ya uamsho wa kiroho hadi tunyanyuliwe hadi kwenye kipindi cha utukufu ambacho kitakuja.. Si kwa kupitia kwenye hukumu kwamba tutayafikia yaliyo mazuri bali kwa njia ya upendo na imani.

Ili tusaidie kuingia katika kipindi cha utukufu ni lazima tuone wema ndani ya watu. Lazima tufahamu kuwa wema huo umo, bila kujali umezama ndani mwao kiasi gani. Ndiyo, ubaridi ndani ya mioyo ya watu umo, na ubinafsi umo, lakini wema umo pia. Si kwa njia ya uamuzi iwezayo kutuonyesha wema huo bali kwa njia ya upendo na imani.

Upendo halisi ni utashi wa kutoa bila ya kuwa na wazo la kutaka kurudishiwa chochote baadaye. Upendo waweza kuiokoa dunia kutokana na uharibifu wa kinyukilia. Mpende Mungu. Mgeukie Mungu umpokee kwa moyo wa imani. Wapende wenzako. Wageukie kirafiki na uwagawie ulicho nacho wawapo na shida. Jitengeneze ipasavyo ili uitwe mtoto wa Mungu kwa kuishi maisha ya upendo.

Je, unamfahamu Mungu? Je, unafahamu kwamba ipo nguvu kubwa kuliko sisi inayojiendesha ndani mwetu, halikadhalika na ndani mwa viumbe vyote duniani na mbinguni?

Hii ninaiita Mungu. Je unajua ilivyo kumfahamu Mungu pamoja na kuwa na ulinzi wake? Kumfahamu Mungu ni kuuendeleza upendo kwa watu wote pamoja na viumbe wote.

Kumfahamu Mungu ni kujisikia kuwa na Amani miongoni mwetu utulivu, kutotishika kunakoweza kukufanya kupambana na lolote lile unalokutana nalo. Kumfahamu Mungu ni kujawa na furaha inayotoa povu liwezalo kusambaa na kuibariki dunia yote.

Sasa ninayo hamu: Kufanya yale Mungu atakayo kwa ajili yangu. Hakuna ugomvi. Mungu anaponiongoza kutembea safari za hija ninatembea kwa furaha. Mungu anaponiongoza kutembea Hija nnafanya shughuli kwa furaha. Wakati Mungu anaponiongoza kuyafanya mambo mengine, nanayafanya kwa furaha. Kama yale niyafanyayo yananiletea sifa; mara moja, sifa hizo ninaziweka mikononi mwa Mungu kwani mimi ni chombo ambacho Mungu anatumia kufanyia kazi zake. Wakati Mungu anaponiongoza kufanya jambo hunipa nguvu, hunipa nyenzo za kazi, hunionyesha njia.

Hunipa maneno ya kuzungumza. Iwe njia ni ngumu ama nyepesi ninatembea kwenye mwanga wa upendo wa Mungu, amani na furaha. Na mimi humgeukia Mungu na zaburi za kumshukuru na kumhimidi. Huku ndiko kumfahamu Mungu. Na kumfahamu Mungu siyo jambo walilowekewa watu wakubwa tu, hata kwetu watu wakawaida. Mungu kila mara anakutafuata wewe, yaani kila mmoja wenu.

Utampata Mungu kama tu, utamtafuta kwa kutii sheria takatifu, kwa kuwapenda watu, kwa kuukana ubinafsi, kujiondoa kwenye mawazo ya kupenda vitu vya kumiliki. Ikiwa ni pamoja na mawazo na hisia potofu. Na wakati utakapompata Mungu itakuwa kwenye utulivu. Mungu utampata ndani.

**MAWAZO YA KUTAFAKARI:**

Huwezi kuona hata kiasi kidogo cha mwanga bila kuenenda katika njia yake. Mwanga huo hauwezi kuupata kutoka kwa mtu yeyote; na wala kuugawa kwa mtu yeyote. Hivyo chukua hatua chache na nyepesi ambazo kwako unaona zinawezekana na mara uanzapo kuuona endelea kuongeza hatua zingine zaidi ili uufikie kabisa.

Mara tu ujuapo nafasi yako katika mpangilio wa mambo kwenye mpango mtakatifu kamwe hutakuwa na ile hali ya kujihisi upungufu. Muda wote utapewa msaada katika hali yoyote utakayopambana nayo. Hakuna kukwama, daima utapata ulinzi.

Wakati unapokuwa na mawasiliano ya muda wote na Mungu, mapokeo ya muda wote kutoka ndani, kamwe huwi na mashaka utakuwa unafahamu njia yako. Wewe utakuwa chombo cha kufanya kazi zenye muelekeo wa mambo ya kiroho. Hivyo huwezi kuwa na hisia zenye mawazo ya ubinafsi.

Maisha ya kiroho ni maisha halisi vinginevyo ni ubatili na uongo. Wale wote ambao wanajihusisha na Mungu ndio walio huru. Wale tu ambao wanaishi kwenye mwanga, wa kiroho ndio walio kwenye upatanisho. Wale waishio kwa kuutegemea uchocheo wa maisha ya kiroho ndio nguvu pekee ya uzima. Siyo muhimu kwamba wengine wataathiriwa: matokeo kamwe hayatatafutwa na wala kutamamniwa. Ufahamu kwamba lolote la ukweli ulifanyalo, neno lolote jema usemalo, lolote jema ulifikirialo yote hayo yana matokeo mazuri.

Wachache hupata Amani ya ndani mwao si kwa sababu wanajaribu na kushindwa bali huwa hawajaribu kabisa.

Hakuna lolote lifanyikalo kwa kudra kwenye ulimwengu wetu. Kila jambo hujikunjua kutokana na uwezo wa zile sheria za juu zitawalazo mbingu na dunia kila jambo hujirekebisha kwa Amri ya Mungu.

Kuwahukumu wenzako hakukupatii lolote lililo la manufaa, bali kunakudhuru kiroho. Kama tu, utawashawishi wengine kujihukumu nafsi zao jambo lolote la maana lingefaa.

Nilikuwa mwangalifu kutokana na mambo ya kibinafsi ambayo hayakuwa na thamani kwenye maisha yangu. Kama uyafanyayo hayana thamani kwa wenzako zaidi yako, pia na kwako hayafai uyaendeleze.

Njia ya Mungu ni mojawapo ya miongozo michache ya tabia ambazo hata mtoto anaweza kuelewa. Ukweli ni kawaida. Ni vema kuutumia. Watu ambao hawajapata mwanga wa kiroho hujitahidi kuupotosha ukweli kwa kutoa maelezo ya hapa na pale kwa kutumia tafsiri mbali mbali bora yale wayateteayo yakubalike.

Utu uko kwenye hatua ya umuhimu wake. Mtu yeyote aweza kujihusisha kimawazo kwenye mkondo wa Umungu kwa kuugundua ukweli wa Yesu na mitume wake yale waliyotufundisha kuhusu Ufalme wa Mungu kwamba uko ndani mwetu.

Kama unataka kuwafundisha watu wawe wachanga wa umri ama wakubwa ni lazima uanzie mahali pale walipo kiuwezo. Na utumie maneno wayajuayo. Mara utakapokuwa umeelewana nao kihisia na kimawazo utaweza kuwachukua hadi pale ambako utahitaji kuwafikisha. Ukishang'amua kwamba tayari wamekwishafikia kiwango kilichoko juu yako katika kuelewa acha wao wakufundishe.

Hatua za kuelekea kwenye ukomavu wa kiroho zinachukuliwa hivyo. Wengi wetu tunafundishana mmoja kwa mwingine.

Maisha ni mchanganyiko wa mafanikio na mapungufu. Unaweza kutiwa moyo kwa mafanikio yako na ukakomazwa kwa mapungufu yako vile vile. Maadam hupotezi imani yako kwa Mungu, utakuwa mshindi katika hali yoyote itakayojitokeza mbele yako.

Ukiyatazama mambo kwa kutumia hisia zako tu za nguvu za mwili hutayaona kikamilifu, lakini ukiyatazama kwa uwezo wa nguvu za kiroho utayaelewa mara moja.

Yajali yale ya sasa. Fanya mambo yahitajiyo kufanyika. Fanya yote yaliyo mazuri kadri iwezekanavyo kwa siku. Yale yajayo yatajikunjua yenyewe.

Yapo mafunzo mengi ya kujifunza pamoja na vipimo vya kulinganisha. Sheria za mbingu na nchi haziwezi kugeuzwa kwa lile ambalo mtu mmoja kwake analiona ni jema. Mwanadamu ni lazima ajifunze kukubali kila kitu ambacho maisha yanamletea kama mkondo uwezao kumkomaza kiuzoefu. Ni kwa sababu hii ya kiroho iwezayo kuwakomaza watu ambao bado ni wachanga kiroho bila kuwategemeza kuishi kwa kuipokea misaada kutoka kwa wenzao. Mtafutaji lazima atembee mwenyewe na Mungu.

Ukiyatoa maisha yako kama mwombaji uipanue sala yako nje ya mipaka yote.

Ingawaje wengine watakuonea huruma, kamwe wewe usijionee huruma. Tabia hiyo yaweza kukupoteza kiroho. tambua matatizo yote bila kujali tatizo linao ugumu gani ikiwa ni njia ya kukukomaza kiroho. Na njia hiyo uitegemee.

Ili kuipata amani ya ndani huna budi kujitoa maisha yako yote. Siyo vitu vyako. Mara utakapokuwa umetoa maisha yako, ukaziweka imani zako kwenye fungamano na namna uishivyo, hapo, hasa hapo, utakuwa umeanza kuipata amani ya ndani.

# SURA YA NANE

## NJIA YA AMANI

Hii ndiyo njia ya amani: *shinda ubaya kwa wema, uongo kwa ukweli na chuki kwa upendo.*

Ni vigumu kwa watu kuelewa kwamba aina yoyote ya vita ni mbaya na inaangamiza. Watu ndani ya upofu wao wanajaribu kuushinda ubaya kwa kuyatenda yaliyo ya mabaya na hali hii inauzidisha ubaya. Ni mema tu, yawezayo kuushinda ubaya.

Ujumbe wangu ulio rahisi kuhusiana na amani unatosha- ni ujumbe usemao kwamba njia ya amani ndiyo nia ya upendo. Upendo ni nguvu kubwa zaidi ya zote duniani. Unayashinda mambo yote.

Mtu aliye kwenye upatanisho na sheria ya Mungu ihusuyo upendo anazo nguvu nyingi kuliko jeshi. Mmoja hatashinda adui bali uadui unageuzwa kuwa upendo.

Siku moja wakati nilipokuwa ninatembea kwenye barabara kuu nilianza kuimba wimbo wenye maneno ya amani kwa sauti ya kawaida ambao unatuonyesha matokeo yanayoendana na hali ngumu ya ulimwengu wa sasa:

> ***Ulimwengu uko kwenye mahangaiko ya utengenezaji wa zana za kivita,***
> ***Ulimwengu uko kwenye maandalizi ya maangamizo ambayo hayajawahi kutokea,***
> ***Nasikia laana nyingi za maadui na majadiliano yanaongezeka.***
> ***Lakini oh, dunia inacho kiu ina hamu kubwa.***
> ***Inasali ikiomba Amani- Amani!***

Bomu la nyuklia linatuambia: " Fanyeni amani ama muangamie!" Tunatambua kwamba hatuwezi tena kufikiria kupata ushindi kwa njia ya vita, kwamba vita vya nyuklia vina maana ya kutuangamiza kabisa. Wengi wanaiangalia hali hii kwa kufahamu matokeo yake yatakavyokuwa mabaya na mioyo yao inakuwa ya baridi. Baadhi kwa kuchanganyikiwa lakini wachache wao wanaiangalia hali hii kimatendo.

Ipo haja kubwa ya kufanya matendo ya kuleta amani. Tunaishi kwenye kipindi kigumu cha maisha ya mwanadamu na baadhi yetu tunaoishi sasa inatulazimu tuchague kati ya haya yafuatayo: Tuingie kwenye vita vya nyuklia vyenye kutuangamiza ama kipindi kizuri chenye maisha ya amani. Wote wanaoishi sasa watasaidia kutoa uamzi huu kwani hali ya sasa ya kiulimwengu inatuongoza katika mkondo wa uharibifu huu.

Hivyo wanaoamua kukaa kimya wanataka kuiacha dunia ielekee kwenye mkondo wa maangamizi. Wale wanaotaka amani lazima wafanye juu chini kuileta amani. Wawe chachu iwekayo nguvu ambayo hivi sasa imekwishaanza na inaendelea miongoni mwa jamii katika harakati za kuleta Amani. Na wasaidie kuiendeleza vilivyo ili kuubadili mwelekeo wa wimbi hili hatari. Katika hali hii ya kuelekea kwenye uharibifu wa ulimwengu amani iwe shughuli kuu ya kila mmoja wetu. Muda wa kushughulikia amani ni huu!

Amani kamili inaanzia ndani mwetu.

Tukipata amani ya ndani hakutakuwapo na ugomvi, hakuna tena vita. kama hii ndiyo amani uitafutayo, utakase mwili wako kwa kuyatenda yaliyo ya tabia njema, yatakase mawazo yako kwa kuziondoa fikra potofu, takasa mwenendo wako kwa kuyaondoa mawazo mabaya ya uchoyo ama ubinafsi na utake muda wote kuwasaidiawenzako, itakase hamu yako kwa kuondokana na tamaa ya kumiliki vitu na uwe na hamu ya kumjua Mungu na yale ayatakayo uyatende. Uwashawishi wengine kufanya kama hayo.

Baadhi watapendelea kufanya shughuli za amani, kuunda mbinu za kuondoa ugomvi katika ulimwengu ambao migongano inaendelea- kiasi kwamba ingawaje migongano ya kifikra na kisaikolojia itakuwa bado ipo, lakini migongano ya kivitendo itakuwa imemalizika. Kama hii ndiyo Amani uitafutayo fanya juu chini katika ngazi ya kimataifa kutangaza upunguzaji wa silaha kali duniani na uijenge upya, serikali ya ulimwengu itakayojumuisha watu wote, kwa fikra za kiulimwengu, tuuweke mbele utu wa mwanadamu badala ya kutanguliza utaifa wa mtu atokako. Nikiwa na maana kwamba watu wote ni sawa. Fanya juu chini kubadilisha kazi ya idara ya ulinzi kwenye taifa lako badala ya kushughulikia maangamizi ya watu ifanye kazi ya kujenga amani. Kazi kubwa ya kujenga amani inatakiwa kufanyika ili kuokoa watu wenye bahati mbaya duniani pamoja na urekebishaji wa uchumi wetu ndani ya hali yenye amani. Kama yapo matatizo mengi ya kutatua wapate wengine msaidiane.

Kwa wakati ule ule tunaweza kushughulikia amani ya ndani mwetu na amani ya ulimwengu. Kwa upande mwingine watu wamepata amani ya ndani mwao kwa kuzama wenyewe ndani ya chanzo kilicho kikubwa zaidi yao. Kama chanzo cha amani ya ulimwengu.

Kuipata amani ya ndani ni kujiondoa kwenye hali ya ubinafsi na kuelekea kwenye nguvu za kiroho, kwa mema ya vyote .

Kwa maana nyingine mojawapo ya njia za kushughulikia amani ulimwenguni ni kuishughulikia amani kwanza ndani mwako. Kwa sababu amani ya ulimwengu haiwezi kuwa imara mpaka wengi wetu wapate amani ya ndani mwao kuiimarisha.

Amani ya ndani mwangu inabakia bila kujali mambo ya nje. Ninavyoendelea kudumu kwenye upatanisho ndivyo nitakavyowavuta wenzangu kuingia kwenye upatanisho. Na upatanisho mkubwa unahitajika kwanza kabla ulimwengu haujapata amani. Hii haina maana kwamba sihusiki na matukio ya ulimwengu. Muda kama huu unaita \ aombezi wa amani pamoja na juhudi za kuleta amani. Kazi zote za kweli pamoja na sala zote za kweli vinayo majibu mazuri.

Juhudi bora huzaa matunda bora, bila kujali kama matunda hayo yanaonekana kwa macho au la. Pamoja na giza kuu katika hali ya dunia hii ya sasa sikatishwi

tamaa. Najua kwamba kadri maisha ya mwanadamu yanavyoelekea kwenye upatanisho kupitia kwenye milima na mabonde, hivyo jamii nzima ina kupanda na kushuka katika kuitafuta amani.

Ndani ya mioyo ya watu imo hamu kubwa ya kupata amani hapa duniani, wangeongea amani kama wasingekuwa wamefungwa na hali ya giza la kutojua wafanye nini, hali ya woga na ujinga.

Ni kazi ya waleta amani kuwashawishi watu hao waondokane na hali hiyo. Kuondoa ujinga kwa kuuelekea ukweli kuondoa woga wao kwa imani ambazo sheria ya Mungu hutengeneza, ambazo ni za kudumu.

Wajue kwamba mambo yote kinyume na sheria ya Mungu niubatili. Tuache kukata tamaa na tuitumaini dunia isiyo na vita. Amani inawezekana kwani mawazo yanayo nguvu ya ajabu.

Wachache ambao kwa hakika wameyatoa maisha yao kumtumikia Mungu wanaweza kuyaepusha mabaya yasiwapate wengi walio nje ya upatanisho na sheria takatifu za Mungu. Hivyo sisi tufanyao kazi kwa ajili ya Amani hatutababaika. Tuendelee kusali tukiombea amani na kuyafanya matendo ya amani kadri iwezekanavyo. Lazima tuongelee amani na tuishi maisha ya amani. Kuwashawishi wenzetu lazima tuendelee kuifikiria amani na tuamini kwamba amani inawezekana. Tutegemeacho ni kusaidia kuifanya ionekane kuwapo. Mtu mmoja mdogo anayeutumia muda wake wote kwa ajili ya kutangaza Amani huleta taarifa. Watu wengi ambao wanatumia muda wao kwa kutangaza Amani wanaweza kufanya jambo la kihistoria.

Siku moja mwanamke mmoja aliniambia; " Amani, ninasali pamoja na wewe kuomba amani lakini siamini kama inapatikana."

Nilimjibu; " Huamini kwamba amani kuwepo kwake ni utashi wa Mungu?" " Ndiyo!" Alinijibu. " Ninajua ndivyo ilivyo." ' Sasa wawezaje kuniambia kwamba lolote lililo utashi wa Mungu haliwezekani?" Na hatusemi inawezekana tu, bali ni hakika inawezekana. Na inachukua muda gani kwetu kuipata hali hiyo?

Jibu ni kwamba; uamuzi umo ndani mwetu.

Kamwe usiidharau nguvu ya kikundi kidogo kifanyacho kazi yenye kuleta mema kwa watu. Sisi sote tunashughulika pamoja kwa ajili ya amani, sisi sote tunaosali kwa pamoja kuomba amani ni kikundi kidogo cha watu lakini kinayo nguvu kubwa ya kiroho. Nguvu yetu ni kubwa kuliko idadi yetu.

Wale wanaoonyesha kushindwa wanatengeneza njia na mara nyingi wanatoa mchango mkubwa kuliko wale ambao hatimaye hushinda.

Siwezi kueleza ukubwa wa furaha yangu kwa waasisi wote wa
amani waliotetea amani kwenye hali ya machafuko na hakuna matokeo ya wazi yaliyoonekana.

Mojawapo ya maswali ya kawaida mengi niliyoulizwa lilikuwa: " Umewahi kuona matokeo yoyote kutokana na shughuli zako za hija ?" Na nilijibu kwamba mimi sihitaji kuona matokeo. Matokeo nayaacha mikononi mwa Mungu. Matokeo yanaweza yasionekane katika kipindi cha uhai wangu lakini mbeleni yataonekana.

Na, amini usiamini, matokeo nimeyaona: Nimepokea barua nyingi zikinijulisha jinsi watu walivyokwisha shawishika kufanya mambo ya Amani na wengine wakiandika kwa rafiki na ndugu zao bunge la Congress kuwashawishi kuhusu uenezaji wa amani. Yote hayo ni matokeo.

Sasa ninapoangalia nyuma kwenye juhudi zote ambazo zimekwishafanyika kutokana na waeneza amani, ninayaona matokeo.

Nilipoanza shughuli za hija, watu waliona vita kama sehemu muhimu ya maisha yao. Sasa waenezao amani wako kwenye upande wamafanikio, wamejulikana. Nilipozianza shughuli zangu watu wengi hwakuwa na moyo wa kutafuta amani ya ndani mwao. Nilipofanya uchunguzi wangu niligundua kwamba kati ya wanafunzi theluthi mbili na robo tatu wa chuo fulani hawakuamini uwepo wa Mungu.

Sasa ni vigumu sana kumtafuta mwanafunzi wa aina hiyo ukampata. Kwangu mimi hilo ni tumaini kubwa kuliko yote.

Kwa upande mwingine itasemwa kwamba; *ni hatari iliyoje ya watu kukomaa kimaarifa katika kiwango cha juu kiasi cha kujitengenezea zana za kutudhuru sisi na ulimwengu wetu!* Upande mwingine pia itasemwa kwamba: *Vema iliyoje hadi tukagundua kwamba ushindi wa kuleta amani kwa njia ya vita ni muhali hivyo hata wale waliomo gizani na wale walio wabaya wameng'amua jambo hili na wameziweka silaha zao chini.* Taarifa zote mbili ni sahihi.

Hakuna kizuizi chochote kikubwa katika kupatikana kwa amani ya ulimwengu ama amani ya ndani kuliko woga.

Woga umetuongoza kutengeneza silaha kubwa ziwezazo kutuharibu kabisa ikiwa ishara ya kujihami. Tukiogopacho hutufanya kujenga chuki isiyo na sababu hivyo kujikuta tunabeba mambo mawili ambayo ni woga na chuki. Hii pekee haiwadhuru watu kisaikolojia pamoja na kuuweka ulimwengu katika hali ya wasiwasi ila tunajiweka kwenye mfumo wa kuvutia lile tuliogopalo litutokee.

Kama hatutaogopa kitu na badala yake tuenende katika upendo tutakuwa tunategemea yaliyo mema. Ni kiasi gani ulimwengu huu unauhitaji ujumbe na mfano wa upendo pamoja na imani!

**Amani na uhuru! Mambo haya yatakuwa! Ni lini mambo haya yatakuwa iwe sasa ama baada ya maangamizi makubwa na mwanzo mpya, yote ni juu yetu.**

Uchunguzi mwingi na majaribio vyahitajika kufanywa kama njia za amáni kuifuta migongano ya dunia. Tufanye kazi kwa vikundi ama mtu mmoja mmoja kutegemeana na pale alipo, ikifanyika miradi ya kueneza amani tukisifia na kutia nguvu mazuri popote yanapofanyika.

Unaweza kutegemea kugeuza taifa moja lile lako. Baada ya taifa lako kuwa limebadilika, mfano wake utayashawishi mataifa mengine yabadilike. Kama taifa moja kubwa litakuwa na nguvu za kiroho kiasi cha kuamua kuweka silaha zake chini na kutokeza kwenye uso wa dunia likiwa na mikono mitupu, ulimwengu utakuwa umebadilika. Sioni ushahidi kwamba taifa lolote kubwa linazo nguvu kubwa za kiroho na moyo wa kuyafanya hayo. Kwa hiyoupunguzaji wa silaha utafanyika kwa hatua za taratibu, utasukumwa na utashi wa kuishi.

Giza tulionalo kwenye uso wa dunia hii leo, ni kutokana na kutokuwapo na mshikamano wa vitu ndani ya upatanisho na sheria ya Mungu. Msingi wa migongano sio kati ya taifa na taifa bali ni **kati ya tofauti za kiimani.**

Tofauti ya kwanza ikiwa kwamba ubaya unaweza kumalizwa na ubaya zaidi. Imani hii ndiyo itumikayo katika ulimwengu wetu wa sasa. Ni njia ya vita. Ni nafasi itawalayo kwa kila taifa kubwa.

Kuna njia nyingine iliyofundishwa miaka elfu mbili iliyopita ya kuushinda ubaya kwa mema, ambayo ndiyo njia yangu aliyotufundisha Yesu. Kamwe usipoteze imani. Njia ya Mungu itadumu milele.

Ili ulimwengu upate amani watu lazima wawe na amani. Miongoni mwa watu ambao wamekwisha pata mwanga wa kiroho vita kwao halitakuwa tatizo.

Haitawezekana. Katika kipindi chao cha giza watu kwa wakati mmoja wanataka amani pamoja na mambo ya kivita. Hata hivyo, watu wanaweza kuupata mwanga wa kiroho taratibu kama vile mtoto akuavyo. Ndiyo, serikali zetu na viongozi wake ni taswira ya hali hii ya giza. Hii mara kwa mara inaturudisha nyuma kule ambako wengi wetu tunataka kupaepuka. Kufanya mambo ya kunufaisha nafsi zetu tu. Tutakapokomaa kiroho tutawachagua viongozi wazuri watakaotuongoza kuzipata serikali nzuri.

Masikani matakatifu ya amani yamo ndani mwetu. Itafute na vingine vyote utaongezewa. Tunasogea karibu na muda ambao wengi wetu tutakuwa tunayo amani ya ndani mwetu kuzijenga serikali zetu kwa furaha ya wengi. na haya yakishatokea, serikali zenyewe kwa njia ya mifano, zitawaongoza wachache walio gizani kuupata mwanga wa kiroho.

Amani itakuja ulimwenguni sawa na ilivyokuja kwetu.

Tumepitia kwenye vita vya kitaifa, vita vya wahindi wekundu pamoja na mapigano ya kushindanisha watu wawili mambo ambayo yamedumu mamia ya miaka iliyopita. Mbinu zimewekwa kuondoa mapambano halisi wakati mapambano ya kisaikolojia yanaendelea. Vitongoji vidogo, nchi ama majimbo vimejitoa na kuachia Taifa moja kama Marekani kuwa na haki ya kupigana vita. Ninaamini kutatokea kipindi ambacho, ndiyo; ninaamini kipindi kitakuja ambapo vitongoji vidogo, nchi ama majimbo, mataifa vitajitoa na kuaachia uongozi ulio mkubwa zaidi yao kama vile Umoja wa Mataifa ili kuwa na haki moja ambayo ni haki ya kupigana vita.

Siamini kwamba mataifa yataondoa haki zingine. Watu wanao uwezo wa kudhibiti mambo yao kuanzia ngazi ya chini. Lolote liwezekanalo kufanyika kwenye ngazi ya chini ni vema lifanyike na pia lielekezwe kwenye ngazi za juu kama haja ipo.

Umoja wa mataifa utafanya kama wajibu wake kuimarisha amaniulimwenguni. Endapo tutaendelea na hali ya kutokukomaa kiroho Umoja wa Mataifa utumie nguvu ya polisi kuwashughulikia wote walio wahalifu wa Amani ya ulimwengu. Kwa kufanya hivyo, ninatumaini kwamba watarekebishwa. Pia Umoja wa Mataifa utakuwa na jeshi lisilokuwa na silaha la kuzuia vita.. Pia kutakuwepo na jeshi la kuleta amani ambalo askari wake hawatakuwa na silaha yoyote ili kuzuia vita visitokee. Wakati taifa letu linashughulika na matatizo kama yale ya ukosefu wa chakula, Umoja wa Mataifa ushughulikie masuala ya nchi zinazodai uhuru- uhuru kwa sasa ni kiu ya kila moyo wa mwanadamu.

Niliwahi kuongea na mwanamke mmoja aliyependelea vita na wakati mwingine akiamini imani za ukristo, nilimwuliza; " Upande mmoja unaongelea umuhimu wa masuala ya ukristo na upande mwingine unasema; utumiaji wa nguvu si ndicho kitu pekee wanachokiheshimu?" Hili ndilo limekuwa tatiZo letu kwa vipindi vingi vya maisha. Tumekuwa tukiusifu ukristo midomoni mwetu tu lakini tukiyaendesha maisha yetu kwa ukali wa kucha na meno yetu! Tumenukuriwa; *" Hiyo siyo njia ya kuushinda ubaya, ushinde ubaya kwa wema."* Halafu tunashawishika kuushinda ubaya kwa kuutenda ubaya zaidi, kwa maana kwamba tunazidisha matendo mabaya.

Tunamuabudu Mungu, lakini hatuna imani katika kushughulika na sheria za Mungu zihusuzo upendo. Ulimwengu unasubiri maisha yenye sheria ya upendo ambayo itagusa mioyo ya jamii, yote na ibadilike kumuelekea Mungu.

Mchungaji wa Kanisa kubwa la huko Kanada ambaye majuzi amerudi kutoka matembezini huko Mashariki ya Mbali aliniambia kwamba Wabudha wanawatuma wamisionari elfu mbili kuwageuza wakristo waelekee kuishi kwenye njia za amani.

Wakati wa vita kuu ya pili vya dunia, mwalimu mmoja wa Kimarekani ambaye alikuwa anafundisha Shule ya Jumapili, akiwa kwenye eneo la Pasifiki alimteka askari wa Kijapani. Alipokuwa anamuongoza askari huyo kuelekea kambini, Mmarekani huyo akagundua kwamba mateka wake anaongea Kiingereza.

" Unajua kwamba ." Alisema huyo mateka, " Niliwahi kuwa Mkristo." Yule Askari Mmarekani alisita kwa muda kisha akasema; " Ni kwa nini uliuacha Ukristo?" Mtazamo wa mshangao uliutawala uso wa yule mateka wa Kijapani naye akajibu kwa sauti yenye kukanganyikiwa akasema; ***" Nitakuwaje askari na bado niendelee kuwa Mkristo?"***

Kitu ambacho watu hawakuking'amua ni kwamba amani inaweza kutumiwa kudhibiti kila aina ya ghasia hata vita ya pili ya dunia.

Nilikutana na Wadenimaki (Wadenishi) wanne waliotumia mbinuza amani na upendo kwenye vita ya pili ya dunia. Walisimulia

hadithi ya kushangaza.

Ni hivi, Wajerumani walipoiteka Ufaransa, Wafaransa wakawa wanawaua maaskari wa Kijerumani waliokuwa kwenye doria na matokeo yake Wajerumani wakalipiza kisasi kwa kuwaua watu wengi sana. Baadaye Wajerumani walipoingia Denmark; Wadenishi walianza mpango wa kutokushirikiana na maadui. Unaujua ule msemo usemao njia ya kuelekea kwenye moyo wa mtu hupitia tumboni. Wadenishi wengi waliitumia njia hii. Walimuongelea askari wa Kijerumani aliyekuwa katika doria; " Wewe ukiwa mwakilishi wa serikali ya Nazi, huna haki ya kukaa hapa kwetu zaidi kama ambavyo sisi tusivyo na haki ya kuja na kukaa katika nchi yenu, lakini utambue kwamba wewe ni kijana mdogo ambaye ametoka nyumbani kwao mbali sana na hapa. Na yawezekana hapa ulipo unatamani sana kurudi kwenu, na wewe kama mwanadamu mwingine yeyote alivyo utapenda kuitua silaha yako chini upumzike, tunakuomba uingie ndani ya nyumba ili ushiriki na sisi kwenye mlo wa jioni, hivyo karibu sana."

Haikuchukua muda yule askari Mjerumani akaafikiana nao.

Baada ya hapo askari wa Kijerumani alibakia akifikiri. " Watu hawa ni wazuri, tunachokifanya hapa ni nini?"

Wadenishi pia walitumia mtindo huo huo kuwakinga Wayahudi waliokuwa wakiishi Denmark.

Nilikutana na mwanamke mmoja wa Kiyahudi ambaye alikuwa ameolewa akiwa anaishi na wazazi wake huko Ujerumani chini ya utawala wa Adolf Hitler kwenye vita kuu ya pili ya dunia.

Aliolewa akiwa na umri wa miaka kumi na sita. Mtoto wake wa kwanza alizaliwa wakati mama huyo alikuwa na umri wa miaka kumi na saba na mtoto wa pili, akamzaa alipokuwa na umri wa miaka kumi na minane. Alikuwa na umri wa miaka kumi na tisa mambo matatu yalipomtokea.

La kwanza nyumba yake iliharibiwa na wazazi wake wakauawa kwa bomu la Waingereza. Ninadhani kwamba walikuwa wakifikiri kwamba wanamkomboa.

Jambo la pili lililomtokea, mumewe alichukuliwa na maaskari wa Nazi na alijua kwamba mumewe amekufa kwa kuwa hakumuona tena.

Jambo la tatu lililomtokea ni kwamba alijeruhiwa na watoto wake wawili kuuawa kwa bomu la Wamarekani. Tulipokutana naye alikuwa bado anaonyesha athari za majeraha yake.

Mara nyingine tulikuwa tunamkomboa kiroho. Akiwa katika hali ya majeraha alizunguka huku na huko akiwa na wakimbizi wenzake. Wakati mwingine matukio kama ya yule mama yanaweza kukufanya uongee kiroho. Mwanamke yule alianza kufikiri: *Wamejeruhi na hata kuharibu miili yetu, lakini wamejeruhi roho zao na hii ni mbaya zaidi.*

Ilimbidi asamehe na awaombee wote waliohusika na matatizo yake waliouawa na waliouа.

Aliweza kuiendeleza tabia yake hii nzuri kiasi kwamba; alifanya urafiki na Wajerumani ambao kwa kujitoa maisha yao waliweza kumtorosha hadi Uingereza, ambako pia alifanya urafiki na Waingereza wakamsaidia kusafiri hadi Marekani.

Sasa hii inadhihirisha ushindi wa ajabu wa kiroho ndani ya matatizo makubwa. Na hii pia inafafanua jambo lingine. Ni niniama ni nani aliyekuwa adui ya yule mwanamke? Alikuwa Mwingereza aliyeiharibu nyumba yake na kuwaua wazazi wake, ama Wajerumani waliomuua mumewe, au Wamarekani waliomjeruhi na kuwaua watoto wake wadogo? Jibu liko wazi na la kushangaza: ***vita ndiye aliyekuwa adui yake halisi.*** Ilikuwa ni imani potofu kwamba, mapambano ya kivita yangefaulisha jambo lolote, kwamba uovu ungeweza kuondolewa kwa kuutenda uovu zaidi. Huyo ndiye aliyekuwa adui wake zaidi na ni adui halisi wa wanadamu wote.

Mara moyo wa mwanadamu ukabiliwapo na matatizo makubwa pia hupewa nafasi kubwa ya kukua kiroho, hivyo jamii ya mwnadamu ambayo hukabiliwa na maangamizi pia hupewa nafasi ya kuingia kwenye kipindi cha kuinuka upya yaani

kipindi cha wokovu. Ninafikiri kwamba kuondoa ajali utashi wa kuishi utatuondolea vita vya nyuklia. Na ninaamini pande zote mbili zitabadilika. Tutajiongoza kuelekea kwenye maisha ya uchumi na demokrasia ya kijamii. Na wataelekea kwenye shughuli zaidi za kisiasa na demokrasia ya mtu na mtu. ***Taifa lenye itikadi yenye kulinganisha maisha bora ya mtu binafsi na maisha bora ya jumuiya halijajengwa.***

Hadithi zihusuzo maisha pasipo mapambano ya matumizi ya nguvu.

Siku moja nilipokuwa nikitembea kando kando ya ngome kuu kuu nilijiuliza ngome hii ingesema nini kwa watu wa ulimwengu kama ingekuwa na uwezo wa kuongea, na niliandika makala ifuatayo kuhusiana na ngome hiyo.

## NGOME KUU KUU INAONGEA:

" Nilipojengwa, muda mwingi na fedha vilitumika juu yangu kwa sababu ilifikiriwa kwamba ningelilikinga jiji lote dhidi ya wavamizi. Sasa nimesimama kwa upweke kwani haihitaji busara kubwa kuwaeleza watu kwamba hivi sasa sina kazi tena. Lakini si mimi tu nisiyekuwa na kazi tena bali hata na wengine wa kisasa hawana kazi tena. Ingawaje wewe kwa woga wako na kuchanganyikiwa kwako bado unawang'ang'ania wakulinde. Na wakati wewe kutokana na kuwa gizani bado unautumia muda wako mwingi na hazina yako kuwaimarisha, unajua moyoni mwako kwamba umesimama bila kinga ukiangalia kwa hamu kipindi kijacho wakati bomu la nyuklia ulilo nalo wewe linakuambia; **" Ufanye amani vinginevyo uishe!"**

Lakini si umekaa bila kinga kwa sababu, zana zote za kukukinga zimechakaa kama zinavyoonyesha kuwa? Je, umeisahau kinga ambayo haiwezi kuchakaa kinga ambayo imo ndani ya utii wa sheria zitokazo juu?

Kwa miaka mingi umekuwa ukiambiwa kwamba ubaya utaondolewa kwa mema na uzoefu unakuonyesha kwamba ukitaka kuwa na marafiki ni lazima uwe rafiki wa kila mtu.

Ni lini utakapokuwa na busara ya kutosha kukuongoza uache njia ikupelekayo kwenye maangamizi uifuate njia yenye kinga ya muda usiokwisha na umri usiozeeka na kubadilika? Watu wa dunia uamuzi uko mbele yenu! Bado unaweza kuchagua maisha na uchagueharaka iwezekanavyo."

## KIUMBE WA AJABU AITWAYE MWANADAMU:

Yeyote atokaye nje anaweza kukiona kiumbe hiki kiitwacho mwanadamu kama ifuatavyo:

" Kiumbe mmoja kutoka ulimwengu mwingine alikiegesha chombo chake cha kusafiria kwenye eneo fulani lililojitenga hapa duniani kwetu.

Kesho yake asubuhi akapita karibu na kambi moja ya jeshi ambapo aliona askari wakichoma singe kwenye mifuko fulani iliyokuwa imejazwa vitu ndani yake na

kusimamishwa kama nguzo." Hiki ni nini?" Mgeni huyo alimuuliza askari mmoja kijana aliyekuwa akikazana kuchoma singe kwenye mojawapo ya nguzo hizo.

" Tunafanya mazoezi ya kuchoma singe. Inatubidi tujifunze jinsi ya kutumia singe kama njia ya kuwaua adui vitani. Hata hivyo, hatuui watu wengi kwa singe, wengi huwa tunawauwa kwa mabomu.

" Lakini kwa nini mnajifunza kuwauawa watu? " Mgeni huyo aliuliza kwa mshangao !

" Hata sisi hatupendi. Tunaletwa hapa si kwa utashi wetu na hatuna la kufanya." Kijana huyo alijibu kwa uchungu.

Mchana huo kiumbe huyo mgeni alipita jijini akiwa kwenye matembezi yake akawaona watu wengi wamekusanyika kwenye uwanja wa taifa kuwashuhudia maaskari vijana ndani ya sare zao za kijeshi wakipambwa medali.

" Kwa nini wanapambwa medali?" Aliuliza huyo mgeni.

" Kwa sababu kila mmoja wao aliwaua mamia ya watu vitani. " Mwanamume mmoja aliyekuwa kando ya huyo mgeni alijibu.

Mgeni huyo kutoka mbali, kwa hofu kuu alimuangalia kijana mmoja miongoni mwa wale maaskari aliyeua watu mia moja akatoka salama.

Upande mwingine wa jiji mgeni huyo alisikia redio inatangaza kwa sauti ya juu kwamba mtu mmoja atanyongwa.

" Kwa nini anyongwe?" Mgeni huyo aliuliza.

" Ni kwa sababu aliua watu wawili." Alijibiwa na mtu mmoja aliyekuwa kando yake.

Mgeni alitoka pale ameshangaa.

Jioni hiyo baada ya mgeni kuwa amewaza sana alichukua daftari lake dogo la kumbukumbu akaandika yafuatayo:

> ***Inaonyesha kwamba vijana wote wanalazimishwa kuua watu kiufundi. Wale wanaofanikiwa kuua idadi kubwa ya watu wanatunukiwa medali. Wale wanaojitokeza kuwa wauaji wadogo wakafanikiwa kuua watu wachache sana wanaadhibiwa kwa kunyongwa!***

Mgeni huyo alitikisa kichwa kwa huzuni akaongeza maneno yafuatayo:

> ***Inaonyesha kwamba viumbe hawa wa ajabu waitwao wanadamu wanajimaliza wenyewe haraka sana.***

## ONO LENYE TUMAINI LA AMANI

---

Mnamo mwisho wa siku zangu arobaini na tano za kufunga kwa maombi nilikuwa nimelala nusu usingizi na nusu niko macho nilipoona ono la ajabu—lilikuwa ono la tumaini.

Niliyaona mataifa ya ulimwengu yanajiandaa kivita. Niliongea nayo lakini hayakusikia. Niliyalilia lakini hayakunijali.

Niliyaombea kwa Mungu na wakati nikisali, na mara nilipogeuka pande zilizonizunguka niliona watu wa mataifa yote wakisali na mimi.

Tena nikaona ukungu uliokuwa unang'aa ukipanda juu kutoka kwetu wakati tulipokuwa tunaendelea kuomba. Taratibu huo ukungu ulianza kujiumba katika kiumbe ambacho kilionekana kung'aa na mavazi yake yaling'aa sana. Uso wake ulikuwa na mng'ao wa ajabu usio kifani; hata nikashindwa kuuangalia.

Kiumbe huyo alipoongea sauti yake ilikuwa kama ngurumo ya radi.

" Wekeni chini majambia yenu!"

Kiumbe huyo alisema. " Wale wakamatao jambia kwa mapambano wataangamia kwa jambia!" Na hapo hapo mataifa ya ulimwengu yakionyesha mshangao wenye woga yaliangusha chini silaha zao, na watu wa ulimwengu wakafurahi pamoja.

MAWAZO ZAIDI KUHUSIANA NA AMANI PAMOJA NA UPUNGUZAJI SILAHA:

---

Ninapenda kusisitiza tena kwamba sala za kweli huongoza kwenye matendo ya kweli, kwamba imani bila matendo si imani.

Njia nzuri ya kuyaweka mawazo katika vitendo ni kuandika barua uzisambaze kote kueneza amani.

Upunguzaji wa silaha ni jambo linalokwenda taratibu. Kwa sababu labda woga bado unatawala mawazoni mwa watu, labda bado yapo matumaini kwa baadhi ya watu kwamba matumizi ya silaha yatasaidia kuuzimisha moto wa mapambano uliopo sasa, labda utengenezaji wa silaha na kuziuza kwenye maeneo ya mapambano kiuchumi ni shughuli iletayo faida.

Huu umri mpya unahitaji kuthaminiwa.

Wale waliokuwa wanaongelea amani waliitwa kuwa na mawazo ya kiitikadi. Katika wakati huu wa matumizi ya nyuklia wale wenye mawazo ya matumaini mema wamekuwa ndio wasemao la kweli. Mara nyingi tumejifikiria wenyewe kuwa na mawazo ya juu kiitikadi. Sasa tutumie baadhi ya itikadi hizo katika kipindi hiki cha hatari.

Tuamini kwamba vita ni kinyume na utashi wa Mungu na nikinyume na mazoea ya maisha yetu na tuhisi kwamba njia ya amani ndiyo njia ya upendo.

Nitashughulikia amani kwa kutumia njia ya upendo, kwa kukisaidia kikundi chochote ili kitumie amani, kwa kulisaidia taifa ambalo mimi ni raia wake litumie amani, kwa kusaidia Umoja wa Mataifa utumie Amani na kwa kumuomba Mungu kwamba njia ya upendo itumike kote ulimwenguni.

Ningesema kwa majeshi, kwamba tunahitaji ulinzi, ndiyo; tunawahitaji.

Jeshi la anga lingesafisha anga, Jeshi la nchi kavu lingefanya uangalizi wa misitu ambayo haijaharibiwa, Jeshi la majini lingeisafisha bahari, walinzi wa pwani wangeiangalia mito yote nalo jeshi lifanye kazi ya utengenezaji wa miradi ya kuzuia mafuriko pamoja na mambo mengine yenye manufaa kwa maisha ya mwanadamu.

Tunajifungia wenyewe kwa kufikiri kwamba mambo hayawezi kufanyika. Wengi hufikiri kwamba amani duniani ni jambo lisilowezekana. wengi hufikiri kwamba amani ya ndani mwetu haiwezi kupatikana. Ni mmoja asiyefahamu kwamba haiwezekani yule ambaye amefanya.

Chanzo kikubwa cha ugumu wa maisha yetu ni kule kukaa gizani.

Hii ndiyo sababu ninaongelea sana ile amani ya ndani mwetu kama hatua ya kuelekea kwenye amani halisi ya ulimwengu. Kama tungekuwa tumekomaa kiroho, vita visingetokea, na amani ingedumu ndani. Kutokana na giza letu, la kuikosa nuru ya kiroho, hatufahamu sheria za mbingu na nchi na tunafikiria kwamba uovu unaweza kudhibitiwa na uovu.

Dalili mojawapo ya ugiza wetu ni uroho na tamaa ambavyo vinatufanya kushindwa kujifunza lile somo la maisha ya ushirika.

Sasa ninang'amua kwamba tusipowahi kuzidhibiti dalili hizo, hatutapata nafasi ya kuishi ili tupambane na chanzo chake.

Wakati wa vita vya Vietnam nilishiriki kikamilifu katika maandamano ya amani kwa ajili ya amani. Hicho kilikuwa kipindi cha kushangaza sana. Watu wa nchi hii (Marekani) walisimamisha vita vya Vietnam pamoja na serikali kuwapo. Hiyo inaonyesha jinsi gani umma ulivyo na nguvu katika nchi hii.

Tena zipo dalili za dalili, kama vile balaa la njaa la kulikumba eneo kubwa. Ningependa kumpa kila mmoja wetu ziada ya chakula safi, maji safi pamoja na hewa safi. Ningependa kusambaza mgao wa mahitaji yao na pia kuwapa ziada ya chakula kizuri kiondoacho mawazo pia na kuwapatia mazingira safi na mambo mengine yenye kupendeza. Vipi kama ungekuwa mwana mahesabu ukafanya hesabu uone watu wa mataifa wangekuwa na maisha mazuri kiasi gani kama mataifa yote ulimwenguni yangeacha utengenezaji wa zana za maangamizi na badala yake wawe na viwanda vya kuzalisha zana za kuiendeleza jamii ya wanadamu!

Lazima tutembee kutegemea nuru ya juu tuliyo nayo. Tuwasiliane na ndugu zetu ambao bado wako gizani kwa upendo mkubwa. Tujaribu kuwashawishi wafuate njia nyoofu. Wakati wowote uletapo upatanisho kwenye mazingira yoyote yasiyo na amani utakuwa unachangia kwenye chanzo cha Amani. Ufanyapo lolote kwa ajili ya amani ya ulimwengu, amani miongoni mwa vikundi, amani miongoni mwa watu binafsi, ama kwa ajili ya amani ndani mwako lazima ufanikishe picha kamili ya amani.

Tusisahau kwamba, kutokuzitii sheria za Mungu huleta maafa, ingawaje watu hatimaye huja kujifunza tokana na makosa.

Sasa hebu tuuangalie ulimwengu wetu. Ulimwengu masikini uliovaa vazi la vita. Tatizo letu ni nini?

Tumeelekeza mawazo yetu mabli sana upande wa vitu vya kumiliki. Hata kama hatunavyo, tunavitamani. Tunapungukiwa upande wa wokovu wa kiroho. Wakati wowote tunapofanya ugunduzi wa zana mbali mbali kwa njia ya teknolojia na ufundi jambo letu la kwanza ni kuzigeuza zana hizo kuwa silaha za kuwaua watu. Hii ndiyo sababu maisha yetu kiroho bado yanao upungufu. Uchunguzi sahihi kwa maisha yajayo uko upande wa wokovu wa kiroho.

Tunahitaji kuyaweka mambo yote mawili katika uwiano ili tuweze kufahamu matumizi ya zana tuziundazo kwa manufaa ya watu duniani.

Wakati wa vita vya Vietnam kulikuwa na shughuli mbalimbali za kueneza amani. Vita vilipokwisha kulikuwapo kutokujali tena shughuli hizo na kipindi cha kukata tamaa kilitokea. Ninadhani hiyo ilikuwa ni hali ambayo haingezuilika. Hali hiyo hutokea kila baada ya vita.

Baada ya kila vita huwa inatokea kipindi cha migongano ya kutumia nguvu. Hali hii niliiona baada ya vita kuu ya kwanza kadhalika ya pili. Ninakumbuka baada ya vita kuu ya pili; mwanamume mmoja huko Camden huko New Jersey aliwaua watu watano mtaani, na walipomkamata alisema; " Mlinifundisha kuua." Alifundishwa na jeshi. Mwanamume aliyekuwa kwenye mnara wa Chuo Kikuu cha Texas akatumia bunduki kuwaua watu kumi na watano na kuwajeruhi wengine alifunzwa na jeshi kuua alipokuwa kwenye vita vya Vietnam.

**GHARAMA YA AMANI:**

Tunavyoonyesha, daima tuko tayari kugharimia vita. Mara nyingi, tena kwa furaha kubwa tunatumia muda wetu na hazina yetu- viungo vyetu na hata maisha yetu- kwa ajili ya vita. Lakini tunategemea kwamba gharama ya kutuletea amani ni bure. Tunategemea kwa matendo yetu yasiyokuwa na utiifu wa sheria ya Mungu ndani yake yatatuletea matokeo ya amani.

Hakika, hatuwezi kupata amani bure- na hatuwezi kupata amani kwa kutozitii sheria za Mungu. Tutapata amani tu; wakati tutakapokuwa tayari kuigharimia hiyo amani. Na kwa ulimwengu uliolewa madaraka na kutawaliwa ma rushwa kutokana na uchoyo ukiongozwa na mitume wa uongo, gharama ya kuipata Amani kwa ulimwengu wa aina hii lazima iwe kubwa sana. Gharama ya amani ni utii wa sheria zilizoko juu. Ubaya anaweza kudhibitiwa na matendo mema na chuki kudhibitiwa na upendo. Ni njia njema tu ziwezazo kutufikisha kwenye mwisho mzuri.

Gharama ya amani ni kuondoa woga na badala yake imani itawale.Imani ambayo itatuongoza kutii sheria za Mungu ili tupate baraka zake. Gharama ya amani ni kuondoa chuki na kuuruhusu upendo kwa kiasi kikubwa mioyoni mwetu. Gharama ya upendo ni kuyaondoa majivuno na badala yake toba na unyenyekevu viyatawale maisha yetu tukikumbuka kwamba njia ya amani ndiyo njia ya upendo.

Gharama ya amani ni kuondoa uchoyo badala yake tujenge tabia ya kutoa, kwa maana hiyo hakuna atakayedhurika kiroho kwa kuwa na vitu zaidi ya mahitaji yake wakati wengine duniani wanavyo pungufu ya mahitaji yao.

Walimwengu, muda wa majadiliano ni mfupi. Unapimwa kwa miaka michache. Uamuzi ni wetu kama tutagharamia amani ama la! Kama hatutaki kuigharimia vitu vyote tulivyo navyo ikiwa ni pamoja na uhai wetu vitaishia kwenye ndimi za moto wa vita.

Giza lililoko ulimwenguni. Kwa sasa limetokana na utengano wa vitu vilivyo kinyume na sheria za Mungu. Kamwe tusiongee bila matumaini tukidai kwamba, hili giza kabla ya dhoruba bali kwa imani kuu ; tuseme kwamba hili ni giza kabla ya mapambazuko ya mwanga wa dhahabu wenye amani, ambao hivi sasa hatuwezi kuulinganisha na chochote. Kwa ajili hii hebu tutumaini tufanye kazi na tuombe.

## SURA YA TISA

### *UENDELEZAJI NA UPATANISHO*

Watu wengi wanao ufahamu m 'ogo wa sheria za kiroho kwamba uovu unaweza kudhibitiwa na matendo mema. Wapatanishi siyo kwamba wanazifahamu tu bali wamejaribu kuzitumia katika maisha yao. Katika kuzitumia wao hujaribu kuepukana na matumizi ya nguvu. Wale wanaopinga vita lakini wanapendelea kutumia nguvu ningependa niwaite wapinzani wa vita bali si wapatanishi. Wale ambao wanatumia njia za kukwepa mapambano yoyote ya kutumia nguvu kwa sababu wanaamini kwamba, ndizo njia bora ziwezazo kuleta matunda mema; ningependa niwaite wapinzani wa mapambano ya matumizi ya nguvu bali siyo wapatanishi. Wapatanishi hutumia njia isiyo ya mapambano ya kutumia nguvu kwa sababu wanaamini kuwa ndiyo njia sahihi. Itokee kwa vyovyote iwavyo wao hawaendi kinyume cha hapo.

Asili ya maumbile ya wanyama hufikiria njia za matumizi ya sheria za mwituni katika meno na kucha zao ili kukabiliana na upinzani. Lakini, sheria hizi hazitatui matatizo ya binadamu, kutumiwa kwake kwaweza kuahirisha utatuzi wa matatizo na mnamo muda mrefu baadaye tatizo laweza kutokeza uharibifu mkubwa.

Baadhi ya mataifa, hata wakati wanapokuwa wanatumia sheria za msituni katika mapambano yao kivita, huwa wanatambua kwamba; wapatanishi hawawezi kufanya vile wao wafanyavyo na huwaondoa kwenye shughuli za kijeshi. Badala yake huwapa shughuli ambazo hazihusiani na jeshi ama hutumia muda wao mwingi gerezani. Hakika watu hawa huitwa waaminifu katika malengo.

Hakika idadi yao ni ndogo sana. Hii ni kwa sababu katika kipindi hiki cha mwanzo, ni watu wachache ambao wamekwishapata utimilifu wa mwamko wa kiroho.

Ninapoongea kuhusu upanukaji wa upatanishi, ninang'amua kwamba ninaongea na ndugu zangu wapatanishi ambao ni kikundi kidogo kwenye jamii ya kisasa.

Nikiwa na kikundi hiki kidogo, ninakistaajabia na kukiheshimu sana, ningependa nijadili njia tatu za uendelezaji wa upatanishi ambazo nimezifanya.

Nimepanua upatanishi wangu kwa kutokutumia mapambano ya nguvu kisaikolojia hali kadhalika na mapambano ya nguvu kwa kutumia viungo. Kwa hiyo sikasiriki kwa lolote.

Na si kwamba ninaweza kuzungumza maneno ya hasira bali pia siwi na fikra za hasira. Kama mtu ananitendea tendo lisilokuwa jema ninamhurumia badala ya kumchukia. Hata pamoja na wale wasababishao mateso kwa wenzao ninawaonea huruma sana nikifahamu mavuno ya masikitiko ambayo yamewekwa akiba kwa ajili yao. Kama wapo wale walionichukia badala yake nitawapenda nikijua kwamba chuki itaondolewa na upendo. Nikijua kwamba, yapo mazuri kwa wanadamu wote ambayo yanaweza kufikiwa kwa njia ya mawasiliano ya upendo. Wale watumiao njia ya kutokutumia nguvu bila kuwa na upendo ndani mwao wanao ugumu waupatao. Kama utawalazimisha watu kuyafanya mambo kwa kuifuata njia yako bila ya kuwasaidia wabadilike na kuielewa njia hiyo na manufaa yake tatizo

halitakuwa limetatuliwa kikamilifu. Kama unaweza kukumbuka kwamba hatuko tofauti kwa kila hali itakuongezea utashi wa kubadili badala ya kushinda kwa njia ya mapambano ya nguvu kwa matumizi ya viungo.

Na upanuzi wa upatanishi ni pamoja na kuondokana na matumizi ya nguvu kisaikolojia halikadhalika kihali.

Nisingependekeza maasi ya kienyeji isipokuwa kwenye hatua ya mwisho. Kwa ujumla watu wanaweza kupata ufumbuzi wa matatizo yao nje ya gereza kulikoni wawapo gerezani. Pia sitii moyo tendo lolote la kitisho litakalotumiwa kama njia ya kupata ufumbuzi wa tatizo. Litendekalo kwa mtu mmoja linakuwa limetuathiri sisi sote.

Nimeupanua upatanisho kwa kuongeza kutohitaji malipo ya vita hali kadhalika na kutoshiriki vita. Ninaposema kutohitaji nina maana ya kutoshiriki malipo yoyote yahusuyo vita. Kwa hiyo mimi sina nilijualo kuhusiana na kodi ya Jumuiya. Zaidi ya miaka arobaini na tatu nimeishi maisha ya chini ya kutoweza kushiriki malipo ya kodi ya mapato. Ninakubali kwa sababu hii kwamba siwezi kupokea zaidi ya kile ninachokihitaji wakati wengine duniani wanacho kidogo zaidi ya mahitaji yao. Kiasili sijawahi kulipa kodi kupitia kwenye pombe ama tumbaku kwa sababu sijawahi kuvitumia vitu hivyo. Pia sihitaji kulipa kodi kupitia kwenye mambo ya anasa kwa sababu sifanyi mambo ya anasa.

Serikali ya Shirikisho ingekuwa inatoa msaada kwa baadhi ya vitu tunavyovikubali lakini kwa bahati mbaya haiko tayari kutoa. Mpatanishi angesema *hapana* mahali ambapo Serikali ya Shirikisho ingesema, " Kama mtatumia nusu ya muda wenu kwenye shughuli za kivita mtumie nusu nyingine ya muda wenu kwa kazi zilizo nzuri." Bado wako wapatanishi wasemao *ndiyo* kama ni suala la fedha badala ya muda. Ninang'amua kwamba wanadamu hujichunga kwa njia moja ama nyingine. Lakini tangu nijihisi kuwa naweza kujichunga nijuavyo nimeupanua upatanishi wangu kwa kutotoa michango yoyote kivita pamoja na kutokushiriki vita.

Nimeupanua upatanisho wangu kwa kutodhuru kiumbe chochote halikadhalika na mwanadamu. Kwa hiyo kwa miaka mingi sijala nyama ya kiumbe chochote ikiwa ni pamoja na samaki. Pia situmii sufu wala manyoya ya mnyama ama ndege, ngozi ama mfupa.

Nimeng'amua kwamba baadhi ya watu hupendelea mboga za majani kwa ajili ya sababu za kiafya na wala hawabanwi na sababu za kivita.

Wengine husikitika wakoswapo nyama, mimi la! Sina hamu tena ya nyama, kama wengine wanavyokuwa na hamu na nyama ya watu.

Ninafikiri wapatanishi wengi, hakika wengi, watu wa kisasa hawangekula nyama kama wangeua viumbe hao wenyewe. Ninafikiri kama ungetembelea machinjioni hali ambayo ungeikuta pale ingekutia moyo kuendeleza upatanisho ukiongezea tabia ya kutodhuru viumbe pamoja na kutowadhuru wanadamu.

Kuna mwamko unaojitokeza leo ambao kwa njia nzuri unakuwa katika mwelekeo mpya wa mageuzi. Labda utashi wa kuishi ndio utusukumao kuelekea huko---- Labda upo ung'amuzi kwamba ipo haja ya kufanyika jambo kuhusiana na hali yetu ya sasa ikiwa ni ushawishi kwetu. Vikundi ambavyo kwa desturi vimekuwa vikitumia nguvu za kimapambano ndivyo vinavyoongelea upinzani wa

matumizi ya nguvu. Watu ambao wameshiriki kikamilifu katika mambo ya vita sasa hivi wanaibukia kuwa wapinzani wakubwa wa vita. Idadi ya wapatanishi inaongezeka. Mimi, na kwa hiyo ninategemea wapatanishi kusonga mbele waendeleze upatanishi wao.

***Majadiliano yafuatayo ni miongoni mwa maandishi machache ambayo hujaji wa amani alibeba kwenye mifuko ya kisibau chake.***

**General Omar Bradley:** Vita vinaweza kuzuiwa ilivyo kama iwezavyo kuchochewa katika kuanza kwake, na sisi tushindwao kuizuia tunawajibika kwa vifo vya wote waathirikao kwa vita.

**General Douglas Mac Arthur:** Nimevifahamu vita kama watu wachache waishio sasa wanavyovifahamu. Vinao uharibifu mkubwa kwa pande zote mbili, upande wa marafiki (washirika) na upande wa maadui hali hii imeonekana kutokuwa na msaada katika harakati za kutafuta usuluhishi katika migongano ya kimataifa.

**Papa John wa XXIII:** Kama tawala mbalimbali zinatunga sheria ama kuruhusu matendo ambayo yako kinyume na utashi wa Mungu, si sheria zitungwazo wala mamlaka yatawalayo, vitakuwa na manufaa kwa raia kwani Mungu anayo haki kubwa ya kutiiwa kuliko mwanadamu.

**Dwight D. Eisenhower:** " Kila bunduki itengenezwayo, kila meli ya kivita itumiwayo kwenye mashambulizi, kila ndege ya kivita itumiwayo ni isharar ya mwisho kuonyesha wizi wa wazi wazi kwa wale wote wenye njaa wanaohitaji msaada wa chakula, wale ambao wanakufa kwa baridi na hawana nguo za kujisetiri." Akiongeza- kama mmoja wa walioshuhudia vitisho na kihoro cha vita-kama mmoja ajuaye kwamba vita nyingine itaweza kuangamiza kabisa ustaarabu wa mwanadamu." Alionya dhidi ya viwanda vya kutengeneza zana za kijeshi.

**John F. Kennedy:** Mwanadamu lazima akomeshe vita, vingenevyo vita itammaliza mwanadamu----. Vita itaendelea kuwapo mpaka siku ya mwisho ambapo waaminifu wa malengo watakuwa wanafurahia hadhi yao kwa waliyoyafanya kama ilivyo kwa mashujaa wa hivi vita vya sasa.

**Lyndon B. Johnson:** " Bunduki na mabomu, ndege za kivita pamoja na meli za kivita, vyote vinapotumiwa ni alama ya kushindwa kwa mwanadamu."

**Papa Yohana Paulo wa II:** " Kwenye uso wa maafa yatokanayo na mkono wa mwanadamu yahusuyo kila vita, mtu lazima aape na arudie kuapa tena na tena kwamba thamani ya vita haiwezi kuzuilika wala kubadilika. Utu haukupangwa

kujiangamiza wenyewe. Migongano ya kiitikadi, ushawishi pamoja na mahitaji lazima vitafutiwe ufumbuzi na ikiwezekana vimalizike kwa njia zisizo za kivita wala mapambano ya aina yoyote ya kinguvu."

**Herman Goering:** *Akiwa kwenye kikao cha mashauri Nuremburg:* " Kwa nini watu wanavichukia vita? Kwa nini mtu masikini anayeishi kwa kutegemea kijishamba tu cha kawaida akubali kuyatoa maisha yake mhanga kwenda kupigana vita wakati akisha rudi anakuwa hana lolote aliloliambulia zaidi ya kuendeleea kuishi maisha ya kawaida. Kiasili watu wa kawaida hawapendi vita. Si wale walioko Urusi tu; bali hata wale walioko Uingereza, Ujerumani na kwingineko. Hiyo inaeleweka. Zaidi ya yote ni viongozi wa nchi wanaopanga sera za nchi zao na ni jambo dogo tu kuwavuta watu waowazifuate sera zao bila kujali niza kidemokrasia, za kifashisti, za kidikteta, za bunge ama za udikteta wa ukomunisti.

Kwa sauti ama bila sauti watu daima huweka chini mamlaka ya watawala wao. Hiyo ni rahisi. Unaloweza kufanya ni kuwaambia kwamba wanashambuliwa. Unawatangazia kuwa wapatanishi wanakoswa uzalendo kwa kuiweka serikali yao hatarini. Yote ya aina hiyo hiyo yanafanyika katika kila nchi.

Sijawahi kuona yeyote aliyewahi kujenga hifadhi ya kujikinga na mlipuko wa bomu na ajihisi kwamba yuko salama. Sijawahi kuona askari jeshi mwenye hali ya kileo ambaye hakung'amua kwamba ushindi wa kijeshi ni wazo ambalo limefutwa na matumizi ya kipindi cha sasa cha nyuklia. Na hata raia walio wengi wanafahamu hivyo. Hekima inadai kwamba tuache maandalizi ya kugharimia vita ambayo itaufuta uhai wetu kwenye uso wa dunia, na tuanze maandalizi ya kufuta kabisa mbegu za vita.

## SURA YA KUMI

### *WATOTO NA NJIA YA AMANI*

*Nilikutana na mume na mke wake ambao walikuwa wamepania kwamba watawafundisha watoto wao wanne njia ya amani.* Kila usiku wakati wa chakula walikuwa wanatoa mahubiri juu ya amani. Lakini jioni moja nilisikia baba yao akimgombeza kwa sauti mtoto wao mkubwa wa kiume. Jioni ya pili yake nilisikia kijana mkubwa wa kiume akimgombeza mdogo wake wa kiume kwa sauti ile ile kama niliyoisikia jana yake. Walichokisema wazazi hakikufurahisha hata kidogo-waliyoyafanya ndiyo watoto waliyofuata.

Kupandikiza mawazo ya kiroho kwa watoto ni jambo muhimu sana. Walio wengi huishi maisha kutegemea mawazo waliyopandikizwa utotoni. Watoto wakitambua kwamba watapewa upendo endapo wataenenda katika matendo mema kamwe hawawezi kuwazia kutenda yaliyo mabaya.

Muhimu zaidi ya yote kumbuka kwamba watoto hujifunza kwa mifano. Bila kujali yale uyasemayo, ni yale uyatendayo ndiyo watoto wanafuata. Huu ndio mtihani mgumu kwa wazazi.

Je, unawafundisha watoto wako katika njia ya upendo ambayo ndiyo njia salama ya maisha yajayo?

Huwa inanigusa moyoni ninapoona mtoto mdogo anaangalia televisheni ambapo shujaa anamuua mtenda mabaya. Hali hii inamfundisha mtoto kuwa kuua mtu ni ushujaa. Shujaa alitenda jambo hilo na akapongezwa. Hiyo ilikubalika na shujaa aliendelea kufikiriwa vizuri hata hapo baadaye.

Kama wengi wetu tunaitafuta amani ya ndani kwa kutumia vyombo kama televisheni, mtoto mdogo angeona shujaa akimbadili mwenye matendo mabaya kuenenda katika matendo yaliyo mema. Angeona shujaa akifanya jambo la manufaa kuyaokoa maisha ya mwanadamu kimatendo. Kwa hiyo watoto wangepata fundisho kwamba utakapo kuitwa shujaa lazima uwasaidie watu.

Mzee mmoja wa kanisa ninayemfahamu aliwahi kuishi nchini Urusi. Hakuwahi kuona mtoto yeyote wa Kirusi akicheza na bunduki. Alitembelea bohari kubwa zenye bunduki za bandia mjini Moscow, akagundua kwamba bohari hizo hazikuwa na bunduki za bandia ama zana zozote zenye muundo wa maangamizi zilizo za bandia.

Mafunzo ya amani hutolewa katika vikundi vidogo vidogo vya jadi ambavyo vimo ndani ya vikundi vikubwa vya jadi. Ninawakumbuka Bwana na Bibi walioishi kati ya miaka kumi na miwili miongoni mwa wahindi wa kihopi. Waliniambia; " Amani, hali hii inashangaza wale watu hawajawahi kumdhuru mtu yeyote."

Nimetembea miongoni mwa Waamishi mimi mwenyewe. Wanazo jumuiya za watu zenye ukubwa wa kadri. Jumuiya hizo zina Amani na salama, zisizokuwa na migongano. Niliongea nao na nilitambua hali hii kuwa inatokana na watu kufunzwa

amani tangu utotoni, na kwamba litakuwa jambo lisilokuwa la fikra kumdhuru mwanadamu.

Kwa hiyo hawajawahi kutenda jambo kama hilo. Hali hii inaweza kufanikiwa kama umelelewa hivyo tangu utotoni.

Wakati fulani mwanamke mmoja aliniletea binti yake aliyekuwa na umri kati ya miaka minne na miaka sita akasema; " Amani, unaweza kumueleza binti yangu yaliyo mazuri na yale yaliyo mabaya?"

Nilimwambia mtoto; " Mabaya ni yale yenye kumdhuru mtu. Kama utakula chakula kisichofaa ambacho kitakudhuru hicho ni kibaya." Binti huyo alinielewa.

Niliendelea; " Mema ni yale yasaidiayo mtu. Ukichukua zana zako ziwezazo kudhuru zilizo za bandia ukazirudisha katika kasha lake kwa msingi wa kutozitumia tena hiyo itamsaidia mama yako. hilo ndilo jema. " Alinielewa. Wakati mwingine maelezo rahisi ni bora zaidi.

Walezi wangu waliponilaza kitandani walizoea kusema maneno mazuri ya busara wakisema; " Kumekuwa giza hivyo hiyo ndiyo hali ikufaayo wewe kupumzika na kupata usingizi."

" Sasa nenda ukalale kwenye hali nzuri yenye giza la kupendeza." Hivyo kwangu mimi giza nililizoea kama hali yenye pumuziko la kirafiki na kupendeza. Na wakati niamuapo kutembea usiku kucha kuuchangamsha mwili wangu ama nikiamua kulala usingizi kando ya barabara majira ya usiku, huwa najisikia mwenye furaha ya hali ile yenye giza.

Watoto huhitaji misingi bora mahali wanapokulia. Na wazazi lazima waone vema kuwachagulia watoto wao mazingira bora ya kukulia kabla hawajaanza kuishi nao.

# SURA YA KUMI NA MOJA

## *MAGEUZI YA JAMII YETU*

Nimekuwa nikiulizwa kama ninayo mawazo yoyote kuhusiana na ufumbuzi wa matatizo ya amani katika sehemu za maeneo ya ulimwengu pamoja na matatizo ya taifa.

Mojawapo, ninafikiri hatua moja ndefu iwezayo kutufikisha kwenye amani ya ulimwengu ni kuanzishwa kwa lugha ya ulimwengu.

Niliwahi kukutana na kizuizi cha lugha nilipokwenda kwa watu waongeao Kihispania huko Meksiko. Ilinilazimu kuongea kwa kumtumia mkalimani, ujumbe wangu uliotafsiriwa pamoja na tabasamu yangu.

Tena kwenye Jimbo la Kwebeki nchini Kanada nilikutana na tatizo hilo; kwa kuwa huko Kanada wanazo lugha kuu mbili (Kiingereza na Kifaransa).

Shule zote huko Kwebeki hutumia lugha ya Kifaransa, na watu walio wengi huko Kwebeki hawawezi kuongea Kiingereza. Nilitoa ujumbe wangu kwa njia ya kutafsiri na nilipewa chakula ma hifadhi kwa njia ya ishara! Pale mawasiliano ya kiuhuru yaliishia hapo. Hiyo ilinifanya nitambue upya, umuhimu mkubwa wa kuwa na lugha moja ya ulimwengu.

Ninafikiri kamati ya wataalam iliyoteuliwa na Umoja wa MAtaifa itaamua haraka iwezekanavyo ni lugha gani itakayofaa. Mara lugha ya ulimwengu itakapokuwa imetangazwa itaweza kufundishwa katika shule zote sambamba na lugha ya kila taifa.

Hivyo baada ya muda mfupi kila mtu ajuaye kusoma ulimwenguni ataweza kuongea na mwenzake msomi ulimwenguni. Ninafikiri hii itakuwa hatua moja kubwa tutakayokuwa tumeichukua katika maelewano ya lugha ulimwenguni, na hatua moja ndefu kuelekea kwenye amani ya ulimwengu. Tutakapokuwa tumeongea kwa pamoja tutagundua kwamba yale tuyapendeleayo ni makubwa zaidi ya tofauti zetu. Bila kujali tofauti zetu kubwa zitakazokuwa zikijitokeza.

## KWENYE DEMOKRASIA NA JAMII

Ninaieleza **demokrasia kama:** Udhibiti utolewao na watu. Watumwa ni wale wanaowaruhusu wengine kuyadhibiti maisha yao yote.

Zaidi ya hapo kadri watu wanavyofanikiwa kuyatatua maisha yao vema na kwa ufasaha kuanzia ngazi za chini wanakuwa na uwezekano mkubwa wa kuyadhibiti maisha yao. Zaidi ya hapo wanapoamua kushitakia matatizo yao ili yatatuliwe na ngazi za juu za utawala watakuwa wanapoteza udhibiti juu ya maisha yao.

Tunayo nafasi kubwa na nzuri ya matumizi ya demokrasia kwa mtu mmoja-mfano, haki ya wachache kwa mmoja kupata nafasi ya kuongea.

Tunazo demokrasia nyingi na nzuri za binafsi, kwa mfano, haki ya wachache impayo mtu nafasi ya kuendelea kuongea. Na tunazo demokrasia nyingi sana za kisiasa. Tunajenga maendeleo kwenye demokrasia ya kijamii.

Kama tungekuwa na demokrasia ya jamii kila mtu angefanyiwa tathmini kutegemeana na uzoefu wake katika mambo fulani fulani nawala siyo kutegemeana na vikundi.

Tumejitungia sheria kuelekea huko, inatubidi tuelekee huko kikakamavu, lakini tutafika.

Mahali ambapo tunaanguka ni kwenye demokrasia ya kiuchumi. Hapa hatunao udhibiti kamili, na hali hii inaugusa sana moyo wangu. Kumbuka kama tunataka kuonyesha mfano ulimwenguni ni lazima tuziinue hali zetu. Nitakusimulia habari ya kusikitisha:

- Nilikuwa ninatembea nikawa nimefika kwa mtu mmoja. Nilipokuwa kwenye chumba cha maongezi wachezaji wa michezo ya kuigiza walikuwa wawili wanaonyesha mchezo mbele ya watazamaji kwenye televisheni na mmojawao alisema; " Nilipata medali kutoka kwenye kampuni yangu."

" Kwa nini?" Mwenzake aliuliza.

" Niligundua njia ya kuifanya bidhaa izalishwayo kuharibika haraka!"

Kila mmoja kwenye halaiki ya watazamaji alicheka.

Hili siyo jambo la kuchekesha. Malighafi zinapatikana kwa shida, nguvu za kuendesha mitambo ya viwanda zinatumika bure. Vizazi vijavyo vitatuona sisi kama wendawazimu waliotengeneza bidhaa zilizoweza kutumika na kuisha baada ya muda mfupi.

Ndiyo, kila mmoja anafahamu tulifanyalo na hata wanatucheka. Hii inahitaji marekebisho, ni wazi kabisa.

Jambo lingine linalohitaji marekebisho ni ukosefu wa ajira. Hali hii nayo inaugusa sana moyo wangu. Kiasi cha watu milioni nane katika nchi hii (Marekani) hawana ajira. Hali hii inawahusuje? Jibu ni kwamba wanadidimia kisaikolojia kwa sababu wanaambiwa na jamii kwamba hawatakiwi, kwamba hakuna nafasi yao. Kukosa ajira ni jambo la hatari sana. Tunahitaji kulirekebisha jambo hili kwa haraka sana.

Ningependa kushauri kwamba; baada ya kipindi kirefu, cha muda wote walioajiriwa na wale wasioajiriwa wataomba kufanya jumuiya ambapo watalipwa kama jumuiya zinavyolipwa. Kazi yao haitahitaji kuchukua muda wa mtu sana, bali watakuwa wanatumia walichopokea kwenye hiyo kazi yao.

Hakuna mtu aliye na akili timamu asiyependa kuwa na shughuli ya kumshughulisha. Ninajua wapo wachache wenye akili za kuchangayikiwa hasa hasa wale ambao wamekaa bila ajira kwa muda mrefu hali hiyo imewadidimiza kiakili. Lakini hali hii si kweli kwa walio wengi. Wengi wao wakiona wamekosa ajira mara moja hupanga la kufanya.

Kutokana na mtazamo wa kiroho, ni kwamba; njia nzuri ya kushirikiana na chochote kilicho nje ya upatanisho na mapenzi ya Mungu kama vile Ukomunisti unavyoendeshwa hivi sasa, kamwe usikiogope. Hali ya kutoogopa inakuongezea nguvu.

Ulete mawasiliano mazuri kati yako na wale walioko nje ya upatanisho wa kiroho ili ulitakalo lilete matunda.

Uwe mfano mzuri. Kamwe usidhibiti matendo yao mabaya kwa kutumia falsafa mbovu. Mathalani, sehemu ya falsafa zitawalazo serikali za kikomunisti inasema: ***" Mwisho huthibitisha jinsi ya jambo " ambayo ni falsafa ya nchi zote zitumiazo vita kama njia ya mafanikio. Ni vema ufuate falsafa ya kiroho isemayo; " jinsi ya jambo hudhihirisha mwisho wake." Na kumbuka tu kwamba njia njemahakika ina mwisho mwema.***

Tunaweza kubadilika kutokana na mifano mizuri. Kwa hiyo kama ningekuwa na uwezo wa kufanya hivyo katika nchi hii ningeweka mfano mzuri.

Ningeanzisha idara ya amani kwenye serikali yetu. Ingefanya kazi muhimu. Ingefanya uchunguzi wa njia ambazo zingeondoa migongano ya kiugomvi, uzuiaji wa hatua za kivita na marekebisho ya uchumi kwa njia ya amani. Idara hiyo ingeanzishwa kwa shamra shamra na tungeomba kila taifa kuanzisha idara yenye malengo kama hayo ambayo ingeshirikiana na idara yetu kueneza amani. Ninafikiri kila taifa lingeridhia wazo hilo.

Mawasiliano miongoni mwa idara za amani ulimwenguni ingekuwa ni hatua ya kuelekea kwenye amani ya dhati ulimwenguni.

Wakati wa vita vya Vietnam niliwaandikia rafiki zangu wa kalamu kote duniani nikiwauliza swali lifuatalo: " Ni nchi gani ambayo wananchi wenzenu wanaiona kuwa ni tishio kubwa la amani ya ulimwengu?"

Jibu nililolipata lilikuwa la aina moja. Haikuwa Urusi wala Uchina. **" Tulikuwa ni sisi wenyewe Wamarekani!"**

" Kwa nini?" Niliwauliza.

Majibu yao yalitofautiana kiasi, wale wa kutoka nchi za mashariki walijibu kwamba; **" Kwa sababu ninyi ni taifa pekee lililotumia bomu la nyuklia kuua watu na hatuna ushahidi kuwa hamtafanya hivyo tena."** Huko Marekani ya Kusini na nchi nyingine za Latin Amerika waandishi wangu walisema; **" Leo ni kwa Vietnam-kesho ni kwetu."** Huko Ulaya pamoja na maeneo mengine jibu lililotoka huko lilikuwa; **" Uchumi wenu unajengeka vizuri kwenye nyakati za vita ama nyakati za maandalizi yake, " au" katika nchi yenu kuna fedha nyingi za kutumika vitani ama kwa ajili ya maandalizi yake."**

Sitaki kueleza haya niliyojibiwa kwamba si sahihi. Lakini sifikiri kwamba tunahitaji kuona kuwa nchi za ulimwengu mara kwa mara hazioni wema wetu zivushapo macho yao hadi kwetu kupitia baharini. Badala yake wanakuwa waoga wa matendo yetu.

Ningependa tujione kuwa siyo tu tunachukua hatua zote kadri tuwezavyo kupambana na ongezeko la silaha kali na tueneze amani ulimwenguni, pia ningependa sisi tuweke mfano mzuri na mzuri zaidi katika utetezi wa amani ulimwenguni kote.

Miaka miwili iliyopita, baadhi ya rafiki zangu kutoka nchi za nje waliniambia; " Urusi ilitia sahihi mkataba wa SALT II kwa nini ninyi hamkutia sahihi kwenye mkataba huo? Ina maana ninyi Wamarekani hamfurahishwi na kitendo cha upunguzaji silaha kali kuliko Warusi?"

Sikuweza kuwajibu. Laiti kama tungekuwa tumeweka sahihi!

Ilikuwa ni hatua nzuri ya kishujaa, si kama ingeleta matunda ya haraka sana lakini tungetia sahihi kwenye mkataba huo baadayetufanye kazi sana kuufanikisha mkataba wa SALT III pamoja na kushiriki kila mkataba wa amani ambao ungefanyika hapa ulimwenguni.

Kwenye hija yangu nchini Kanada nilialikwa kuongea kwenye tamasha la waimbaji vijana wa Shirikisho la Jumuiya za Kiroho la Kikristo, ambao kwa kawaida walijulikana kwa jina la Doukhoborda. Hiki ni kikundi cha wapatanishi waliohamia Kanada kutoka Urusi kwenye karne iliyopita.

Niliwaambia; " Mnao ujumbe muhimu hapa ulimwenguni; hasa hasa eneo la urusi. Kwa vile wengi wenu mnaongea Kirusi, ni kwa nini msitumie ujumbe wa amani huko Urusi? Kwaya hii kwa mfano, ikitumiwa, mnayo nafasi ya pekee kuongea na Warusi katika lugha yao kulikoni unavyoweza kwenda ujumbe mwingine huko usioweza kuwasiliana nao kwa lugha. Aina hii ya mabadilishano ni muhimu katika kipindi hiki chenye historia ya mapambano."

Umoja wa Mataifa unahitaji kuimarishwa. Sisi watu wa ulimwengu tunahitaji kujifunza kuiweka jamii yote ya mwanadamu iwe juu ya jamii ya kikundi chochote kiishicho. Njaa na mateso vinahitaji kupunguzwa. Majadiliano mapana ya watu miongoni mwa mataifa ulimwenguni ndio utakaokuwa msaada.

Yapo matatizo ya kitaifa yanayohusishwa na amani- kazi inatakiwa kufanywa kuhusiana na amani miongoni mwa vikundi. Tatizo letu la kwanza kitaifa hata hivyo; ni marekebisho ya uchumi wetu, kujengwa kwa njia za kiamani.

## MATENDO YA AMANI KWENYE JUMUIYA:

Katika kipindi hiki cha hatari kungekuwepo na kamati ya amani ya Jumuiya katika kila mji. Kamati hii ingeshirikisha watu wale waguswao kiroho.

Nimekuwa nikishauri kwamba Wanajumuiya ya Amani waanze na **kikundi cha maombezi ya amani** kwa ajili ya kutafuta amani. Mara ya kwanza mkutanapo mzingatie amani ya ndani. Iombee na mjadiliane kuihusu. Endapo mtagundua kizuizi miongoni mwenu kinachokwamisha maendeleo yenu kiroho, mzingatie sana kukutana ili mkiondoe hicho kizuizi. Mkutano wenu wa pili zingatieni upatanisho wa kiroho miongoni mwa kila mmoja wenu. Mking'amua kwamba mnapungukiwa upatanisho na mmoja wenu, fanyeni kadri inavyowezekana kwa kutumia mikutano kulirekebisha jambo hilo. Kwenye mkutano wenu wa tatu zingatieni upatanisho kati ya vikundi. Katika mikutano yenu jaribuni kufanya jambo kwa njia ya kikundi mkionyesha urafiki kwa yeyote na kuvisaidia vikundi vingine.

Kwenye mkutano wenu wa nne zingatieni suala la amani miongoni mwa mataifa. Chukueni hatua za kumpongeza mtu yeyote ambaye ametenda jambo jema katika kueneza amani. mkutano mwingine endeleeni kama mlivyoanza mwanzo.

Kwenye baadhi ya maeneo fasihi yangu imekuwa ikitumika kwa maombi ya vikundi kwa vile inahusiana na amani ipatikanayo kwanjia za kiroho. Soma aya, husika nayo kwa mapokezi ya kimya halafu izungumzie. Muwe na mikutano ya maombi, kadri iwezekanavyo kutegemeana na mahitaji yenu kutokana na fasihi hiyo.

Mtu yeyote atakayeweza kuelewa na ajihisi ukweli wa kiroho umeingia ndani mwake, tayari atakuwa amekamilika kuifanya kazi ya amani.

Baada ya maandalizi hayo kitakuja kikundi cha mafunzo ya amani.

Tunahitaji kupata taswira kamili kuhusiana na hali ya ulimwengu ilivyo sasa na ni mambo gani yatakiwayo ili kuubadili ulimwengu uingie katika mkondo wa amani.

Bila shaka vita zote zinazopiganwa hivi sasa lazima zikomeshwe. Ni dhahiri kwamba inatubidi tutafute njia ya kuweka silaha zetu chini sisi kwa pamoja. Inatubidi tuweke mikakati yenye miundo na mbinu zitakazo tuondolea mapambano ya silaha. Ulimwenguni mahali ambapo mapambano ya kisaikolojia bado kabisa yanaendelea.

Baada ya matatizo ya ulimwengu na hatua za ufumbuzi wake kuwa wazi kwako,wewe na rafiki zako muwe tayari kuunda **kikundi cha matendo ya amani.** Unaweza kuwa mwanachama wa kikundi hiki taratibu, mkishughulikia kila tatizo ambalo umelipata kutokana na mafunzo yako. Matendo ya amani lazima yaende sambamba na maisha ya amani. Pia yanaweza kwenda na muundo wa kuandika barua kwa watunga sheria kuhusiana na utunzi wa sheria zenye mwelekeo wa kudumisha amani, kwa wahariri wa magazeti mbali mbali ukitoa makala za kueleza amani, kwa rafiki ukiwaeleza yale uliyojifunza kuhusiana na amani. Hali hii inaweza kuchukua muundo wa kufanyika kwa mikutano ya hadhara ikiwa na wasemaji mashuhuri wa kuzungumzia amani, utawanyaji wa maandishi ya kueneza amani, kuongea na watu kuhusiana na amani. Kuwapo kwa wiki ya amani,

matembezi ya amani, maonyesho ya siku ya amani, gwaride la amani, maonyesho ya uogeleaji ya amani. Wale wote watakaochaguliwa kujiunga na vikundi mbalimbali vilivyotajwa hapo juu wawe ni wale wanaojihusisha kikamilifu na masuala ya Amani.

Mnayo nguvu kubwa mnapokuwa mnashughulikia jambo hili lililo la haki kuliko mnapokuwa mnashughulikia lile lisilo la haki. Na ilivyo ni kwamba jambo la haki likianzishwa yale yote yasiyo ya haki yanajifuta yenyewe. Shughuli za amani kuanzia ngazi za chini ni muhimu. Wale wote washughulikiao amani wawe kwenye kikundi maalum cha ndugu wa amani. Hata kama tunafanya shughuli hizo pamoja ama mbali mbali.

Baadhi ya hatua kuelekea kwenye amani ambazo niliziongelea wakati nilipoanza shughuli ya hija zimekuchukuliwa na zingine angalau zimeanza kuchukuliwa. Mzunguko mkubwa wa kuwasiliana na watu ana kwa ana unaendelea, kwa majadiliano ya wanafunzi pamoja na yale ya utamaduni. Uchunguzi kuhusiana na njia za kukomesha migongano hivi sasa unafanywa na vyuo vyetu, na mafunzo yanatolewa na jirani yetu; Kanada.

Ninaamini kwamba, inawezekana kabisa kwetu sisi kupata amani ya nje mnamo nyakati hizi. Kihistoria tunasema wakati wanadamuwanakabiliana na uamuzi kuhusu uchaguzi kati ya maangamizi na mabadiliko, lazima wachague mabadiliko, na ni jambo moja tu litakalowafanya wachague mabadiliko. Hivyo tunao uwezekano sasa hivi wa kuchukua uelekeo tofauti na huu uliopo leo ulimwenguni uwezekano hudumu.

Nyie watu wadogo wa ulimwengu. Tuache kujiona hatuna msaada tena. Hebu tukumbuke kwamba kama wengi wetu kwa kauli moja tutatamka jambo lolote tusilolitaka ili liondolewe, hata kama ni kubwa, mfano wa suala la upunguzaji wa silaha kali duniani; pamoja na utetezi wa amani, yote yatawezekana.

***Hebu tuombe kwa pamoja!***

## SURA YA KUMI NA MBILI

*NJIA ZA HUJAJI*

Niliwahi kuulizwa; " N' **mambo gani ambayo hujaji wa amani hufanya?"** Hujaji wa amani huomba na kufanya shughuli za kuieneza amani ndani na nje. Hujaji wa amani huamini kwamba njia ya upendo ndiyo njia ya amani na kutengana na njia ya upendo ndiyo kutengana na njia ya Hujaji wa Amani. Hujaji wa amani huzitii sheria za Mungu na huutafuta mwongozo wa Mungu katika maisha yake kupitia katika mapokezi ya kimya. Hujaji wa amani mambo yote katika maisha yake huyaona kwa kulingana na ndivyo awezavyo kuyatatua. Huweza kuuchimbua undani wa tatizo ili aligundue likoje. Hujaji wa amani hahitaji mrundikano wa vitu bali vitu rahisi na kiasi kwa ajili ya maisha yake. Mahitaj' ya lazima kwake ili aishi ndilo lengo lake kuu.

Hujaji wa amani huusafisha mwili wake daima kwani ıekalu la Bwana. Hujiweka kwenye utakaso wa mawazo, utakaso wa hamu, utakaso wa matendo. Hujaji wa amani huondokana kabisa na ubinafsi, hisia za upweke, umilikaji wa vitu pamoja na hisia potofu.

Sasa, kiutamaduni hujaji hutembea kwa imani bila kutegemea msaad wa chochote kionekanacho, bali kwa uwezo wa Mungu. Ninatembea hadi ninapewa hifadhi. Ninafunga kula hadi nipewapo chakula. Ni lazima vitu hivyo vitolewe, siviombi. Lakini vinatolewa!. Kila kitu ninapewa na baada ya kupewa ninatoa kwa mwingine. Ni lazima utoe kama unataka kupokea. Iruhusu 'si yako ya roho ikupe nafasi ya kutoa, toa, toa. Utakuwa umetoa vingi sana na hapo utagundua kwamba huwezi kutoa bila ya kupokea. Maisha ya aina hii hawakuwekewa watakatifu tu, bali yapo kwa watu wadogo kama wewe na mimi- endapo tutakuwa tayari kutoa kwa kila mtu.

Ni ujumbe wangu kama hujaji kufanya utarishi nikiwaeleza watu ukweli wa kiroho. Hii ni kazi ambayo nimeikubali kwa furaha na sitamani chochote kama malipo. Iwe pongezi ama heshima, sarafu zing'aazo ama dhahabu hakuna ninachokitamani. Ninafurahia kuufuata mnong'ono wa sauti nyororo niongelewayo na utashi ulio juu.

Ninavyo vingi vya kutoa. Kimsingi ninashughulikia sheria za Mungu ziishizo. Ninawasambazia wengine namna ya kumuelekea Mungu, ufalme wa amani ya ndani. Vyote hivyo ninavitoa bure, hakuna gharama.

Ulitokea wakati- nilipopata amani ya ndani, nilipokufa na kufufuka. Kipindi kile kabla sijafa nilikuwa sijaipata amani ya ndani. Kufufuka kwangu kulikuwa na ukombozi wa kiroho, hivyo kitambulisho changu cha wakati ule kabla ya kufufuka kwangu kiroho ninakikana.

Sioni sababu yoyote kuishi kwa yale yaliyopita. Hayo yamekufa na hayatafufuliwa. Usizipeleleze hizo habari zangu uniulize kuhusu ujumbe wangu huo

niutoao sasa. Siyo muhimu kumkumbuka mjumbe,la msingi ni kumkumbuka ujumbe aliokuletea.

Mimi ni nani? Ni vema kwamba wewe hujui mimi ni nani; hiyo haina umuhimu kwako. Hili vazi langu la udongo ni mojawapo ya mavazi mengine yasiyopatikana kwa gharama, ambalo linasafiri kwa kuhiji likieneza amani. Ni lile ambalo kwako huwezi kulionea umuhimu wowote. Mimi ni yule ninayetembezwa kwa nguvu za imani, ninaogelea kwenye nuru ya hekima ya milele. Ninadumishwa na nguvu zisizoisha ziwekazo mbingu na nchi; huyo ndiye mimi.

Mara kwa mara nimekuwa na hisia zenye mchanganyiko wa hofu na mshangao wa ajabu kuhusiana na nini Mungu awezalo kunifanyia kwa kunitumia mimi kama chombo chake. Ninaamini kwamba yeyote awezaye kujitoa kwa Mungu kikamilifu ataweza kutumiwa kwa heshima na hakika atafahamu baadhi ya mambo na yawezekana akaitwa mwenye nafsi ya haki. Unaitwa mwenye nafsi ya haki kama unao ukombozi wa kiroho kiasi kikubwa kuweza kufahamu kila kitu lakini pia waweza kuitwa mwenye nafsi ya haki na wale watu ambao hawajapata nuru ya kiroho ikuwezeshayo kufahamu baadhi ya mambo.

Hamu yangu ni kukazana kuelekea kwenye utimilifu, kuwa ndani ya upatanisho na utashi wa Mungu kadri iwezekanavyo. Kuishi katika nuru iliyo juu. Hadi sasa sijawa mtimilifu itakiwavyo, lakini ninakua kuelekea kwenye utimilifu huo kila siku. Kama ningekuwa mtimilifu ningekijua kila kitu na ningekuwa na uwezo wa kutenda lolote. Ningekuwa kama Mungu. Japokuwa ninaweza kulifanya lolote nipangiwalo na Mungu, na ninafahamu lile nitakalo kulifahamu kutenda wajibu wangu ndani ya mpango wa Mungu. Na nimepata furaha ya kuishi ndani ya upatanisho na utashi wa Mungu kwa ajili yangu.

Pongezi zote nizipatazo hazinigeuzi, kwani zote ninamkabidhi Mungu. Ninatembea kwa sababu Mungu ananipa nguvu za kutembea, ninaishi kwa sababu Mungu ananipatia mahitaji ya kuishi, ninaongea kwa sababu Mungu ananipatia maneno ya kuongea. Yote niliyoyafanya ilikuwa ni kuacha mambo yangu yote mikononi mwa MUngu ayatawale. Maisha yangu yote yaliniandaa kwa hatua hii ya kumkabidhi MUngu yaliyo yangu. Huu ndio wito wangu. Hii ndiyo kazi yangu. Hiki ndicho ninachostahili kukifanya. Sitakuwa na furaha kama nitayafanya mengine.

Wakati nilipoanza hija, niliondoka Los Angeles bila fedha yoyote, nikiwa na imani kwamba Mungu atanipatia kila kitu ambacho ningekihitaji. Ingawaje sijawahi kuomba chochote kutoka kwa mtu, Mungu amekuwa akinipa kila kitu niwapo kwenye njia zangu za hija. Bila kuomba chochote katika vile nilivyogawiwa.

Nina imani kwamba Mungu atanitunza, na Mungu atakidhimahitaji yangu.

Kwa namna yoyote ile sijisikii kukosa usalama kwa sababu sijui ni wapi nitalala giza likiingia, wapi au lini nitakula. Ukiwa na ulinzi wa kiroho, huwi na hali ya kuhitaji msaada wa usalama. Simfahamu yeyote ajisikiaye kuwa salama zaidi yangu- na ilivyo watu hunifikiria mimi kuwa fukara wa mafukara.

Ninafahamu sana, kuwa mimi ni tajiri mkubwa kati ya matajiri wote duniani. Ninayo afya njema, furaha, amani ya dhati- vitu ambavyo huwezi kuvinunua hata kama ungekuwa tajiri sana!

Mimi huzifanya shughuli zangu kwa urahisi na kwa furaha kubwa. Ninajisikia uzuri umenizunguka kote na ninaona uzuri huo huo kwa kila mtu ninayekutana naye, kwa sababu ninamuona Mungu ndani ya kila kitu. Ninautambua wajibu wangu katika mpangilio wa maisha na ninapata upatanisho kupitia kwenye furaha iishiyo ndani.

Ninatambua umoja wangu wa nafsi pamoja na watu wote waishio na umoja wangu wa nafsi na Mungu. Furaha yangu haielezeki katika kupenda na kutoa kila kitu nilicho nacho kwa kila mtu.

Kwa mwanga, ninakwenda moja kwa moja kwenye chanzo cha mwanga, na siyo kwa chochote kifananacho na hicho bali mwanga halisi. Pia ninafanya uwezekano wa kupata mwanga zaidi kwa kuuendeleza ule mwanga ulio juu kabisa ambao nimekwisha kuupata. ***Huwezi kukosea mwanga utokao kwenye chanzo kwani wenyewe huja na ufahamu kamili kiasi kwamba unaweza kuuelezea na kuujadili.***

Ninaipendekeza njia hiyo kwa wote wawezao kuupokea. Na baraka kubwa wamewekewa wao wale walio na busara ya kutosha iwawezeshayo kuiweka njia hiyo katika matendo kuhusiana na mwanga waupatao kutoka juu.

Kile kinachopokelewa kutoka nje kinaweza kulinganishwa na ujuzi. Kinamuongoza mtu kuamini, ambacho kwa nadra huwa na nguvu za kutosha kushawishi kufanyika kwa matendo. Kile ambacho kimethibitishwa toka ndani baada ya kuwa kimekutana na kile cha nje au kile ambacho moja kwa moja kimetambulika kutoka ndani (ambayo ndiyo njia yangu) kinaweza kulinganishwa na hekima. Kinaongoza kwenye ufahamu, na tendo huenda sambamba pamoja nacho.

Katika kushughulika na watu, mimi sitoi adhabu, sitoi amri na wala sifanyi shughuli za kiserikali. Kazi yangu ni kuamsha nguvu za kiroho kutoka ndani mwetu. Huu ndio wito wangu, kufungua milango yenye ukweli na kuwafanya watu wafikiri, kuwaamsha wengine waondokane na kukata tamaa pamoja na hali ya kuchoka na huwasaidia kuitafuta wenyewe ile amani ya dhati iishiyo ndani mwao. Hapa ndipo wajibu wangu unapokomea, siwezi kufanya zaidi. Yanayosalia nayaacha mikononi mwa nguvu iliyo juu.

Imani ni kuyaamini mambo ambayo fahamu zako hazijakutana nayo na akili zako haziyajui bali umefanikiwa kuyagusa kwa njia zingine na kuyakubali. Ni rahisi kwa mtu kuzungumzia Imani Ni jambo lingine la kuendeleza. Kwangu mimi, Imani huwakilisha kile ambacho watu wanaweza kukifanya kutokana na utashi wao ulio huru, wajitokeze na kumgusa Mungu kila wakati huwafikia watu. Kwangu mimi ni muhimu kwamba ninabakia kuwa karibu na Mungu muda wote bila kubadilika ama kuwa karibu na kusudio takatifu.

Watu walifikia kutokomaa kiroho kwa sababu ya kujirundikia mali na vitu. Wakati baraka za kiroho zijapo, vitu ulivyojirundikia pamoja na mali, kwako huonekana si muhimu. Lakini baraka za kiroho haziji hadi hapo tutakapokuwa tumezihitaji ikiwa ni pamoja na kuikana ile tamaa ya kujirundikia vitu na mali. Mara tunapokuwa tumetamani vitu na mali, hicho ndicho tupatacho bali roho zetu zinabakia na nguvu duni.

Wale ambao wameishinda nafsi yao na wakawa vyombo vya kufanya kazi ya Mungu wanaweza kukabiliana na majukumu mazito ambayo mtu wa kawaida hawezi. Lakini, hawahisi kujivunaia lile walifanyalo. Na wanashuhudia kutokuwapo na haja ya kutojivunia lile walifanyalo. Hivi sasa ninajua mwenyewe kuwa ni sehemu ya mbingu na nchi isiyoisha. Sitengani na roho zingine ama Mungu. Tabia yangu ya ubinafsi imekufa, nafsi yangu ya kweli inalidhibiti vazi langu la udongo na inalitumia kwa kuifanya kazi ya Mungu.

Nilipoanza shughuli yangu hii, nywele zangu zilikuwa zimeanza kuwa za mvi. Rafiki zangu walifikiri nimechanganyikiwa. Hakuna hata mmoja aliyenitia moyo kwa kazi yangu hii. Walifikiri mimi kutembea mwendo wote huo nilikuwa nikijitafutia kifo. Hilo sikulijali. Niliendelea na shughuli yangu nikakifanya kile nilichokidhamiria. Hawakufahamu kwamba mimi kuwa na amani ya dhati nilikuwa nimejazwa na Chanzo cha nguvu isiyoisha. Kulikuwapo na msukumo mkubwa wa kupinga hizo imani zangu lakini sikutetereka.

Kwa upendo niliwajulisha rafiki zangu wa kweli kuhusiana na njia mbili zinazotengana kwenye maisha pamoja na mtu kuwa na uchaguzi wa kuona ni ipi imfaayo aifuate.

Ipo njia ambayo imepambwa vizuri ipendezayo na huyakidhi mahitaji yote ya ulimwengu lakini haimfikishi mtu mahali popote!

Na ipo njia isiyotumiwa na walio wengi ambayo huitaji utakaso na kukana mambo ya kidunia. Lakini matokeo yake hukufikisha kwenye baraka za kiroho zisizoelezeka.

Ipo cheche ya uzuri ndani ya kila mtu, bila kujali imezama kiasi gani. ***Na hiyo ndiyo wewe haswa!*** Ninaposema " ***wewe*** " nini ambacho huwa ninakiwazia?

Huwa ninaliwazia vazi hilo la udongo yaani mwili wako?

La, hasha! Kwani hilo siyo wewe haswa! Je, ninafikiria ile asili ya unafsi wako? Hapana, Hiyo siyo wewe haswa! Wewe haswa ni ile cheche ya Ki-Mungu, wengine huiita nafsi ya ki-Mungu iliyo ndani mwako, wengine huiita asili ya ki-Mungu ama ufalme wa Mungundani mwetu.

Wahindi huiita nirvana; Wabudha huiita roho iliyoamka, Waquaker huiona kama Mwanga wa ndani. Maeneo mengine hujulikana kama Kristo ndani mwako, ufahamu wa Kristo, tumaini la heshima ama (nafsi hai) Roho iishiyo ndani mwako.

Hata Wanasaikolojia wanalo jina la kitu hicho- yaani ufahamu wa pekee. Lakini kitu ni kile kile kimevalishwa majina tofauti.

Jambo muhimu la kukumbuka ni kwamba kimo ndani mwako.

Usijali ni jina gani unalokiita kitu hicho, bali uwepo wake kwako utakufikisha mahali ambapo utaiona mbingu na nchi kwa mtazamo wenye U-Mungu ndani yako. Hisia zikiambatana na mazoea haya ndiyo umoja wa nafsi ulio kamili pamoja na mbingu na nchi kwa utimilifu wake. Mtu hutokea kuingia kwenye umoja na maisha ya kila kitu kimzungukacho kama vile : Utu, viumbe wote wa dunia, miti na mimea, hewa, maji na hata dunia yenyewe.

Hii hali ya kiroho inasubiri daima kuyatawala maisha yako kwa heshima. Unao utashi wa kuiruhusu iyatawale maisha yako ama la sivyo usubiri kuathirika na matokeo yake. Uamuzi daima ni wako.

Kutokana na vitu vyote ulivyovisoma, kutokana na watu wote unaokutana nao, chukua yale yaliyo mazuri kwako; yale mengine yaache. Kwa mwongozo na kwa ukweli ni bora sana kutafuta chanzo kupitia kwa mwalimu aliye ndani mwako kulikoni kutafuta vitabuni au kwa watu.

Kama sauti ndani mwako itasema;" Hili ni kweli. Hili ni kwa ajili yangu." Hali hiyo itakuwa sehemu ya mazoea yako.

Baada ya kuwa umesoma vitabu vyote, na umesikiliza mihadhara, bado unao ulazima wa kuamua yakufaayo. Vitabu na watu vinaweza kukuchochea kwenye mwanga wa kiroho. Labda kama vimeamsha jambo kutoka ndani mwako, lakini hakuna la maana linalofanyika. Lakini kama utalazimika kusoma vitabu vingi kiasi

kwamba utagusa migongano mingi ya kimawazo kadri iwezekanavyo. Kwa utaratibu huu utatakiwa kuunda ushauri wako.

Fikiri kuhusiana na mambo mema ya maisha yako. Kamwe usifikiri taabu na matatizo yako. Jisahau nafsi yako na uzingatie kuwa uko kwenye huduma kiasi uwezavyo hapa ulimwenguni. Baadaye, upotezapo ule unafsi wako wa chini kutokana na chanzo kikubwa zaidi yako, utaupata unafsi wako ulio juu yaani; unafsi wako halisi..

Kile nikizungumuzacho siyo cha kuchukuliwa kirahisi rahisi tu; lakini ninaweza kukuhakikishia kwamba mwisho wa safari yako ya kiroho utakuwa na thamani sawa na gharama iliyotolewa.

Ipo milima mingi na mabonde. Juhudi za mapambano ni kama kukwea mlima, kila ufikapo juu ya kilima kazana ufike juu ya hapo hatimaye utafika uendako.

Baadhi wameniuliza kama ninawakubali mitume.

Hakika sikubaliani nao. Siyo jambo jema kumfuata mwanadamu mwingine. Kila mtu lazima atafute mafanikio yake mwenyewe ya kiroho.

Shughuli yenyewe kuelekea kwenye mafanikio inachukua muda. Kipindi cha kukua ni tofauti kwa kila mtu.

Kwa nini unaniangalia? Iangalie nafsi yako.

Kwa nini unisikilize? Jisikilize nafsi yako mwenyewe.

Kwa nini unayaamini yale nikwambiayo? Usiniamini mimi ama mwalimu mwingine, bora uiamini sauti yako ya ndani. Huo ndio mwongozo wako, huyo ndiye mwalimu wako. Mwalimu wako yumo ndani na wala siyo nje. Jifahamu siyo kunifahamu mimi.

Tembea na mimi lakini usinifuate kiupofu. Ng'ang'ania ukweli siyo vazi langu la udongo.Mwili wangu ni vazi la udongo; ya leo yako hapa kesho yatakuwa yamekwenda.

Unapojihusisha na mimi hii leo, kesho nisipokuwapo utafanya nini?

Jihusishe na Mungu, jihusishe na utu, hapo tu utakuwa jirani na mimi.

Njia ya mtafutaji imejaa mashimo na vishawishi; naye mtafutaji hana budi kutembea mwenyewe na Mungu.

Ninakushauri kwamba miguu yako uiweke ardhini na mawazo yako uyaweke juu kwa Bwana, kiasi kwamba utavutia mema. Zingatia kutoa kiasi kwamba utakuwa unazifungua njia za kupata.

Zingatia kuishi kwa kuutegemea mwanga ulio nao kiasi kwamba utajifungulia njia za kujipatia mwanga mkubwa zaidi.

Pata mwanga mwingi kadri iwezekanavyo kupitia kwenye njia iliyo ndani mwako. Kama mapokezi ya aina hii yanaonekana kuwa magumu pata uchocheo kutokana na kuangalia ua lililo zuri au mandhari ya nchi iliyo nzuri, pia unaweza

kusikiliza muziki mwororo au maneno matamu. Hata hivyo, kile kipatikanacho nje chaweza kupata uthibitisho wa ndani mwako- kabla hakijawa chako.

Kumbuka kwamba yule atendaye yaliyo mabaya kwa hakika ni mgonjwa kisaikolojia na inambidi aangaliwe kwa macho ya huruma kama vile tumuangaliavyo mgonjwa wa kimwili. Kumbuka kwamba hakuna awezaye kukudhuru ila wewe mwenyewe. Kama mtu atakutendea jambo baya kwako huyo amedhurika. Hutakuwa umedhurika labda kama utauruhusu moyo wako, ama labda kama utakasirika ulipize kisasi kwa kutenda mabaya.

Mimi ninajifikiria kama mtumishi nifanyaye kazi kwenye vyanzo vya matatizo: ***Yaani ugiza wetu.***

Ni watu wachache tu ambao wako tayari kushughulikia vyanzo hivi vya matatizo. Kwa kila mmoja anayeshughulikia vyanzo vya matatizo ya watu wapo maelfu wanaoshughulikia dalili za matatizo hayo. Ninawabariki wote wafanyao kazi nje ya mwili kuondoa dalili za matatizo, lakini kimsingi ninaendelea kufanya kwenye hatua ya ndani kuviondoa vyanzo vya matatizo.

Hii ni kwa sababu watu wengi hawajapata kusudio lao pamoja na matendo kiasi kwamba wanakutana na maumivu yatokanayo na ukosefu wa upatanisho ndani mwao, hivyo kwamba mwili wa utuunaongozwa na vurugu. Wengi wetu tunaangukia katika ile sehemu ya kunyang'anywa badala ya kuzidishiwa:

***Wakati ulimwengu unaangamia sisi tunakwenda na njia yetu: bila lengo lolote, bila bidii yoyote ya moyo, siku baada ya siku.***

Katika kazi yangu nimechagua njia isiyo ya nguvu kuwaelekea watu. Kamwe sijawahi kujifikiria kuwa ninaweka upinzani dhidi ya jambo fulani. Bali kama mshuhudiaji kwenye maisha ya upatanisho. Wale washuhudiao hutoa uamuzi wa kile walichokiona. Wale washuhudiao yasiyotakiwa hawatoi uamuzi, wao huendelea kuishi wakitegemea yale yasiyofaa. Wakielemea kwenye hukumu, lawama na wakati mwingine wakiita majina. Kwa kawaida mwelekeo usiofaa unayo matokeo yenye kudhuru. Mwelekeo unaofaa unayo matokeo mazuri. Mbaya akishambuliwa, ubaya uliomo ndani mwake hujiandaa kuyajibu mashambulizi ingwaje ubaya huo unaweza kuwa na unyonge na kutokujiandaa. na kwa hiyo, mshambuliaji akajiona ni mwenye nguvu na afaaye. Kama mashambulizi hayakutumika na badala yake mwelekeo ulio mzuri ukatumika kukabili hali, si tu ubaya utakimbia bali yule mtenda maovu atumiwaye na ubaya atabadilika kuwa mtenda mema. Makabiliano mema hushawishi, mabovu hujenga hasira. Uwakasirishapo watu jibu lake ni kuwa watatenda lolote kutegemeana na mapambano ya kimwili pasipo kufikiri.

Unapowachochea watu kwa ushawishi wa kiroho watatenda kutegemeana na ushauri utokao juu kwa Mungu. Pia hasira ina mwisho mfupi wakati ushawishi na uchocheo wakati mwingine vinaleta matokeo ya muda mrefu.

Kuna kigezo ambacho kinaweza kukusaidia kuamua iwapo yale unayoyawaza na yale unayoyatenda yanakufaa. Kigezo hicho ni:

*Je, mambo hayo yamekwisha kukuletea amani ya dhati ndani mwako?*

Kama jibu ni bado basi ujue kwamba yana kasoro. Hivyo endelea kutafuta. Kama yale uyatendayo yamekuletea amani ya dhati ndani mwako; endelea na kile unachokiona kinafaa.

Ukiipata amani ya dhati ndani mwako, unakuwa mtu ambaye wakati wote anaweza kuishi na wenzake vema. Amani ya ndani haipatikani nje nje tu kwenye maisha, ama kwa kujaribu kuyakimbia maisha kwa namna yoyote ile. Amani ya ndani inapatikana kwa kuyaona maisha kuwa ni ya kawaida na sawa, kutatua matatizo yake. Na kupenya hadi ndani ya maisha kiroho kadri iwezekanavyo ili kugundua uhakika wake na uhalisi wake. Amani ya ndani huja kupitia kwenye imani inayokuweka mbele ya sheria za Mungu ambazo tayari zimekwisha fahamika zihusuzo tabia za mwanadamu kama vile sheria isemayo kwamba matendo huunda sura ya wakati wa baadaye.

Kwamba ni matendo mema tu yatufikishayo kwenye mwisho mzuri. Amani ya ndani hupatikana kutokana na kuikana nafsi ikutumayo kuyafanya yasiyotakiwa, kukana umilikaji vitu pamoja na hisia na mawazo yasiyofaa.

Amani ya dhati huja kutokana na kufanya kazi kwa faida ya wote. Sisi sote ni chembe chembe hai kwenye mwili wa utu, yaani sisi sote tulioko duniani kote.


Kila mmoja wetu anao mchango wake wa kutoa, na atafahamu kutoka ndani kuwa mchango huo ni nini. Lakini hakuna yeyote awezaye kupata amani ya dhati isipokuwa kwa kufanya kazi siyo kwa ajili yake tu; bali kwa ajili ya familia nzima ya wanadamu.

## NYONGEZA I.

### MUHTASARI WA MAISHA YA MSAFIRI WA AMANI.

1908: Alizaliwa Marekani Mashariki.
1938: Alianza maandalizi. Kuishi kwa kutoa badala ya kupata tu.
1953: Januari 1, aliamua kuitwa Hujaji wa Amani kama jina lake la maisha. Kwa mara ya kwanza aliianza safari ya Amani nchini Marekani kutoka mji wa Pasadena California. Desemba 17, aliimaliza safari yake ya kwanza kwenye jengo la Umoja wa Mataifa, Jijini Newyork.
1954: Alifunga kula kwa muda wa siku arobaini na tano.
1955: Aliianza safari ya pili ya kueneza Amani kutoka San Fransisco California. Alitembea angalau maili 100 (sawa na kilometa 160) kila jimbo la Marekani, akiizuru kila miji mikuu ya majimbo hayo. Pia alizitembelea Meksiko na Kanada.
1957: Alitembea maili 1,000 nchini Kanada (ambazo ni sawa na kilometa 1,600). Kila jimbo la Kanada alilitembea maili 100 (sawa na kilometa 160).
1964: Alikamilisha maili 25,000 (sawa na kilometa 40,000) kwa miguu kwenye Jiji la Washington DC kwa ajili ya Amani. Aliacha kuhesabu maili, lakini aliendelea kutembea kupitia njia zake za awali.
1966: Aliianza safari yake ya nne ya Amani.
1969: Aliianza safari ya tano ya Amani.
1973: Aliianza safari ya sita ya Amani.
1978: Aliianza safari ya saba ya Amani.
1979: Juni, alifanya ziara ya kuelimisha na kutoa maongozi ya Mungu huko Alaska.
1980: Agosti, alifanya ziara ya kuelimisha na kutoa maongozi ya Mungu huko Hawaii.
1981: Julai 7, aliingia katika maisha huru baada ya Mungu kumchukua alipokuwa karibu na mji wa Knox Indiana. Wakati huo alikuwa katika safari yake ya saba ya kuizunguka nchi.

**CHATI YA MSAFIRI WA AMANI IONYESHAYO KUKUA KWAKE KIROHO:**



## NYONGEZA II

CHATI YA MSAFIRI WA AMANI IONYESHAYO KUKUA KWAKE KIROHO:

1.Kupanda na kushuka kwa matendo yake alipokuwa akiongozwa na nafsi ya mwili wake bila ya uongozi wa utakatifu ndani mwake.

2.Mwinuko wa kwanza wa mwanga wa kiroho, alipoona ameupata utashi kamili usiorudi nyuma wa kujitolea maisha yake kutumikia mapenzi ya nafsi iliyo juu.

3.Mashindano kati ya uta  fu wa Mungu na nafsi ya mwili ijiongozayo bila msaada wa roho wa kweli.

4.Kilele cha kwanza cha ujuzi wa mambo ya kiroho: Hali yenye mwanga wa Amani ya dhati inaanza kujitokeza.

5.Uwanda mrefu wenye maisha yenye Amani ya dhati ndani ya moyo.

6.Amani kamilifu ya dhati ndani mwake.

7.Kuendelea na ukuzi wa kiroho kwa kuifuata njia ielekeayo juu.

# NYONGEZA III

***Maswali na majibu kutoka kwa watu aliowasiliana nao kwa barua.***

Hujaji wa Amani alifikiri kuwa ni moja ya wajibu wake kuzijibu barua za maelfu ya watu waliomuandikia kwa kipindi cha miaka kadhaa. Alikuwa anazikusanya barua zake kutoka Posta mbalimbali nchini_______________ baada ya barua hizo kuwa zimetumwa na rafiki yake N.J. Concisely toka Cologne, mji ambao ndiko zilikokuwa zikifikia kwanza.

Kwa makini sana aliyajibu maswali yaliyokuwa yameulizwa kwenye barua zile, alitoa maoni kuhusiana na matukio na alielezea kuhusu safari zake za karibuni na mipango ya safari zake. Barua zake mara kwa mara zilianza na: " **Salaam toka Dakota ya Kusini! ( Ama Iowa , na pengine New Orleans)**;" kutegemeana na mahali alipokuwa wakati anaandika barua.

**Swali:***Ninawezaje kujihisi nipo karibu na Mungu?*

**Jibu:**Mungu ni Upendo. Mara uifikiapo hatua ya upendo wa juu kwa jamii ikuzungukayo utakuwa unamueleza Mungu alivyo. Mungu ni Ukweli na mara uutafutapo ukweli utakuwa unamtafuta Mungu. Mungu ni uzuri na mara uugusapo uzuri wa kitu kama ua, au; uuonavyo mng'ao wa mwanga wa asubuhi utakuwa unamgusa Mungu. Mungu ni nguvu yenye maarifa ya juu iviumbavyo vyote na kuvidumisha, ikiviweka pamoja na kuvipatia uzima. Ndiyo, Mungu ni muhimu kwa vyote______ hivyo wewe umo ndani ya Mungu na yeye yumo ndani mwako. Huwezi kuwa mahali ambapo Mungu hayupo. Kinachoruhusu vyote ni sheria ya Mungu kwa maana ya kuwa ipo sheria ya mwili na sheria ya roho. Uikiukapo utakosa raha utajihisi kuwa na utengano na Mungu. Ukiitii utajihisi kuwa ndani na upatanisho na roho wa Mungu na utajisikia uko karibu na Mungu. Unapoishi ndani ya upatanisho na sheria takatifu utajisikia sana na utajenga upendo mkubwa kwa Mungu.

**Swali:***Ili mtu awe na mafanikio yenye uhusiano mzuri na wenzake ni vema aonyeshe moyo gani?*

**Jibu:**Awapende watu, auone uzuri ndani mwao, aelewe kwamba kila mtu duniani ni muhimu na anao wajibu katika mpango wa maisha matakatifu.

**Swali:***Kukua kiroho kunaweza kutimilika haraka ama ni jambo linalochukua muda?*

**Jibu:**Kukua kiroho ni hatua sawa na kukua kimwili au kukua kiakili. Watoto wenye umri wa miaka mitano hawategemewi kurefuka sawa na wazazi wao mnamo mwaka wao wa sita. Mwanafunzi wa mwaka wa kwanza chuoni hategemewi

kuhitimu mnamo mwisho wa muhula wa kwanza wa masomoyake. Mwanafunzi mkweli hategemei kuipata Amani ya dhati kwa siku moja. Mimi ilinichukua miaka kumi na mitano kuipata. Kukua kiroho ni jambo la kupendeza na ni hatua ifurahishayo. Haina utashi wa aidha kuiharakisha, au kwenda nayo taratibu. la msingi ni kwamba wewe uifahamu kwanza na uchukue hatua za kuelekea kwenye Amani ya dhati ndani mwako na ukuzi wa kiroho utajifungua wenyewe.

**Swali:***Ni vipi mtu awezavyo kuipata Amani ya dhati?*

**Jibu:**Kupata Amani ya dhati ama furaha, ni lazima apitie kwenye ukuzi wa kiroho, ni lazima aondokane na kuyategemea maisha ya kidunia aingie kwenye maisha yamtegemeayo Mungu. Maisha ambamo yeye atajiona kama sehemu ya uzima na kufanya kazi kwa mema ya uzima.

**Swali:***Umesema kwamba upendo wa dhati ni ufunguo wa maisha yenye furaha. Budha alizoea kusema kwamba," ni hali ya mtu kuutawala uwezo wake wa akili. Alisema; kufurahia afya njema, kupata furaha kamili ndani ya familia yake, kuleta amani kwa wote, na kwamba ni lazima mtu ajenge nidhamu na kudhibiti fikra zake. Yote yatajileta. Kama mtu ataweza kudhibiti uwezo wake wa fikra atajikuta ameifikia njia ya mwanga wa mafanikio, hekima pamoja na mema yote yatajileta kwake?"*

**Jibu:**Upendo wa kweli ni ule utashi wa kutoa bila wazo la kutaka malipo baadaye. Ukiishapata roho wa aina hiyo atawale ndani mwako tayari utakuwa unatawala fikra zako kikamilifu halikadhalika na kwa mwili wako pamoja na matendo yako.

**Swali:***Umesema kuwa unao wito. Je, wanadamu wote wanao wito wa kiroho?*

**Jibu:**Ndiyo, wanadamu wote wanao wito ambao hujitokeza kwao kutokana na mwamko wa matendo matakatifu ya kiroho wayaonyeshayo.

**Swali***Tupo hapa duniani kuutumikia utu ikiwa ni pamoja na kujifunza yale yatuhusuyo kiroho?*

**Jibu:**Ndiyo, na hapo inatubidi tutumikie kadri ya wito wetu unavyotuongoza. Ni lazima tujifunze kuishi ndani ya upatanisho na maisha matakatifu lakini hiyo ni sehemu tu ya mafunzo yetu. kadri unavyoishi ndani ya upatanisho wa kweli wa Mungu na kwa kujitokeza kutumia wito huo unakomaa kiroho.

**Swali:***Nini lengo na madhumuni ya mwanadamu?*

**Jibu:**Lengo na dhumuni la mwanadamu duniani ni kuyawekamaisha yake ndani ya upatanisho na yale atakayo Mungu ayafanye.

**Swali:***Mungu ni nini?*

**Jibu:**Tunavirundika pamoja vitu vyote ambavyo viko nje ya uwezo wetu kuvielewa, na kwa jina moja tunaloviita vitu hivi kwa pamoja ni Mungu. Kwa hiyo Mungu ni nguvu ya uumbaji, Nguvu idumuyo ambayo huchochea mabadiliko ya kudumu ndani ya vyote vionekanavyo na visivyoonekana, Uwezo wa juu kimaarifa, utawalao mbingu na nchi kwa sheria ile ya mwili na roho. Mungu ni ukweli, upendo, mema, wema, uzuri wa jana na leo, roho imara na muhimu iliyosambaa kote. Mungu ni uwezo unaoviweka pamoja vitu vyote vilivyomo kwenye mbingu na nchi na kuvipa uzima.

**Swali:***Kwa nini watu hawana furaha?*

**Jibu:**Watu hawana furaha kwa sababu wako nje ya upatanisho na mapenzi ya Mungu.

**Swali:***Je, matatizo yanao mwanzo wake kwa watu wenye mtazamo hafifu wa kiroho?*

**Jibu:**Matatizo huja tunapoishi nje ya upatanisho wa kiroho wenye maisha matakatifu. Matatizo hutukumba ili tuongozwe kwenye njia njema ya upatanisho.

**Swali:***Kwa mawazo yako ni tatizo lipi namba moja liusumbualo ulimwengu?*

**Jibu:**Tatizo namba moja liusumbualo ulimwengu hivi sasa ni uchanga wa kiroho. Tunachagua kuishi ndani ya sehemu ndogo tu ya maisha yaliyo bora.

Ndani ya uchanga wetu tunaishi kwa kutawaliwa na tamaa kiasi kwamba baadhi yetu hujinyakulia vitu zaidi ya mahitaji yetu, hivyo wengine huachwa wanaishi bila kitu na wengine kufa njaa. Ndani ya uchanga wetu tunaishi kwa uoga mkubwa mno kiasi kwamba tunalazimika kujitengenezea silaha ili tujihami dhidi ya wenzetu, matokeo yake tunajikuta vitani. Tunapoamua kuyashughulikia matatizo ya kiulimwengu tunalolizingatia ni dalili za matatizo hayo! Kimsingi mimi nimechagua kuyashughulikia kwa kuanzia kwenye chanzo chenyewe cha tatizo na wala siyo dalili.

**Swali:***Lengo la kujifahamu mwenyewe ni kumfahamu Mungu?*

**Jibu:**Kama kweli unajifahamu mwenyewe, utafahamu mara moja kuwa wewe u mtoto wa Mungu na utamfahamu Mungu.

**Swali:***Ni nini imani iliyofichika?*

**Jibu:**Yule auchukuaye mwelekeo wa imani iliyofichika hupokea maono ya moja kwa moja toka ndani mwake. Hiki ndicho chanzo kilichowaonyesha watu ukweli wa kiroho nyakati zile za mwanzo.

**Swali:***Ni vipi mtu awezavyo kuyapata majibu ya kiroho ndani mwake yaani kutoka rohoni?*

**Jibu:**Usemapo "roho" unakuwa na maana ya asili ya utakatifu, ambapo wengine watamaanisha asili ya nafsi ya mtu ama vyote viwili. Asili ya utakatifu yaani; tone la Mungu, yaweza kuamshwa mara tu uugusapo ukweli kutoka nje. Ama ukweli huo waweza kutoka ndani mwako. Tumia muda wako kuupata uchocheo wa kiroho uyajaze maisha yako pamoja na uchocheo wa vitu ili uamshe nguvu ya utakatifu ndani mwako.

**Swali:***Ni wapi ulipojifunza fikra hizi za wokovu wa kiroho?*

**Jibu:**Sikujifunza popote. Nilichokifanya, nilitembea kimya nikaupokea wokovu tokana na uzuri wa maumbile ya asili, nikayaweka kwenye vitendo maono ya ajabu yaliyonitokea ndani mwangu.

**Swali:***Je, una ushauri kwa mtu atafutaye wokovu wa kiroho atumie njia ya kufikiri ama njia ya mazoezi ya kupumua?*

**Jibu:**Ninashauri mtu atumie muda wake mwenyewe na Mungu; atembee katika mapokezi ya kimya akisisimuliwa na ule uzuri wa maumbile ya asili. Kutokana na uzuri huo atapata uchocheo. Kutokana na mapokezi ya kimya mara moja ataingia kwenye fikra za wokovu wa kiroho. Akifanya matembezi siyo tu kuwa atafanya mazoezi bali pia upumuaji. Yote kwake ni mafunzo yenye upendo.

**Swali:***Je, yawezekana utakatifu wa mtu ukaamshwa kwa njia ya fikra?*

**Jibu:**Kama kweli unafikiria kuhusu wokovu wa kiroho, mwili wako utakuwa katika hali nzuri kiasi kwamba hautachoka. Matendo yako yatakuwa yametulia. Maono yako ni safi, yametakata. Fikra zako zitakuwa kwenye Amani zikisubiri bila msukumo wowote katika mapokezi ya kimya, maisha matakatifu yataingia kupitia kwenye roho yako mwenyewe. Ni muhimu kuweka katika vitendo maono matakatifu yajitokezayo rohoni mwako.

**Swali:***" Kundalini " ni nini?*

**Jibu:**" Kundalini, " kiasili ni muamsho wa maisha matakatifu ndani ya mtu; lakini kiasi nijuacho baadhi hulitumia neno hilo kumaanisha kujiingiza kwenye chanzo cha nguvuizitawalazo mbingu na nchi.

uatshinda kwenye ulimwengu huu. Wale waliojazwa na mioyo ya chuki hawana furaha pamoja na kwamba hawajui lile walifanyalo wanatafuta njia bora. Ni wale tu waliojazwa na upendo wanaishi maisha tulivu na yenye Amani.

**Swali:** *Ni vipi mtu awezavyo kuachana na tabia mbaya zitokanazo na matendo na mawazo mabaya?*

**Jibu:** Mawazo yenye tabia mbaya pamoja na matendo yake mabaya hupungua nguvu zake wakati ukuaji wa kiroho unapoendelea. Unaweza kuyabadili mawazo mabaya yakageuka na kuwa mazuri. Kama unayo mawazo mabaya kumhusu mtu unaweza kuyabadili ukajenga mawazo mazuri kuhusu mtu huyo.

Mawazo na fikra potofu vyaweza kugeuzwa kuwa na mwelekeo mwema; kwenye hali hiyo hiyo ya ulimwengu. Unaweza kujirudi kutoka kwenye matendo mabaya na ukazitumia nguvu ulizonazo kuyatenda yaliyo mema.

**Swali:** *Unakubali kuwasamehe wale watendao mabaya hata kabla hawajaomba msamaha?*

**Jibu:** Sihitaji hata kuwasamehe watu. Mimi sijengi uadui na mtu. Endapo watu wanafanya yaliyo mabaya ninawahurumia sana kwani wayatendayo ni ya kujidhuru. Ninatumaini watajisikitikia, kwa sababu hiyo, nataka wapone matendo yao hayo.

**Swali:** *Unayo mawazo yoyote katika kuimarisha shughuli za afya kwa watu?*

**Jibu:** Vitu muhimu vihitajikavyo katika utaratibu wa mpango wa maisha ya mwanadamu ni kuwepo kwa vituo vya Afya ambavyo vinazingatia udumishaji wa Afya bora za watu ili watu hao waweze kuwa ndani ya upatanisho na sheria ile ya mwili na roho. Na hii ni tiba kwa maisha yajayo. Ninafikiri kumekuwapo na hali ya kutokujali afya za watu hadi wengi wao wanaugua maradhi mbali mbali na hatimae kujikuta wanautafuta msaada kutoka mahali popote. Ninaamini la kuzingatiwa ni lile la kuwaweka watu katika hali nzuri kiafya. Kwa hiyo uchunguzi ufanywe katika mambo yawezayo kudumisha afya za watu. Kwa muda mrefu tumekuwa tukishughulikia upunguzaji wa dalili za matatizo yetu. Sasa yatupasa kuvishughulikia vyanzo vya matatizo hayo.

**Swali:** *Je, ni lengo la roho iliyo ndani mwa mtu kujisalimisha kutokana na mwili muovu ili kwamba iweze kuona ukweli kwa ukamilifu?*

**Jibu:** Roho ndani mwa mtu huuona ukweli wote kwa ukamilifu. Ukiiruhusu iyatawale maisha yako utakuwa na uwezo wa kuuona ukweli kwa ukamilifu. Utakalolisema ni kwamba roho yako inajaribu kukusalimisha kutokana na uovu, ili uweze kuishi ndani ya upatanisho na kusudio takatifu.

**<u>Swali</u>:***Kama tutadhania kwamba kila mtu anayo roho iwezayo kumsalimisha tokana na uovu, kwa nini wachache pekee ndio wapatao wito wa kiroho? Je, wale walio wengi wanaadhibiwa kwa matendo yao mabaya yaliyopita ama wanashindwa kuonyeshwa mwanga wa kweli katika maisha yao haya?*

**Jibu:**Hii ni kwa vile Mungu amewapa wote uhuru wa kuchagua lipi walifuate. Wale wengi uwasemao wanajiadhibu kwa kuchagua njia yenye mwenendo mbaya. Daima mwanga wa kweli hutolewa kwao lakini wanakataa kuupokea. Kwa hiyo wanafunzwa na matatizo yawapatayo baada ya kukataa kwao kuichagua njia yenye mwenendo mwema kwa hiari yao.

**<u>Swali</u>:***Kwa nini ulimwengu huu uweze kuwachanganya watu kimatendo?*

**Jibu:**Watu hawaitii sheria takatifu, hivyo matatizo yanajitokeza kuwawekea msukumo wa kuwaongoza kwenye upatanisho na lile kusudio takatifu. Kama wewe ungeelewa ni vipi maisha ya hapa duniani yalivyo mafupi ukiyalinganisha na yale maisha yajayo, usingejisumbua kushughulika na maisha magumu ya duniani kama ufanyavyo hivi sasa.

**<u>Swali</u>:** *Kipindi cha kuuona Mwanga Mtakatifu (ama ule wokovu) huwa kinatokea wakati gani?*

**Jibu:**Wakati unaponyanyuliwa kiroho hadi juu kabisa ukayaona mambo kupitia kwenye macho ya Mungu hali hii huitwa kuuona mwanga Mtakatifu ama wokovu.

**<u>Swali</u>:***Je, Mungu huongea kupitia kwako?*

**Jibu:**Ilivyo ni kwamba Mungu huongea kupitia kwa kila mtu ambaye maisha yake yanatawaliwa naye.

**<u>Swali</u>:***Je, uliuona ufunuo Mtakatifu? Kama ndivyo, kwa nini Mungu alikuchagua ili aweze kuuneza ujumbe wake kwa watu kupitia kwako?*

**Jibu:**Nilikuwa na msukumo wenye nguvu kuhusiana na mambo ya kiroho moyoni mwangu, au hali ile iitwayo wito. Wakati wa kuanza ziara yangu ya hija rafiki zangu wotewalinishauri kuachana na ziara hiyo.Nilichagua mwenyewe kuwa mpokeaji wa ukweli wa kiroho wakati nilipojitoa kuutumikia wito wa Mungu. Na wewe pia waweza kufanya hivyo. Sote duniani tunao umuhimu sawa wa kuyafanya yale Mungu ayatakayo. Mungu hujitokeza kwa yeyote amtafutaye, Mungu huongea na yeyote amsikilizaye. Unapojitoa maisha yako Kumtumikia Mungu; mara moja unaingia kwenye maisha ya kushughulika ambayo ni maisha mazuri yapendezayo.

**<u>Swali</u>:***Je, maisha yasiyotegemea uongozi wa Mungu hayadumu?*

**Jibu:**Maisha yasiyomtegemea Mungu yana kipindi cha kuishi kama mwili ulivyo, lakini ni juu yetu kuamua mioyoni mwetu, je, maisha ya aina hiyo yataendelea hadi lini kuutawala uhai wetu?

**Swali:***Je, ipo sheria iutawalayo wajibu wa nafsi ya mtu?*

**Jibu:**Wewe unawajibika kwa matendo yako yaliyo mema na yaliyo mabaya. unadaiwa kutenda yaliyo mema si kwa wenzako tu hata na kwako.

**Swali:***Ni zipi ndoto zako za upeo wa hali nzuri ya maisha ya kiroho? Je, zinaweza kutokea ukamilifu wa mawazo ya maisha bora ya kiroho hapa duniani?*

**Jibu:**Ukamilifu wa nje wa mawazo ya hali nzuri ya maisha ya kiroho utajitokeza wakati tutakapokuwa tumejifunza kuishi maisha ya ushirika ya upendo na yasiyokuwa na misingi ya kuuana. Ukamilifu wa ndani wa mawazo ya hali nzuri ya maisha ya kiroho utajitokeza wakati wote tutakapokuwa tumeipata ile Amani ya dhati ndani mwetu. Wengi wetu itatubidi kuipata Amani zaidi ya dhati ndani mwetu kabla ya ukamilifu wa nje wa mawazo ya hali nzuri ya maisha ya kiroho haujatufikia. Ukamilifu wa nje ni rahisi kujitokeza, ukilinganishwa na ule wa ndani ambao huchukua muda mrefu.

**Swali:***Yupo Mungu ambaye daima atakuwa zaidi yangu?*

**Jibu:**Umfikirie Mungu kama Bahari Takatifu na wewe kama tone moja tu la maji lenye utashi wake kwenye bahari hiyo. Unaweza kuamua kuendelea kujitenga na ile Bahari lakini ujue hautakuwa na furaha rohoni mwako. Unaweza kuamua kuwa sehemu ya Bahari kwa maana kwamba utaachana na ule utashi wako utegemee nguvu za ile bahari. Lakini maisha yako yatakuwa ya furaha ndani ya upatanisho na mapenzi ya Mungu. Utaendesha maisha yako kama sehemu ya Mungu na hasa kama nafsi moja na Mungu.

**Swali:***Ni yapi maisha ya kiroho?*

**Jibu:**Yale ambayo hayaendeshwi na milango mitano ya fahamu. Mambo ya kiroho yataendelea. Yale ya kimwili yana mwisho wake.

**Swali:** *Ukweli ni upi?*

**Jibu:**Ukweli ni ule ulio kwenye upatanisho na sheria takatifu. Ukweli ni Mungu, na Mungu ni Ukweli. Sala yangu daima ni kumuomba Mungu anifanye chombo cha kuueneza Ukweli wake pekee.

**Swali:***Niutafute wapi ukweli wa kiroho?*

**Jibu:**Katika hatua ya mwisho utaupata ukweli wa kiroho kutokana na ile nguvu iliyo juu rohoni mwako. Nguvu hiyo ni tone ndani ya Bahari ya Mungu. Na hilo tone linayo nafasi ndani ya Bahari hiyo. Wakati mwingine nguvu hii iliyo rohoni mwako yaweza kusisimuliwa tokana na vichochocheo vinavyokuzunguka kama vile mazingira mazuri yenye maumbile ya asili, ama muziki mzuri, hivyo ni vitu viwezavyo kukuletea maono yenye ukweli rohoni mwako. Wakati mwingine waweza kuuona ukweli umeandikwa mahali ama kusikia ukweli huo unazungumzwa mahali na nguvu hiyo ikaimarishwa moyoni mwako. Ama moja kwa moja unaweza kuupata ukweli kutoka rohoni mwako kupitia kwenye nguvu iliyo juu itokayo moyoni mwako ambayo ndiyo njia yangu. Maandishi yote matakatifu yalipatikana kutokana na maono yatokayo ndani, hivyo hata wewe pia waweza kuupata ukweli tokana na maono yatakayoamshwa rohoni mwako kuueleza ukweli Mtakatifu. Tulia na uelewe.

**Swali:***Je, daima kutakuwepo na mtu kupambana na maumivu wakati anapoelekea kwenye ile hali ya uzuri wa roho?*

**Jibu:**Kutakuwapo na maumivu wakati wa kukua kiroho mpaka hapo mtu atakapokuwa amekomaa kiasi cha kutenda kila jambo lililo ndani ya mapenzi ya Mungu na wala asisukumwe kutenda. Wakati utakapokuwa nje ya upatanisho na Mungu ndipo matatizo yatakapoanza kukutokea. Kusudi la matatizo hayo ni kukuweka kwenye upatanisho na Mungu. Kama kwa utashi wako utafanya kila jambo lililo ndani ya mapenzi ya Mungu utakuwa umeondokana na matatizo.

**Swali:***Je, itatokea kipindi ambacho nitaishi kwa raha bila kukutwa na matatizo yoyote ya kuhitaji utatuzi wangu?*

**Jibu:**Mara utakapokuwa umeipata Amani ya dhati kamwe hutakuwa na hisia za matatizo yahitajiyo utatuzi wako. Utakuwa umetosheka. Hivyo utakuwa unaishi chini ya uongozi wa maisha matakatifu ambayo hayakuongozi kukutana na matatizo. Hata hivyo endelea kukua kiroho ukiwa kwenyeupatanisho na maisha matakatifu.

**Swali:***Mimi ni mpweke. Je, nifanyeje ili kuondokana na jambo hilo?*

**Jibu:**Kamwe haujawahi kuwa mpweke. Mungu yuko pamoja nawe. Mgeukie Mungu ili umpate mwenzio wa kuwa karibu naye kwenye maisha yako. Soma vitabu, usikilize muziki wa mambo ya kiroho; vyote vitakuhamasisha katika ukuaji wako kiroho. Watembelee ama uwapigie simu waliofungwa ama wapweke kwa matatizo mbalimbali. Unaweza pia kuwatembelea wale wanaoishi maisha ya upweke. Katika kutoa tunapokea, hivyo upweke wetu unakwisha.

**Swali:***Je, unawezaje kuishi ndani ya afya njema na mwenye furaha?*

**Jibu:**Ninaishi ndani ya afya njema na furaha kwa kuishi daima nimemgeukia Mungu. Hii ina maana kwamba ninazitii sheria za Roho wa Mungu. Ninaishi ndani ya utumishi, sifikirii mawazo potofu na kadhalika. Hii inamaanisha kuwa ninazitii sheria za Mungu kuhusiana na mwili wangu. Yale mambo nijuayo kuwa ni mabaya kwa afya yangu siyatendi, na yale yaliyo mazuri kwa afya yangu ninayatenda. Tuzo yangu ni mimi kuishi katika afya njema na hali nzuri ya akili na yenye furaha.

**Swali:***Ni kwa vipi mwanamke wa kawaida aliyeolewa na mwenye watoto awezavyo kuwa na hali ya maisha kama uliyo nayo?*

**Jibu:**Yule ambaye yumo ndani ya utaratibu wa kutunza familia kama wengine walivyo, hupata Amani ya dhati ndani mwake sawa na mimi nilivyopata. Tii sheria za Mungu ambazo ni zile zile kwa kila mmoja wetu. Siyo tu sheria zihusuzo miili yetu bali hata sheria za kiroho ambazo huyatawala matendo ya wanadamu. Unaweza kuanza kwa kutegemea mambo yote mema uyaaminiyo kama nilivyofanya mimi. Itafute Amani ya dhati ndani mwako uiweke kwenye sehemu ya mpango wako wa maisha matakatifu ambayo ni ya pekee kwa kila moyo wa mwanadamu. Utajaribu kuitafuta Amani ya ndani mwako kwa mapokezi ya kimya kama nilivyofanya mimi. Kuwa kwenye utaratibu wa kuangalia familia siyo kinga katika ukuaji wa kiroho na kwa maana nyingine ni faida. Tunakua kiroho kutokana na utatuzi wa matatizo ya maisha yatupatayo. Na uwapo kwenye uangalizi wa familia, yapo matatizo mengi yanayojitokeza yawezayo kukukuza kiroho. Mara watu waingiapo kwenye utunzaji wa familia hujikuta mawazo yao yanahama kutoka kwenye hali ya kujali nafsi zao, wanajali zaidi masuala yahusuyo familia zao. Mapenzi timilifu ni yale yatumikayo kutoa bila kufikiria kurudishiwa baadaye. Na utunzaji wa familia unatuonyesha mfano wa mapenzi ya aina hiyoyaani yale mapenzi wayaonyeshayo wazazi kwa watoto wao. Kwani wazazi humtolea mtoto chochote bila matumaini ya kurudishiwa baadaye.

**Swali:***Kwa nini wewe ni mlaji tu wa mboga za majani, na ni kwa vipi kuushikilia msimamo huo?*

**Jibu:**Mimi kama mlaji wa mboga, ninafanya vizuri niwezavyo. Kamwe sijawahi kurudi nyuma katika kufanya jambo niliaminilo ni sahihi eti kwa vile sikuweza kulifanya ipasavyo. Siamini kwamba ni vema kwangu kumuomba mtu anifanyie kazi yangu iliyo chafu. Sitakiua kiumbe chochote kilicho na pumzi ya uhai, sitamuomba mtu yeyote aniulie kiumbe kama hicho, hivyo kwa maana hiyo kamwe sitakula nyama ya kiumbe kiishicho.

**Swali:***Mume wangu anatakiwa kutibiwa kwa njia ya kupasuliwa. Lakini anasitasita. Je, nifanyeje?*

**Jibū:**Kama mumeo ni lazima akatibiwe baada ya kupasuliwa ni muhimu aende lakini apunguze uoga kadri iwezekanavyo. Mwanamke mmoja ninayemfahamu alipambana na tatizo kama hilo hilo. Alijadiliana na mumewe kuhusu tatizo hilo na akafanikiwa kumshawishi mumewe kwamba Mungu anatuhitaji sisi wanadamu tujichagulie kufanya lolote liwezekanalo maadam liwe jema. Hivyo walijichagulia tabia fulani ya ulaji wa chakula pamoja na tabia za kutenda mambo mengine waliyoyaona yanawafaa. Walipanga kutembelea sehemu nzuri zenye mandhari zivutiazo na zilizo pweke wakae huko kwa muda ili kurekebisha na kuzijenga afya zao. Walipanga baadaye kufanya matembezi mengine ambayo yangekuwa mazuri zaidi na ya kuvutia. Mume aliona ni vema awahi kuyapata matibabu ili baadae aweze kuungana na mkewe kuendelea na safari yao ya matembezi waliyokuwa wameyapanga. Tatizo lilionekana kuwa dogo badala ya kuwa kubwa kama lilivyokuwa linaonekana. Mwanamume alitibiwa akapona hivyo safari iliyokuwa imepangwa kuwa ni ya kurekebisha afya na kuwa matembezi ya kawaida yalionekana kama ya Bwana na Bibi arusi katika siku zao mara baada ya kufunga ndoa.

**Swali:***Mimi pamoja na wengine wasiovuta sigara, tulishukuru ulipowaamuru watu wasivute sigara kwenye mkutano, lakini nilikuwa ninajiuliza kama wewe unao upendo kwa wavutao sigara?*

**Jibu:**Kazi ya Hujaji ambayo ni ya kuwaamsha watu kuondokana na ubaridi wa mawazo na kuwafanya wawaze, wakati mwingine hukuelekeza kukugonganisha katika upendo unaokuwa nao kwa watu, hata hivyo; kama ningemuona mtoto mdogo anataka kuligusa jiko la moto hakika ningemzuia asifanye hivyo na hilo kwangu lingekuwajambo la upendo kulifanya ingawaje mtoto asingependezwa na tendo langu hadi kulazimika kulia kwa mayowe. Mwanamke mmoja majuzi ameniandikia akisema kwamba mimi nilipokataa kukaa kando yake kwa sababu alikuwa anavuta sigara, alikosa usingizi kwa saa kadhaa akilitafakari jambo hilo na kulipokucha kesho yake aliacha kabisa tabia ya kuvuta sigara.

**Swali:***Mume wangu ni mvuta sigara. Na mimi siipendi kabisa tabia hiyo. Je, unaweza kuniambia nifanye nini?*

**Jibu:**Huo ni ushahidi kuonyesha kuwa hupatani kabisa na uvutaji wa tumbaku. Kwa hiyo kamwe hutakiwi kuwa kwenye chumba ambamo kuna mvuta sigara. Moshi kama vile wa miti hauna madhara. Lakini moshi wa tumbaku unayo madhara makubwa na hakika siyo mzuri kwa mwanadamu yeyote. Bila shaka itakuwa vema kwake na kwako pia endapo mumeo ataiacha kabisa tabia ya uvutaji wa sigara lakini kama hatakuwa tayari kufanya hivyo kamwe asivute sigara ndani ya chumba ulimo. Anaweza kutafuta sehemu nyingine nje huko ama kwenye vyumba vingine akavuta akiwa peke yake ama sehemu nyingine mbali na nyumbani? Hakuna haja ya

kugombana juu ya jambo hili. Ni bora utumie nguvu zako kutafuta jawabu la tatizo lake.

**Swali:***Ni vipi mtu awezavyo kuibadili hamu yake ya kitu kwa kufanya kingine badala ya kuachana kabisa na kitu kile akioneacho hamu?*

**Jibu:**Tunapokuja katika mambo kama uvutaji wa sigara, tumbaku, na unywaji, mimi ningeachana navyo kabisa kama nilivyoachana na unywaji wa kahawa muda mrefu uliopita. Nilijiondoa haraka kwenye tabia hiyo. Hata hivyo baadhi ya watu huona ni vema kubadili tabia waliyoizoea ya kufanya jambo katika tabia nyingine. Niliwahi kukutana na mwanamke mmoja aliyeacha tabia ya kutengeneza kinywaji cha chai na badala yake anatengeneza kinywaji cha kahawa kilichoungwa kwa majani ya mimea fulani. Ninamfahamu mwanamke mwingine aliyeiacha tabia ya kunywa pombe mchanganyiko na badala yake akawa anatumia maji ya matunda. Na anasema kuwa hata rafiki zake hawajui kuwa kile akitumiacho si pombe. Yupo mwanaume mmoja ninayemfahamu aliyezoea kuweka mfukoni mwake matunda fulani makavu pamoja na karanga sehemu ambayo hapo awali alizoea kuweka sigara zake. Matendo kama hayo mara nyingi yanafanikiwa.

**Swali:***Je, katika kukua kiroho inafaa tuelekee wapi, nje ama juu?*

**Jibu:**Daima tuelekee juu kuutafuta mwanga mtakatifu wakati huo huo tunaelekea nje kuueneza upendo kwa walewanaohitaji msaada wetu? Ndiyo, wakati mtu anapokuwa anatembea kwenye njia ya roho mwema ataendelea kuomba uongozi wa Mungu na anajitokeza katika kutoa. Kwa hiyo, washiriki siyo wale tu ambao wamekwisha kukomaa kiroho tunaojifunza kutoka kwao, bali hata wale ambao bado ni wachanga wanaohitaji msaada wetu.

**Swali:***Kwa nini Mungu yupo?*

**Jibu:**Mungu ni nguvu ya uzima ambayo bila kuwapo kwake mbingu na nchi haziwezi kuwapo. Mungu anathibitishwa kupitia kote kwenye umbile na roho ya mbingu na nchi.

**Swali:***Ni uhusianao upi aujengao mtu na Mungu?*

**Jibu:**Unaweza kujenga uhusiano na Mungu kwa kuyaweka maisha yako ndani ya upatanisho na sheria za Mungu ambazo ni zile zile kwetu wote. Sheria hizo utazitafuta na ukisha kuzipata unaziweka ndani mwako zikienda na mpango mtakatifu ambao ni wa pekee kwa kila moyo wa mwanadamu.

**Swali:***Yesu ni nani?*

**Jibu:**Yesu alikuwa Mwalimu Mkuu wa mambo ya kiroho aliyewahi kuishi kwenye dunia hii. Maisha yake daima yalitawaliwa na Kristo aliyeishi ndani mwake. Alifundisha kile ambacho hata sisi wanadamu wengine twaweza kukifanya.

**Swali:***Unawaambia nini watu wakuulizao kama wewe ni Mkristo?*

**Jibu:**Mimi sijawahi na wala siyo sehemu ya imani ya dhehebu la aina yoyote la kidini. Mimi ni mwanamke nilyezama ndani ya dini ambayo imechukua njia ya ndani ya kiroho iliyonifikisha kwenye maisha matakatifu, siyo kwa njia ya elimu ya shuleni; ama mafunzo ya awali. Kamwe sitasema hii ni njia pekee. Bila shaka hii ni njia safi kabisa. Na watu wako huru kuchagua na kujiendeleza kiroho kwa kuzifuata njia zao.

**Swali:***Je, unaamini kwamba Yesu Kristo ni Mkombozi wa wanadamu ama unaamini kwamba hakuwa na tofauti na wanadamu wengine bali alikuwa na ule wito timilifu wa kiroho?*

**Jibu:**Yesu, alikuwa mtu mwenye wito timilifu wa kiroho aliyetokea wakati huo kuishi ndani ya watu wenye giza zito la dunia lisilomfahamu Mungu. Kristo ni utakatifu ulio juu ambao unaweza kutawala maisha yako kama ulivyoyatawala maisha ya Yesu. Kristo aishiye ndani ndiye mwokozi wa maisha ya watu, Kristo atawalapo ndani mwako utakuwa na furaha maishani mwako.

**Swali:***Je, unasadiki kuwa Yesu atakuja mara ya pili duniani?*

**Jibu:**Wale wote wasadikio kuwa maisha yatadumu (na baadhi ya wale wasiosadiki); wanakubali kuwa Yesu atarudi. Mimi ninaamini kuwa tumruhusu Kristo aishi ndani mwetu ili ayatawale maisha yetu.

**Swali:***Yesu alikuwa na maana gani alipofundisha kuhusu ufalme " ambao si wa ulimwengu huu?"*

**Jibu:**Alikuwa na maana ya ufalme wa Mungu ndani mwetu yaani ule utakatifu wa ki-Mungu, Kristo aishiye ndani mwetu.

**Swali:***Ni kipi kipaumbele cha maisha?*

**Jibu:**Yesu alisema, " Utafuteni kwanza Ufalme wa Mungu na ukweli wake wote. Mengiine yote utayapata kwa kuongezewa." Hii ni kweli. Baraka zote ziko juu zaidi ya chochote kile kielezwacho kwa maneno. Afya, furaha, Amani ya dhati, vyote hivi utakuwa navyo uwapo na Mungu karibu nawe. Uimara, utimilifu usiokuwa na haraka. Uoga utaisha kabisa maishani mwako. huwezi kuhisi uoga ukifahamu kuwa Mungu yuko nawe. Kias..i wewe unaye Mungu.

**Swali:** *Kama wewe umekomaa kiroho kwa nini siyo mtu mashuhuri?*

**Jibu:** Watu wengi ambao wamepata Amani ya dhati siyo mashuhuri hapa ulimwenguni.

**Swali:** *Je, wewe ni Avatar mwenye umbile la utakatifu?*

**Jibu:** Mimi ni Hujaji wa Amani nashughulikia Amani ya ndani na ile ya nje. Ninatembea nikisali kwa ajili ya Amani. Ninajaribu kuwahamasisha wengine wasali na kufanya kazi kwa ajili ya Amani. Nitafurahi kuwa mtumishi, yaani mtu anayekwenda na kurudi tena na tena kusaidia watu kuhusiana na mambo ya kiroho.

**Swali:** *Je, wazo la kumtumainia masihi linatokana na uchanga wa watu kiroho? Je, Yesu alikuwa Masihi? Je, wewe ni masihi?*

**Jibu:** Ndiyo, wazo la kumtumainia masihi linatokana na uchanga wa watu kiroho. Watu ambao ni wachanga kiroho wanamtafuta masihi badala ya kumtafuta Kristo aishiye ndani ndani mwao. Yesu alikuwa Mwalimu Mkuu wa mambo ya kiroho. Ninafundisha namna ya kuenenda na kuishi na sheria za Mungu. Ndani ya kila mtu upo utakatifu wa asili ambao unapewa majina mbalimbali na watu kutegemea mazingira walipo. Baada ya kipindi fulani cha maisha ya mtu, utakatifu huo huanza kuyatawala maisha ya mtu. Ni baadhi ya watu wanaojitokeza kuuonyesha wito wa pekee kutokana na kukomaa kwa utakatifu ndani ya mtu. Na watuwa aina hii ni wachache sana. Jambo muhimu ni kwamba utakatifu huu unaweza kukutawala.

**Swali:** *Kwa nini watu waligundua kuishi kwa imani mbali mbali duniani?*

**Jibu:** Imani za aina hiyo hazikuwa na umuhimu wowote kuanzishwa. Zilianzishwa kutokana na ujinga, uoga, pamoja na uchanga wa nguvu za kiroho ndani mwao. Wakati mwingine imani hizi zinatumiwa kwa watu ambao hawajakomaa kiroho wakiongozwa na watu wasiotegemea kuwepo kwa Mungu. Watu wanaamini imani mbali mbali kwa sababu wanafundishwa kuziamini.

**Swali:** *Kwa nini watu huishi duniani kwa kuamini imani za kidini zilizo potofu?*

**Jibu:** Watu ambao hawakukomaa kiroho huishi kwa kuzitegemea dini zenye imani potofu kwa sababu ya uoga ndani ya maisha yao. Wakishakomaa kiroho na wakawa wamegundua upotofu uliomo ndani ya imani zao, mara moja hutengana na imani hizo.

**Swali:** *Je, waweza kuzifafanua imani potofu zilivyo?*

**Jibu:**Chukua tunda ulifananishe na imani yoyote ile. Toa nyama ndani ya tunda hilo ambayo ndiyo yenye kuliwa tuifananishe na ukweli wa kiroho ulio kwenye imani hiyo. Makapi ya tunda ytasiyofaa kuliwa ambayo yanasalia ni sawa na upotofu ulioko kwenye hiyo imani ambao hufai kabisa kufuatwa.

**Swali:***Kuwasiliana na Mungu kukoje?*

**Jibu:**Kuwasiliana na Mungu ni ufahamu wa ndani wa roho yako unaokujulisha kuwa Mungu yumo moyoni mwako na amekuzunguka. Mungu "huongea" kwa sauti imara ya kimya na nyembamba moyoni mwako.

**Swali:***Je, sayansi na dini havipatani?*

**Jibu:**Utasema kwamba sayansi hufanya kazi yake kwa vitendo vya utafiti vyenye kuhitaji matokeo yaonekane kwa macho ama hisia. Na dini hufanya kazi kwa kuongozwa na ule wito mtakatifu. Kama kitafutwacho ni sahihi kwa pande zote mbili hatima yao itakuwa sawa ila sayansi itachukua muda mrefu kuifikia ile hatima.

**Swali:***Je, unaweza kuyafafanua mabadiliko ya kukua kiroho?*

**Jibu:**Mabadiliko ya kukua kiroho hujitokeza maishani mwako mara uishipo ndani ya upatanisho na lile kusudiotakatifu. unapozitii sheria takatifu ambazo ni zile zile kwetu wote ukifanya kazi nyeti iliyo kwenye mpango mtakatifu.

**Swali*****Wasiomuamini Mungu hudai kwamba hakuna njia iwezayo kuthibitisha kuwa kuna Mungu. Je wewe waweza kuthibitisha kwamba kuna Mungu?***

**Jibu:**Hakuna kitu kiitwacho kutokumwamini Mungu. Kwani ndani ya mtu ajiitae hamuamini Mungu moyoni mwake umo utakatifu ambao kama utaamshwa, mara moja atajihisi kuwa karibu na Mungu. Wapo wale wajiitao wasiomuamini Mungu. kwa baadhi yao nimewafafanulia kiutaalam kuwa Mungu ni ile nguvu ya uumbaji, nguvu idumuyo, ichocheayo mabadiliko, yenye maarifa ya juu yatawalayo vyote vilivyo kwenye mbingu na nchi, ukweli, hisia za matendo mema kama vile upendo, wema, uzuri, roho ya kweli idumuyo na iliyoenea kote ambayo imevifunga vitu vyote kwa pamoja vilivyo kwenye mbingu na nchi ikavipa uzima.

**Swali:***Yawezekana kuwa uumbaji wa mbingu na dunia ulifanyika bila ya chanzo chochote kijulikanacho?*

**Jibu:**Uumbaji wa mbingu na dunia ulifanyika kwa maarifa ya juu kabisa ambayo hayana udhanifu kwetu sisi. Na sisi tunayo nafasi ya ajabu ya kujifunza na kukua tukiwemo ndani mwake.

**Swali:***Ni nini asili ya mbingu na nchi?*

**Jibu:**Asili ya mbingu na nchi ni maisha kuelekea yote yaliyomema ama kamilifu.

**Swali:***Ni lini mbingu na nchi viliumbwa; na, ni lini vitaharibiwa?*

**Jibu:**Hatufahamu tarehe kamili mbingu na nchi zilipoumbwa, japokuwa tunajaribu kubuni. Ilivyo hatujui tarehe ya mwisho wake wala tusiliwazie hilo sana. Yote tuwezayo kusema ni kwamba mbingu na nchi vilianza wakati umuhimu wa kuumbwa kwake ulipowadia na vitakwisha wakati umuhimu wa kuhitajika kwake utakapokwisha. Kwa wakati huu vinahitajika sana. Na ujumbe muhimu ni kwamba; tuyaangalie yale yanayotukabili sasa badala ya kuyahangaikia yaliyopita na yale yajayo. Ilivyo ni kwamba mojawapo ya masomo yatupasayo kujifunza yatubidi tuelewe kuwa sisi ni roho. Hilo ndilo somo muhimu. Tunaweza kusema kuwa ni lengo letu kuwa na mabadiliko ya maisha. Hata hivyo mabadiliko yetu ya haraka ni kuyaweka maisha yetu kwenye upatanisho na sheria takatifu ili tuifanye kazi iliyotuleta.

**Swali:***Je, unaamini kwamba kuna sehemu iitwayo peponi na ingine iitwayo jehanamu?*

**Jibu:**Peponi na jehanamu ni masikani ya wanadamu. Peponi ni kule kuishi ukiwa ndani ya upatanisho na sheria takatifu za Mungu. Na jehanamu ni kuishi nje ya upatanisho na sheria hizo takatifu. Unaweza kuishi kwenye masikani yoyote katika upande wowote wa maisha yako. La kufahamu ni kwamba masikani ya jehanamu hayadumu. Mara tu uamuapo kumgeukia Mungu masikani ya jehanamu kwako yatafutika. Mungu ni wa milele.

**Swali:***Je, tunao uzoefu wowote tuupatao kabla ya maisha ya duniani na baada ya maisha ya duniani?*

**Jibu:**Lipo jambo likuwezeshalo kutambua uzoefu wa maisha ya duniani kama vile utambuavyo uzoefu wa maisha kwenye mojawapo ya siku zako kuonyesha lililopita na yale yajayo. Kama vile ujuavyo kuwa lile ulilolifanya jana laweza kuyaathiri ya kesho, hivyo wazo langu ni kwamba uzoefu wa yale yafanyikayo sasa yaweza kuyaathiri yale yajayo katika maisha. Kwa hiyo ujue kuwa ulimwengu uko kwenye mpangilo wake wa maisha ya kila siku na unajiendesha kutegemeana na sheria. Sheria zitawalazo zinapotiiwa upatanisho hutokea na zisipotiiwa migongano hutokea. Na hali hii haionekani kwa wale ambao upeo wao wa kuona hauvuki uwezo wa maisha ya duniani. Kwao wataendelea kuiona dunia inavurugika na kujaa ukorofi wa aina aina.

**Swali:***Kwa nini watu huogopa kifo?*

**Jibu:**Ilivyo ni kwamba karibu yote yaogopwayo na watu ni yale yasiyojulikana. Watu hukiogopa kifo kwa sababu yatokeayo kwenye kifo hayajulikani. Hata hivyo nilishuhudia na ninaelewa mabadiliko yaitwayo kifo. hali hii ilinitokea kwenye dhoruba ya barafu nilipoanza kupooza mwili kwa sababu ya baridi, hivyo mimi kifo sikiogopi. Nilichokishuhudia kwenye usiku ule kuhusiana na badiliko liitwalo kifo, ilikuwa ni uzuri mtupu. Ninatazamia kuliona badiliko hilo liitwalo kifo kama mwisho wa kisa cha maisha yangu. Nafurahi pamoja na wapendwa wengine wanapokuwa ndani ya maisha haya ya mpito kuelekea kwenye maisha yale huru. Utaushinda uoga wa kitu baada ya kuwa umejenga mazoea na kile ukiogopacho.

**Swali:***Mtu aogopapo kifo ina maana anao mtazamo potofu wa mambo ya kiroho?*

**Jibu:**Uoga wa kifo unamaanisha kuwa mtu huyo anauthamini mwili wake badala ya roho na huo ni mtazamo potofu wamambo ya kiroho.

**Swali:***Je, unafikiri roho yaweza kutengana na mwili kabla ya kuukamilisha wajibu wake duniani?*

**Jibu:**Ni kweli kwamba mbingu na nchi hufanya kazi kutegemea sheria kamilifu. Ni kweli kabisa kwamba watu wengine huja kuishi duniani ili waishi kwa muda mfupi sana. Wengine huja kuishi duniani mpaka hapo mambo fulani yanapokuwa yamekamilishwa. Wengine huja kuishi duniani hadi hapo miili yao inapokuwa imezeeka sana hadi kushindwa kuishi tena. Wengine huja kujifunza mambo fulani, wengine kulipa madeni, wengine kufanya utumishi ama kuyafanya yote hayo. katika yote hayo wewe unao uamuzi wa hiari. Kama utajali kuutunza mwili wako utaishi maisha marefu zaidi kuliko kama ungeufanyia yale yasiyoufaa. Fikra na matendo pia vinao wajibu wake. Hivyo utaona mambo yanakuja na kupita kutegemeana na wito. Utaishi muda mrefu kama utayafanya yale yapasayo.

**Swali:***Kama roho iishiyo ndani mwetu huishi milele, je, hufanya nini mara baada ya kifo cha mwili? Je, roho ya aina hiyo daima ni nzuri ndani ya kila mwili wa mtu?*

**Jibu:**Kama ile asili ya ubinafsi kwenye mwili wa mtu itashindwa kabisa kutawala ndani ya mtu, roho wa kweli yaani wewe utakwenda kwenye milki ya roho ya unafsi wa mwanadamu. Sasa haitaendelea kuishi kwa kutegemea nyenzo za kidunia na itakuwa inajifunza masomo mbalimbali. Maisha ya kiroho daima ni mazuri na yanaenenda pamoja na mapenzi ya Mungu. Maisha ya kutegemea asili ya ubinafsi wa mwili yanacho kipindi chake kifupi cha kuishi wakati mwingine huyafanya yaliyo mema na wakati mwingine huwa nje ya upatanisho wa kiroho.

**Swali:***"Karma" ni nini?*

**Jibu:**" Karma " ni sheria ishughulikayo na chanzo cha jambo ili kuona matokeo yake_ " Ukiyapanda mazao matokeo yake ni kuvuna." Maana hiyoni kwamba uvunaji ni matokeo ya upandaji. Na huu ni mzunguko wa maisha ya muda mrefu. Wale wapatao vidonda vya tumbo kwa sababu za kujenga chuki kwa wenzao ni mashahidi wa hali hii (kama wanayo macho ya kuona yale yawatokeayo). Hivyo ndivyo sheria ya " Karma " ifanyavyo kazi.

**Swali:***Matatizo mengine huonekana ni ya kurithi ama ya kudumu. Na haya yanasababishwa na " Karma?"*

**Jibu:**Tatizo lolote likutokealo linalo kusudio lake kwenyemaisha yako kutokana na utatuzi wa matatizo yako utajifunza na kukua kiroho. Hakuna tatizo liletwalo kwako ambalo liko nje ya uwezo wako kiutatuzi. Mara ukutanapo na tatizo lililo kubwa itakuwa ni ishara kuonyesha kwamba wewe unazo nguvu nyingi ndani mwako zikuwezeshazo kulikabili tatizo hilo. Baadhi ya matatizo mengi yaletwayo kwako unaweza kuyasababisha wewe na hiyo ndiyo tuitayo " Karma " yaani ile sheria ya kushughulika na chanzo ukayaona matokeo yake.

Mfano: kula mlo usiofaa, kuishi kwa hisia zisizofaa. Hivyo unategemea matokeo gani ufanyapo hayo? Wakati huo huo yapo matatizo yajayo kwa kurithiwa kama utashi kwa masharti ya kuzaliwa kwako. Ninawatakia nyote tiba iliyo timilifu na wala siyo kuyaondoa matatizo kwa kumeza vidonge vya kulevya ama kutumia vileo bali ushughulike moja kwa moja na chanzo cha tatizo likupatalo. Ninatumaini utahamasishwa kujiweka kwenye hali safi ya kula chakula kamili cha kukujengea afya bora. Ninatumaini utahamasishwa kutafuta na kuondoa mawazo yote potofu uliyonayo pamoja na hisia zake. Ninatumaini utahamasishwa kujaza maisha yako mambo yaliyo mazuri kama utajali uzuri wa maumbile ya asili, muziki mzuri wa mambo ya kiroho ukuamshao, maneno mazuri na matendo yaliyo bora. ukae mbali na chochote kiwezacho kukuangusha kiroho na uzingatie yale yawezayo kukunyanyua juu kiroho.

**Swali:***Ni njia ipi ifaayo kukuondolea "karma" mbaya?*

**Jibu:**Njia nzuri kwako wewe kuondokana na karma mbaya ni kujishughulisha na utumishi wa Mungu kwa hali yoyote iwezekanayo. Utakapokuwa umetoa kiasi cha kutosha utamfahamu Mungu na kuipata Amani ya dhati. Ni kutokana na kutoa ndipo tunapopokea.

**Swali:***Je, unaweza kuyakumbuka maisha yaliyopita?*

**Jibu:**Unaweza kabisa kukumbuka matendo ya maisha yaliyopita kwa kujifunza yale yaliyokuleta hapa duniani. Kabla ya hayo ni bora usiyakumbuke mambo hayo kwa maana kwamba utashindwa kulitatua tatizo kama utakuwa na jibu lake. Lipo

pambio la zamani lisemalo: " Siombi kuona lile tukio la mbali hatua moja mbele inanitosha." Huo wimbo unao ujumbe wenye busara.

**Swali:***Je, utakatifu uliomo moyoni mwangu waweza kuzidhibiti hasira na ukali wangu?*

**Jibu:**Hali ya utakatifu iliyomo moyoni mwako yaweza kudhibiti matendo yote ya mwili wako pamoja na akili zako zote. Unafsi wa mwili hauwezi, ingawaje unafsi huo unaweza kuyatawala matendo hayo kwa kiasi fulani. Nguvu yahasira haifichiki, kwani inaweza kukudhuru kwa ndani, na wala haiwezi kuonyeshwa wazi wazi nje kwani itakudhuru ndani mwako pamoja na kusababishia ugumu wa mambo kwenye mazingira yakuzungukayo. Nguvu hii yaweza kubadilishwa kwa kutenda matendo yawezayo kuipunguza. Matendo hayo ni kama vile mazoezi ya viungo ama shughuli yoyote ya jasho iwezayo kukuletea faida. Kama utamgundua mtu atendae mambo yasiyofaa kwa hali fulani yumo kwenye maumivu kisaikolojia, hasira yaweza kugeuzwa kuwa huruma kwake.

**Swali:***Ni vipi watu wawezavyo kuimarisha ile tabia yao ya kujiamini?*

**Jibu:**Tabia yako ya kujiamini waweza kuiimarisha kama utajigundua ulivyo. Wewe ni mtoto wa Mungu hivyo tenda kama mtoto wa Mungu atakiwavyo kutenda.

**Swali***Kwenye nchi hii yenye utajiri mkubwa kwa nini watu wengi wanalalamikia matatizo ya kifedha?*

**Jibu:**Watu wengi wasemao wana matatizo ya kifedha wana maana ya kutaka zaidi ya kile wanachokihitaji. Ilikuwa rahisi kwangu kuyafanya maisha yangu kuwa ya kawaida mno. Nilijiona kwamba nisingeweza kupokea zaidi ya kile nilichokuwa ninakihitaji, wakati wenzangu ulimwenguni wanacho kidogo zaidi ya mahitaji yao. Nimegundua baada ya kuyachunguza maisha ya watu wanizungukao kwamba madeni mengi yalipwayo na watu hayalipi vitu muhimu vitakiwavyo kwa maisha ya wanadamu bali vingi ni vile vya anasa. Kwa nini watu hupendelea vitu ambavyo sio muhimu kwa mahitaji yao? Wakati mwingine mtu huamua kufanya hivyo katika kukidhi haja tamaa tu hali ambayo inaweza kudhibitiwa kwa kujijengea nidhamu ya kuyatawala matendo ya mwili. Wakati mwingine mtu huamua kufanya hivyo katika kuonyesha sifa ili awakoge wenzake hali ambayo haiwawezeshi kufikia lengo la kile wakitafutacho hadi hapo hiyo hali ya kujitukuza nafsi itakapokuwa imeondolewa na nafsi iliyo juu yenye mwenendo mtakatifu. Ndiyo, wengine hujaribu kutumia vifaa mbalimbali kujikinga na mabaya yoyote yawezayo kuwatokea badala ya kutafuta msaada wa kiroho kujikinga. Hali hii huwawia vigumu sana. Matatizo ya kifedha huja kutufundisha kwamba tuache kuzingatia vitu vya kumiliki; bali tuyazingatie mambo ya wokovu wa kiroho. Ninaamini kuwa wewe unafahamu kusudi la ajabu la

kupatwa kwetu matatizo hayo yanayokuja kutupatia fundisho na namna tuwezavyo kuyatatua daima kwa kuutegemea msaada wa Mungu.

**Swali:***Tuwe na tabia ipi kuhusiana na mwelekeo wa kumiliki vitu maishani mwetu?*

**Jibu**Kama vitu tumilikivyo vitawekwa kwenye sehemu yake bila ya kutuchukulia muda wetu katika kuviwazia, ni maisha huru yaliyoje tutakayokuwa nayo! Pia hatujajibebesha mzigo wa kujihusisha na vitu visivyo muhimu maishani mwetu. Kama tutajigundua kwamba sisi ni chembe chembe kwenye mwili mmoja wa utu tutafikiria kusaidiana katika kukidhi mahitaji ya kila mmoja wetu ambayo ni ya lazima, isiwe badhi kujikusanyia vingi na baadhi kuishi kwa kidogo zaidi kisichoweza kuyatosheleza mahitaji yao.

**Swali:***Unayo maelezo gani kuhusiana na utabiri utolewao kuhusu maangamizi ya dunia mnamo siku za usoni?*

**Jibu:**Kumbuka nguvu za fikra na ufikirie mema tu yatakayotokea. Shughulikia yale yaliyo mema tu ambayo ndiyo utakayo yatokee.Fuata yale tu yaliyo mema utakayo kuona yanatokea. Kumbuka kutokana na mawazo unajenga tabia ndani mwako ambayo ndiyo iyasaidiayo matendo yako kwenye mazingira yatuzungukayo. Uamuzi wa ama kufanikisha mwisho wetu ama kutokufanikisha umo mikononi mwetu sisi wanadamu. Kumbuka kwamba saa ya giza ni wakati kabla ya mapambazuko.

**Swali:***Je, nifanye nini kuhusiana na mjukuu wangu anayezaliwa kwenye ulimwengu huu uliojau migongano na vurugu za kila aina?*

**Jibu:**Kwa nini usifikirie kuhusiana na mjukuu wako anayezaliwa kwenye ulimwengu huu uliojazwa na uwepo wa Mungu? Sheria ya Mungu hapa ulimwenguni ipo daima. Kila kitu kilicho nje ya upatanisho wa mambo ya kiroho kitakuwa nje ya sheria hii. Giza tulionalo ni mfarakano uliopo kati ya baadhi ya vitu hapa ulimwenguni na sheria ile ya upatanisho. " Mungu hafi wala halali usingizi...mabaya yatashindwa na mema yatadumu...dunia iishipo kwa Amani ndiyo mapenzi mema kwa watu." Ni vipi mtu yeyote awe na mashaka kwamba hatimaye Mungu atadumu? Majibu yake yote yamo ndani ya uamuzi wetu.

**Swali:***Ni upi uamuzi wako kuhusiana na matatizo yafuatayo?*

*(a)Kipindi cha matumizi ya zana za nguvu?*

**Jibu:**Unatakiwa uwepo utafiti mkubwa kuhusiana na upatikanaji wa zana za nguvu ambazo hazina uharibifu kwa maisha ya mwanadamu bali zile tu ziletazo

faida. Kama vile nguvu za mwanga wa jua, nguvu za upepo, nguvu za maji na na nguvu za mawimbi ya maji zilivyo. kwenye maeneo mengine nguvu za mvuke zinasaidia. Niliwahi kuishi kwenye shamba la mifugo ambako watu wa pale waliishi kwa kutumia nguvu za mwanga wa jua pamoja na nguvu zaupepo.

*(b)Ugaidi?*

**Jibu:**Magaidi ni watu ambao hakika ni wachanga katika mambo ya kiroho ambao kwa kawaida wamefunzwa kuamini kwamba ubaya utaondolewa kwa kutendewa ubaya zaidi. Watu hawa wanahitaji mpango wa kuwasaidia ili wabadilishe tabia yao.

*(c)Matendo ya jinai yanayoandaliwa na kufanywa kuanzia mtu mmoja hadi vikundi vya kimataifa?*

**Jibu:**Matendo ya aina hii yanaonyesha dalili ya watu ambao hawajauona mwanga mtakatifu ambao mawazo yao yanawaelekeza kupima mafanikio ya maisha yao kwa kuangalia vitu walivyo navyo pamoja na fedha. Pia watu wa aina hii wanahitaji msaada mkubwa wa kiroho ili warekebike.

*(d)Vikundi viovu vya vijana?*

**Jibu:**Vikundi vya aina hii havina budi kukomeshwa. Jamii haina budi kuwafanyia maandalizi mazuri watoto kama vile maeneo ya kuchezea na shughuli zingine ziwezazo kuwajenga katika tabia zifaazo maishani mwao.

*(e)Utoro kwenye maeneo ya kazi?*

**Jibu:**Utoro mwingi ufanyikao hutokana na watu kujikuta wanafanya kazi ambazo hawana wito nazo. Ni vema watu waajiriwe kazi wazipendazo bila kujali ukubwa wa pato.

*(f)Wivu?*

**Jibu:**Wale wasio na wokovu wa kiroho huona wivu kwa wenzao kwa sababu hawajui kuwa wao ni muhimu sawa na wenzao walivyo. Watu wote wanao wajibu sawa katika mpango Mtakatifu.

***(g)Chuki na ubaguzi wa rangi?***

**Jibu:**Unaweza kuishinda chuki kwa kuyatenda yaliyo ya upendo. Chuki humdhuru yule achukiae na wala siyo mchukiwa. Wale watendao matendo ya kibaguzi wanadhurika. Wale wanaobaguliwa wanao uhuru wa kuchagua. Waamue kupambana kwa hasira ili kulipiza kisasi dhidi ya wale wanaowabagua, jambo ambalo litadhuru nafsi zao ama wautafute ukweli wa kiroho katika kukabiliana na matatizo yao ili waimarishwe.

*(h)Ubatilifu ?*

**Jibu:**Hali ya kuutegemea unafsi wa mwili hujihisi ubatilifu mara moja ishindwapo kupata njia za ufumbuzi wa matatizo. Nafsi ya roho iliyo juu inao uvumilivu mkubwa kuhusiana na yale yanayokukabili ikijua kwamba kwa mwelekeo ulio timilifu kila kitu kitapatiwa ufumbuzi.

*(i) Mateso ?*

**Jibu:**Huu ni mpangilio wa mbingu na nchi, na mateso yatupatayo yanalo kusudi maishani mwetu. Yanajaribu kutufunza jambo. Yatulazimu tulitafute somo lake.

**Swali:***Je, wewe ni mpenda mageuzi ama ni mtetezi wa mambo yaliyopo?*

**Jibu:**Mimi ni mtetezi wa mambo yote mazuri yaliyopo na pia; ninapenda mageuzi yafanyike ili kuyaondoa mambo yote yasiyo mema.

**Swali:***Ni nini hasa, siasa na falsafa yako kuhusiana na maisha kwenye jamii?*

**Jibu:**Siasa na mpangilio wetu wa maisha ya jamii ni lazima vielekezwe kuingia kwenye upatanisho na lile kusudio takatifu.

**Swali:***Je, ni lipi ulifikirialo kuhusiana na ubepari?*

**Jibu:**Kama ubepari, una maana ya utaratibu uliopo wa kiuchumi ambao umesababisha ukosefu wa ajira nchini na uzalishaji wa mali ambao mfumo wake umepitwa na wakati; hakika hali hii inabidi irekebishwe. Mgawanyo wa madaraka kwa kile kizalishwacho hauna budi uwaelekee wote. Kama wote wafanyao kazi kiwandani watakuwa na hisa katika shughuli za uzalishaji kiwandani humo, migongano itakwepwa. Ubepari kwa kawaida una maana ya mashindano na kazi ya wakati ujao imelenga kwenye ushirikiano.

**Swali:***Je, unafikiri kwamba matumizi ya demokrasia ni muundo bora kwa serikali?*

**Jibu:**Kama demokrasia yenyewe inadhibitiwa na watu wote kama itakiwavyo iwe, ni bora kwa serikali yoyote ile duniani. Mimi ninakubaliana na demokrasia kama inatumiwa kikamilifu, iwe kwa mtu mmoja mmoja, kisiasa, kimaisha na kiuchumi. Kama tungekuwa na kitu kama hicho ambacho hatukulifahamu, kingekuwa kwenye upatanisho na lile kusudio takatifu.

**Swali:***Ni watu gani waitwao ni wa mlengo wa kushoto na ni wapi watu wa mlengo wa kulia?*

**Jibu:**Wale watakao msukumo wa mara moja wa mabadiliko ya maisha wanaitwa wa mlengo wa kushoto. Na wale wasiotaka mabadiliko ya haraka bali kufuata hatua kwa hatua huitwa wa mlengo wa kulia. Kwa ujumla wote wanalo jambo moja la kuzingatia. Ni kwamba wote huamini falsafa potofu kwamba; **" tatizo lifumbuliwe kwa kuzitumia njia za tatizo."** Hii ni falsafa ya kivita. Mimi ninaamini kwamba njia itumiwayo ndiyo itatathmini kile utakachokipokea mwishoni. Kama unatumia njia ya wema mwishoni utayapokea matunda ya wema. Hii ndiyo falsafa ya Amani na falsafa ya dini zote zilizo sahihi duniani. Utakatifu ulio ndani mwako unategemea falsafa ya Amani.

**Swali:***Je, unaamini kwamba Ukomnisti utautawala ulimwengu uweze kuifuta dini?*

**Jibu:**Kusema kweli, dini itadumu kwani inawakilisha roho wa kweli aliye rohoni mwa kila mtu ili kuleta maisha bora kwa wanadamu wote. Ukomunisti kwa maana halisi unawakilisha maisha yenye misingi ya ushirika. Kama ukomnisti ulivyofanyiwa kazi kwenye baadhi ya jumuiya ndogo ndogo unaonyesha kwamba siyo adui wa dini kama wengine wanavyo fikiria. Ukomunisti haujawahi kufanyiwa kazi kwenye jumuiya kubwa duniani. Kwa kifupi, Ukomunisti haujawahi kufanyiwa kazi kwenye jumuiya yoyote kubwa duniani. Na jumuiya kubwa iliyokuwa ya kwanza kuufanyia kazi, itikadi yake iliipinga dini ambayo ilikuwa imeelekezwa kwenye msingi wa kitaifa kwa sababu ilihisiwa kuwa, dini hiyo ilikuwapo ili kuwanyanyasa watu. Na hatimaye kujikuta inatawala kidikteta. Mambo ambayo hayamo ndani ya upatanisho na roho wa kweli katika nchi yao, nchi yetu na nchi nyingine zote ni kuwapo kwa mfarakano. Ndani mwao zimo mbegu za kuziangamiza nchi hizo. Ukomunisti wa kweli ungeweza kuufunza ulimwengu jambo lihusulo uchumi wa kidemokrasia.

**Swali:***Je, unafikiri kwamba Ukomunisti utauangamiza ulimwengu kwa kuvianzisha vita vya nyuklia?*

**Jibu:**Hapana, sifikiri kwamba kuna nchi yoyote iliyotayari kuvianzisha vita vya nyuklia. Lakini hali hii inaweza kutokea kama ajali endapo tutaendelea kuzitunza silaha za nyuklia karibu nasi.

**Swali:** *Je, ni vema kujifunza sanaa za viungo kama vile " karate " ili kujilinda?*

**Jibu:** Silaha yangu ni upendo, hata sifikirii kujifunza njia nyingine ya kujikinga na lolote lijalo zaidi ya upendo. Wale ambao bado wachanga wa kiroho na waoga ndio wajifunzao vitu kama " karate " kujilinda.

**Swali:** *Je, mtu kuwa mvumilivu wa kutokutaka ugomvi ni maana ya kuwa mtu huyo ni mpenda Amani, na mtu kuwa mgomvi ni maana ya kuwa anapenda vita?*

**Jibu:** Ungeweza kusema kwamba, mtu mvumilivu hapendi mapambano ya kutumia nguvu kwa sababu ya unyonge alio nao, na mpenda amani hawezi kutumia mapambano ya nguvu kwa sababu yeye anazingatia kanuni za wapenda amani. Mgomvi anaweza kuishi ndani ya upatanisho lakini, matendo yake humuongoza vitani.

**Swali:** *Asilimia themanini na nane (88%) ya wanaume duniani huyafanya matendo ya jinai hali kadhalika na matendo ya kupigana vita zote; hata hivyo wapo wachache wasiofanya hayo. Lakini je, unaamini kwamba wanawake kwa ujumla wameamka kiroho na ni watii wa sheria kuliko wanaume? Je, wanaishi na roho wa kweli ndani mwao?*

**Jibu:** Wanaume wanafunzwa kuishi maisha ya ukali, ukakamavu na vurugu. Na hii ni alama ya unyonge tukiyazingatia maisha ya kuitegemea sheria ya upendo amabyo ndiyo itegemewayo kwao. Inafikiriwa kikamilifu kwa wanawake kuishi kwa kutegemea sheria ya upendo. Kwa uhakika katika hali zote za maisha, hivyo ndivyo inavyotegemewa kwao. Wanaume wanao umuhimu katika mambo ya kiroho sawa na wanawake, lakini kwa sababu ya tabia yao hii ya ukali na vurugu hushindwa kuyapata mafanikio ya kiroho. Kwenye nchi yetu ya Marekani ni wanaume tu hupigana vita kwa sababu hiyo ndiyo mila yetu, lakini kwenye nchi zingine hata wanawake hupigana.

**Swali:** *Je, wazazi wawaadhibu vipi watoto wao watendapo yaliyo ya utovu wa nidhamu?*

**Jibu:** Utaratibu wa kutoa tuzo kwa yule mtoto atendaye mema ni mzuri sana. Na adhabu itolewayo kwa yule mtenda mabaya ni kumnyima tuzo.

**Swali:** *Uovu ni nini?*

**Jibu:** Wakati mwingine watu wazungumzapo kuhusu uovu huwa wana maana ya matendo yaliyo nje ya upatanisho na desturi za maisha ya watu. Lakini uovu kwa maana ya uovu ni yale matendo yaliyo nje ya upatanisho na lile kusudio takatifu.

**Swali:***Je, akili ni kama kipande cha ubao kilicho wazi kwa ajili ya kuziorodhesha kumbukumbu za matendo ya maisha ya mwanadamu kichwani mwake?*

**Jibu:**Akili ni chombo kiwezacho kutumiwa na, ama unafsi wa mwili wenye muelekeo wa mambo ya duniani tu; ama ileasili ya utakatifu. Ndiyo ilivyo ni kwamba inatokana na kuongozwa na uzoefu.

**Swali:***Ni nini tafsiri yako kuhusu ndoto?*

**Jibu:**Ndoto zilizo nyingi huuwakilisha mzunguko wa mawazo ya mtu rohoni mwake ama mauzauza yawezayo kuletwa na kile mtu apangacho kukifanya. Na hii mara moja husahaulika. Mara chache waweza kutokewa na maono ambayo huwa hayasahauliki.

**Swali:***Je, unafanya kazi ili uishi?*

**Jibu:**Ndiyo, ninafanya kazi ili niishi. Na ninafanya katika njia isiyo ya kawaida. Ninatoa niwezavyo kwa njia ya ushauri wa mawazo, maneno na vitendo kwa wale ambao ninayagusa maisha yao, halikadhalika na kwa nafsi ya utu. Na matokeo yake ninakipokea kile ambacho watu wako tayari kunipa, lakini simuombi mtu. Wote wanabarikiwa kwa kutoa kwao na mimi ninabarikiwa kwa kutoa kwangu.

**Swali:***Kwa nini hukuajiriwa?*

**Jibu:**Mimi sikuajiriwa? Ninafanya kazi saa kumi na sita kila siku, siku saba kwa juma. Una maana kuwa siupokei ujira wa fedha. Sihitaji kupokea ujira wa fedha. Kila kitu nikitakacho hupewa. Huu ndio wajibu kwa maisha yangu. Ningeweza kuishi kihalali kwa kuwategemea walipa kodi kama ningeweza kufanya hivyo, lakini wao hawapendelei kutoa. Hivyo nikaona bora niishi kutegemea kile kitolewacho kwa hiari. Wale wote watoao kwa hiari yao watabarikiwa. Ninaipenda kazi yangu. Ninayo kazi ya kufanya. Kwa mazungumzo tu niyafanyayo, baadhi ya watu wengine hupokea malipo makubwa, mimi sikubali kupokea chochote. Mimi huzijibu barua nyingi niandikiwazo nikiwa ninautoa ushauri kwa watu. Watu wengi wanalipwa malipo mazuri kwa kuutoa ushauri. Mimi sikubali kupokea malipo kwa kazi hiyo. Sasa ninaanza kuwafundisha na kuwahamasisha watu kwa kuwaongoza kuzitembelea sehemu mbalimbali ambayo ni hali ya kujirudi. Shughuli hii inayo matokeo mazuri kwa watu. Ninakumbuka kipindi tulichokwenda Alaska, wale watu niliokwenda nao waliporudi walikuwa wamehamasishwa kiasi kikubwa na kunyanyuliwa juu kiroho na ionyeshavyo ni kwamba kila mmoja wao anafikiri kuhusu kuyashughulikia yale yaliyo mema na kuenenda kwenye njia bora ya utumishi wa kiroho. Ninaamini baadhi ya wale watu waliotoka Alaska kwenye hamasa ya kiroho, hakika hivi sasa wanafanya kazi kubwa ya kuwasaidia watu.

**<u>Swali:</u>***Ni kwa nini hutaki kupokea fedha?*

**Jibu:**Kwa sababu mimi huzungumzia ukweli wa kiroho. Na ukweli wa kiroho hauuzwi asilani. Wale wauuzao hujidhuru kiroho. Mimi huzipokea fedha ninazotumiwa kwa njia ya barua (lakini siziombi) na pia sizitumii mwenyewe. Fedha hizo ninazitumia kwa kupigia chapa barua na gharama za utumaji kwa wale ninaowajibu. Wanaojaribu kuununua ukweli wa kiroho huwa wanajaribu kuupata kabla hawajawa tayari. Ndani ya mazingira haya ya mbingu na nchi yaliyo ndani ya mpangilio mzuri na wa ajabu, wale wautakao ukweli wa kiroho wataupata muda wake ukiwa tayari.

**<u>Swali:</u>***Ni ipi nadharia ya dhana " Usiununue ukweli wa kiroho?"*

**Jibu:**Dhana hii ina maana ya; yule aliye na ukweli wa kiroho hawezi kuuuza, hivyo aonekanae anauuza hakika hanao. Hizi ni lulu zipatikanazo bila gharama yoyote. Mara tu unapokuwa tayari kuupata ukweli huu wa kiroho utaupata bila kipingamizi chochote. Kwa upande mwingine unapewa kadri utoavyo. Lakini kulipa ujira wa kitu chochote huwa siyo kutoa zawadi. Na pia huna haja ya kutoa kwa yule akupaye tu, kwani sisi sote ni chembe chembe hai kwenye mwili wa utu.

**<u>Swali:</u>***Je, huwa hujisikii mpweke, mchovu, ama mwenye hali ya kukata tamaa uwapo kwenye shughuli zako?*

**Jibu:**Sijawahi kujihisi upweke, uchovu, wala kukata tamaa. Ukiishi ndani ya hali ya kuwasiliana na Mungu; daima huwezi kuuhisi upweke. Ukiishi ndani ya mpango wa Mungu na ukajua kwamba juhudi bora katika kazi huleta matunda mazuri huwezi kuwa katika hali ya kukata tamaa. Ukiisha kuipata Amani ya dhati ndani mwako utakuwa unaunganishwa na chanzo cha nguvu ya mbingu na nchi hivyo huwezi kuuhisi uchovu.

**<u>Swali:</u>***Je, ni wapi ulipojifunza mambo hayo unayozungumza? Ni dhahiri kwamba, umekipata kitu ambacho sisi sote tunakitafuta, na huna haja ya kuuficha mwanzo wa habari hii uliyonayo?*

**Jibu:**Sijawahi kuuficha mwanzo wa habari hii yangu. Kuhusu mwanga mimi nanaelekea kwenye mwanga wa kweli na siyo kwa chochote kifananacho na hicho. Pia ninajitahidi kujiongezea mwanga kwa njia ya huu ambao tayari ninao. Huwezi kukosea ule mwanga utokao kwenye chanzo cha ukweli kwani ukishaupata hujazwa na ujuzi ndani mwako ukuwezeshao kuufafanua na kuujadili bila tatizo lolote.

**<u>Swali:</u>***Je, una umri gani?*

**Jibu:**Kwenye sehemu nilizopita nikiwa kwenye safari zangu zaHija ya Amani watu wengi waliniuliza umri wangu. Niliwaambia kwamba mimi sikuujua umri

wangu na nisingeweza kuukisia. Nijuacho ni tarehe yangu ya kuzaliwa. Tarehe hiyo inazunguka kichwani mwangu lakini siwezi kuitangaza. Je, nikiitangaza itasaidia nini? Wengi wamejaribu kulibuni jina langu la zamani. Jina la kuvutia lililobuniwa na wengi ni: **Amelia Earhart**. Ninashukuru kwamba mawazo ya umri hayamo kichwani mwangu. Mara nilipoanza kuihesabu miaka yangu ya kuzaliwa nikaanza kufikiri kuwa ninaelekea uzeeni; na kweli nimezeeka. Umri ni mpango wa akili za mtu. Mimi ninajiona kuwa ni mtu asiye na umri. Na huu ndio ushauri wangu kwa wengine. Endelea kukua kadri utakavyo iwe na uache kuuhesabu umri ulionao.

Hivyo ni kwamba, siwezi kutangaza alama yangu ya ukanda wa nyota. Je, kwa uaminifu, unafikiri ninaweza kuendeshwa na sayari? Nafsi yako takatifu daima iko huru. Ni nafsi ya mwili wako isiyoutegemea uongozi mtakatifu ambayo siyo huru. Ninazo sababu mbili ni kwa nini sitangazi alama yangu ya ukanda wa nyota. Mojawapo ni kwamba, baadhi ya wanajimu jasiri wangeweza kuyachunguza maisha yangu kwa kutumia alama hiyo ya ukanda wa nyota, jambo ambalo lingekuwa la kupoteza muda. Na kama tarehe ya kuzaliwa kwangu ingefahamika, ningesumbuliwa na kadi nyingi ambazo zingetumwa kwangu kunipongeza kwa kutimiza umri fulani tangu kuzaliwa pia na kwa barua kem kem. Usumbufu huu pia, ninaupata kwa kutumiwa kadi nyingi za sikukuuuya Krismasi. Na hali hii, ingekuwa inanichukua muda mwingine zaidi wa majuma mawili kila mwaka kuwajibu waandishi wa barua hizo.

**Swali:***Jina lako halisi ni nani, na ni ipi historia ya maisha yako?*

**Jibu:**Sina jina jingine zaidi ya **"Hujaji wa Amani."** Sina kwetu ila anuani niitumiayo kupokea barua zangu ni Cologne New Jersey. Kuhusiana na historia ya maisha yangu nitasema haya tu: Ninatoka kwenye familia maskini, nina elimu ndogo, sina ujuzi maalum bali ninaishi maisha yenye uongozi wa kiroho.

**Swali:***Je, umewahi kupata watoto?*

**Jibu:**Sikuitwa duniani kuja kushughulika na familia. Walio wengi wamejihusisha na kitu hiki kiitwacho kuhusiana kimapenzi na hatimae kujikuta wanaunda familia. Mimi sikuweza kupewa wito huo. Wapo watu wachache ambao hawana wito wa kushughulika na familia. Wanawake wasioolewa ni wale tuwaitao "Wawachukiao wanaume." Mimi siyo kama wao, ninaelewana vizuri na wanaume.

**Swali:***Je, nguvu nyingi hizi ulizo nazo unazipata vipi?*

**Jibu:**Baada ya kuwa umeipata Amani ya dhati ndani mwako unakuwa nazo zile nguvu zisizoisha. Kadri utoavyo ndivyo kadri upokeavyo zaidi. Baada ya kuwa umeupata wito wako unazifanya shughuli zako kwa urahisi na furaha zaidi. Kamwe huwezi kuhisi uchovu.

**<u>Swali:</u>***Ukiulinganisha umri wako na ule wa wanafunzi, huoni kwamba hustahili kuhusiana nao? Kwani unawazidi mbali.*

**Jibu:**Ninafikiri tuzingatie thamani ya uhusiano wangu na wanafunzi badala ya kuzingatia umri. Wanafunzi wako kwenye uasi mkubwa dhidi ya matendo maovu ya jamii kama vile; vita, dhuluma, umilikaji wa vitu pamoja na unafiki kwenye jamii. Kwa vile mimi mwenyewe sipendelei matendo ya aina hiyo, sina sababu yoyote ya kunizuia kuhusiana na wanafunzi.

**<u>Swali:</u>***Je, unauamini utabiri wa nyota?*

**Jibu:**Kama tuwezavyo kuutafsiri utabiri wa nyota, ni jambo ambalo haliko kwenye upatanisho na roho wa kweli. Wale walifuataο wamezama katika utegemeaji wa nafsi ya mwili bila kuutegemea utakatifu ndani mwao.

**<u>Swali:</u>***Kama nimepatwa na tatizo; je, ninaweza kulikabili kitaalamu?*

**Jibu:**Ukipatwa na tatizo la kiafya jaribu ujiulize mwenyewe kama umeukosea mwili wako kwa kushindwa kuutunza ipasavyo. Kama unalo tatizo la kifedha, jiulize kama umekwenda nje ya taratibu zako za maisha ya kila siku. Kama umepatwa na tatizo la kisaikolojia jiulize kama umo ndani ya upendo wa watu kama vile Mungu atakavo ufanye. lile ulifanyalo sasa linakujengea matokeo ya baadae hivyo utumie muda wa sasa ili uyajenge mazuri ajabu kwa wakati ujao.

**<u>Swali:</u>***Ninasumbuliwa sana na dhana ya ulipizaji kisasi kwa watu wanisemao na kunitendea mabaya.*

**Jibu:**Kama hakika unafahamu kila kitu, badala ya kulipiza kisasi kwa yale mabaya ufanyiwayo; yageuze kuwa huruma kuu kwa wabaya wako. Wale wote wakufanyiao mabaya wako nje ya upatanisho na ukweli mtakatifu, hivyo wanahitaji upendo. Ni muhimu sana kupenda. Jaribu kukabiliana na hali yoyote ile kwa upendo ili ufanikiwe kirahisi. Endapo mtu atanitenda ubaya nitamhurumia sana na itanipasa nimuombee. Siwezi kujidhuru kwa matendo mabaya yashinikizwayo na hali ya uchungu ama hasira.

**<u>Swali:</u>***Je, nidhamu ya kujituma inafaa?*

**Jibu:**Labda njia kuelekea kwenye Amani ya dhati ndani mwako siyo rahisi kupitika. Lakini ukishafika uendako utashangaa na kuanza kufikiri; " Ni vipi nilivyoweza kupata baraka kubwa kirahisi tokana na Amani ya dhati ndani mwangu? "

**<u>Swali:</u>***Ni nini atakiwacho kukifanya mtu yule mwenye tabia ya kupenda kula sana na yule alaye chakula kisichofaa?*

**Jibu:**Kama mwenye tabia hii atagundua tatizo hilo alilonalo na atake kulirekebisha; itambidi aanze kwa kukipata chakula kizuri kiufaacho mwili wake kilichopo. Kama utalichukua suala la chakula kama kitu cha muda tu, na ukajali kuutumia muda wako kufanya mambo mengine yenye manufaa, kamwe hutapata muda wa kuuwazia mlo tu; kwa muda wako wote.

**Swali:***Je, twawezaje kuieneza Amani kwa njia ya michezo ya kuigiza?*

**Jibu:**Ninafikiri, njia moja ya kuieneza Amani kwa njia ya michezo ya kuigiza ni kufanya maonyesho ya kutembea sehemu mbali mbali. Kwa muda mrefu nimefikiria uanzishwaji wa maonyesho ya michezo ya sanaa kama njia mojawapo ya kuieneza Amani ulimwenguni. Ni watu wachache sana wasikilizao mihadhara ya kuieneza Amani. Wengi wakipewa vitini vyenye maandishi ya kuieneza Amani wataweza kusoma nusu ama kitini kizima kadri watakavyoona inawafaa. Wengine watasikiliza radio ama televisheni endapo utatangazwa ujumbe wa kuieneza Amani. Hata hivyo karibu kila mtu ataangalia michezo ya kuigiza ama michoro yenye malengo ya kuieneza Amani kama itaanzishwa mahali pale walipo.

**Swali:***Je, tunahusika kwa mawazo na hisia zetu? Je, kimsingi kuna tofauti, na uwajibikaji utokanao na tabia zetu?*

**Jibu:**Tukiongea kwa misingi ya kiroho, wewe unadhurika kutokana na mawazo pamoja na hisia potofu kama udhurikavyo kutokana na tabia mbaya. Hata hivyo utadhurika zaidi kama unalijua tatizo na usilitafutie ufumbuzi. Ndiyo, wewe unawajibika kwa yote matatu.

**Swali:***Je, kustaafu kazi kuna maana gani kwa mtu?*

**Jibu:**Kustaafu hakuna maana ya mwisho wa uwajibikaji. maana yake ni kubadilisha shughuli ili uzame zaidi kwenye shughuli za kujitoa maisha yako katika utumishi. Kwa hiyo utakuwa umepata kipindi cha ajabu maishani mwako. Kipindi ambacho kitakuwa cha furaha zaidi na chenye shughuli za manufaa kwako.

**Swali:***Je, nifanye nini endapo maisha yangu yataonekana kuwa matupu yaani kutokuwa na lolote nilifanyalo duniani?*

**Jibu:**Endapo maisha yako yataonekana matupu, utakuwa unayo nafasi ya kutosha ajabu! Maisha mengine kiasi yaliyopita yatakuwa yamekwishajazwa na mambo ambayo siyo mazuri. Hivyo uyaonapo maisha yako kuwa na utupu, itumie nafasi ya wakati wako uliosalia kuyajaza yale mazuri tu yenye misingi ya ukweli wa kiroho.

**Swali:***Je, nifanye nini endapo nitajisikia kuupata wito?*

**Jibu:**Jiulize kama wito wa lile utakiwalo kulifanya lina sababu ya maana. Kama ndiyo, utaupata ukuaji wa kiroho kwa kutumika. Kama sivyo, ujifunze kusema " hapana." Kwa kauli ya upendo.

**Swali:***Ni kitu gani cha kuushinda uoga?*

**Jibu:**Ningesema kwamba ni matendo mema ya kidini ambayo huushinda uoga. Kama unayo matendo ya upendo kwa wanadamu wenzako, hautawaogopa. Upendo kamili huuondoa uoga. Tabia ya utiifu kwa Mungu itakuingiza kwenye upatanisho wa daima na uwepo wa Mungu hivyo uoga hautakuwepo. Ukijitambua kwamba wewe umeuvaa mwili uharibikao, kwamba wewe ndiye ukweli uuendeshao mwili na ukweli huo hauharibiki; ni kwa nini uogope?

**Swali:***Je, ninawezaje kuushinda uoga mdogo kama vile uoga wa giza niwapo nje mwenyewe?*

**Jibu:**Mimi hulifikiria giza kama rafiki yangu. Giza hutuletea hali ya kujisikia tumo kwenye pumziko lishinikizalo usingizi. Ninakushauri usubiri giza lianze kutanda, uuangalie uzuri wa giza linavyotanda nchi taratibu, uziangalie nyota zinavyoanza kujitokeza moja moja. Zoea taratibu giza hilo. Endelea hivyo kila siku hadi utakapozoea. Uoga ni kukiogopa kile usichokifahamu.

**Swali:***Wataalam wa magonjwa ya akili husema kuwa wanadamu wote huisi uoga, na wewe unasema kwamba huogopi chochote hata kiwe ni kifo. Ni kwa vipi wewe mwenyewe ujifanye huna hali yoyote ya woga? Una maana wewe unao udhibiti wa akili kuliko watu wengine?*

**Jibu:**Katika maisha yetu ya mwanzo huwa tunahisi uoga zaidi kama tulivyojifunza kwa njia moja au nyingine. Akili zako, mwili wako, pamoja na matendo vyaweza kudhibitiwa na ile nafsi takatifu ndani mwako na wala siyo nafsi ya mwili usiotegemea uongozi wa kiroho. Kama hakika wewe unawapenda watu huwezi kuwaogopa. Kama unaishi ndani ya upatanisho na yale mapenzi matakatifu, uoga utakwisha.Kama utajihusisha na kile kilichomo ndani mwako ambacho kinaishi milele huwezi kukiogopa kifo. Kama utaogopa; ni wazi kwamba maisha yako bado yanatawaliwa na nafsi ya mwili isiyokuwa na uongozi wa roho ndani mwako. Kwa kutumia juhudi kubwa ya akili unaweza kujifunza mwenyewe hali ya kutohisi uoga kwa jambo lolote. Lakini wakati utawaliwapo na utakatifu ndani mwako hutakuwa na uoga.

**Swali:***Ninaweza kufanya nini ili maisha yangu yawe ya manufaa?*

**Jibu:**Miaka kumi na mitano kabla sijaianza safari yangu ya Hija, nilijihisi utashi kamili usiorudi nyuma wa kujitolea maisha yangu kwa Mungu nikiwa tayari kumtumikia. Nilianza kuishi kwa kutoa badala ya kutaka kupata. Kila siku asubuhi

nilimfikiri Mungu nikafikiri ni jukumu gani ningalilifanya siku hiyo ili liwe la manufaa kwa watoto wa Mungu. Niliiangalia kila hali niliyokutana nayo kuona kama lipo lolote ambalo ningelilifanya katika kumtumikia Mungu. Kila siku niliyafanya mambo mengi mazuri kadri ilivyowezekana bila kuusahau umuhimu wa kuyatumia maneno mazuri kwa watu pamoja na tabasanu la furaha usoni mwangu. Nilisali nikimuomba Mungu kuhusiana na mambo yaliyoonekana makubwa kwangu kuyakabili. Sala ya kweli huyachochea matendo ya kweli. Maisha yangu yalijengeka kiroho. Nawe jaribu uone!

**Swali:** *Je, nianzeje kuishi maisha ya uhakika?*

**Jibu:** Nilianza kuishi maisha ya uhakika wakati nilipoanza kuiangalia kila hali iliyonizunguka na kufikiri ni vipi ningeweza kuitumikia hali hiyo kiufasaha. Niligundua kwamba, nitawasaidia watu katika hali yoyote ile kwa hiari yangu mwenyewe na wala siyo kwa kulazimishwa. Mara kwa mara nilitoa msaada ama labda kwa tabasamu la upendo ama furaha. Nilijifunza kwamba, kwa kutoa tunavipata vitu vya thamani sana maishani.

**Swali:** *Je, maisha ya mtu yanaweza kuimarishwa vipi?*

**Jibu:** Tafuta majibu ndani mwako. Asili ya utakatifu ndani mwako, mwanga wa dhati ndani mwako unayo majibu. Tumia muda wako kuyaweka maisha yako kwenye upatanisho na sheria takatifu. Shughulika kuushinda ubaya kwa kuutenda wema, uongo kwa ukweli nayo chuki kwa upendo.

Shughulika ukijijengea utaratibu mzuri wa maisha yako. Uwe ndani ama nje ya utaratibu wa kuitunza familia yafuatayo ni muhimu kwako:-

1.Jenga tabia ya kuishi ambayo ni ya manufaa kwenye jamii.

2.Uwe na tabia nzuri pamoja na kufanya mazoezi ya viungo na upumuzishaji wa akili bila kusahau tabia ya kukipata chakula na zaidi ya yote jenga tabia ya kuyafikiria yaliyo mema usiyafikirie mawazo potofu.

3.Pata hamasa ya mambo yawezayo kukuinua kiroho maishani mwako, kama vile kusoma maandishi mazuri, kusikiliza nyimbo nzuri zenye mafunzo ya kiroho na uuangalie uzuri wa maumbile ya asili.

4.Mtumikie Mungu kwa kadri inavyowezekana. Fanya kadri iwezekanavyo kuwasaidia wenzako kwani ulimwenguni humu utapewa kadri utoavyo.

**Swali:** *Je, nitasaidia nini katika kuyaimarisha maisha yangu wakati watu walio wengi wako nje ya upatanisho na ukweli mtakatifu?*

**Jibu:** Utu huimarika kadri watu waimarikavyo. Unapokuwa umeyaimarisha maisha yako unawahamasisha wale waliokuzunguka kutaka kufanya kama wewe

ulivyofanya. kumbuka kwamba wachache walio ndani ya upatanisho na mapenzi ya Mungu wanazo nguvu zaidi ya wengi sana walio nje ya upatanisho huo.

**Swali:** *Je, mtu mdogo kama mimi ni lipi niwezalo kulifanya katika kueneza Amani?*

**Jibu:** Kwa mamilioni ya watu waishio ndani ya ulimwengu huu leo hii, ninasema kwamba yapo mambo mengi yenye thamani ambayo watu wadogo wanaweza kuyafanya awe ni mtu mmoja ama kikundi cha watu. nilipojitoa maisha yangu kuufanya utumishi wa Bwana, kwa watu; mtu mmoja kwa mzaha aliniuliza swali akisema: " Wewe unafikiri unaweza kufanya nini? " Na mimi nilimjibu ;" Ninafahamu kuwa mimi ni mtu mdogo na nitaweza kukifanya kile kidogo kilinganacho na uwezo wangu, lakini yapo mambo mengi madogo yanayohitaji kufanyika. " Na kamwe sikupata tatizo lolote katika kufanya mambo madogo lakini yenye thamani kubwa kwa watu. Nilipozianza ziara zangu za Hija nilikuwa ninaulizia mambo makubwa ya kufanya, na mtu mmoja alinijibu; " Unaweza kuuliza hata mwezi. " Lakini mimi nilimjibu; " Kama sisi watu wadogo kwa pamoja tutaweza kutaka yafanyike yaliyo makubwa sana, yatafanyika. " Ninaweza kusema jambo hili kwako: Yazingatie ya sasa. Yafanye yale ujuayo yanahitaji kufanyika. Fanya mema yote kadri uwezavyo kwa kila siku. Yale yajayo yatajifunua yenyewe.

## NYONGEZA YA IV

## TENZI, SALA NA NYIMBO

---

*Nyingi za tenzi hizi zifuatazo zilizotungwa na hujaji wa Amani ziliandikwa mapema kwenye kipindi chake cha hija zilizoonekana kwenye kijarida chake kilichoitwa " **Tenzi za nyakati zetu.**"*

*Toleo lake liitwalo " **Sifa za heri za msafiri wa Amani** " lilitolewa kwenye mojawapo ya magazeti yake ambayo yalikuwa hayatokei mara kwa mara yaliyoitwa " **Maendeleo ya Hujaji wa Amani**" na pia kwenye matoleo ya " **Hatua za kuielekea Amani ya dhati.**"*

*Amani, alipendelea kufundisha nyimbo kwa wenzake. Na mara kwa mara alizoea kuvuta mikusanyiko ya watu ili waungane naye kuimba " **Chem. chemi za upendo.**"*

### KANISA LA KIKRISTO

**Alisema; yawezekana nikawa nimekosea
lakini sitashangaa,
Kama hilo ndilo lililokuwa kanisa kubwa
la Kikristo,
Ambalo mwanadamu aliwahi kulianzisha.
Vinanda vyetu ni bora sana
Kwaya yetu iko tayari tayari
Madirisha yetu ya vioo hayana gharama yoyote.
Madhabahu ni bora kama utakavyoona.**

**Lakini ni matajiri tu, wakaribishwao pale.
Nilisikia hoja zenye matamshi yasiyofaa yenye uchochezi
Na pale madhabahuni alisimama mhubiri
Mwenye tuzo ya kuenzi mapambano ya kivita.**

**" Kuna lolote zaidi uwezalo kuihitaji mle kanisani?"
Kwa kujisifu alinihoji.
" Jambo moja tu," nilimjibu.
" Nalo ni Ukristo."**

### ULIMWENGU BILA MWANADAMU:

**Mbele yangu mto unatiririsha maji kwa sauti
Nyuma yangu uliinuka mlima uliosheheni miti**

ukiwa umesimama kwa Amani.
Mwanadamu anasema huu ni ulimwengu wake, niliwaza.
Na bado ulikuwapo wakati kabla
mwanadamu hajaishi kwenye ulimwengu huu.
Je, Ulimwengu huu mkongwe wakati huo uliishi sawa
na leo bila kuwa na wanadamu?
" Wakati huo nilikuwa ninatiririka hivi hivi."
Mto ulinong'ona.
" Nilikuwa nimesimama imara hivi hivi."
Mlima ulinong'ona.
" Mwanadamu sasa," niliwaza, " anaonyesha kuinamia
maangamizi yake mwenyewe."
Mamilioni ya vitu viovu alivyovivumbua
Kila kimoja kikiwa na nguvu za kuua
zaidi ya kile kilichotangulia kabla.
Kama atafanikiwa kujiangamiza kabisa,
Je, huu ulimwengu asemao ni wake
Utaendelea kuishi bila yeye?
" Nitakuwa ninaendelea kutiririka hivi hivi."
Mto ulinong'ona.
" Nitakuwa nimesimama imara hivi hivi."
Mlima ulinong'ona.

<u>HOMA YA VITA:</u>

Upofu huo wa hatari,
Umfanyao adui yako aonekane kama ibilisi,
mbele yako.
Na wewe ukakufanya uonekane kama
ibilisi mbele yake,
Homa ya vita.

Wazimu huo utishao,
Uwafanyao wale wale kupanga mapambano
ya kivita juu yako.
kupanga hila zenye ubaya kwa adui.
Homa ya vita.

Ulevi huo utishao,
Uchanganyao akili mpaka zikauona ubaya
kuwa ni wema,
Chuki ionekane ni wema na mauaji
Kuhalalishwa,

Homa ya vita.

Ugonjwa huo utishao,
Ambao hautafutiwi tiba na badala yake
Zinatafutwa njia za kuusambaza,
Homa ya vita.

## KAFARA

Siku nyingi sana zilizopita wakati
wanadamu walipokuwa bado ushenzini,
Walichagua mtu mmoja ama wawili,
Kufa kwa kutolewa kafara
Kwa ajili ya mungu wa dhoruba
aliyeitwa, Thor.
Lakini wakati huu ambapo wanao ustaarabu
wa Kikristo.
Wanachagua milioni moja ama mbili za watu,
Kutolewa kafara kwa ajili ya mungu asiye na huruma
aitwaye vita.

## VITA

Kwenye uwanja wa mapambano ya kivita
Walikonilazimisha kwenda,
Huko nilikutana na mtu ambaye walidai ni adui yangu
Nilimkimbilia na kumchoma singe!

Nilipoichomoa mwilini mwake, damu ilimtoka kwa wingi.
Mara moja nilijawa na uchungu
wa majuto moyoni mwangu.
" Oh nimeua mtu, " Nilijisemea.

Alikuwa kijana mwembamba, mchanga
kiumri mwenye uso wa uoga kama wangu.
Haonyeshi hali ya ubaya kama walivyosema.
" Walinituma nikuue." Alidai.

" Kwa uwezo wake Mola! laiti ungefanya hivyo! "
Nilimuapia.

" Kwa nini, sijui hata nikipiganiacho! "
Aliniuliza kwa mshangao
" Hata mimi sijui. " Nilimjibu.
Alipumua akakata roho.

## MSHINDI

Ndani ya maangamizi yaliyoletwa na mwanadamu
Maumbile ya asili yanaendelea
Kuwapo kiutulivu.
Ndani ya sauti za mayowe za watu wanaokufa
zikiambatana na milio ya kutisha ya bunduki
Kipupwe kinakuja na kupita.

Kuzunguka ncha ya bunduki iliyo katika
Majani machanga yenye uzuri wa
aina yake yanaonekana.
Kupitia kwenye matundu ya macho
ya fuvu la mwanadamu aliyekufa
Kwenye uharibifu huo,
Mmea wa maua unaota.

## KWA YULE MPENDA HAKI

Bwana aliutazama Ulimwengu,
Mwaka elfu moja mia tisa sabini na mbili,
Akaona wanadamu wanateseka kwa chuki.
Ni wachache walioonekana mbele ya Bwana
wako kwenye njia ya kweli,
Aliona watu wanamwaga damu ya
wanadamu wenzao,
Wakiwapa wenzao mateso yenye maumivu yasiyoelezeka,
Nilisikia Bwana akinong'ona,
"Kwao ninaongea bali hawanisikii."

Wakati huo Bwana alimpeleleza
Mtu mmoja mwenye hekima,
Aliyeonekana kudharauliwa kulaumiwa
na aliishi kwa upweke.
Kwa sababu hakupenda matendo ya
chuki na mauaji.
Gereza ndilo yalikuwa masikani yake.

Lengo lake halikuwa la kujilimbikizia utajiri.
Bali aliwatumikia wenzake kwenye shida.
Nilisikia Bwana ananong'ona,
"Ndani ya huyu nitaishi tena!"

## TAMAA
(Hadithi ya watu ama mataifa)

Walikuwapo watu wawili waliokuwa na uadui
wa kugombania mpaka wa ardhi.
Mmoja wao alisema, " Hii ardhi ni mali yangu."
Mwingine naye alisema; " Ni mali yangu."

Hivyo walipigana, wakapigana
Kama wanyama wawili wa porini.
" Oh laiti ungeona damu iliyomwagika, "
Hadi mmojawao alipata kilema cha kudumu.
Na mwenzake alikufa!
Huyo mlemavu aliishi kwa taabu na mashaka.
Akatoa kilio cha kukata tamaa.
" Upumbavu gani tuliokuwa nao
wa tamaa ya kugombania ardhi!
Ilikuwapo ardhi ya kutosha kabisa
kwetu sote wawili kugawana! "

## WAKATI WAKO UJAO

Kwenye Ulimwengu huu
Unapewa kadri utoavyo,
Na unasamehewa kadri unavyowasamehe wenzako,
Wakati unapokwenda njia yako
Kwa kila siku ya upendo ipitayo,
Unajijengea wakati mzuri ujao
Kutegemeana na jinsi uishivyo.

## SIFA ZA HERI ZA HUJAJI WA AMANI

Wamebarikiwa wale watoao
bila kutegemea shukrani
Kutoka kwa wale wawapao.
Kwani watazawadiwa kwa kiwango kikubwa.

Wamebarikiwa wale watafsirio kila jambo jema walijuslo
katika matendo mema
Kwani ukweli ulio juu
Utafunuliwa ndani mwao.

Wamebarikiwa wale wafanyao
Yale yaliyo ndani ya mapenzi ya Mungu
bila kuuliza matokeo ya kazi yao
Kwani malipo yao yatakuwa makubwa.

Wamebarikiwa wale wapendao
na kuwaamini wanadamu wenzao,
kwani wataufikia ule wema uliomo ndani mwa wenzao
na kuupokea.

Wamebarikiwa wale waliouona ukweli
Kwani wanafahamu kwamba utu siyo vazi la udongo
Walilo nalo,
bali kipo kitu ndani mwao
Kiliendeshacho hilo vazi
na ambacho ni cha kweli
Na hakiharibiki milele.

Wamebarikiwa wale wakionao
Kifo kuwa ni badiliko
kuelekea kwenye maisha huru kutoka
kwenye maisha haya ya mipaka yaliyo ya duniani,
kwani watafurahia
pamoja na wapendwa wao
ambao wanaendesha maisha ya mpito
kuelekea kwenye kilele cha uhuru.

Wamebarikiwa wale ambao
baada ya kuyatoa maisha yao kwa ajili ya Bwana
na kupokea baraka, wanaonyesha moyo wa juhudi
kupambana na njia yenye matatizo
kuelekea kwenye kilele cha uhuru.
Wakifanikiwa watabarikiwa mara ya pili.

Wamebarikiwa wanaosonga mbele
kuelekea kwenye njia ya kiroho
bila tendo lolote la kibinafsi

Katika kuitafuta amani ya dhati ndani mwao.
Kwani hali hiyo itajitokeza yenyewe.
Wamebarikiwa wale ambao
badala ya kujifungia milango ya Ufalme wa mbinguni
wanatembea kwa madaha
kuielekea wakiwa na roho wa kujituma, upendo na utakaso,.
kwani wataingia
pasipo kipingamizi chochote.

ALOHA OE!

*(Amani alifundisha wimbo huu ambao ni wimbo wa watu wa Hawaii, ujulikanao sana. Aliwafundisha watu wale alioongozana nao kwenye safari ya kuhamasisha kiroho watu wa Visiwani humo mwaka 1980).*

Angalia nchi hii ya uchawi yenye maji yachezayo,
Imejazwa na joto la mionzi ya jua
itokayo kwenye bahari ya Kusini,
Utembeapo kwenye mashamba
yenye harufu nzuri za maua.
Ukisikiliza sauti nzuri
ya muziki wa Kihawaii.

Aloha O!________ Nikupendaye,
Tembea taratibu kwenye nchi hii ya jua pamoja na maua,
Aloha O!_______ Mungu anakupenda pia,
Na anazibariki hatua zako utembeapo njiani.

CHEMI CHEMI YA UPENDO

Chemi chemi ya upendo
Chanzo changu kimo ndani mwako
Napenda mapenzi yako
Roho yangu i huru
Siku ipendezayo
Wakati sisi wote tuonapo
Tumaini la ulimwengu
Ni upendo.

## SALA YA AMANI KWA AJILI YA ULIMWENGU ULIOVAA VAZI LA VITA

Oh, Roho wa ajabu ulie mtaratibu utuguse,
ututulize na ututie moyo sisi na watu wote,
Uchukue mabomu na singe toka mikononi mwetu iogopayo,
Badala yake utuzatiti zana ya Imani,
Utupatie zana ya hekima na upendo,
Kiasi kwamba, wakati wowote na mahali popote tutembeapo,
Maisha ya uzima wa milele yatajaa
ndani mwetu badala ya kifo.
Haya tunajua ndiyo mapenzi ya Bwana wa Amani,
**Amina.**

NYONGEZA YA V

## MSAFIRI WA AMANI KWENYE VYOMBO VYA HABARI

***Hujaji wa Amani alifurahia kukutana na waandishi wa habari mara kwa mara, hali kadhalika watangazaji wa redio na televisheni.***

***Alihisi kwamba njia ya utangazaji wa habari ilikuwa muhimu kusaidia kusambaza ujumbe wake kote kwa watu wa Jumuiya mbali mbali.***

***Ilivyo kawaida, baada ya waandishi wa habari kuonyesha mashaka yao kuhusiana na jinsi walivyomuona katika hali aliyokuwa nayo kwa wakati huo, hatimaye walikubaliana na uwezo wake katika mambo ya kiroho aliyokuwa anaelezea wakati anahojiwa na waandishi hao.***

***Baadhi ya vichwa muhimu vya habari vilivyojitokeza kwenye magazeti mbalimbali kama ionyeshwavyo hapa chini:***

**MSAFIRI WA AMANI KUANZA MATEMBEZI YAKE KWA MIGUU NCHINI MAREKANI IKIWA NI KAMPENI YAKE DHIDI YA VITA.**
**(Los Angeles Times 4 Januari 1953).**

**MSAFIRI WA AMANI HUKO TOREDO ANATEMBEA MAILI ELFU TANO (5,000) AMBAZO NI SAWA NA KILOMETA ELFU NANE (8,000).**
Mwanamke asiyetambulika jina anapanga kutoa ombi lake kwenye IKE Umoja wa Mataifa.
**(Gazeti la Toledo Blade 17 Septemba 1953).**

**MSAFIRI WA AMANI ASIMAMA SEDALIA AKIWA KWENYE MATEMBEZI YAKE KWA MIGUU YA MAILI ELFU KUMI (10,000) AMBAYO NI SAWA SAWA NA KILOMETA ELFU KUMI NA SITA (16,000) KUUSHAWISHI ULIMWENGU DHIDI YA ONGEZEKO LA SILAHA KALI DUNIANI.**
**(Gazeti la Sedalia Missouri Democrat la Novemba 7, 1955).**

**MSAFIRI WA AMANI ANATEMBEA KWA AJILI YA ULIMWENGU WA AMANI.**
**(Gazeti la The Clarion- Ledger, Jackson, Miss, Januari 19, 1956).**
**MAENDELEO YA MSAFIRI YAMFIKISHA KENTUCKY.**
**(Gazeti la The Courier Journal, Louisville Februari 27, 1956).**

**ANATEMBEA KWA KUIWEK \ MAREKANI TAYARI KUHUSIANA NA UMUHIMU WA KUHITAJI AMANI.**
**(Gazeti la Bloomington, Indiana, Daily Herald Telephone 8 Machi 1956).**

***Mwanamke huyu anatembea kwa ajili ya amani akiiongelea:***
**HAKIKA ANAO MPANGO WA KUSHUGHULIKIA AMANI.**
**(Gazeti la The Indianapolis Star Machi 12, 1956).**

**AKIWA NA AMANI AMBAO NDIO UJUMBE WAKE, MAILI ZINAONGEZEKA KWA MSAFIRI.**
**(Gazeti la Northern Arizona University Student, Flagstaff 4 Oktoba 1969).**

**MSAFIRI WA AMANI ATEMBEA MAILI ISHIRINI NA TANO ELFU (25,000) SAWA SAWA NA KILOMETA AROBAINI ELFU (40,000) KWA AJILI YA AMANI YA ULIMWENGU.**
**(Gazeti la St. Louis Post Disparch, 25 Aprili 1971).**

**Mwanamke mdogo na mkongwe huko Tennies:**
**MSAFIRI WA AMANI ANATEMBEA ZAIDI NA ZAIDI.......**
**(Gazeti la Los Angeles, Times 3 Desemba 1973).**
**Miaka 21 ya kuzunguka matembezini:**
**BINTI MFALME ATEMBEA KWA AJILI YA WANADAMU.**
**(Gazeti la Pasadena Calfornia, Star News 16 Desemba 1973).**

**Mwenye hatua za nguvu akamilisha maili 25,000 ambazo ni sawa na kilometa 40,000:**
**MWANAMKE ATEMBEAYE MASAFA MAREFU MAISHANI MWAKE AKIHIJI KWA AJILI YA AMANI.**
**(Gazeti la Pomona California. Progress Bulletin 2 Februari 1974).**

**MALAIKA MLINZI WA MSAFIRI WA AMANI AFANYA KAZI KWA MUDA WA ZIADA.**
**(Gazeti la Norfolk, Va--, Star Ledger 20 Aprili 1977).**

Anatembea akiwa mwepesi bila mzigo wowote mzito alichonacho ni ramani ya kumuongoza, ujumbe wake, chanuo, mswaki wa kukunja na kalamu:
**MSAFIRI WA UPENDO NA AMANI ALIYE WA KISASA.**
**(Gazeti la South Jersey Courier Post, Cherry Hill N.J. Oktoba 11, 1977).**

**MSAFIRI WA AMANI BADO ANATEMBEA LAKINI SASA AMEACHA KUHESABU MAILI ATEMBEAZO.**
**(Gazeti la Upper Sun Coast News, Florida 7 Desemba 1977).**

**MSAFIRI WA AMANI AANZA MATEMBEZI KUELEKEA MASHARIKI YA PWANI YA FLORIDA.**
**(Gazeti la St. Petersburg Times January 5 1978).**

**MSAFIRI WA AMANI ATEMBEA KIPINDI CHA ROBO KARNE AKIENEZA AMANI.**
**(Gazeti la Whittier, California, Daily News 30 Desemba 1978).**

**MSAFIRI ATHIBISHA KUWA UKOMAVU WA KIROHO HUONGOZA KWENYE AMANI.**
**(Gazeti la Corolado Springs Telegraph 28 Aprili 1979).**

**MSAFIRI ASIYE NA UMRI ANAENDESHA UJUMBE WENYE UMRI.**
**(Jarida la Milwaukee June 22, 1981).**

**BADO ANATEMBEA NCHINI AKISAIDIA KUENEZA VYANZO VYA AMANI.**
**(Valparaiso, Ind. Post Tribune Julai 3, 1981).**

**MSAFIRI WA AMANI ALETA UJUMBE WA AMANI HAPA KNOX.**
**(Gazeti la Starke County Leader, Indiana Julai 7, 1981).**

## MSAFIRI WA AMANI KUANZA MATEMBEZI YAKE NCHINI MAREKANI IKIWA KAMPENI YAKE DHIDI YA VITA.

Msafiri wa Amani kama apendavyo kuitwa mpaka hapo atakapokuwa amemaliza ujumbe wake, anapanga kuondoka Los Angeles kesho asubuhi akiwa katika matembezi yake nchini akieneza Amani ya ulimwengu.


" Hali ya ulimwengu inatuelekeza kwenye kifo, " alisema. "Labda tuamke kutoka kwenye ulegevu tulionao tujisukume kwa nguvu zote na haraka sana ili tuondokane na hatari ambayo inatunyemelea. Vile vyote tunavyovitunza kwa furaha na upendo vitaangamia kwenye maangamizi yajayo."

Akiwa kwenye maandalizi yake kwa ajili ya matembezi ya masafa marefu, alitembea kiasi cha maili 2,500 ambazo ni sawa sawa na kilometa elfu nne-(4,000) kwenye kipindi cha masika iliyopita akizunguka ukanda wa Appalachia kutoka Maine hadi Georgia akipitia na kwenye njia zingine. Alisema kuwa alijifunza namna ya kuishi nje ya nyumba na kulala usingizi mahali popote njiani awapo matembezini. Anaamini kwamba njia ya kupata Amani ni kuushinda ubaya kwa kuyatenda yaliyo mema, uongo kwa ukweli na chuki kwa upendo. Alisema, sheria takatifu hapo, itafanya kazi yake.




**Mtembeaji , anataka aitwe**
" Msafiri wa Amani."
Huyu mwanamke wa ajabu ataondoka Los Angeles leo akiwa katika matembezi yake ya Amani kuelekea upande wa pwani ya Mashariki.

***(Gazeti la Los Angeles Times 4 Januari 1953).***




**Ujumbe kwa watu wa Boston-** Akijieleza kuwa yeye ni "Msafiri wa Amani" lakini akikataa kujitambulisha zaidi, mwanamke huyu aliongea na watu wa Boston Common jana, na anasema kwamba amekwisha kutembea umbali wa maili 8,900 ambazo ni sawa na kilometa 14,040 kwenye majimbo 37 nchini Marekani akieneza Amani ulimwenguni. ***(Gazeti la Boston Herald 30 Julai 1956).***

---




*(Gazeti la Kansas City Star times Novemba 2, 1955)*

MATEMBEZI YA AMANI, **mwanamke ambaye amekamilisha umbali wa maili 7,100 ambazo ni sawa na kilometa 11,360 kati ya maili 10,000 ambazo ni sawa na kilometa 16,000 alizopanga katika matembezi yake, jana aliwasili jijini Kansas.**

**Mwanamke huyu ambaye anapendelea aitwe Msafiri wa Amani anasafiri bila fedha zozote mfukoni mwake.** Anaishi kwa kuutegemea uhisani wa watu anaokutana nao ili wampe hifadhi ya pumziko na chakula. Huvaa vazi la rangi ya bluu ambalo linalegea mwilini mwake na juu yake

amevalia kisibau nyuma ya vazi lake la kisibau yapo maandishi yasomekayo: " **Matembezi ya maili 10,000 ambazo ni sawa sawa na kilometa 16,000 kwa ajili ya upunguzaji wa silaha duniani."** Kifuani vazi hilo linasomeka; **" Msafiri wa Amani." (Na mpiga picha wa Kansas City Star).**

**ALITUKUSANYA KWA MAONGEZI YAKE NA TULIPENDEZWA SANA (Habari kutoka Wilaya ya Harvey Newton Kansas 25 Juni 1953. Zimehaririwa na Floyd Geyman).**

Akishirikiana nasi chini ya anga hii leo ni mwanamke asiyekuwa na masikani wala uangalizi wa yeyote yule, ambaye pia ameguswa na upendo wa Mungu maishani mwake. Amebahatika kupewa kipaji kimuwezeshacho kukaa na utulivu unaotawaliwa na uso mchangamfu uvutiao kila mtu. Akitembea hatua za uhakika, alieleza kwa ushawishi mkubwa habari zionekanazo kutofurahiwa akizielekeza kwenye ukweli utakiwao. Alionyesha ushindi mkubwa wa hoja kwa mazungumzo yake na alipoondoka alituacha na mawazo mazito yenye mchanganyiko.

Aliingia hapa, akiwa amevalia kama aonekanavyo pichani, aliisogelea kaunta ya juu, uso wake ukiwa umekingwa na urefu wa kaunta hiyo. Tulipomuona mara ya kwanza tulidhani ni nyani aliyevalia mavazi yaliyochafuliwa kwa mafuta ya grisi akitokea kuhudumia kwenye kituo cha kuuzia mafuta ya petroli. Lakini ukimtazama mara ya pili utagundua kwamba alama ile iliyopambwa kifuani kama ni maandishi basi siyo kampuni ya kuuza mafuta bali yanaeleza **" Msafiri wa Amani."**

Kama tutaufurahia ujumbe pamoja na habari zake, basi ziko hapa___ akitoa karatasi ambazo kurasa zake zimepigwa chapa vizuri. Baada ya kutazama haraka haraka, jambo moja muhimu laonekana kukosekana labda kutokana na kutoona vizuri.

Jina lako? Nikiwa nimeshikilia penseli yangu tayari kuandika nilimuuliza jina.

Hapo ndipo mjadala wa maneno ya mzaha lakini yenye maana ulipozua vita.

" Jina langu halihusiani na lolote," alitangaza.

"Mimi si chochote wala lolote. Mwanzo wangu ni kila kitu.Sitafuti kutangazwa kwa ajili ya nafsi yangu. Kwa vyovyote uhusikavyo, zaidi yako wewe pamoja na ulimwengu wote, jina litabakia **Msafiri wa Amani.**

Sasa upo mtindo wa kizamani kwenye mzunguko wa magazeti kwamba; majina ni habari. Kwa makusudi ukiamua kukataa jina lako lisiandikwe wakati unatafuta kutoa habari kwenye vyombo vya habari, unaifanya iwe ngumu, kusema kidogo. Mtafutaji wa habari atakuweka kwenye kundi moja na mtu anayetupeleka kwenye sahihisho la tano la sheria alipoulizwa lini na wapi alipozaliwa.

" Kama Yesu Kristo angeonyesha tabia kama hii yako ya kutokutaka kulitaja jina lake, ninaamini kamwe usingemsikia. Majina ni vielelezo vitusaidiavyo kumtambulisha mtu, vyanzo na mambo mengine mengi. Hivyo jitose, kama unataka nikufikirie, mimi ni shupavu unaona!"

Alitabasamu. Tabasamu lake halikuwa la kawaida. Lilikuwa na mvuto wa ajabu, tabasamu ling'aalo, lenye asili na lililo tulivu. Kwa msaada wa mguso wenye udhanifu ungeweza kuona mng'ao wa rangi nyeupe kama theluji kumzunguka ambayo ni ishara ya utakatifu.

" Siogopi." Alisema bila ya kutumia lugha ya majivuno bali kwa utaratibu na dhamira timilifu.

" Ninao ulinzi bora." Alimalizia. "Una maana kuwa unatembea na silaha kama alivyo Jane Muuaji?" Tulimuuliza kwa upole. " Hebu itoe tuione."

Tuliendelea kumdodosa.

" Mungu ndiye ngao yangu." Alijibu.

Usiku mmoja akiwa kwenye jangwa la Arizona alikuwa anatembea kwa miguu kueneza Amani kutoka Los Angeles kuelekea Pwani ya Bahari ya Atlantiki mwendo wenye umbali wa maili 5,000 ambazo ni sawasawa na kilometa elfu nane (8,000). Njiani aliona gari dogo likiwa limesimama kando ya barabara. Wakati huo hali ya hewa ilikuwa ni baridi sana. Mwanamume mmoja mwenye umbile la kutisha alikuwa peke yake ndani ya gari hilo, alimkaribisha Msafiri wa Amani aingie ndani ajikinge baridi. Alipoingia ndani, hali ilikuwa ya joto. Alikaa kwenye kiti na muda siyo mrefu alichukuliwa na usingizi mtulivu. Alipoamka, yule mwenyeji wake mwenye uso kama nyani naumbile la kutisha akiwa katika hali ya mshangao alimwambia Msafiri wa Amani ya kwamba, mwanamke huyo alikuwa na kitu kikubwa mwilini mwake ambacho hakukielewa. alijaribu mara mbili kumtenda mabaya bila mafanikio yoyote.

Aliendelea kueleza kwamba, wakati mwanamke huyo yumo usingizini, mwenyeji wake alipambana sana na dhamira ya kutaka kumdhuru lakini akashindwa kuitekeleza dhamira hiyo.

" Una kitu gani?" Yule bwana alimuuliza.

" Ni Mungu." Msafiri wa Amani alimjibu na baadaye alimuaga mwenyeji wake akaendelea na safari yake kuelekea Pwani ya Atlantiki. Bado tukiwa tumeshangaa kwa maelezo hayo, mawazo yetu ghafula yalituruidisha kwenye chimbuko la mpango wa shetani uliotokea kwenye bustani ya Edeni, miaka iliyopita.

" Hebu tuone mkono wako." Tulimuomba.

Alitoa mkono wake wa kuume bila ya kuonyesha hali yoyote ya kusita.

Ulikuwa mdogo lakini imara ambao haukuonyesha hali ya kuelekea kirahisi tulipojaribu kuushika na kuutomasa tomasa katika ule mtindo wa kizamani wa watu wahusianao kimapenzi.

" Unazo hisia za umeme mwilini mwako." Tulidanganya, wakati huo tukiongea kwa kauli ambayo aghalabu haishindwi kumlainisha mwanamke yeyote.

" Niambie, wewe ni Salome____ mrembo aliyecheza kwa ajili ya kutuzwa kichwa cha Yohana Mbatizaji na baada ya muda fulani akaungana na msafara wa

waumini waliomfuata Yesu wakati anakwenda kuwambwa msalabani? Ama wewe ndiwe Mariamu Magdalene?

Ujanja wetu wote wa kurusha kete za kumnasa, haukufua dafu. Kete tulizozirusha, kwake zilionekana usumbufu mtupu.

" Mimi ni Msafiri wa Amani;" alisisitiza.

" Hakika wewe ni mshawishi wa maovu ambayo yanawaangusha walio wanyonge wa roho na kuudidimiza ulimwengu." Tuliendelea kurusha kete tukitegemea kuamusha cheche za hasira ndani mwake.

" Wewe ni mmojawapo katika kundi la makahaba na tunaye mmoja wa aina yako hapa Newton." Tulimalizia.

Alitabasamu, hakikuwa kicheko, ilikuwa ni tabasamu iliyoonyesha meno zaidi ya kuonyesha wazo lililokuwa moyoni mwake.

" Nimekuwa jela kwa tuhuma za uzururaji, lakini mara kwa mara huachiwa mara wanielewapo ninafanya nini." Alisema.

Sasa ni lipi la kufanya kwa mtu kama huyu?

" Karibu sigara." Tulimkaribisha kwa kumnyooshea paketi nzuri iliyokuwa na sigara ndani mwake.

" Aina gani ya pombe uitakayo unywe? Taja tu na mara moja utapata." Tuliendelea kurusha kete.

Hakujibu; " *Toka nyuma yangu shetani.* " *Lugha waitumiayo walio wengi katika kumkemea shetani, na badala yake alisema;* " *Upo wema ndani mwenu. Laiti ningewaambia jina langu. Lakini haitakuwa vema kwa waandishi wengine pamoja na wale wa redio na televisheni walioko kati ya hapa na Los Angeles. Ninafikiri msingependa nifanye hivyo.*" Alimalizia.

" Ndiyo tulimjibu. Niambie jina lako la kwanza kwa kuanzia tu. Nitapata lingine baadaye. Umekwamisha msimamo wangu kama mwandishi wa habari. Kiurahisi hiyo haiwezekani."

"Lakini, unafahamu," alisita kwa muda na tena akatikisa kichwa alama ya kukataa.

"Haitakuwa vema kwa wengine." Na hivyo ndivyo ilivyokuwa.

Tungemwambia kusema kweli kwamba tusingehitaji atuambie jina lake ama majina yote ya ukoo wake. Kwamba sisi tulikuwa tunatumia silaha tuliyokuwa nayo mkononi kuona kama huyo tuliyezungumuza naye ndiye mwenye wokovu wa kiroho kweli ama ni mtu tu; mwenye maigizo ya kutenda vichekesho.

Tukiwa tunachunguza maandishi yake baada ya kuwa ameondoka, tuliyakuta yafuatayo.

" Mimi ni nani? "

Niiteni tu Msafiri wa Amani. Kwa kuifanya kazi hii ya hija ya amani, sijichukui mimi kama nafsi moja bali kama mjumuisho wa mioyo yote ya wanadamu ambao wanaililia amani."

Sasa, kaka pamoja na dada zangu, hayo ndiyo niliyoyapata.Ila mahali fulani siku moja imeandikwa kwamba mtu fulani wakati fulani alimkirimu Malaika bila kufahamu.

Na wala siyo nguo ya ndani ya malaika kama kijana mdogo alivyosoma.

Huenda ikawa tumewahi kupata mjumuiko wa pamoja na malaika. Ni nani ajuaye?

## KIFUNGU CHA MANENO KUTOKA MOJAWAPO YA HABARI NDANI YA GAZETI:

Kikundi kisingepata hamasa, uamsho, pamoja na starehe kama kwaya za Boston Symphony na Mormon Tabenacle zingetumbuiza badala ya yule mwanamke Msafiri wa Amani. Mtu angetegemea mwanamke huyu mkongwe ndani ya mavazi ya bluu na juu yake kisibau chenye maandishi yasomekayo: **Msafiri wa Amani kifuani na maandishi yaonyeshayo maili 25,000 alizotembea kwa mguu yakiwa mgongoni**-kuonekana katika hali ya namna hii bila ya kuwepo sababu yoyote?

Hakuna lolote ambalo lingekuwa zaidi ya ukweli. Majadiliano mengi ya mizaha yamejionyesha lakini hakuna upuuzi wowote ndani ya matendo ya mwanamke huyu asiyependa kulitaja jina lake, mahali alipozaliwa na wala tarehe ya kuzaliwa kwake kwa sababu alielewa kuwa taarifa za utambulisho hubeba uzito mkubwa kwa mtu zaidi ya kile akisemacho.

" ----- Alikwea jukwaa la kuzungumzia akionyesha ukakamavu kama wa kijana mwanamichezo. Mguu wake mmoja akiwa ameusimika wima sakafuni na mguu wa pili ameukunja kuelekea mbele kana kwamba yuko tayari kuyaanza mazoezi ya riadha, aliongea zaidi ya saa nzima, sauti yake imara isiyo na mikwaruzo iliyovuta usikivu wa watu wote kwa maneno yake rahisi na yenye maana kubwa."

(Na mwandishi wa Habari wa California).

" ----- Ndani ya maendeleo yote ya kitekinolojia na ufundi ----- wasi wasi wa vita ya nyuklia ----- nchi ya Marekani inaye angalau mtu mmoja ambaye anaona kwamba njia ambayo inafurahisha mawazo ya watu na kuridhisha tamaa ya ulimwengu haielekezi kwenye amani ya dhati. Ipo njia inayohitaji utakaso na kukana kila aina ya ubaya ambayo matokeo yake ni baraka zisizoweza kuelezeka. Amani inaweza kupatikana tu; kama upo utashi wa kuilipia gharama. Mwanamke huyu aongeapo ni kama vile sauti ya Ghandhi ndiyo iongeayo ndani mwake. Gharama ya Amani ni utii kwa sheria zilizo juu."

(Na mwandishi wa habari huko India).

" ----- Uangalizi wake pamoja na mwongozo wake hutoka kwa Kristo. Ni kama unamuona akiwa kando yake. Hakuna mwanamke awezaye kusafiri mwenyewe pasipokuwa na ulinzi mtakatifu. "

(Na mwandishi kutoka Pittsburg).

" Hakupata kitu bali mvuto, msaada pamoja na kutiwa moyo na watu aliokutana nao. Na ameshawishika kwamba mataifa kama vilewatu, wanaweza kuishi kiroho

katika hali timilifu itakiwayo na kwa njia hiyo Amani ya kweli ni rahisi sana kupatikana."

(Mhariri wa Gazeti la Religion Los Angeles Times).

" ---- Kwa baadhi ya wenzetu ambao nyakati zingine hufikiria kwamba ulimwengu unazama kwenye tamaa izushayo rushwa na ubadhilifu ---- ugeni wa mwanamke huyu, hapa ulimwenguni ni hatua kamili ya kukomesha mawazo haya yatiayo uchungu."

" ---- Ulimwengu ulizoea kuwa na watu kama vile manabii, mitume wenye mitindo mbali mbali na watabiri wa mambo mabaya yajayo, lakini Msafiri wa Amani ni tofauti na hawa kwa sababu maneno yake yenye mvuto ayatoayo kwa watu angalau yana maana kubwa."

" Mwingereza mmoja aliwahi kumwambia Gandhi maneno yafuatayo: Mheshimiwa wewe ni mpole mno, unatuchanganya sana. Uwapo mwema unatuachia tashwishi. ' Kwa heshima ningekiri kwamba usemi huu ungetolewa pia kwa mwanamke huyu mdogo, mkongwe muhimu sana ajulikanaye kwa jina la Msafiri wa Amani."

" ---- Mtu huyu asiye wa kawaida katika kueneza masuala ya amani ulimwenguni amezaliwa nchini Marekani, jambo ambalo sisi Wamarekani linatupatia baraka.

Taifa ambalo lina utamaduni pamoja na uchumi wa kivita. Taifa ambalo lilithubutu hata kuangusha bomu la Atomiki na limekuwa likitishia kuangusha bomu lingine la Haidrojeni. Taifa hilo sasa limezaa mwanamke mpweke, mkongwe ambaye maisha yake ya kutembea akiongea kila hatua aikanyagayo, kwamba ipo njia bora ya kuishi na kuyatatua masuala yote ya ugomvi----. Kwa kutumia ukakamavu wake wa kiroho kuliko mtu mwingine yeyote yule. Msafiri wa Amani aliutangaza ujumbe wake kwa ufasaha ukaeleweka kikamilifu kwa kila mtu. Alisali, akiombea hija yake na hatimaye akagundua kwamba hija hiyo hiyo ilikuwa ni sala kwa umuhimu wake. "

" Kukutana na mtu mtakatifu, inasemekana ni tukio la kila saa huko India pamoja na nchi nyingine za Mashariki. Lakini kukutana na mtu huko Marekani anayesafiri nchini bila senti hata moja mfukoni mwake, nchi ambayo fedha ni kitu cha kuabudiwa kama isivyokuwa katika nchi zingine ni jambo listaajabishalo! Na bado mtu wa aina hiyo anaendelea kutembea kwenye majimbo ya nchi akitoa mihadhara kuhusiana na Amani ya Ulimwengu. Mwanamke ajiitaye Msafiri wa Amani hana uoga wa kitu kiwacho chote. Ana mbabuko wa jua na anayo furaha kwa hali ya juu sana kuliko mtu yeyote tuliyewahi kukutana naye. Hakuna tajiri yeyote mwenye fedha nyingi aliyewahi kuwa na furaha pamoja na amani akilini mwake kama yeye."

" Msafiri wa Amani ---- alikuwa mwanamke mwenye wajibu uliopanuka , ukasambaa kuvuka upeo wa udhanifu wa mwandamu mwingine yeyote. Alikuwa ni msafiri kwa maana halisi ya neno. Alinigusa kwa njia ambayo mimi mwenyewe sikujifahamu. Alisimamakiutulivu mbele ya darasa la Chuo cha Waandishi wa habari Jijini Kansas, bila kufahamu kuwa alikuwa anachukuliwa picha na mpigaji picha wa gazeti la P.M. (Makala ya alasiri). Alipoanza mbinu zake za kuzungumza katika kutoa ujumbe wake, nilijengwa hisia za mashaka kama huyu mwanamke alikuwa kichaa; ama, alikuwa anajijengea utambulisho kwa ajili ya kitabu ambacho nilihisi alitaka kukiandika kuhusiana na safari zake. Lakini kadri alivyoendelea kuzungumza, jambo fulani lilinitokea. Alionyesha uungwana wa kipekee katika kuutoa ujumbe wake. Alimtazama kila mwanafunzi na akamfanya kila mmojawao ajione kuwa alikuwa akiongelewa yeye pekee.

Macho yake yalimgusa kila mmoja mle chumbani yakitangaza upendo na amani, vitu alivyokuwa anaviongelea-----.

Kulitokea hali ambayo haikutegemewa iwe kutokana na mwanamke huyo kuwa mle darasani. Kwani mafunzo ya Msafiri wa Amani pale chuoni ni jambo ambalo lingeonekana halina thamani kwa wale wote waliokuwepo. Chuo ni chambo kwa wafanya biashara wa Kimarekani na mabepari nyakati zijazo. Wengi wa wanafunzi kama siyo wote walikuwa pale chuoni kwa tumaini la kupata kazi nzuri mara baada ya kuhitimu; ikiwa pia na uhakika wa kujipatia pato kubwa. Lakini hapa mbele yao alikuwa kasimama mwanamke ambaye alikuwa tayari ameutupa utajiri wote wa ulimwengu hewani ili aishi maisha aliyoyaona bora. Kwa nini mtu aamue kufanya mambo kama haya? Jibu pekee nililolipata ni kwamba kwa kweli alitaka kuutimiza wajibu wake katika kuleta amani kwenye ulimwengu wenye matatizo. Alihisi kwamba amani kupatikana kwa ulimwengu wote ilibidi ianze kupatikana kwa .atu mmoja mmoja. Falsafa hii aliishikilia hadi kufa kwake.

Chumba cha darasa kikiwa kimejaa wanachuo, kilikaa kimya wakiwa wanamtazama kwa makini na kwa usikivu uliojaa mchanganyiko wa mawazo vichwani mwao kwamba, mtu kama huyu angewezaje kuishi, si ndani ya mazingira ya baridi tu nyakati za usiku, bali hata mwendo mugumu alioweza kutembea kwenye safari zake hadi mipakani mwa nchi ya Marekani. Hadi siku ya leo ni vigumu kuelewa ni vipi mwanamke huyo kikongwe angeweza kujitenga na vitu vya kumiliki vinavyokidhi tamaa ya ulimwengu wa sasa na badala yake asafiri kwa miguu akieleza upendo na amani. "

(Na mwandishi kutoka Kansas).

**MSAFIRI ATEMBELEA SANTA FE ANAUTEMBELEA ULIMWENGU HUU AKIWA PEKE YAKE LAKINI ANATEMBEA AKIWA NA WATAKATIFU:**

(Habari pamoja na picha vimetolewa na Richard Polese).

Anatembea mwenyewe katika nchi ya Marekani pamoja na kona zake zote akiwa ameubeba ujumbe wa kawaida wa amani, amani miongoni mwa watu na amani kwa mtu mmoja mmoja. Anatembea na kile ambacho anakimiliki maishani mwake, hapokei ufadhili wa kifedha na mara chache sana anakubali msaada wa kutembea kwa gari. Ataongea popote na wakati wowote akutanapo na mtu anayevutiwa na shughuli zake za hija. Amekuwa akitembea na kuongea kwa mtindohuu kwa zaidi ya miaka kumi na mitatu.

Juma lililopita Msafiri wa Amani alitembelea Santa Fe akaongea kwenye mkutano wa hadhara huko La Posada kwenye chuo cha Santa Fe na chuo cha Santa John.

Msafiri wa Amani ni jina lake pekee alilo nalo. Na ingawaje nywele zake zimebadilika kuwa na mvi kutokana na uzee na uso wake unaonekana kunyauka kwa maili nyingi alizotembea, bado anaongea kwa ufasaha akionyesha vitendo, akili zenye uangavu, pamoja na ukakamavu.

Uimara wa mwili wake unashangaza. Huvaa vazi la bluu lenye maandishi " **Msafiri wa Amani** " kifuani mwake na maandishi ya maili 25,000 kwa ajili ya amani yakiwa mgongoni mwake ingawaje lengo la maili 25,000 alilivuka miaka iliyopita na alikwishaacha kuhesabu maili wakati atembeapo.

Kwa nini aamue kuyaita matembezi yake " **Hija?** "

Hija huusisha mifano bora ya matendo pamoja na sala. hatuiiti " **Jihadi** " ambayo huusisha matumizi ya nguvu kisaikolojia.

Ni matokeo gani ambayo huyu mwanamke anayatumainia? " Hija yangu yaweza kuwafanya watu angalau wafikiri kujiuliza maswali. Matokeo hayo ninayaacha mikononi mwa Mungu. "

Kwenye mazungumzo ya hadhara, mwanamke huyu anaongelea mambo ambayo yanazuia kuwapo kwa amani, na namna mtu awezavyo kuipata Amani ya dhati ndani mwake pamoja na kutokana na hija yake.

Kwa nini kutokee vita duniani? " Tatizo halisi ni kuwapo kwa uchanga wa kiroho miongoni mwa watu. Kuwapo kwa ukuaji wa watu kiroho vita haiwezi kutokea. Na kamwe vita haitafikiriwa kama suluhu ya matatizo miongoni mwa wanadamu, kama upo ukomavu halisi wa kiroho."



***Mjadala wa kawaida**, Baada ya mazungumzo ya Msafiri wa Amani katika Chuo cha Mtakatifu John akiwa amezungukwa na wanafunzi kwenye ukumbi wa maakuli. Walipokuwa mle ukumbini alikubali kuyajibu maswali yao yaliyohusu vita, amani pamoja nashughuli zake za hija.*

*Msafiri wa Amani anasema kuwa mtu kupata Amani ya dhati ndanimwake lazima mabadiliko yafanyike katika nyendo za maisha yake.*

*Hii ina maana kwamba ni lazima mtu aishi kwa kuzingatia yaliyo mema niliyoyaamini mimi. " Ilinichukua muda mrefu wa maisha yangu kuenenda katika njia timilifu za imani nikafanikiwa. "*

*Rahisisha maisha yako. Upo uhuru mkubwa katika urahisi huo. Kumiliki vitu zaidi ya vile utakavyo kwa ajili ya matumizi ya kila siku ni mzigo mkubwa kwako. Vitu tunavyovimiliki hugeuka vikatumiliki sisi baada ya kubainika kwamba havihitajiki katika matumizi yetu ya kila siku.*

*" Yatakase mawazo yako, tamaa pamoja na matendo. Chuki humdhuru yule achukiaye na wala siyo mchukiwa. Uwe na tamaa ya kweli kwa jambo moja tu ambalo ni kuyafanya yale yaliyo ndani ya mapenzi ya Mungu kwa ajili yako."*

*" Endapo mambo hayo utaamua kuyaita mafunzo ya kidini yaliyo mazuri ama matendo bora ya kisaikolojia ni yale ambayo siyo mageni bali yanakubalika kwenye maumbile ya mbingu na nchi."*

***Amani pamoja na uhusiano mwema na wengine, yaweza kuwa kazi rahisi kwako. " Ufunguo ni kukabiliana kwa njia ya upendo na iliyo wazi kuliko kukabiliana kwa chuki na kwa kutokuaminiana. Hii ndiyo maana yangu nisemapo kukomaa kiroho."Anasema, " Watu ambao ni wachanga kiroho wana mpangilio wa mawazo yaliyo potofu kama vile mawazo ya vita ambayo kwao huona ndiyo suluhu ya mambo yote.***

***Mtu wa dini na bado siyo Mkristo ajihusishaye na dhehebu lolote litambuliwalo rasmi na serikali, Msafiri wa Amani yeye hutumia mapokeo ya kimya kama njia ya kukabili sala zake.***





***Muongeaji avutiaye, Msafiri wa Amani anatoa rufaa yake kwa ajili ya amani ya ulimwengu, na mwongozo wake wa mtu kupata amani ya dhati ndani mwake. Amevalia vazi lenye maandishi ambalo huonekana nalo daima matembezini. Matembezi yake yameendelea zaidi ya kumi na mitatu. Nywele zake za rangi ya kahawia zinatofautiana na hali yake ya mwili, hali iliyo imara sana. Kwenye picha anaonekana alipokuwa anaongea kwenye Chuo cha Mtakatifu John huko Santa Fe juma lililopita.***

***Mimi ni mtegemeaji wa yaliyo mema kwa sababu ninaamini kwamba sheria ile itawalayo mbingu na nchi hufanya kazi kwa yaliyo mema daima endapo tutakuwa tayari kuzitii. Uamuzi ni wetu. Ushuhuda wa mwanamke huyu katika tegemeo lake la mema ni matumaini yake kwamba kutatokea upunguzaji wa silaha ulimwenguni katika kipindi chote cha maisha yake.***

***Msafiri wa Amani aliusia kwamba kipindi kipya cha mwongozo wa maisha yake kiroho kilianza miaka ishirini na nane iliyopita pamoja na kipindi cha miaka kumi na mitano ya maandalizi ya kiroho na kisaikolojia kabla ya kuanza hija. Bila ya kupata msaada wa jumuiya ya aina yoyote, mtu yeyote aweza kuwasiliana naye kwa kutumia kituo cha Cologne New Jersey ambapo rafiki yake mmoja hufanya kazi ya kutuma barua zake mahali popote anapokuwa kwa muda huo.***

*SWALI:*

***Je, hija inakwisha lini?***

*JIBU:*

*Hija itamalizika wakati mataifa yote kama vile Marekani na Kanada ambapo bado kuna kutokukubaliana kiamani, watakapo kuwa wameacha kabisa kuota ndoto za kuuana.*

*Mpaka muda huo; Msafiri wa Amani ataendelea kutembea. alitembea hadi Albuquerque siku ya Jumamosi wakati akiwa hapa. Na anapanga kurejea Santa Fe 1970. Utamuona anatembea akiwa ndani ya vazi la bluu lenye maandishi kifuani na mgongoni akiwa barabarani mahali popote nchini. Tulimuona akitembea miaka michache iliyopita sehemu fulani usawa wa Magharibi mwa Marekani.*

**Silaha yake pekee ikiwa ni mswaki, chanuo na nguo zilizofunika mwili wake.**




Mwanamke huyu wa kushangaza ajiitaye Msafiri wa Amani amesafiri maili 30,000 ambazo ni sawa sawa na kilometa 48,000(Kati ya hizo 25,000 ni maili alizosafiri kwa mguu **ambazo ni sawa na kilometa 40,000**). Kuzungukia nchi za Marekani na Kanada tangu mwaka 1953 akiwa na ujumbe wake binafsi kueneza amani. Aliwaambia waandishi wa gazeti la **Family Weekly** haya yafuatayo: " **Nilikana nyumbani** kwetu, vitu vya kumiliki, umri pamoja na jina langu mwaka 1953 kwa sababu vitu hivyo niliona havina maana yoyote kwangu mimi. Amani ya dhati ndani mwangu niliyojikuta nayo inatosha kunifanya niishi. Kipindi fulani nilihisi

kama ninasikia sauti inaita kutoka nyikani, lakini sasa niko kwenye upande wa kutambulika na **Msafiri WA NYAKATI ZA SASA** kufahamika kwa sababu Wamarekani **ANAO UJUMBE**.walio wengi wamejitokeza kulikubali wazo la Amani." " Lakini maendeleo ya ulimwengu hayakubadili hija yangu. Amani ni bora zaidi ya kutokuwepo kwa muda kwa kile kiitwacho vita. Amani inaondoa vyanzo vya vita. Ninaamini itachukua miaka mingine kumi kwa amani ya nje kujijenga pamoja na kujidumisha lakini hata baada ya hapo nitaendelea kuzungumza kuhusu amani ya dhati ndani mwetu ambayo tunaihitaji ili kuiimarisha amani ya nje."


Anasema kwamba hija yake haifadhiliwi na kikundi chochote cha watu.

(Kutoka Gazeti la Family Weekly la 7 Desemba 1975).

## HIJA YA BINAFSI:

**(GAZETI LA TOPEKA CAPITAL JOURNAL-JUMAMOSI NOVEMBA 8, 1980)**

(Na Paul R. Jefferson, mwandishi wa gazeti la kidini la Capital).




***Barney Hubert, Topeka alisimama kwenye US-40 Mashariki mwa Topeka kuongea na Msafiri wa AmaniMara alipomuona anatembea.***

Kusikia Msafiri wa Amani sema kuwa, ni kutembea Marekani nzima kwa miaka karibu ya thelathini ili kulieneza neno la Mungu lenye imani ya kidini pamoja na imani ya binafsi ni mojawapo ya mambo ya asili ambayo mwanadamu aweza kuyafanya.

Akiwa amevalia vazi lake lenye maandishi kifuani akielezea safari yake ndefu ya kidini yenye visa vingi vya ajabu, mwnamke huyu alijitangaza na kutoa ujumbe wake wakati akiendelea na hija yake ya saba nchini Marekani alipopita Topeka juma hili.

" Ninakwenda kokote nialikwapo. "Msafiri wa Amani ambaye ndilo jina lake la kazi alisema. Alieleza kuhusu matembezi yake kwenye makanisa mbali mbali akiongea na waumini. Akiwa katika juma lake la kuishi pale Topeka, mama huyu mkongwe alihutubia madarasa ya Sosholojia na

Saikolojia kwenye Chuo Kikuu cha Washburn na akatoa nakala kadhaa za vitini zionyeshazo muundo na mbinu alizonazo katika ufumbuzi wa migongano ya kila aina kwenye jamii. Kanuni hiyo alishauri itumike kwa dhumuni la kufumbua tatizo la migongano na wala siyo kutafuta faida.

" Kila mtu anazaliwa kwa kusudi fulani," alisema. Na akaongeza kwamba hakujali alipofikiriwa na watu kuwa yale yote aliyokuwa anayafanya yalikuwa matendo ya mtu aliyerukwa na akili.

Ingawaje Msafiri wa Amani alikuwa mtu asiyetambulisha historia ya maisha yake, ujumbe wake ulichomoza mionzi ya mwanga kupitia kwenye macho yake wazi yenye rangi ya bluu.

" Ni lazima uishi kwa kutoa badala ya kupokea, " alisema, " ikiwa ni pamoja na kuinua vyanzo vya amani. Amani ya kweli ni zaidi ya kutokuwepo kwa vita. "

Alianza safari yake mnamo mwaka 1953, mwanamke huyu mwenye umri wa miaka sabini na moja, alitembea zaidi ya maili 25,000 maeneo ya kutoka Mashariki kwenda Magharibi, kutoka Kaskazini kwenda Kusini akiwa anakwenda na kurudi nyumbani kwake kwenye mji wa Cologne New Jersey. Zana zake pekee ambazo husafiri nazo zaidi ya nguo alizozivaa ni chanuo la nywele, mswaki na kalamu.

Msafiri wa Amani aliufafanua ujumbe wake kuwa ni mojawapo ya mambo yaliyo ndani ya sheria ya Mungu kama ielezwavyo ndani ya Biblia na ni mchanganyiko wa mawazo ya kibinadamu yaliyo mema pamoja na utajiri wa umuhimu wa mwanadamu.

" Watu wote ni muhimu, bali uamuzi ni wako wewe kama utaukamilisha ukuaji wa mwili na roho ili uweze kuupata umuhimu huo," alisema. Mwanamke huyo atembeaye katika hali nzuri aliongeza kwa kusema kuwa, msaada mwingine uwezao kumfikisha mtu katika kuitwa " Muhimu " ni kukomaa kiroho.

" Kadri mtu awazavyo moyoni mwake ndiye yeye." Alisema akiwa anahusisha vifungu kadhaa ndani ya Biblia ambavyo hujitokeza awapo katika mazungumzo yake na watu. Msafiri wa Amani ameuchukua ujumbe wake wa kueneza amani akautangaza mashuleni kama vile Harvard, Yale, pamoja na Vyuo Vikuu vya; Pennsylvania na California Berkeley na yuko njiani kwenda Dallas kutoa mihadhara kwa watawa wa madhehebu ya Kikatoliki.

" Safari yangu ya saba ya hija ya Amani itanichukua muda wa miaka sita kuyazunguka majimbo yote arobaini na manane nchini Marekani." Alisema akiongeza kwamba vituo vyake vyote vitakuwa sehemu zile alizopokea mialiko.

Baada ya kuwa ameubeba mzigo wa kuizunguka nchi ya Marekani kwa gharama zake mwenyewe, Msafiri wa Amani sasa hupokea fedha kidogo kwa ajili ya shughuli za magazeti, fedha ambazo hutoka kwa wafadhili wasiojitambulisha bali hajihusishi na shirika lolote, kikundi chochote cha watu, jumuiya yoyote ya kitaifa na kimataifa na wala muungano wa madhehebu yoyote ya kidini. Barua zote ziendazo kwake zina utambulisho wa anuani yake ya Clogne New Jersey Marekani.

" Inaonyesha kana kwamba nimeishi maisha ya aina tatu; " alisema akiwa anafafanua namna alivyoanza 'Jihadi' yake. Baada yakuishi katika kile alichokiita; " Maisha matupu yasiyo na fedha pamoja na vitu vya kumiliki," akiwa ni mwanamke mwenye umri mchanga, alisema, alianza maisha magumu ya kujinyima mwishoni

mwa mwaka 1930, alipoanza kufanya kazi miongoni mwa watu wazee akayafanya maisha yake kuhitaji chini ya yale mahitaji ya maisha ya kawaida. Aliishi kwa matumizi ya dola kumi kwa juma. Ilikuwa ni wakati huo alipojitangazia yafuatayo: " Nitaendelea kuzunguka huku na huko hadi mwanadamu atakapojifunza njia ya kuishi kwa Amani. Nitatembea hadi hapo nitakapopewa hifadhi na nitafunga kula hadi nitakapopewa chakula." Kamwe hachukui fedha zozote mfukoni mwake. "Siogopi chochote. Na muda wote ninategemea mema na hivyo mema hunijia."

**Gazeti la Honolulu Advertiser -Ijumaa ya Agosti 15,1980).**

**KULETA AMANI YA ULIMWENGU NI KUISHI.**

(Na Beverly Creamer Mhariri wa gazeti la Advertiser).




*Msafiri wa Amani: Hiki ndicho nikifanyacho kwenye miaka yangu ya uzeeni.*

Anaonyesha umbile lenye furaha muda wote--atazamavyo, nywele zake ndefu zilivyoangukia mgongoni, suti ya kibluu ya kutembelea, kila kitu ni zawadi kutoka kwa marafiki mbalimbali watokao maeneo tofauti hapa nchini. Ndani ya mfuko wake mpana ulioshonewa kwenye nguo alizovaa. Eneo la kuzungukia tumboni ametunza vifaa vyake vyote atumiavyo kwa mahitaji yake yote kama vile chanuo la plastiki, kalamu, karatasi za bluu, ambazo zimeandikwa ujumbe wake uelezao Amani ya ulimwengu na lundo la barua kutoka kwa rafiki zake mbali mbali walioko hapa nchini.

"Kwa kawaida mimi huvaa kila kitu kilicho changu hapa duniani." Alisema akiwa ameshika mfukoni mwake na kutoa barua alizokuwa amezitunza sehemu ya nyma ya mfuko. Nyakati za baridi usiku hujikunyata kando kando ya

barabara mahali popote na kulala usingizi. Anasema njia aipendeleayo kuitumia awapo kwenye hali hii ni kwamba; huchukua lundo la barua na kuzipanga mfukoni sehemu ile alaliayo ili zimkinge na baridi ya ardhi.

Kwa miaka ishirini na saba na nusu iliyopita, mwnamke huyu ajiitaye Msafiri wa Amani amekuwa akizungukia nchi ya Marekani na safari zake zilizo nyingi zimetumiwa kwa mguu, akiueneza ujumbewa amani. Kwa miaka kumi ya kwanza alihesabu umbali katika maili (aliotembea).

Husema kwamba; mnamo mwaka 1964 alikamilisha lengo la kutembea maili 25,000 kwa mguu. Hatimaye aliendelea kutembea bila kuhesabu umbali alioutembea na akawa ameelekeza zaidi shughuli zake kwenye mazungumzo ya Amani na watu maeneo ya vyuoni, vituo vya magari, makanisani na kadhalika.

Kwa miaka yote hiyo, hakuwa na fedha, hakukubali kupokea fedha zozote kutoka kwa mtu na wala hakununua kitu chochote tangu alipoingia kwenye shughuli za Hija ya Amani.

"Nilichunguzwa sana kwenye kipindi cha McCarthy kuona kama mimi nilikuwa mzururaji ama hujai wa kidini."

Niliruhusiwa kuendelelea.

Mimi ni mwanamke mfuata dini kwa ukamilifu, anasema Msafiri wa Amani. Mimi sihusihwi na kikundi chochote cha dhehebu la kidini.

Kwa muda wote huo hakuna yeyote ambaye amemdhuru? " Hakika hapana." Alijibu akiwa amefurahishwa na swali.

"Mimi ninaishi ndani ya imani timilifu."

Imani hiyo aliyonayo kamwe haijamuangusha, muda mrefu amabao amewahi kuishi bila ya kupata chakula kabisa ni siku tatu.

Hajawahi kuhitaji msaada wowowte wa mganga, ili kuuchunguza mwili wake, na hana mashaka yoyote ya kwamba ataugua na anasema hajawahi kuhisi maumivu yoyote ya mwili, yawe ya kichwa, mafua wala sehemu nyingine yoyote ya mwili wake kwa muda wote aliokuwa barabarani akiwa kwenye matembezi yake. Ingwaje amewahi kukumbwa na tufani ya barafu na hata mara kwa mara amekuwa akikesha kwa kulala sehemu wazi zilizo ndani ya kumbi za mikutano na mara moja kwenye kiti cha mbele cha injini ya moto huko Tombstone, Arizona.

Hatakuambia jina lake la asili na pia hatakuambia umri wake, pengine kiasi fulani umri huo ameusahau (Ingawaje anakiri kwamba anaweza akakumbuka endapo atafikiri vizuri, kitu ambacho hapendi). Na kwa kiasi fulani hapendi kuhusisha vitu kama vile tarehe yake ya kuzaliwa pamoja na vingine viwekwavyo rehani.

"Lakini anaelekea kuwa na umri wa miaka themanini," alisema rafiki yake mkubwa, Mchungaji William Kautz ambaye ni mchungaji wa United Church oc Christ hapa Honolulu.

Kwenye majira ya saa 3.30 Asubuhi ya Jumapili. Msafiri wa Amani ataongea kwenye kikundi cha mjadala kitakachokuwa kwenye kanisa la Crossroads barabara ya CHuo Kikuu nambari 1212.

Saa moja na robo baadaye ataongea kwenye kanisa la Good SHepherd Lutheran lililoko mtaa wa Kuakini 638N. Ataongea yale aongeayo popote, kule apitako, yale yahusuyo maisha mazuri yenye neema.

Je, yeye humpenda yeyote anayekutana naye?

Swali hilo linamfanya aonyeshe furaha ambayo huandamana na jibu la, ***"hakika ndivyo!"*** Anajibu; "Kwa nini nishindwe kumpenda kila mtu?" "Ndani ya kila mtu ipo cheche ya Umungu. Watu wananiona kama mwanga ung'aao----."

Msafiri wa Amani anasema ameona maendeleo kuhusiana na amani kwenye kipindi cha miongo mitatu alichotumia kuzungukia nchi ya Marekani. Kazi ya Msafiri ni kuziamsha ari za watu waachane na ile hali ya kukata tamaa na badala yake wafikiri yahusuyo wokovu waowa kiroho. Nywele zake zenye rangi ya ukahawia kisogoni zinacheza huku na huko kadri aongeavyo. Huwa anazinyoa mwenyewe. Na huzitunza vizuri.

Anasema, "Kulikuwapo na hali ya kukata tamaa wakati nilipoanza safari yangu ya hija. Wakati huo nchi ilikuwa kwenye kilele cha vita ya Korea pamoja na kipindi cha McCarthy----.

Ulikuwa ni muda mzuri wa hija, kuanza----.

Mwanzoni watu walifikiri vita ni sehemu muhimu katika maisha yao. Hawakuona njia nyingine ya kuyakabili matatizo yao zaidi ya vita.

Na sasa wanaamini kuwa zipo njia bora zaidi za kukabili matatizo na ndizo wazitafutazo sasa.

"Nilipoanza," aliendelea, "hakukuwepo na mvuto wa watu katika kuitafuta amani ya dhati ndani mwao. Ninaendelea kuwahamasisha watu wafikiri na kujiona kuwa wao ni muhimu na waishi kwa kutegemea umuhimu wao huo."

Msafiri anasema, ilimchukua miaka kumi na mitano kuchukua hatua ya kwanza iliyomfikisha kwenye ugunduzi uliomuelekeza kuachana na kila kitu abakie anazunguka kutoka sehemu hadi sehemu. Anasema, alipata mafanikio kifedha, aliishi Los Angeles kwenye jengo zuri sana akiwa na mavazi mazuri. Lakini mnamo miaka arobaini na miwili na nusu iliyopita; maisha yake yalianza kuonekana matupu, na urafiki wake ulianza kuwa wa hivi hivitu, na hapo akagundua kwamba lipo jambo ambalo alitakiwa kulifanya kuhusiana na maisha yake.

"Sikuanza ziara yangu ya hija hadi hapo nilipoipata Amani ya dhati ndani mwangu."

Aongeapo, mikono yake iliyoathiriwa na hali ya mazingira anamotembelea hunyanyuliwa juu, vidole vyake vikinyooshwa juu angani, macho yake makubwa yenye rangi ya bluu huyazungusha juu kwenye dari ya nyumba na kuyateremsha tena chini. "Ilikuwa wakati huo," anasema, alipoingizwa kwenye uhusiano na vyanzo vya nguvu za mbingu na nchi,-----mgawo wa mbingu na nchi.

Ahitajipo mavazi mapya hujitokeza mtu yeyote akampa. Ahitajipo chakula hupewa kwa urahisi.

Msafiri hawaonyeshi watu wamsikilizao maneno ya ushawishi yasiyo na maana kwao na wala hatoi maelezo yake kwa njia ya mafunzo ya vitabu, badala yake ujumbe autoao ni wa kawaida na upo kwenye karatasi zake za bluu anazotembea nazo zikiwa tayari kugawiwa kwa watu, zikieleza utambulisho wake. Na upande wa

pili wa karatasi zake unaonyesha kanuni yenye nguvu za ajabu ya Msafiri wa Amani. Ipo kanuni ya ajabu katika kukomesha migongano ya kivita. Inasomeka nayo ni hii; "Ifanye kama lengo lako katika kukomesha migongano ya kivita na wala siyo utafutaji wa faida----." Na, "Jiepushe na kutenda lile liwezalo kumdhuru ama kumkosesha raha mwenzio; ilivyo kwamba, **usivyotaka kudhuriwa ama kukoseshwa raha kwa namna iwayo yote.**

Yote haya hayamaanishi kwamba Msafiri hana matatizo. Ilivyo ni kwamba kwake matatizo anayatazama kama hatua bora za kumkuza mtu kiroho.

Mmoja angesema maisha ambayo si ya imani kwa dhehebu lolote yangeweza kumkomaza kiroho haraka kadri iwezekanavyo.

Fikiria hili kwamba safari yake ya pili huko Hawaii, aliongoza ujumbe wa kujitegemea wa watu kumi na watano ili uweze kujifunza kutokana na safari zake. Mashirika ya ndege huwa hayapendelei ziara za aina hii, lakini yanaruhusiwa chini ya sheria za utawala wa shirikisho la safari za anga, jambo limuwezeshalo Msafiri wa Amani kupewa tiketi ya bure kwenda

Hawaii akiwa kiongozi wa msafara. Anasema; "Mwanzoni walijaribu kuniambia kwamba nimuone wakala wa safari za ndege," alisema akiwa anatabasamu.

"Sawa," aliwaambia siwezi kufanya hivyo kwa sababu mimi ni mtangatangaji, "Msafiri."

**"Wewe ni nani?"** Wakala aliniuliza. Msafiri alitabasamu wakati akiongea hayo. Hatimaye nilisema; "unifikirie kama mhubiri asafiriye." Wangeweza kuhusisha hivyo.

Kikundi kidogo cha Msafiri wa Amani kilitumia muda wa majuma mawili huko visiwani Hawaii wakiwa wanalala ufukoni mwa bahari na kwenye vituo vya magari wakipikia kwenye kambi za moto. Aliendesha ziara kama aendeshavyo maisha yake.

Msafiri ataondoka Jumatatu kwa ndege kurudi Los Angeles, baadaye atakwenda Bismarck huko Dakota ya kaskazini kwa tiketi ya ndege iliyotolewa zawadi kwake ili kuanza safari yake nyingine ya Hija. Safari yake ni ya kuzunguka na kupinda pinda hadi kaskazini mwa nchi na kurudi akijaribu kupitia Cologne New JErsey kila mara ili kumuona rafiki yake ambaye hutuma barua zake mahali anapokuwa. (Anuani yake ni Msafiri wa Amani Colognbe New Jersey 08213).

Mara kwa mara hupata barua kutoka kwa watu ambao husema maneno kama; "Tangu tuongee na wewe nafikiri nitafanya kadri niwezavyo na mimi nieneze Amani.."

Wanaandika kueleza watakavyoeneza Amani kijumuiya ama watakavyoeneza Amani miongoni mwa marafiki zao----. Yote hayo yanaogeza mafanikio, husema.

Msafiri huwasiliana mara kwa mara na watu 10,000 ambao amewahi kukutana nao, akiwatumia magazeti yake ambayo hayachapishwi; mara kwa mara akiwajulisha nyakati atakazo watembelea. Katika hali isiyobadilika ameelemewa na mialiko mingi ya watu mbali mbali wamtakao afike kulala kwao.

"Kama huhofu chochote, na daima unategemea yaliyo mema, basi, mema hutokea." Aliyasema hayo akiwa anakwenda nje ya ukumbi kuchukuliwa picha.

Alilala chali kwenye nyasi, kichwa chake kikiviegemea viganja vya mikono yake katika ule mtindo wa usingizi wa usiku wa joto, chini ya mwanga wa nyota.

Halafu akajikunyata kwa mbele akiwa amelala ubavu, mikono yake imekunjwa kwa kupishana, viganja vya mikono yake vimegusa kwapani kuonyesha jinsi alalavyo usingizi kwenye mazingira ya hali ya baridi nyakati za usiku.

Aliongezea akifafanua kwamba; "Mguu mmoja waweza kuhisi baridi zaidi kama sitakuwa nimeuweka vizuri ipasavyo."

Tayari mara moja husimama juu na kupeana mikono na watu. "Fedha," husema; "fedha sipokei." Ninaishi kwa kuutegemea ukweli wa kiroho ambao kamwe hautauzwa na wala kununuliwa. Wakati wowoteuwapo tayari utaupata.

Je, anategemea na wengine wafanye yale ambayo ameyafanya? "Oh, hapana." Anasema. "Hali hii kamwe haijamhamasisha yeyote kufanya matembezi ya Hija."

**Msafiri athibitisha: *Ukomavu wa kiroho huwaongoza watu kwenye amani ya kweli.***

(Na John Fetler Mhariri wa mambo ya kidini Gazeti la Colorado Springs Telegraph la Aprili 28,1979).

Anakiri kwamba lipo jambo kati yake na Mtakatifu Fransisco katika Jihadi yake ya kueneza amani.

Mahali popote aongeleapo, pawe Chuo Kikuu ama kwenye Chuo chochote, Makanisani, mashuleni, au mitaani anaonyesha hali inayowadhihirishia watu kwamba anao " mwanga wa kiroho ndani mwake " jambo ambalo hata vijana wanaonyesha kuvutiwa naye. Baadhi yao wamemuomba wawe mitume(wanafunzi) wake.

Jambo la kuangalia ni kwamba, kwenye kipindi hiki kilicho jaa udanganyifu, hila za kutafuta fedha na maslahi, hakuna mtu amuwaziaye mwanamke huyu tabia ya hila ama ujanja wenye hali ya udanganyifu kwa visingizio vya ujuzi fulani.



MSAFIRI WA AMANI

Hata angalau kumuona kama kichekesho tu. Badala yake mwanamke huyo mkongwe, mwenye macho maangavu ya rangi ya bluu na ambayo huashiria mkazo wa kile akiongeacho, anachukuliwa kama alivyo kwa jina la " Msafiri wa Amani." Alikuwa Colorado kwa juma moja. Aliongea kwenye mikutano kumi na miwili, kwa watu waliokutana katika mikutano hiyo, idadi yao ilikuwa kati ya watu watano na mia tano kwa kila mkutano. Baadaye mapema juma hili, aliondoka kwenda Denver kuendelea na Jihadi yake ya upweke. Hii ni hija yake ya saba, ikiwa

ni safari yake ya saba nchini Marekani Kabla ya kutoka mjini hapa aliongea na waandishi wa habari.

Hataki kulitaja jina lake halisi ama muda wa miaka aliyoishi hapa ulimwenguni. Lakini aonekanavyo ni mtu mchanga asiye na umri mkubwa. Matendo yake anapoongea huweka msukumo wenye kuthibitisha ule ukweli ausemao, macho yake yakiwa yanaonyesha uangavu utawaliwao na uchangamfu. Kuna uimara fulani machoni mwake nakwenye sauti yake wakati aongeapo. Anakiri kuwa yeye anazo nguvu za ajabu zitokanazo na amani ya dhati iliyo ndani mwake.

Alipoulizwa: Je, hali ya amani ulimwenguni siyo kwamba inaendelea kuchafuka hivi sasa? Alijibu kwa mshangao; " Oh, la hasha! "

Jaribu kukumbuka miaka michache iliyopita kuhusiana na hali ilivyokuwa wakati wa vita ya Korea. Nyakati hizo vita ilikuwa ni njia pekee iliyokubaliwa na jamii kuwa ni msuluhishi wa migongano ya kimataifa. Tazama hali ya sasa. Nyakati hizi kila mtu anaongelea umuhimu wa kuwapo Amani. Hivi sasa haikubaliki tena. Upevu wa yale ayazungumzayo ulionekana wazi wazi machoni mwake.

Hata kwa mtu mwenye mashaka kabisa kuhusiana na matendo yake angesema, " Kama sitakubaliana naye juu ya tumaini la yale yajayo lakini ninakiri kwamba kwenye mazungumzo yake yamo mambo yenye ukweli."

Anamfafanua mwanadamu aliye wa kweli kwamba ni yule " aongozwaye na mapenzi ya Mungu, kwa maana hii imani yake ni imara kama jabali."

Anaendelea kusema kwamba hakunyanyuliwa kiroho kutoka miongoni mwa dhehebu lolote la kidini. Hii inamrahisishia kuwazungukia watu wa madhehebu yote bila kipingamizi chochote. Utaratibu wake ni kuhudhuria ibada saba kwa kila siku ya Jumapili.

Kwa kawaida yeye huongea yale ayazungumzayo kila siku. Lakini tabia ya kuzingatia mwenendo wa kidini humjengea fikra bora. Ni imani yake imara inayomuongoza kusema kwamba ili mtu aweze kumpata Mungu, hana budi kwanza aupate mwelekeo wa kidini, halikadhalika atawapata na wanadamu wenzake bila kusahau pia nafsi yake.

Anapoulizwa kwa nini matendo mabaya yamejaa duniani, hujibu kwa kusema kwamba, hii ni kwa sababu ya watu kutokukomaa kiroho. Hili siyo jibu la kidini tu, hata wale wataalam wa masuala ya saikolojia wanasema hivyo.

Vipi mtu mmoja kwa unafsi wake awezavyo kuleta amani ya ulimwengu? Anajibu kwamba ni kutokana na mtu huyo apatapo amani ya dhati ndani mwake. Anaendelea kueleza kwamba, kila mmoja wetu anao utashi wake awezao kuutumia hadi akakomaa kiroho.

" Mimi mwenyewe ni lazima nitambue kwamba ninao wajibu mtimilifu kuhusiana na maisha yangu. Hakuna njia nyingine." Hakuna njia nyingine. "

Na hii ndiyo sababu hakubali kufuatana na mitume (wanafunzi).

" Ni Mungu pekee achukuaye Mitume; anasema. Siyo vema kumfuata nyuma mwanadamu mwenzako kwa yale ayatendayo. Hii ni alama ya kutokukomaa kiroho. Bali hilo ni jambo lichukualo muda. Mimi hali hiyo ilinichukua miaka kumi na mitano kuupata ukomavu wa kiroho. Lakini ni bora pia tuelewe kwamba kipindi cha mtu kukua kiroho kinategemea na mtu mwenyewe alivyo tayari. Muda wwaweza

kuwa mrefu ama mfupi kwa mtu, hivyo tuamini kwamba vipindi vya watu kukomaa kiroho vinatofautiana."

" Oh," anaongezea (atanikapo neno hili humtoka kwa furaha kubwa katika hali ionyeshayo kuwa linaupeuya moyo wake kwa hali isiyokuwa ya kawaida).

" Ninajaribu kuwahamasisha watu watafute kile kiitwacho kusudiola maisha yao duniani. Hakuna watu wawili wafananao. Kwa hiyo hakuna watu wawili walio na wajibu mmoja. Kila mtu lazima atafute nini wajibu wake wa maisha hapa ulimwenguni. Hivyo wajibu huo aupatapo utamfanya ashughulike kwa ukamilifu na kwa furaha kubwa."

Anasema kuwa baadhi ya watu wamemshawishi aanzishe jumuiya yake mwenyewe itakayoshughulikia masuala ya amani ya ulimwengu lakini amekataa. " Ninaongea na watu wengi vyuoni, kwenye vyuo Vikuu, mashuleni, makanisani." Anasema. " Hakuna haja ya kuunda jumuiya nyingine ya amani." Lakini anaamini kwamba taasisi mbalimbali ndiyo maeneo muhimu yatakayokuza amani ulimwenguni.

Alieleza kuwa; " Wakati wengi wetu tutakapokuwa tumekomaa kiroho tukaweza kuieneza amani kwenye taasisi zilizopo, mambo mengi yatabadilishwa haraka sana kwa njia ya amani."

" Ninampokea kila mwanadamu ninayekutana naye," anaongea kwa uchangamfu uonyeshao urahisi wa mwenendo wake. Ninaamini kwamba wanadamu wote hupenda kufanya yaliyo mazuri, lakini kwa kawaida hawajui ni yapi mazuri yatakiwayo wayafanye."

" Kama ni lawama ama chuki," anasema; " Simdhuru yeyote, labda mimi nijidhuru kutokana na upotofu wa matendo yangu."

Kwa nyongeza, yeye hupokea barua zake kutoka kwa wale wamuandikiao walioko kote nchini. Anuani ya Msafiri wa Amani ni: **" Msafiri wa Amani, Cologne, New Jersey 08213."**

" Cologne ni mji mdogo ushughulikao na mambo ya kilimo, alieleza, " Rafiki yangu mmoja alikubali kufanya kazi ya posta ya kuwa anachukua barua nitumiwazo na kuzisambaza mahali ninapokuwa kwenye safari zangu za hija."

Mradi wake huu wa kutembea maili 25,000 kwa ajili ya amani ulikamilishwa mwaka 1964 lakini ameendelea kutembea akieneza amani kama alivyokuwa hapo mwanzo na utambulisho wake umeandikwa kifuani mwa vazi lake.

Kama alivyokuwa Mtakatifu Francis, Msafiri wa Amani hajihusishi na vitu vya aina yoyote viwezavyo kumilikiwa. Daima husaidiwa mahitaji ya kawaida na rafiki zake aliowapata kwenye mizunguko yake ya matembezi ya hija.

Ila hakubali kuupokea ufadhili wa fedha zozote kutoka kwa watu.

Mwanzoni alikuwa Msafiri aliyekuwa anatembea peke yake. Hivi sasa umuonapo barabarani hakosi kuwa na watu. Kuanzia mwaka 1984 atakuwa amepangiwa vituo vyote ambapo atakuwa anasimama na kuongea na watu.

Matukio ya hija yake yanafanyiwa uratibu na Chuo cha Swarthmore.

## MAHOJIANO NA MSAFIRI WA AMANI TAREHE 6 JULAI 1981:

*(Mahojiano haya yaliendeshwa na Ted Hayes Meneja wa Kituo cha Redio WKVI kule Knox Indiana siku moja kabla ya kifo cha Msafiri wa Amani).*

**Ted Hayes:**

Amani (akiwa na maana ya jina la Msafiri wa Amani): Hebu tuongee kidogo kuhusu haya ambayo umeyafanya kwa ajili yaamani. Ulianzaje?

**Msafiri wa Amani:**

Ndiyo, matembezi yangu yalianza Januari Mosi, 1953 kwa kuanzia Los Angeles California. Mwaka huo niliondoka nikatembea kuzunguka nchi, jambo ambalo nililifanya. Nilizunguka zunguka mfululizo wa maili elfu tano. Na baadaye niliendelea. Sasa niko kwenye safari yangu ya saba ambayo ni hija yangu ya saba kuizunguka nchi. Nimezungukia majimbo hamsini, majimbo kumi nchini Kanada na sehemu za Meksiko. Ni juhudi ya kufanya kila kitu ambacho mtu mdogo aweza kukifanya ili kuieneza amani. Ninatembea nikisali, na kama njia iniwezeshayo kuongea na watu wengi na labda kuwahamasisha wafanye jambo liwezalo kuleta amani kwa kutumia njia zao wazijuazo.

**Ted Hayes:**

Amani, ni nini kilichokutuma uje hapa Knox kwa hakika?

**Msafiri wa Amani:**

Nilipata mwaliko wa rafiki yangu Gertrude Ward. Nilikutana naye sehemu fulani. Na hii ndiyo mara yangu ya kwanza kutembelea Knox. Na hakika ninafanya hivi muda wote.

Ni sehemu ya hija yangu kwa kila mara kueneza amani. Sina fedha. Na sikubali kupokea fedha zozote kutoka kwa mtu. Sihusiani na jumuiya yoyote. Hivyo, sina jumuiya inipatiayo msaada. Mali yangu niliyo nayo ni kile nilichobeba na nilichokivaa mwilini mwangu. Ninatembea hadi hapo ninapopewa hifadhi ya mapumziko. Ninafunga kula hadi nipewapo chakula. Siombi hivyo vitu kwa mtu. Ninapewa bila kuomba. Ninakwambia, watu wote ni wema. Ipo chembe ya wema ndani ya kila mtu bila kujali chembe hiyo imezama kiasi gani ndani mwake.

Mwanzoni ilikuwa kwamba, mialiko niliyopewa na watu, ilikuwa ni ya muda mfupi lakini baadaye nilianza kupewa malazi karibu robo tatu ya muda wote. Na ilikuwa nadra sana kupata zaidi ya milo mitatu ama minne kwa siku, lakini sasa mialiko yangu inaletwa mapema kabla ya mimi kufika kule itokeako. Na hivi ndivyo ilivyokuwa kwenye mwaliko wangu wa kuja hapa Knox.

**Ted Hayes:**

Amani; hebu nikuulize lifuatalo: Muda wote uliitwa Msafiri wa Amani ama ulikuwa na jina lingine ulipokuwa msichana mdogo?

**Msafiri wa Amani:**

Oh, hilo siyo jina langu la zamani, na kama utaandika barua kwa anuani ya jina langu la zamani sitaipokea. Mimi sasa ni Msafiri wa Amani hasa. Ninaambiwa kwamba hilo ni jina langu la kazi, liendalo na shughuli niifanyayo. Hilo sasa limekuwa ni jina langu halali kwa muda wote wa miaka kumi ama kumi namiwili kwa sababu limetambuliwa tokea mwaka 1953 nilipoanza hija yangu.

Mambo yamebadilika sana tangu wakati huo. Lakini nitasema kwamba jambo moja halijabadilika, nalo ni ule ujumbe wangu wa amani. Bado yafuatayo yanaendelea kuudumisha ujumbe huo nayo ni: ***Shinda ubaya kwa kufanya yaliyo mema na uongo kwa ukweli na kuyatenda yaliyo ya upendo palipo na chuki***. Na huu ndio ujumbe ambao bado nimeubeba kuutangaza kwa watu. Na bado hatujajifunza kuutumia. Na ufunguo wa nyakati zote hizi za sasa ni kuuchukua ujumbe huu tukauweka kwenye vitendo. Siyo kwamba tunahitaji mwanga zaidi wa kiroho bali kwanza tuutumie mwanga ule ambao tumekwisha kuupata tuuweke katika vitendo. Tukisha yafanya haya, maajabu yatatokea ndani ya maisha yetu na katika ulimwengu kwa ujumla.

**Ted Hayes:**

Msafiri wa Amani, unajua kwamba ipo idadi ya watu ambao wala hawawezi kufikiria kuyafanya haya uyatendayo, na hata wanakufikiria kuwa mtu aliyerukwa na akili ama mpumbavu. Je, hupati matatizo yoyote mara ukutanapo na watu wa aina hii?

**Msafiri wa Amani:**

Ninaamini kuwa wale ambao wamewahi kunisikia lazima wanifikirie kuwa niyatendayo yako nje ya matendo ya kawaida ya mwanadamu. Hata hivyo, niyatendayo yako tofauti na yale waliyoyazoea. Na kwa kawaida mtu yeyote aanzishaye jambo fulani jipya kwa watu lazima kwa kiasi fulani aonekane tofauti kwa watu. Lakini mimi ninawapenda watu na ninauona uzuri ndani mwao. Hivyo mtu huna budi kukifikia kile ukionacho. Ulimwengu ni kama kioo, ukikichekea nacho kinacheka. Mimi hupenda kutabasamu na kwa ujumla mimi hupokea tabasamu za watu za aina hiyo hiyo kutoka kwa watu. Nimekuwa nikipewa kila kitu nilichokitaka kwenye hija yangu bila kumuomba mtu yeyote.

**Ted Hayes:**

Unaitembea nchi yetu hii bila hata senti moja mfukoni. Unatembea kwa imani pekee ukiamini kwamba huko mbele utakutana na mtu akupe msaada na hivyo ndivyo iwavyo. Ni lazima uwe na hisia kwamba ni yupi uwasiliane naye, yupi umchekee ama ni yupi awe mwema kwako au siyo?

**Msafiri wa Amani:**

Mimi humchangamkia yeyote. Simfuati mtu. Vazi langu nililolivaa linayo maandishi kifuani yasomekayo; " **Msafiri wa Amani**". Na maandishi mengine

mgongoni yasomekayo " **Maili 25,00 kwa mguu kuieneza amani."** Hivyo watu wanionapo husimama na kuongea nami na wengi wao ndivyo wafanyavyo. Maandishi hayo huniunganisha na watu kwa njia ya wema. Na wale wanifuatao ni wale wenye nia njema ya kuongea nami. Wanaweza kuwa wamevutiwa na wazo la amani au wana hamu ya kujifunza jambo kutoka kwangu. Unaona? Lipo jambo kubwalivutialo kuhusiana na amani hivi sasa. Wakati nilipoanza matembezi yangu ya hija, watu walikuwa wanaamini kwamba vita ni kitu muhimu sana maishani mwao. Na sasa ilivyo, tunatafuta njia nyingine ya suluhu kuliko vita. Hakika huo ni ushindi! Ni bora kuliko ilivyokuwa hapo awali. Nilipozianza shughuli zangu za hija kulikuwapo na wito mdogo sana wa kutafuta mwanga wa kiroho miongoni mwa watu. Sasa hivi wale wautafutao mwanga wa kiroho idadi ni kubwa sana. Hali hii kwangu ni ushindi mkubwa. Na tangu nianze kuongelea amani ya dhati ndani mwetu kuwa ni hatua kuelekea amani ya ulimwengu, watu wanaendelea kuvutiwa zaidi na hilo wazo langu.

**Ted Hayes:**

Amani; Biblia inatuambia kwamba, vita daima itaendelea kuwa pamoja nasi. Je, unasemaje kuhusiana na watu wayasemayo haya? Je, unafikiri kwamba juhudi zako hizi ndogo zitaleta mabadiliko?

**Msafiri wa Amani:**

Inasemwa kwamba: " Kutakuwepo vita na uvumi wa maneno ya vita." Lakini unabii huo 'umeelezwa kwa karne nyingi sasa. Sioni ni kwa nini tuendelee kuusikiliza unabii wa kitu kama hicho ambacho muda wake umepita. Pia unabii unasema kuwa " Watayagonga mapanga yao yawe majembe ya kulimia na mikuki yao yawe majembe ya kulimia magugu shambani. Taifa halitanyanyua upanga juu ya taifa lingine na kamwe hawatapigana tena." Na labda wakati huo umefika wa kuutimiza huo unabii. Ninaamini hivyo.

Ninafikiri hali hii ndiyo tunayoihitaji sisi sote. Na bado kuna wale ambao mawazo yao yanawatuma kuamini kwamba bila vita hakuna ufumbuzi wa migongano ya ulimwengu. Niliongea na mwanamke mmoja aliyesema kuwa; " Ninasali na wewe kwa kuomba amani, lakini siamini kuwa amani hiyo itapatikana." Na mimi nilimuuliza; " Huamini kwamba kuwapo kwa amani ni mapenzi ya Mungu? "

" Ninakubaliana na wewe." Alinijibu.

" Sasa ni kwa nini uniambie kwamba lile ambalo limo ndani ya mapenzi ya Mungu haliwezekani ukiliomba? " Niliendelea kumhoji.

Hivyo, niliendelea kumueleza; hilo si kwamba linawezekana tu, bali sema lipo hakika.

Kupatikana kwake mapema kunatutegemea sisi ni wakati gani tuamue.

Sasa ninaamini kwamba juhudi njema huzaa matunda mema, hivyo mimi ninaendelea kuweka juhudi njema kadri niwezavyo. majibu yatakayotokea ninayaacha mikononi mwa Mungu. Na majibu hayo yanaweza yasijitokeze wakati wa maisha yangu lakini upo wakati yatajitokeza.

**Ted Hayes:**

Amani: Si kawaida; kwa hali ya ubinadamu kukutana na mtu na hapo hapo ukamwuliza umri wake. Lakini mimi nitajaribu leo. Ninaomba nikuulize umri wako.

**Msafiri wa Amani:**

Niwezalo kukujibu ni kwamba; siujui umri wangu. Na hili ni kusudi langu. Tunatekeleza mambo yetu kutokana na namna tuwazavyo ikiwa ni pamoja na kuuzingatia umri. Nilifikisha umri wa kutosha nilipoianza safari yangu ya hija; Januari Mosi 1953 na hapo nilisema " hiyo imetosha." Tangu hapo hadi hivi leo nilijifikiria kuwa mtu asiye na umri na ambaye nina afya bora na hivyo ndivyo nilivyo. Mimi siyo mchanga kiumri, lakini sioni sababu ya kuwa mtu mchanga. Ninaweza kuendelea na shughuli zangu katika hali nzuri na imara bila kusumbuliwa na maumbile ya umri. Na kama nimewahi kujifunza vipindi vya maisha ya watu kabla, wewe huhitaji kurudi katika maisha ya kuhesabu vipindi vya maisha.

**Ted Hayes:**

Msafiri wa Amani amekuwa mgeni wangu leo. Kwenye fasihi yake anasema: " Msafiri wa Amani yuko mgongoni mwangu maili 25,000 kwa mguu akieneza Amani." Na amekwisha maliza kutembea umbali huo, lakini anabaki na kauli ya; " Nitabakia mzungukaji hadi hapo mwanadamu atakapokuwa amejifunza njia ya kuishi kwa amani. Nitatembea hadi nipewe chakula." Anaonekana kuwa mwanamke mwenye furaha ya aina yake.

**Msafiri wa Amani:**

Hakika, mimi ni mtu mwenye furaha. Ni nani amfahamuye Mungu na bado asiwe na furaha? Ninapenda kuwatakieni amani ninyi nyote.

NYONGEZA YA VI

## BARUA KWA MSAFIRI WA AMANI:

*Vifuatavyo ni vipande vya barua zilizoandikwa kwa Msafiri wa Amani, nyingi wakati akielekea mwisho wa safari yake ya hija. Ingawaje alipeleka habari za barua hizo kwenye Chuo cha Swarthmore ili ziwekwe kwenye maktaba ya Chuo hicho cha Swarthmore iliyohusiana na mambo ya amani na ambapo taarifa mbali mbali zilizomhusu zilikusanywa, Msafiri wa Amani aliendelea kufuata kauli yake rahisi na akawa anatupa barua zake nyingi alizotumiwa mara baada ya kuwa amezijibu.*

Rafiki:
Je, umenifanyia nini! Yote niliyoyafanya ilikuwa ni kumwuliza mwanamke mzuri kama alipenda kusaidiwa katika matembezi kwa gari, na niliishia kwenye ulimwengu mzima mpya na wa ajabu mbele yangu. Kila siku sasa maisha yangu yanabadilika kasi. Kiurahisi mimi si mwanamume mwenye hali sawa na ilivyokuwa mwezi mmoja uliopita, juma moja lililopita; haidhuru niseme hata jana. Ninaendelea kupata maana mpya katika mjadala wetu.

Rafiki:
Wakati nilipofungua barua zako, moyo wangu ulikuwa katika mfadhaiko wa mapambano kati ya lipi nilifuate, unafsi wangu wa chini ukishindana na unafsi wa juu; kuhusu lipi nilifuate, matokeo yake ni ushindi. Ujumbe wako wa ajabu ulinisafisha kwa kuniosha. Ulinitakasa. Yale uyazungumzayo yana maana kubwa na **ukweli** mtupu, ulio katika maandishi ya herufi kubwa.

Profesa wa Chuo:
Labda utapenda kufahamu, mtihani wa mwisho wa falsafa 201 kesho utahusisha vipengele kadhaa na maswali kuhusiana na misemo yako yenye busara.

Mwandishi wa barua:
Nimesikia mihadhara ya William Jennings Bryan; Msemaji mashuhuri wa nyakati zake. Pia nilimsikia Dr. Russell Conwell akitoa mhadhara wake mashuhuri uitwao " Ekari ya Almasi" na kwa sasa hivi ninataka kusema kwamba mhadhara wako ulioutoa ulizidi ule wa Bryan na wa Conwell.

Rafiki:
Ninakushukuru sana kwa kunitumia fasihi ya maandishi yaliyonipatia mguso mkubwa moyoni. Maandishi hayo yanaleta kumbukumbu kichwani mwangu kila mara. Barua yako kwangu ilikuwa kama jibu la sala. Ilifika kwenye siku muhimu ya kuhitaji amani ya dhati, mfadhaiko wangu ulielekea kuyeyukia mbali. hali ilikuwa ni ya kuliwaza.

Mhubiri huko Texas:

"-----Nilitoa kijitabu chako **Hatua kuielekea amani ya dhati**, kwa wahubiri wa Kanisa wa sehemu ya Pwani mashariki. Wote watapendezewa kukuona unaongea kwenye makanisa yao. Niliwaambia kwamba wewe ulikuwa ni kitu kizuri ambacho kilikuwa hakijawahi kutokea kwenye kanisa letu. Na nilikuwa na maana halisi ya kutoka moyoni. Ninajua wewe ni baraka kwa ulimwengu wote.

Rafiki huko Baton Rouge:

Kwa hakika ni matumaini yangu kwamba ukweli wako pamoja na ujumbe uutoao kuhusiana na maisha juu ya hali ya amani unapata mapokeo makubwa ya watu mahali popote uendako----.

Wengi wanaguswa sana viajabu kwa namna wanavyoenzi hali ya kivita ambayo inahubiriwa sehemu zote hivi sasa. Hakika, hakuna mtu yeyote mwenye akili timamu awezaye kuunga mkono maandalizi haya makubwa ya kuiangamiza jamii hii ya mwanadamu. Ajabu na kweli iliyoje kutakapobainika ushindi wa amani na haki dhidi ya nguvu za vifo na maangamizi ya aina yake...!

Mtawa wa kanisa Katoliki kutoka California:

" Kwa maana nzuri unaendelea kukanyaga njia pamoja na wakatoliki mkishughulikia amani -----"wewe ni shahidi wa leo wa amani ya Yesu."

Mwanachuo wa huko Illinois:

Imepita miezi michache tangu tulipokutana. Na ujumbe wako umekuwa akilini mwangu tangu wakati huo. Nimesikiliza kwa muda mrefu kutoka kwa watu wenye mafanikio wakinieleza nini maisha na nikawa ninawafuata kiupofu upofu. Hata hivyo; nilipata kile nilichokuwa ninakitafuta kutoka kwa mwanamke mdogo mwenye mvi asiye na chochote cha kumiliki-----."

Kiongozi wa kanisa:

" Ninakushukuru kwa hamasa yako pamoja na maneno ya kunitia moyo. Wewe ni mtu aliyetumwa na Mungu kuhudhuria mkutano wetu. Kanisa letu limepata maisha mapya, upatanisho na ujumbe mkubwa."

Mwanachuo:

Tangu niusikie ujumbe wako nimefanya kazi kubwa ya kujitathimini pamoja na kufanya marekebisho yahusuyo thamani ya vitu na upendeleo maishani mwangu. Niligundua kwamba; nafsi yangu ikiwa na tamaa kubwa ya kushiriki na wengine ambao wamezama kwenye hali ya kujipendelea pamoja na uoga. Nimekuwa nikishughulika sana nikijaribu kuishi na ikiwezekana niendelee kiasi kwamba nilikosa kupata mengi naya manufaa katika maisha. Nilikuwa nikimsubiri mtu ambaye angefungua njia kwenye ukuta wa mfadhaiko na kukata tamaa, mambo yaliyokuwa yamenizunguka. Ujumbe wa matumaini na upendo ambao uliuchangia pamoja na darasa letu usiku huo ulinisaidia kufungua ukurasa mpya wa maisha ambaoulinionyesha mengi mazuri yaliyosalia ulimwenguni. Wako wengi walio nje

ambao ni kama mimi wanasubiri mtu yeyote awezaye kuja kuwagusa roho zao ziamke. Wakati huo mimi nisingeweza kuwa na moyo wa kusafiri safiri kama ufanyavyo. Ninaweza kuwafikia watu wa Springfield---.

Ninataka kukushukuru kwa msaada wako ulioniwezesha kuamini watu. Pamoja na Elimu hii kubwa niliyonayo, hilo ni jambo pekee ambalo nilikuwa sijajifunza. Msukumo ulionao kuhusiana na Amani pamoja na upendo unajionyesha usoni mwako, hakuna haja yoyote kwako wewe kushawishi ama kuwa na mjadala mrefu kuhusiana na hicho ukielezacho. Hakika Mungu amekubariki-----. Mwanga wako na umulike kwa miaka mingi zaidi.

Rafiki:

"----- Kukutana na wewe kumemaanisha mengi kwangu. Kwa mara ya kwanza nimejiuliza kwa mshangao mkubwa kwamba; ni wajibu gani nilionao katika mpango mtakatifu____ haikuwahi kunitokea kabla kwamba linaweza kuwapo jambo muhimu ambalo ningepaswa kulifanya-----."

Msikilizaji wa redio:

" Kwa miaka yangu hamsini na mmoja ya kusikiliza, kusoma na majadiliano sijasikia wala kuona ukweli ukitolewa kama unavyohusishwa nje na ndani kimatatizo kwa mantiki bayana yenye ufasaha kama ulivyoueleza kwenye kipindi chetu cha redio leo. Unao ujuzi wa kushangaza kuhusu matatizo ya maisha yanayowasumbua watu na serikali zao nyakati hizi. Na ufumbuzi wa matatizo haya unaouongelea unaonyesha mantiki pamoja na ahadi nyingi."

NYONGEZA YA VII

## BARUA KUHUSIANA NA MSAFIRI WA AMANI:

*Watu waliokutana na Msafiri wa Amani, siyo kwamba walimuandikia yeye pekee pia waliandika na kwa rafiki zao, ndugu, viongozi wa Makanisa na wahariri wa Magazeti mbali mbali. Wengi walijihisi msukumo mkubwa kuwashirikisha wenzao katika habari njema za huyo mwanamke. Na hata waliwashauri wenzao kutafuta maeneo ambayo Msafiri huyo angeongelea ili waweze kumsikiliza.*

Msikilizaji wa redio:

Sikumbuki wakati nilipofurahiwa na kuhamasishwa na mtu aliyeongelea amani ya dhati ndani mwao pamoja na furaha kama ilivyokuwa jana jioni, nikisikiliza mahojiano na yule mwanamke avutiaye; Msafiri wa Amani-----. Imani yake iliyo na msimamo mkubwa wa kujali watu kuliko nafsi yake imeniathiri baada ya kuwa nimemsikiliza mara moja kuliko wengi ambao nimekuwa nikiwasilikiza mara kwa mara kwenye ibada, mahubiri mbali mbali, sheria, mazungumzo ya falsafa na kadhalika. Mazungumzo yake yalikuwa ni ya kwanza kuigusa roho yangu kuliko yote niliyowahi kuyasikia.

Bwana na Bibi waliowahi kumkaribisha Msafiri wa Amani usiku ule wa kwanza alioanza Hija yake Januari 1953:

Hakika, tulishangazwa sana kukutana na mtu aliyekuwa amechiari kuishi maisha aliyoishi Kristo.Ujumbe wake ni mojawapo ya maelezo yake kuhusu upendo, na upendo ndiyo tiba pekee ya hali ya sasa ulimwenguni.

Kiongozi wa Kanisa:

" Imani ya Msafiri wa Amani kuhusu Mungu na ubinadamu ni nzuri kuichunguza. Anajenga uwiano kati ya maisha ya mtu na maisha ya kila siku ya neno la Mungu kuliko yeyote nimjuaye."

Profesa wa Chuo:

" Mara yangu ya kwanza kukutana na Msafiri wa Amani ilikuwa miaka mitano iliyopita wakati alipoongea kwenye madarasa yangu. Mazungumzo yake yaligusa mioyo yetu katika hali ya pekee kwani yalizungumzwa na mtu ambaye kiukamilifu alikuwa anaishi maisha ya kuamini kwa imani kubwa sana. Mwaka huu wakati Msafiri wa Amani alirudi Los Angeles tena aliweza kukutana na madarasa yangu. Ujumbe wake uling'aa sana ukatoa hamasa ya aina yake. Sijawahi kumsikia yeyote akiongea katika hali ya kupendeza na ya kumfanya mtu ajiulize ni nini maisha yamfaayo mtu ili aweze kuwa mwanadamu. Na ni lipi liwezekanalo kwetu sisi sote kama wanadamu. Maisha yake ni ushuhuda hai wa kuuthibitisha ukweli wa ujumbe wake."

Rafiki:

" Msafiri wa Amani kama si mwanamke mwenye tabia yakuchanganyikiwa na maisha aliye mpumbavu, basi ni nabii wa Mungu mwenye kuaminika. Ni juu yetu kuamua tufuate lipi hapo tunapokutana naye. Lakini la kustajabisha, ni kwamba; maelezo ya kwanza hayathibitishi unabii wake. Kama Msafiri wa Amani ni mpumbavu, basi tuseme upumbavu wake anauficha ipasavyo. Na kama ni nabii, basi ukungu wa kutokutukuzwa umeficha ukuu wake. Mtu huyo ni mugumu sana kueleweka. Mtu yeyote ataendelea kumuweka huku na kule akitafuta ukweli wake. "

Kiongozi wa kanisa:

" Hivi ni mwendawazimu? Je, ni mtu mwenye mambo yake yaliyo ya pekee? Ama ni mtu wa ajabu ajabu asiyefaa kuongea na watu? Hayo yote siyo kweli kabisa. Anazo akili timamu nyingi sana zenye kumfanya aongee mambo makubwa kuliko yeyote niliyewahi kumuona hapa ulimwenguni."

Msikilizaji kwenye mhadhara:

Msafiri wa Amani aongeapo kila mtu hukaa akimsikiliza kwa makini. Maneno yake ni ya kawaida lakini yana maana kubwa izigusayo hisia za watu_ halikadhalika na njia yake. Hali hii imemuondoa katika utaratibu wa kawaida wa kuwasiliana na watu kiasi kwamba anapendwa na wote. Hatetei matendo yake ya kuwafanya watu wote waachane na vitu walivyo navyo na badala yake waishi maisha yale aishiyo na wala yeye si mtabiri wa mambo mabaya ya ajabu ajabu ya kutokea baadaye.

Barua kwa Mhariri wa Gazeti:

" Msafiri wa Amani aliyeutembelea mji wetu kwa siku mbili, amekuja na kuondoka. Hivi, picha yake siyo kwamba imo kwenye mawazo yetu mara tumuwazapo? Hivi, siyo kwamba mtu huyu anatukumbusha mtu mwingine mmoja aliyewahi kuonekana akitémbea kwenye barabara za Galilaya miaka elfu mbili iliyopita? Mtu aliyejikana nafsi yake, familia yake pamoja na vitu vyake vile ambavyo sisi kuwa navyo hujiona kuwa tunayo mafanikio makubwa, na ambaye hakuwa na sehemu kubwa maalum ya kukiegeshea kichwa chake; lakini akaazimia kuueleza ulimwengu habari njema ya wokovu na matumini. Mtu huyo si yule ambaye sasa anaitwa Mwana wa Mfalme aletaye Amani? "

"Tungejivunia kusema kwamba huenda ingekuwa vigumu kutamka na kuutaja mji wetu kama ilivyosemwa miji kadhaa ambayo Yesu aliitembelea. Hapana shaka ya kuhisi kwamba huenda wenyeji wake walikung'uta vumbi la mji wetu kutoka miguuni mwake na kumkana kwa kutokuwa tayari kuusikiliza ujumbe wake---La, hasha! Mtu huyo alikaribishwa vema hapa kwetu."

"Hakika uwepo wa Msafiri wa Amani unatufanya sura yake iendelee kuwa mawazoni mwetu ikiamsha hali ya ukweli wake uliofunuliwa kwetu na roho wake. Bila shaka wote tunafahamu kuwa hivi sasa tumesimama kwenye ncha ya kisu kikali tukiwakati ya hali ya matarajio ya vita ya kutuangamiza ama kipindi kizuri

cha maisha yenye amani. Wote hatuwezi kufanya matembezi ya hija ndani ya lindi la umasikini tukizitegemea imani zetu tu kama vile afanyavyo mwanamke huyo, lakini uwepo na matendo yake, hakika vinatuita tujiulize ni nini tulifanye kwa ajili ya amani ya dunia."

Rafiki:

Wakati fulani katika maisha yangu nilipokuwa ninapambana na uwezekano wa itikadi katika kanuni na matendo nilijikuta nikitafuta watu ambao mafundisho na maandishi yao yangetumiwa kama mfano mzuri wa kutumiwa katika kuyafanikisha maisha. Kila njia ya uwezekano wa kumpata mtu wa aina hiyo ilitumainiwa kwa hali ya juu siku zilivyozidi kusonga mbele. Bila kuficha wazo lingine naweza kusema kwamba hali hiyo iliniongoza kwenye hitima ya kuamini kwamba itikadi ni mpangilio wa mawazo. Niliendelea kupata mvuto mkubwa katika kutafuta itikadi katika maisha ya kila siku. Na bado ukosefu wa kuishi maisha ya kuamini bila uthibitisho uliniacha katika hali ya kukata tamaa. Ilionyesha kwamba wanaitikadi wote walikuwa wanafasihi. Hatimaye, niliongozwa kukutana na mtu mwenye roho wa kweli, mwanamke ambaye hapo awali aliitwa kwa jina la " **Msafiri wa Amani."**

Kiongozi wa Kanisa huko Iowa:

" Tumeshuhudia siku za mwisho wa juma tukiwa na Msafiri wa Amani, tuseme kwamba watu siyo kwamba wanamsikiliza tu aongeapo, pia wanatumia muda wao mwingi wakijadiliana naye mambo mbalimbali yanayohusiana na falsafa yake. Mwanamke huyu anaonyesha kuzoeana na kila aina ya maisha anayokutana nayo."

Aliongea kwenye ibada zetu mbili wakati wa asubuhi na wakati wa jioni alitoa mhadhara kwa watu wengi isivyo kawaida. hii ninaamini ni kutokana na matangazo wayapatayo kupitia kwenye vyombo vya habari. Aliutumia muda wake akiongea na vikundi viwili vidogo na aliongea mara mbili kwa vikundi viwili kwa siku, mkusanyiko wa mazungumzo ya amani uliowahusu wazee wa Kanisa kutoka maeneo mbali mbali. Alijisikia kama yuko nyumbani wakati alipoongea kwa muda wa dakika themanini kwenye mkusanyiko wa wanafunzi wa Chuo Kikuu, Maprofesa, pamoja na watu wengine wa Mjini kwenye eneo la Chuo cha Morningside. Pia aliamuru utii wa kimaombi na heshima kwenye chakula cha jioni ambacho kilihudhuriwa na maprofesa wa chuo pamoja na maafisa wa utawala. Mkutano huo uliwachukua muda wa saa moja na nusu.

Kiongozi wa Kanisa California:

" Mwanamke huyo alinivutia sana, mimi pamoja na familia yangu. Mazungumzo yake (Kuhusiana na namna ya kuipata amani ya dhati) ni ujumbe wenye mantiki kubwa ambao nilikuwa sijawahi kuusikia. Yeye ni nguzo ya nguvu, wakati nguvuzihitajikapo. Yeye ni mwanga ung'aao, wakati mwanga uhitajikapo. Hakika yeye ni kioo cha sifa zote za Ukristo. Mimi binafsi, pamoja na wengine

tuliomsikiliza, tulijihisi msukumo wa aina yake upande wa kiroho na hakika tulibarikiwa."

Kiongozi wa Kanisa huko Kentucky:

" Kumsikiliza Msafiri wa Amani akieleza nguvu za kiroho zilizomhamasisha kufanya shughuli aifanyayo sasa, hakika ni ujumbe wenye mguso wa kiroho kwa yeyote amsikilizaye. Kamwe hutafurahia kama hukuwahi kukutana naye. Mwanamke mwenye wingi wa furaha na ampendaye kila mtu. Mwanamke huyo anaishi kwenye mazingira ya uwepo wa Mungu na kwa kila neno anenalo na kila alifanyalo huonyesha mawasiliano yake ya karibu sana na Nafsi ya juu Aishiye na Nafsi ya juu yenye Nguvu."

Kiongozi wa kanisa huko Houston:

" Urahisi auonyeshao huyo mtakatifu wa kisasa siyo tu kuwa unatuweka katika hali ya kujirekebisha katika hali ya maisha tuishimo, bali pia unatuweka katika hali ya kuyajenga maisha yetu kivitendo kwa njia ya Amani tukiwa tunamuelekea Mungu kwa nyakati zijazo."

Rafiki huko Colorado:

" Nilikutana naye likiwa ni jibu la hamu yangu ya kumuona mnamo mwaka 1968. Alikuwa ameonekana kwenye televisheni kwa hali yenye sura ya kupendeza. " Laiti kama ningekutana na wewe, ninahitaji kukuona tuongee." Nilifikiri baada ya kumuona kwenye televisheni. Hivyo kesho yake asubuhi nilipokuwa nikiendesha gari barabarani, ghafula nikamuona Msafiri wa Amani akiwa anasubiri usafiri. Gari langu lilisimama eneo alilokuwa nikamuomba aingie garini, nikamueleza kuwa nilikuwa nikimsubiri. Niliendesha gari kwa muda wa saa tatu kwenda Nashaville ambako alitakiwa kuongea. Ulikuwa ugeni wa ajabu kuuona maishani mwangu. Niliongea naye kuhusu uandishi wa kitabu kimhusucho."

Meneja wa kituo cha redio huko Maryland:

" Leo nimekuwa na furaha kumhoji mmoja wa watu wasio wa kawaida kati ya waliowahi kukutana nami. Mtu huyo anaitwa Msafiri wa Amani."

" Ni mwanamke msomi mwenye ujuzi mkubwa na ambaye anao uhamasishaji wa aina yake wakati aongeapo na watu. Bila kuwapo na mambo mengine yenye kuzua itikadi zingine za kipumbavu ama kumueleza mtu visivyo, mwanamke huyo ameleta ujumbe uwavutiao watu na wenye mguso kwa kila mmoja."

Mwanamke mwenyeji wake aliyeandaa maeneo ya kuzungumzia kwa Msafiri wa Amani:

" Msafiri wa Amani alipita hapa tena. Mnamo miaka ishirini na minne iliyopita tulikutana na mwanamke huyu wa pekee anayeishi maisha ya amani na upatanisho ambaye halinganishwina yeyote tuliyewahi kumuona. Kwa miaka kadhaa ametembelea nyumba yetu wakati alipokuwa anapita akiwa kwenye safari zake za hija. amekuwa nguvu ya kuendeleza hamasa ya kiroho kwenye maisha yetu. Jambo

ling'aalo sana hakika linaona na kufahamu mtu halisi kwa miaka mingi aliyejawa na nguvu zisizoisha na ambaye amesikika akisema lipo pale kwa ajili yetu wote."

***Kutokana na kifo chake mwezi wa Julai 1981, barua ziliendelea kumiminika kwenye kituo kidogo cha posta huko Cologne New Jersey_ hasa kutoka kwa watu ambao walikuwa wanaandika tu lakini hawamfahamu, ambao pia walitaka kuchangia mawazo pamoja na wale waliokuwa karibu naye. Wengi waliandika habari zenye masikitiko zikiwa na mguso mkubwa wa kiroho kuhusiana na matembezi yake ya amani, maisha yake pamoja na ujumbe wake.***

Kiongozi wa Kanisa huko Dallas:

" Hakukuwepo mtu kama yeye. Alitoa mchango kwenye ulimwengu wetu huu ambao hivi sasa umo kwen: . maisha ya ajabu ajabu. Upweke wake uliokuwa na kusudi, kujitoa kwake kuufan; utumishi wa Mungu, upendo wake, ucheshi, furaha usoni mwake isiyoisha pamoja na muelekeo wake katika maisha matakatifu, ni mambo yaliyoyabadili maisha ya wengi wetu. "

Rafiki huko San Diego:

Uwepo wake daima ulinihamasisha na niliweza kuhudhuria mikutano yake mingi kadri ilivyowezekana mara ilipofanyika kwenye eneo letu. Kamwe sikuchoka mikutano yake, Ni kutokana na maelezo yake ndipo nipoamua kuja California ili niishi maisha ya kawaida na siyo kutafuta pato kubwa ambalo lingeniwezesha kulipa kodi ambayo inasaidia gharama za vita. Najaribu kuepukana na kuwa na kitu ambacho sikihitaji maishani mwangu. Hakuna njia ya kufahamu ni njia zipi alizitumia katika kukuza njia za kuueneza ujumbe wake kwenye ulimwengu unaogeuka, ninaona ni jambo lihitajilo fikra. Alituhamasisha kuishi tukiamini kile tukiaminicho na kukifanyia kazi kwa kadri ya uwezo wetu na kuacha matokeo yake mikononi mwa Mungu----.

Mtumishi wa Shirika la Msalaba Mwekundu la Kimarekani:

" Mara yangu ya kwanza kukutana na Msafiri wa Amani ilikuwa kwenye miaka ya sitini nilipokuwa kwenye Chuo Kikuu cha Wisconsin. Msafiri wa Amani alikuja mjini kwetu. Kikundi fulani kilitembea na mwanamke huyo kutoka kwenye eneo la Chuo Kikuu kuelekea mjini. Kikundi kiliongezeka ukubwa kadri kilivyosogea mjini-----, lakini kikundi kimojawapo kati ya vikundi vya nyakati za sasa kiliongozwa na Msafiri wa Amani."

Profesa wa Chuo:

" Msafiri wa Amani alilitembelea eneo letu la chuo kwa mwaliko. Aliongea na wanachuo kwa mambo ya Saikolojia, Elimu ya jamii, falsafa na dini, hali kadhalika

aligusia baraza la wanachuo kwa ujumla pamoja na vitivo vyao. Hakika alipokelewa kwa shangwe."

Mtawa wa Kikatoliki huko Dakota ya Kusini:

" Msafiri wa Amani alifanya mabadiliko makubwa maishani mwangu. Ni vigumu kufafanua namna alivyonigusa kwa mazungumzo yake. Pia anao mguso mkubwa wenye mvuto usioelezeka kwa wanafunzi hapa chuoni. Wema wake utaishi daima moyoni mwangu. "

Kipande cha gazeti toka Texas:

" -----Kwa maneno yake yenye fasihi kuu, alivuta ,mbingu akaisogeza karibu na nchi. alileta sifa zote za utakatifu kwenye maisha yake hapa---Alibadili maisha ya watu Marekani kote."

Rafiki huko Maryland:

" Msafiri wa Amani hakika alikuwa mwanga na mfano halisi wa maisha ya Kikristo. Aliyeishi kwenye maelfu mengi ya watu. Nilijihisi upendeleo mkubwa ulioje baada ya kujikuta kwa miaka kadhaa niko karibu kimaisha na huo mwanga uliong'aa, wenye upendo, mwalimu aliyejitoa na rafiki wa kweli wa watu."

Rafiki:

" Niliandamana naye kwa majuma kadhaa kwenda Hawaii tukiwa tunalala chini kwenye ardhi. Mbu walituuma sana, wakati huo nilikuwa nimejaribu kupuliza dawa mara tatu kuona kama angalau ningepata usingizi, yeye muda wote alikuwa kwenye usingizi wa pono! Hakuna mbu hata mmoja aliyemgusa na wala hakutumia dawa yoyote kumkinga na wadudu hao. Nilihisi mwenzangu alikuwa ndani ya upatanisho na viumbe vyote, vikiwemo na vile vilivyo hai."

Kiongozi wa Kanisa huko Indiana:

" Kumbukumbu pamoja na kazi zake viko hai kwenye mawazo ya watu, lakini kumbukumbu ni fupi, na kadri muda unavyopita hufanya wengi wetu kusahau kwamba kile tukiwazacho daima tutakikumbuka. Ni jambo la asili kwamba waandishi watataka kunasa roho yake kwa njia ya vitabu na maandishi hayo yatawekwa kwenye fikra. Ya kwake ilikuwa roho kamili iliyojazwa. Na hiyo haitakuwa rahisi kuinasa itakiwavyo. Maisha yake yalikuwa ni ujumbe wake na hiyo hakika ni vigumu kuunasa kwa njia ya maandishi----."

Kiongozi wa kanisa huko Indiana:

"-----Ni kiasi cha uzuri wa ulimwengu huu kwake yeye kuwa ameweza kutembea hivi----. Yeye kwa njia yake akiwa nauangavu wake wa mambo usiomithilika, akiwa anatufahamisha kuwa hata sisi tutabarikiwa endapo tutazifanya shughuli zetu kwa misingi ya amani ndani mwetu sisi na jamii ya ulimwengu kwa ujumla."

Kiongozi mwingine wa Kanisa huko Indiana:

." Msafiri wa Amani alituachia athari yenye hisia kubwa kwenye taifa zima kwa kuyagusa maisha ya watu kwa njia ya mwanga wake ulioongozwa na roho aishiye. Tunamshukuru Mungu kwamba mwanamke huyo aliweza kutembea miongoni mwetu----."

Rafiki:

" Ninaamini kwamba, kila mmoja wetu anaweza kupewa wakati fulani maishani mwake; nafasi ya kukutana na mtakatifu wa ajabu. Baada ya kuwa nimekaa na Msafiri wa Amani kwa wakati fulani ninaamini nilipewa heshima hiyo. Kwangu mimi Msafiri wa Amani ni mtakatifu halisi."

Rafiki:

" Msafiri wa Amani alikuwa mmojawapo wa watu wa pekee katika karne yetu-----."

Mhariri wa gazeti la Metropolitan huko Dallas:

" Upendo ulikuwa ni nia yake, ngao yake, silaha yake, na tuseme kila kitu. Wengine walifikiri kwamba alikuwa mwenda wazimu . Lakini pamoja na hayo yote aliwapenda kikamilifu. ' Ninaamini kwamba; utapenda kuandika kitabu kikuhusucho.' Nilimwambia maneno hayo mara ya mwisho tulipotembea naye. Tunajua, Msafiri wa Amani yuko huru na kazi yake itaendelea. Ninafurahi nilipata nafasi ya kumfahamu na hatimaye nikauelewa ujumbe wake na ninakubali mtindo wa maisha yake. "

Mwanamke aliyekuwa anategemea Msafiri wa amani kuja kwake huko Ann Arbor:

Wakati wowote nisikiapo-----myimbo za amani na kadri tuendeleavyo kufanya kwa ajili ya amani ya ulimwengu tutakuwa pamoja kiroho na mtu yule mashuhuri ambaye maisha yake yaliyagusa yetu kikamilifu na mguso mkubwa kwa watu wote popote kule alikokwenda.

Rafiki huko Portland Oregon:

Kifo chake ni pengo ambalo si kwetu tu; tunaomfahamu bali hata kwa ulimwengu wote---. Wote tulimpenda Msafiri wa Amani. Alibadilisha maisha yetu kwenda kwenye mema----- tunafahamu kwamba anaendeleza ujumbe wake juu kwa ajili ya binadamu.

Mhariri Katika nyumba ya uchapaji wa vitabu:

Ninahisi yupo Msafiri wa Amani zaidi humu ulimwenguni kuliko hapo kabla. Na huyu yuko karibu zaidi kuliko nilivyomfahamu. Sasa hivi kila mmoja wetu anayo sehemu ya huyo Msafiri, na yeye pia ni sehemu ya huyo Msafiri na Msafiri huyo ni sehemu yetu----. Ninaungana nawe katika mzunguko wa upendo, pamojana wengine wanaomfahamu na ambao waliguswa na ujumbe wake, tunalo jukumu kubwa mbele yetu.

Kijana wa kiume huko Virginia Magharibi:

Nilikutana na Msafiri wa Amani wakati nilipokuwa kwenye muda wangu wa mwisho kwenye Chuo mwaka 1973. alikuwa mgeni muongeaji kuhusiana na mambo ya Saikolojia kwenye darasa ( Mjadala wa kukua kisaikolojia). Nilimuona kuwa ni mtu aliyekuwa na hamasa kubwa hivyo nilihudhuria madarasa mengine na mikutano kwenye eneo la Chuo alikoongelea. Zaidi ya miaka kadhaa niliendelea kumfikiria pamoja na ujumbe wake, muda baada ya muda. Kumbukumbu hizo mara kwa mara ziliamsha roho yangu.

Baada ya kuhitimu, nilifanya kazi kwa muda wa miaka mitatu nikiwa na vijana waliotengwa kimaisha, wasiotambuliwa utu na wenye matendo yasiyofaa kwenye jamii wakiwa na zana za kazi zisizo salama. Tulitafuta njia ya kuwafungia watoto kiasi cha mamia na tuliwekwa kushughulika na watoto wagumu bila kuwatisha ama kutumia adhabu yoyote yenye kuumiza miili yao ama kifungo.

Hivi sasa ninashughulika kupata shahada yangu ya pili katika masuala ya jamii nikiwa ninasomea mambo yahusuyo Amani. Kwa miezi sita ninafanya mazoezi kwenye Draft Information and referral Centre, nikitoa ushauri kuhusiana na usajili pamoja na uchaguzi wa kuamua kuhusiana na mambo mbali mbali kuongezea na upinzani wa utumishi vitani kutokana na sababu za amani na upinzani wa mambo ya kivita. Nimesaidia kuanzishwa kwa kilabu ya kujisomea kuhusiana na amani kwenye shule moja ya juu ya Sekondari pamoja na kituo cha kusomea mambo ya amani kwenye Chuo Kikuu.

Nimepunguza idadi ya vitu ninavyovimiliki kiasi kwamba vingine ninaweza kuvitunza kwenye kabati dogo kwenye eneo la Chuo ambako mimi hubadilishia nguo na kuoga. Ninatunza mfuko maalum wa kulalia kwenye chumba cha rafiki yangu na ninamalizia usingizi wangu kwenye miti jirani na huweza nikatafuta hifadhi kwenye egesho la magari wakati mvua inaponyesha.

Baada ya kipindi changu cha mazoezi kumalizika, ninapenda kufanya kazi za muda nikitumaini kiasi cha dola mia mbili kwa juma. Fedha hizo nitazitoa kama mchango wangu kwenye Jumuiya yenye dhiki ifanyayo masuala ya amani, haki za jamii ama uhifadhi wa mazingira. Kwa kila dola kumi nizitoazo, nitaomba mgao wa dola moja kw ajili ya matembezi yangu nipewe. Hivyo nikitoa dola 10,000 kwa mwaka, nitapokea dola 1,000 kutoka kwa watu mbalimbali fedha ambazo zitanifanya niishi kwa kujitegemea.

Msafiri wa Amani alikuwa amepanga kuja Virginia Magharibi nyakati za vuli. Ninafahamu kwamba vilikuwapo vikundi vingi vya watu vilivyokuwa vinajiandaa kumuona na kumpokea. Nilikuwa ninatumaini kujadiliana naye kuhusiana na mipango pamoja na mawazo yangu. Hata hivyo, ninafurahia kwamba niliwahi kukutana naye mara moja, Watu kama Mohandas Gandhi, Martin Luther King, Leo Tolstoy, Albert Einstein, Dorothy Day na wengine, niliposoma habari zao

ziliniamsha kiroho zikajenga imani yangu dhidi ya mapambano ya kutumia nguvu. Msafiri wa Amani amenigusa zaidi kuliko hao niliowataja na upande mwingine anahusika kwa uamuzi wangu wa kufanya shughuli za amani na vijana, mitaala ya masomo ya amani na hasa hasa mipango yangu ya hivi karibuni. Mnamo miaka minane tangu nilipokutana naye, maneno yake yamekuwa burudisho na hamasa kubwa moyoni mwangu. Bado ninaweza kukumbuka mazungumzo yake kikamilifu."

" Msafiri wa Amani amenisaidia kuisikiliza sauti itokayo ndani mwangu ambayo nyakati zile ningeamua kuipuuza nikidai ni upuuzi ama jambo lisilofaa. "

" Ninatumaini ndani ya barua hii nimejaribu kujieleza ipasavyo nikitoa shukrani zangu za dhati kwa kumfahamu Msafiri wa Amani na ujumbe wake, na ni kwa vipi niaminivyo kwamba amenigusa maisha yangu. "

Mke na mume wake huko Calfornia:

" Msafiri wa Amani aliimarisha Imani yetu katika uhalisi wa ulimwengu wa kiroho na amefanikiwa kutupatia mfano kamili wa kitu ambacho kamwe hatukuwahi kuota ndoto ya uwezekano wake. Kitu hicho ni mtu kujazwa amani ya dhati ndani mwake pamoja na nguvu kubwa isiyoisha mwilini mwake. Ametupatia matumini ya kuitafuta nguvu hiyo ya mbingu na nchi kwa sababu yeye anasisitiza kuwa nguvu hiyo ipo tele kwetu sisi sote endapo tutaitafuta. `Kama mimi nimeipata na wewe waweza kuipata; ' alizoea kusema. Hamasa kubwa kuliko zote ni kwamba maisha yake na maneno yake viliwiana. Na huo ndio uliokuwa ujumbe wake."

## NYONGEZA YA VIII

## UZOEFU KWA MSAFIRI WA AMANI

***Barua zifuatazo zimetoka kwa watu waliopata nafasi ya kukaa na Msafiri wa Amani.***

Rafiki mmoja aliyekutana na Msafiri wa Amani kabla hajaanza hija yake: " Si muda mrefu ulikuwa umepita kabla Msafiri wa Amani hajajitokeza machoni pa watu kwenye maonyesho ya maua huko Pasadena mwezi Januari 1953, rafiki mmoja alimsindikiza mwanamke aliyekuwa anatembea bila viatu miguuni na mkononi akiwa ameshikilia viatu vyake akitokea maeneo ya ufukoni mwa bahari. Alivaa kaptura na blauzi yenye maandishi. Muda mfupi baada ya mimi na mume wangu kutambulishwa kwake; majadiliano yetu yalikuwa ya kuvutia sana kiasi kwamba nililazimika kuwapigia simu rafiki zangu watatu na kuwashawishi wawahi kukutana na mwanamke huyo. Baadaye, sisi, rafiki hao, pamoja na huyo mwanamke tulishiriki mlo wa jioni kwa furaha ambapo baadaye tuliungana na kikundi cha wachezaji wa dansi pale kijijini na baada ya hapo tulirudi nyumbani na kuzama kwenye mjadala ulioendelea hadi majira ya alfajiri siku iliyofuata.

Alieleza kuhusu kazi aliyokuwa anaifanya huko Washington D.C. ambako alifanya kazi kama mshawishi wa wajumbe wa Baraza la Kutunga Sheria juu ya masuala ya amani (Miaka kumi baadaye nilihudhuria warsha ya Baraza la Taifa la Kutunga Sheria Mjini Washington ambayo iliendeshwa na Baraza la Kimataifa la wanawake kuhusiana na uhuru na amani. Nilielewa kwamba alikuwa mshawishi wao kuhusu masuala ya amani na hakika aliifanya kazi hiyo zaidi ya mtu yeyote waliyewahi kuwa naye).

Alituambia kwamba, kadri alivyoendelea kuifanya kazi hiyo na watawala hao wa Chama cha Congress nchini Marekani ndivyo alivyoendelea kuamini kwamba njia ya utawala waliyokuwa wanaitafuta isingewachukúa muda mrefu kabla ya kuzua vita. Wazo hilo lilipoendelea kumsumbua alianza kujenga hoja kichwani mwake. Na hoja yenyewe ilikuwa hii: " Mimi sijihofii lakini endapo madhara yatatokea, ni kikundi kipi kitasimama kuitetea jamii? Masinagogi yalitusaidia wakati ule wa kipindi cha giza. Je, ni kikundi gani kilichoandaliwa kutusaidia wakati huu? " Masinagogi yalisaidia nyakati zile za giza kupunguza nguvu za vita. Je, ni kikundi gani hivi sasa kinaweza kuzúia mapambano yoyote ya kivita.

Mara moja aligundua kwamba hangeweza kulipata jibu lake endapo angeendelea kuishi Washington, na kwa vile aliona kuwa, hakuwapo na mtu yeyote aliyeonekana kujihusisha na jambo hili. alijihisi kupata msukumo wa kuacha kazi yake ili aifanye kazi ya kutafuta jibu hilo yeye mwenyewe.

Kwa kipindi cha zaidi ya mwaka mzima, alitembea kuzunguka nchi, akikitembelea kila kikundi kilichojitokeza kufanya shughuli zilizoelekea kwenye msingi wa ushirikiano.

"Baada ya kutafuta kwangu;" nikikumbuka yeye alivyosema, Niliamua kwamba nipate kikundi ambacho kingeonyesha muelekeo wakutetea maisha na utamaduni wetu nyakati za miaka yenye shida ambayo ingetokea mbeleni, nacho kilikuwa kikundi cha ushirika Koinonia huko Georgia. Lakini hata hivyo kikundi hicho hakikufanikiwa kuleta jawabu."

Wakati tulipofikia kuagana, kila mmoja wetu alielewa hamu aliyokuwa nayo mwanamke huyo katika kutafuta majibu ambayo yangemuwezesha kuchangia kikamilifu kwenye jukumu la kujenga ulimwengu katika misingi ya mapenzi na ushirikiano miongoni mwa mataifa yake. Haikupita miezi mingi baadae tulipogundua kwamba rafiki yetu amepata jukumu jema ndani ya ulimwengu huu unaobadilika kwa kasi kubwa kiasi kwamba angeweza kutuhudumia kwa njia itakiwayo.

Miaka mitatu baadaye, tulikuwa tunaishi huko San Bernadino, California, tulipojulishwa kwamba Msafiri wa Amani atapita mjini hapo. Alipofika, nilimuomba akakubali kukutana na watu mbali mbali kwa muda aliokaa mjini kwetu. Kiongozi wa Ka. isa la Ki-methodist alimuandalia kukutana na watu kwenye chakula cha usiku kanisani mwake, na tulishiriki kutekeleza mpangilio wa ratiba ya ugeni wake kama ilivyokuwa imepangwa.

Nilimpangia kukutana na wanachama wa kikundi chetu cha Umoja wa Vijana wa Kiume Wakristo (YMCA), Creative Living Club, kikundi kilicho jihusisha na masomo ya afya. Rais wa kikundi chetu pamoja na nusu ya wanachama wake walikuwa wanatokana na dhehebu la Sabato. Rais alifika kwenye mkutano kwanza ili amuone mwanamke huyo mgeni alikuwa yukoje, kwani wengi wa wanachama wa kikundi walikuwa wameonyesha mshangao wao wakisema; " Ni kitu gani ambacho mwenzetu (wakimaanisha mimi) anakifahamu kwa wmanamke huyu mgeni hadi aamue kumleta azungumze nasi?"

Baadaye, alipokwisha kukutana naye, Rais wetu aliniambia, "Msafiri wa Amani ni mtu wa ajabu! **Ajabu kabisa!** Sijawahi kumuona mtu kama yeye! Na hata wale watu waishio kwa mashaka ya kutaka kuonyeshwa ushahidi kabla ya kuamini wakimuona watampenda. atakuja kuwa msemaji mashuhuri zaidi ya wale tuliowahi kuwa nao."

Asubuhi, siku Msafiri wa Amani alipowasili, Kiongozi mmoja wa Kanisa langu aliniagiza kwamba endapo mwanamke huyo angesikika anakaribia kuingia mjini, nimjulishe ili ampokee kwa gari. Mara alipokaribia nilifanya kama nilivyokuwa nimeagizwa na Kiongozi wa Kanisa. Huko njiani, Msafiri wa Amani alikataa kupanda gari akieleza kwamba; alitaka watu wamuone wakati alipokuwa anauingia mji kwa miguu. Kumuona kwao kulikuwa kunaongeza mvuto wake kwa watu. Siku mbili baadaye, tulielewa ni nini ilikuwa maana yake. Watu wengi walikuwa wakimiminika kwenye mkutano wetu kutoka kila kona ya mji. Hali hii ilitulazimisha tuhame ukumbi na tuutafute ulio mkubwa zaidi kutokana na umati mkubwa. Ongezeko hilo pia lilitokana na mialiko yake aliyokuwa anatoa kwao muda ule alipokuwa anaingia mjini kwa miguu.

" Wakati kabla sijamkabidhi mgeni wetu kwa mhudumu wake, nilimpatia ratiba rasmi tuliyokuwa tumemuandalia ili aongee na watu makanisani pamoja na vikundi

mbali mbali mitaani kwa muda wote ambao angekaa pale mjini. Baada ya kuiangalia aliuliza kama kulikuwa na chuo chochote pale mjini. Baada ya kupata jibu, muda mfupi baadaye alikuwa anaongea kwa simu na mwalimu wa uandishi wahabari wa Chuo Kikuu cha California akimuomba wanafunzi wake wapate nafasi ya kushiriki mazungumzo naye kwa kumhoji maswali juu ya shughuli zake za amani. Ilikuwa baada ya kuwa tumemfahamisha kuwapo kwa Chuo hicho hapa mjini. Pamoja na ratiba yake kuelemewa na shughuli nyingi alifanikiwa kukichomeka kipindi cha kukutana na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha California mara baada ya kuwa amekubaliwa kukutana nao. Ni mpangaji mzuri aliyeje!"

*Rafiki mwingine aliyemfahamu Msafiri wa Amani kabla hajazianza shughuli zake za hija.*

" Nilikutana na Msafiri wa Amani wakati fulani baada ya vita ya pili ya dunia. Wakati huo nilikuwa ninafundisha huko Philadelphia na pia nikiwa ninajitolea kufanya kazi kwenye ofisi ya " **Ushirika na Upatanisho**" ambako nilikuwa nikifanya kazi karibu kila siku nyakati za mchana. Msafiri wa Amani wakati huo alikuwa anatumia sehemu ya ofisi yetu kufanya shughuli zake za uchapaji na usambazaji wa gazeti la Scott Nearings World Events. Gazeti hilo ninafikiri lilikuwa linatoka kila mwezi. Pamoja na shughuli za gazeti, Msafiri wa Amani alikuwa anafanya shughuli nyingine za kujitolea kuhusiana na Baraza la kimataifa la Wanawake katika masuala ya Uhuru na Amani. Alikuwa mtu mkimya na alijali sana kazi yake. Ilipofikia wakati wa kuyatuma magazeti ya World Events kwa wasomaji wake, aliwakusanya marafiki zake ambao walijitolea kuyafunga na kuandika juu Anwani za wasomaji, kazi ambayo ilifanywa kwa muda wa jioni moja. Alichukua dola 10 za Marekani ambazo zilikuwa kwa ajili ya matumizi yake ya Juma. Nazo alidai kuwa; bado zilikuwa nyingi kwake. Ninafikiri wakati huo alikuwa na gauni mbili tu ambazo alizivaa kwa zamu, moja baada ya nyingine. Wakati wote alionekana katika hali ya usafi, makini, na mwenye mpangilio nadhifu wa mambo, hali ambayo aliionyesha dhahiri katika maongezi yake, halikadhalika na katika tabasamu lake. alikuwa kwenye klabu ya watu wazungukao masafa ya mbali kwa miguu, mara moja kwa kila mwaka. Ninafikiri alikuwa anatembea masafa ya maili arobaini au zaidi.

Yeye kidogo aliweza kuridhishwa na juhudi zake zilizomuwezesha kukamilisha matembezi yake ingawaje wanachama wenzake walio wengi walishindwa baada ya kutembea umbali wa maili thelathini.

Alikwenda pwani ya magharibi akatembea kwa kiasi cha miaka miwili bila kuwa na uoga wowote njiani alimopita. Akiwa kwenye safari yake hiyo alihudumia watu kwenye taasisi kadhaa za afya na kufikiria njia za ufanikishaji wa yale yaliyokuwa mbele yake.

Alivutiwa sana na Shelton huko Texas aliyezoea kufunga bila kula kama njia yake ya tiba.

" Kitu kimoja niwezacho kumkosoa (Kama ilikuwa ni kukosoa), ni kwamba; kwa wengi waliomsikiliza, alikuwa anatoa amani ya mawazo, jambo ambalo linahitajika sana kwenye ulimwengu wa kisasa na siyo sehemu nyingine zaidi ya

nchi yetu ya Marekani. Ninafahamu kwamba hakuwahi kushindwa kutumia ujumbe wake katika kutetea amani ya ulimwengu, lakini; ninahisi kwamba, ujumbe huo ulikwazwa na mawazo ya ubinafsi katika mahitaji ya vitu kwa wale waliokuwa wanamsikiliza."

" Lakini alileta ujumbe kwa makumi ya maelfu ya watu ambao vikundi vya kueneza amani visingewafikia."

**Rafiki aliyempeleka Msafiri wa Amani Alaska na Hawaii kukutana na jamaa zake:**

" Ninakumbuka wakati fulani, tulipoanza kufahamiana na Msafiri wa Amani nilimuuliza swali lifuatalo: ' Wakati fulani katika mizunguko yako ya hija ya amani nchini, ghafla ungekutana na kikundi cha wahuni waendesha pikipiki ambao huwa wanaiweka jamii katika hali ya wasiwasi, ungefanyaje? '

Ninakumbuka jinsi alivyoniangalia kisha akanijibu; ' Leon, wewe hujui?' na mimi nikamjibu ' Ndiyo, hali hiyo ninaifahamu.' Ninachokumbuka ni kwamba aliweka kiganja chake mkononi mwangu ili kuniweka sawa katika hali ya kumsikiliza, kisha akasema;

' Hapana Leon huifahamu. Ni hivi, mimi ninakwenda mahali walipo watu wa aina hiyo. Siwaombi kwenda mahali nilipo. ' Niliifikiria kauli yake hii kwa muda mrefu. Ilinichukua mpaka baada ya miaka kadhaa ndipo nilipoijiwa na maono ndani ya moyo wangu kunijulisha kwamba mwanamke huyo alikuwa na maana 'gani kwenye kauli yake hiyo."

**Huko Hawaii walikutana na kijana mmoja kwenye hifadhi iliyo kwenye kisiwa kikubwa:**

Yule kijana aliuliza kuhusiana na Msafiri wa Amani pamoja na mimi. Tulimwambia kwamba tulikuwa tumeingia kwenye hifadhi, ila hatukujua sehemu ile tulikokuwa ilikuwa ikoje! Na hatukuwa na mwongozo wa mahali pa kwenda. Kijana huyo aliomba kutuongoza ili atuonyeshe maeneo yavutiayo na ambayo yalikuwa na mandhari nzuri yenye hali isiyokuwa ya kawaida. Msafiri wa Amani alikubali tuongozane naye ndani ya hifadhi hiyo kwa muda wa saa moja au zaidi. Sijui niwezavyo kueleza hali ya kijana huyo kwa namna alivyoweza kuonyesha silika ya matendo yake yenye ukakamavu, wepesi pamoja na majivuno na madaha makubwa kwenye shughulizake. Pia nina hakika alikuwa na tabia ya ulevi wa kupindukia. aliongea kwa sauti ya juu yenye majivuno yenye kujigamba akijaribu kutuonyesha uwezo wake katika shughuli zake mle hifadhini. Kila sentensi aliyoizungumza ilikuwa na maneno ya ovyo ovyo. Hakuujali kabisa utu wake mbele ya watu. Kusema kweli mimi nilishangaa kabisa kujikuta tunaongea na mtu kama yule. Baada ya muda siyo mrefu tulijikuta tumewasili kwenye kituo cha wageni wa kitalii. Sehemu hiyo ilikuwa imejaa watu wakiwa wamevalia mavazi yaliyorandana na mazingira ya kisiwa kile wakiwa wanapita pita huku na huko. Hali ya hewa ilikuwa ni ya kupendeza sana. Mateso yangu kujikuta ninatembea na kijana mwenye majivuno kama yule yalikuwa hayaelezeki. Je, Msafiri wa Amani alikuwa akifikiri nini kuhusiana na kuendelea kuwa na mtu wa aina hii? Kwangu jibu la swali hilo lilikuwa kitendawili kwa ufupi niliteseka sana. Hatukuwa tumetembea mwendo

mrefu mara tulipojikuta tuko kwenye shimo la kulipukia volkano tukiwa tumesimama kwenye kileletukiangalia mandhari ya kupendeza yaliyokuwa ni ya aina yake. Sasa muda wetu ulikuwa umekwisha, tulitakiwa kuanza safari ya kurudi sehemu moja iitwayo " Hilo " ili tuwahi ratiba ya ndege ya kuturudisha kwetu. Msafiri wa Amani alimshukuru yule kijana kwa msaada wake na akamueleza kuwa muda wetu ulikuwa umekwisha hivyo ilitubidi tuondoke. Hakukuwepo na swali kuhusiana na namna alivyoonyesha kukata tamaa wakati aliposikia tunatengana naye. alisimama pale akilia, machozi yakiwa yanamtiririka mashavuni akiwa anatubembeleza tuendelee kumfuata ili atuonyeshe sehemu moja muhimu iliyokuwa imebakia. Wakati nimesimama pale nikiangalia usoni mwa kijana huyo, mara moja nilikumbuka maneno ya Msafiri wa Amani aliyoyatamka miaka kadhaa iliyokuwa imepita; " Ninakwenda mahali walipo. Siwaombi waje mahali nilipo." Maneno hayo yalinifanya nijihisi lawama moyoni dhidi yangu katika hali ambayo haikuelezeka. Na bado ninafahamu katika muda huo nilipokuwa katika hali ya kujilaumu ambayo ilikuwa imeghubikwa na mshangao wa ajabu kwa mwanamke huyo!

Kadri ninavyojaribu kuachana na mawazo yenye mtazamo tu wa maisha ya kidunia ili niingie kwenye maisha halisi ya kumtegemea Mungu, nimekuwa nikipiga taswira ya mahali nilikotoka inionyeshayo uhusiano wangu na Msafiri wa Amani kwa ule mfano alioniachia ambao unao ujumbe ambao ni hazina niitegemeayo kwa kiwango kikubwa."

***Kutoka kwa Mary O'Kelley rafiki wa Msafiri wa Amani pamoja na mwanamke aitwaye Jeanette Rankin ambaye ni Mbunge huko Marekani. Alikuwa mwakilishi pekee nchini Marekani ambaye alipiga kura bungeni kupinga vita vya ulimwengu.***

(Jeanette alimpigia simu Mary kumjulisha kuwa alihitaji kuongea na Msafiri wa Amani).

" Hatimaye tulifikia makubaliano; tukapanga tuwe na Msafiri wa Amani kwa kipindi cha usiku mzima na kwamba yeye angealika baadhi ya watu kuja kukutana na Msafiri wa Amani waweze kumsikiliza kuhusiana na hija yake. Baada ya mpango wetu huo kuwa umekamilika, Jeanette aliniuliza, " Sasa nimualike nani?" Hapo nikagundua kwamba alikuwa anaishi eneo lile kiupweke upweke bila ya kuwa na rafiki wala jirani.

Jeanette alikuwa amenunua ardhi ile wakati alipokuwa kwenye ubunge. Alikuwa na marafiki wengi huko Athens (Georgia). Wakati alipopiga kura bungeni dhidi ya Marekani kushiriki vita ya kwanza ya dunia watu wengi hawakupendezwa naye. Mara nyingine alipoingia ubunge mwaka 1941 akawa amekazana kupinga mambo ya kivita na hapo watu wakaona mambo yake kuwa yanakithiri dhidi ya vita, wakaamua kumchomea nyumba. Alikuwa na ardhi karibu sana na eneo la katikati ya kitongoji akawa amehamia kwenye nyumba ndogo iliyokuwa mle. Hii ilikuwa baada ya miaka ishirini na moja tangu tukio hilo, lakini bado alihisi uchungu wa mambo yaliyompata. Alikuwa na usongo mkubwa moyoni akiamini kwamba hakukuwapo na yeyote aliyempenda na hivyo kusema watu wote mle bungeni walikuwa wanatuongoza kwenye maangamizi makubwa ya umwagaji damu.

Nilimshauri awapigie simu majirani awaalike. Baadhi yetu walikuja kutoka eneo la Athens na nyumba ilijaa. Ninaaminimkutano wetu ulikuwa na idadi ya watu kati ya hamsini na sitini.

Baada ya mkutano, Msafiri wa Amani pamoja na Jeanette walikesha wakiongea usiku kucha. Jeanette alifurahishwa sana na tendo la kumiminika kwa watu kwenye ule mkutano, na Msafiri wa Amani aliona umuhimu halisi kwa Jeanette kuendelea na mapambano yake ya maisha ya kutafuta amani, na kwamba uchungu wote aliokuwa nao kuhusiana na mawazo ya kwamba hapendwi na watu ikiwa ni pamoja na matukio yaliyopita, aachane nayo kwa sababu uchungu huo ulikuwa unamuumiza yeye. Jeanette aliuliza kuwa ni jambo gani ambalo angeweza kulifanya. Msafiri wa Amani alimjibu kwamba kwa kutumia raslimali zake pamoja na jina lake angefanya mengi zaidi.

Msafiri wa Amani alisema kwamba; " Jeanatte aliongea kwa jazba kubwa akikazia kuhusiana na kuhitajika kwake pamoja na deni alilokuwa nalo kwenye jamii." Alisema kuwa, alihisi Jeanette alikuwa anafikiria kwa makini kujihusisha kikamilifu kwenye masuala ya kuieneza amani. Wakati wa majira ya vuli kulikuwepo na utaratibu ulioandaliwa na kikundi cha wanafunzi wa Chuo Kikuu. kikundi cha kuunga mkono masuala ya amani. Jeanette alihusika.

Alikuwa mwanamke aliyependeka. Msafiri wa Amani alikuwa amemuonyesha njia ya kurudi nyuma na kuanza upya na barabara yenye maisha na uhusiano mzuri na watu. Taratibu Jeanette akaanza kubadilika. Alianzia mahali alipokuwa amepaacha nyakati za miaka ya arobaini. Alikiongoza kikundi cha kitaifa kilichokwenda Washington (Kiliitwa Brigade ya Jeanette Rankin wakati wa vita ya Vietnam). Alitumia muda wake uliokuwa umesalia akishughulikia masuala ya haki za wanawake.

**Mtawa wa Kifransiska:**

Nyakati za miaka ya sabini Sista Johnella alimuona Msafiri wa Amani kwenye televisheni na akawa rafiki yake wa kalamu, lakini iliwachukua kipindi cha miaka sita kabla hawaja kutana ana kwa ana. Sista Driver alimleta Msafiri wa Amani kwenye nyumba yetu ya Villa na alipokelewa kwa shangwe kubwa. Kila mtu alitaka kuongea naye, Sista Johnella alionyesha furaha isiyo kifani na sasa hakutaka kuwa mbali na mahali alipokuwa Msafiri wa Amani. Tuliongea naye ikiwa ni pamoja na kuendesha sala kwenye chumba cha jumuiya.

Miaka mitatu baadaye alitutembelea safari tano, yaani safari tatu alikuja mchana na safari mbili nyakati za usiku. Alijisikia kuwa nyumbani kwa muda aliokaa nasi akiyafurahia mazingira yetu. Nyakati za asubuhi; aliongea na baadhi yetu ambao walikuwa hawana shughuli nyingi za kufanya, halikadhalika nyakati za mchana na jioni. Maongezi yake pamoja na uungwana aliouonyesha kwetu ni baadhi ya mambo mengi yaliyo tuvutia sana kutoka kwake.

Asubuhi moja tulimfulia nguo na yeye akaoga maji ya moto. Tulimuambia kuwa tungefurahi sana kumpatia mavazi mapya kwa ajili ya shughuli zake na akatujibu kwamba alipendelea tusifanye hivyo.

Siku moja nilipata nafasi ya kumtembelea. Tuliongea na kuzoeana kwa kiasi kikubwa. Nilimwambia, " Nitapenda kujiunga nawe na kufanya yale uyafanyayo kwa ajili ya amani. Nitakuwa na wewe ili nikuondolee upweke."

" La, hasha." alisema.

" Huwezi kunisaidia ama kutembea na mimi kadri nitakavyohitajikuwa na wewe. Ujumbe niubebao ni tofauti kabisa na ni kwa ajili ya mtu mmoja tu, mimi, Msafiri wa Amani."

Halafu akaniambia; " Wakati ujumbe wangu huu niuenezao utakapofikia mwisho na mimi wakati huo niwe nimetoweka Amani itakuja." Huyo mwanamke alikuwa nabii." Aliongea mambo aliyokutana nayo barabarani alimokuwa anapita ambayo yalikuwa ni ya kutisha. Mungu aliwezaje kumkinga kiasi hiki!

**Maelezo ya mwenyeji wa Mazungumzo ya maonyesho kwenye televisheni:**

Vita ya Vietnam ilikuwa inapamba moto. Nilikuwa ninaanza kufanya maonyesho ya mazungumzo kwenye televisheni yahusuyo WSM huko Nashville. Nikiwa bado mbichi katika mambo ya kiroho na nikiwa na hamu ya kutaka kuonyesha picha ya mambo niyafanyayo, nilifurahishwa sana na wazo la mtu huyu mwenye mambo ya ajabu ajabu kutokea kwenye onyesho la televisheni.

Nilianza kuiandaa mitambo yangu baada ya kuwa nimesoma barua iliyoletwa kwangu ikinijulisha kuwa alikuwa anatembea kuelekea upande tulikokuwa. Alipoingia kwenye kituo cha televisheni nilicheka pamoja na watu niliokuwa nao mle ndani. Tulijiuliza; " Ni bibi gani huyu anayeonyesha kuchoka na maisha? "

Nilimuonyesha kila aina ya matendo ya kumdhihaki na kumbeza kadri nilivyoweza. Nyakati hizo matendo kama ya ushabiki na utani wa vichekesho kwa watu waenezao amani hasa hasa kwenye maeneo tuliyoishi yalimfanya mtu aliyetaniwa achukie na atende matendo ya hasira. Mnamo muda wa dakika chache za mwanzo za mahojiano yetu, aliongea na mimi kwa hali ya utani. Amani akionyesha uchangamfu wa ajabu. Kamwe katika mazungumzo yake hakutoa kauli za kujitetea au za kuonyesha hasira za ugomvi ugomvi. Lakini macho yake, mikono yake, aliitembeza hewani wakati akiongea ikiwa ni ishara ya kutafuta hoja muhimu ili kujenga kile alichokizungumzia; bila kusahau macho yake ya rangi ya bluu.

Baada ya kama dakika mbili ama tuseme tatu za mazungumzo yake, tayari nilikuwa kwenye viganja vya mikono yake. Aliweza kuuteka moyo wangu kwa maneno yake. Nilijihisi kushangazwa na mwanamke huyu mwenye hoja zichomazo mioyo ya wale wamsikilizao na hapo hapo nikawa ninajionea aibu kwa yale yote niliyokuwa nimemuonyesha kabla. Mara moja alinionyesha kusoma mawazo yangu wakati huo nilihisi kuwa kama alikuwa amejua kuwa ushindi wa ujumbe wake ungepatikana kwenye kipindi cha mahojiano baada ya kuwa ametega mtego wake kwenye mazungumzo.

Dakika nane zilipokuwa zimekwisha walikuwepo watu wachache sana kati ya wale waliokuwa pale ambao bado walimuona kuwa ni mtu mwenye mzaha.

Watu wengi mle walionyesha kuguswa na mazungumzo yake. Utani na mizaha havikusikika kabisa. Siku hiyo nilijengeka kiroho ipasavyo.

Miaka mingine iliyofuata, tuliendelea kuwa na mahojiano na mwanamke huyo wa ajabu; lakini yote hayo hakuna niikumbukayo kama ile tuliyokutana naye kwa mara ya kwanza.



"Msafiri wa Amani katika nyakati za usichana wake.



Picha kwa Uhisani wa Fresno Bee.

# MWALIKO

**Kutoka kwa rafiki wa Msafiri wa Amani:**

Ni matumaini yetu kwamba; umepata uchecheo fulani kutokana na kitabu hiki. Hivyo, utapenda pia kukisoma kijitabu kingine cha kiroho kiitwacho; **Hatua za kuelekea kwenye hatua ya dhati moyoni.**

Kitabu hiki kimetokana na Msafiri waAmani. Kitabu hiki kodogo chenye kurasa chache chaweza kuchukuliwa mfukoni mwako ama kwenye kifurusi kidogo kikatumwa kwa njia ya posta kwa gharama kidogo. Ni jambo la busara upatapo nafasi ya kutuma kadi ya Krismasi kwa rafiki ama ndugu ukaambatanishwa pamoja na kijitabu hicho.

**Rafiki wa Msafiri wa Amani** ni jumuiya inayofanya shughuli zake bila kutoza riba na wala haitozwi riba yoyote; kwani imejitoa kueneza ujumbe wa Msafiri wa Amani. Watu wote waliomo ndani ya jumuiya hii ikiwa ni pamoja na zawadi mbalimbali zitolewazo hata kama ni kidogo vimewezesha kusambaza nakala nyingi za vitabu hivi kwa yeyote anayevihitaji bila kutoza malipo. Gharama za uchapaji wa vitabu hutolewa na rafiki wote wa Msafiri waAmani waliosambaa ulimwenguni mwote ambao wanapenda kushirikiana na wenzao wengine ulimwenguni kupata maneno yenye uchocheo ya Msafiri wa Amani.

Vitabu vyote viwili vinatafasiriwa na kuchapwa katika lugha mbalimbali.Wengi huandika wakisema kwamba Msafiri waAmani amewapa moyo mpya wa matumaini na hivi sasa hata wao pia wanashughulikia Amani.

Wengine huandika kuhusu sala yaAmani pamoja na vikundi vya kuenezaAmani ambavyo vimeufanya ujumbe wake kuwa katika matendo.

Ni jambo lenye mguso wa kipekee kwako wewe ukiwa sehemu ya jumuiya ya rafiki wa Msafiri wa Amani; ukasaidia kuleta Amani ulimwenguni. Tafadhali kama unahitaji vitabu ili visomwe na watu waliokuzunguka; tunakuomba utujulishe.

Anuanu yetu ni:
***Friends of Peace Pilgrim,***
*43480 Cedar Avenue,*
*Hemet, California 92544.*
*UNITED STATES OF AMERICA.*

---

**Kitabu hiki kimetafasiriwa na hawa wafuatao:**
Rev. Christopher Nyamuma - Mwenyekiti
Mwalimu Emmanuel G. Kagoro - Katibu
Emmanuel C. Araka - Katibu msaidizi

---

*Kwa niaba ya:*
THE TANZANIA RELIGIOUS SOCIETY OF
FRIENDS TRANSLATION COMMITTEE
S.L.P. 160, MUGUMU, SERENGETI,
TANZANIA.

---

*Hairuhusiwi kwa mtu yeyote ama kikundi cha watu kuchapa ama kuuza kitabu hiki bila ruhusa ya:*
The Tanzania Religious Society of Friends Translation Committee,
P.O. Box 160, MUGUMU, SERENGETI,
TANZANIA.